



# Twahara na Aina za Maji

## Maana ya twahara

### Utwahara kilugha

Kujisafisha na kujitakasa na uchafu

### twahara kisheria

twahara kutokana na hadathi -Kujitwahirisha na najisi

# Vigawanyo vya utwahara




## 1. Twahara wa ndani

Nao ni kuusafisha moyo na ushirikina na maasia na kila chenye kuutia doa. Haiwezekani kuhakikishika utwahara iwapo kutakuwa na uchafu wa ushirikina ndani ya moyo, kama ilivyo katika maana ya maneno ya Mwenyezi Mungu U:{Enyi Mlioamini! Hakika washirikina ni najisi, basi na wasiukaribie Msikiti wa Haram (Msikiti wa Makka) baada ya mwaka wao huu. Na mkiwa mnaogopa umasikini, basi Mwenyezi Mungu Atawakwasisha nyinyi kwa fadhla Zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni mjuzi Mwenye hekima} [8: 28]

Na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema: “Muumini hanajisiki.” [ Imepokewa na Bukhari na Muslim]

## 2.Twahara wa Nje

Nao ni twahara wa mwili kutokana na hadathi na najisi.
Na inagawanyika vigawanyiko viwili:

### 1.Utwahara kutokana na hadathi (hali ya kutokuwa na udhu na kuwa na janaba)

Hadathi ni kile kinachotukia katika mwili kikamzuia Mwislamu kufanya ibada ambazo zinahitaji utwahara, kama kuswali, kutufu kwenye Alkaba na zinginezo. Na inagawanyika vigawanyo viwili:
Hadathi Ndogo
Ni ile inayopasisha kutawadha kama vile kukojoa, kwenda haja kubwa na vitanguaji udhu vingine. Kujitwahirisha kwake

kunakuwa kwa kutawadha. Mwenyezi Mungu U Anasema: {Enyi mlioamini! Mkiinuka kutaka kuswali, osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpanguse vichwa vyenu na mwoshe miguu yenu mpaka vifundoni} (5: 6)

Hadathi Kubwa

Hiyo ni ile inayopasisha kuoga kama vile janaba, hedhi na vinginevyo. Na kujitwahirisha nayo inakuwa kwa kuoga. Mwenyezi Mungu U Anasema i: {Na mkiwa na janaba, jitwahirisheni} (5: 6)



Hadathi inazuiya kuswali



Kutawadha ni kujitwahirisha na hadathi ndogo

## 2. Kujitwahirisha na Najisi:

Nao ni kuiyondoa najisi mwilini na nguoni na sehemu ya kufanya ibada, Na kuondoa najisi ni lazima kwa neno la Mwenyezi Mungu U: {Na nguo zako zitwahirishe} (74: 4)

na neno lake Mtume (s.a.w) [Mmoja wenu akija msikitini na atazame, akiona uchafu au kitu cha kuudhi kwenye viatu vyake basi na avipanguse kisha aswali navyo]

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
Ghuslu - Twahara Najisi



twahara wa mwili




twahara wa mahali



twahara wa nguo

## Vigawanyo vya maji




## Kwanza: Maji Yenye kutwahirisha

### 1. Maji ya Kawaida:

Nayo ni maji ambayo yamebaki katika sifa yaliyoumbiwa nayo, kama maji yanayoteremka kutoka mawinguni, kama vile mvua, theluji na mvua ya barafu [ Barad (barafu) ni maji makavu yanayoteremka yakiwa vipande vidogovidogo.], au yenye kutembea ardhini, kama maji ya bahari, mito na maji ya mvua na maji ya visima. Mwenyezi Mungu U Anasema: {Na tumeyateremsha kutoka mbinguni maji safi }(25: 48)

Mwenyezi Mungu U Amesema: {Na akakuteremshieni maji kutoka mbinguni ili kukusafisheni kwayo} [8: 11]

Na mtume ﷺ alikuwa akiomba na kusema (Ewe Mola wangu! Nitakase na makosa yangu kwa theluji, maji na barafu) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim].

Na alisema tena ﷺ kuhusu maji ya bahari maji yake ni yenye kutwahirisha na mfu wake ni halali) [ Imepokewa na Ahmad na Abu Daud.].



Visima



Mvua



Mito



Bahari

## 2.Maji yaliyotumiwa:

Nayo ni maji yanayotiririka kutoka kwenye viungo vya mwenye kutawadha au mwenye kuoga. Hayo si makosa kuyatumia kujitwahirishia, kwa kuwa ilithubutu kutoka kwa Ibn Abbas t kuwa alisema kuwa mmoja katika wake wa Mtume (s.a.w) alioga kwenye chombo, na Mtume wa Mwenyezi Mungu U akataka kutawadha kutoka kwenye chombo hicho. Yule mkewe akasema: «Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi nilikuwa na janaba." Akasema: (Maji hayaathiriki na Janaba) [ Imepokewa na Tirmidhi.].

## 3. Maji Yaliyochanganyika na kitu Twahara:

Nayo ni maji yaliyochanganyika na kitu twahara kama majani ya mti au mchanga au kutu kwenye matanki ya maji na kisiache athari kwenye yale maji yenye kuyafanya yasiitwe maji ya kawaida. Kwa kauli ya mtume (s.a.w) kuwaambia wanawake waliosimama kumshughulikia binti yake aliyekuwa amekufa(nae ni bi ruqiya): (Mwosheni mara tatu au nne au zaidi ya hizo kama itahitajika, kwa maji na majani ya mkunazi, na mwishoni mwake kafuri) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim]



Maji yaliyochanganyika na mchanga



Kutu za matanki ya maji



Maji yaliyochanganyika na majani ya mti

## Kugeuka kwa Maji

Maji yakigeuka kwa kitu kilichoathiri na kuyatoa kwenye jina la maji na kuyapa jina lingine kama chai au maji ya tamu (juice) na visivyokuwa hivyo, basi haisihi kujitwahirisha nayo, kwa kuwa hayaitwi maji tena.



Mchuzi



Wino



maji ya tamu, (juice)



Chai


## 4. Maji yaliyochanganyika na najisi na isiyabadilishe:

Nayo ni yale ambayo yaliingia ndani yake najisi, kama mkojo au mfu na vinginevyo na isibadilishe sifa zake zozote.hukmu ya Maji haya ni yenye kutwahirisha, kwa kauli ya Mtume (s.a.w) juu ya kisima cha Budhaah (Hakika maji yanatwahirisha hakuna kitu cha kuyafanya najisi) [ Imepokewa na Ahmad na Tirmidhi].


Maana yake: Watu walikuwa wakitupa uchafu pambizoni mwa kisima, na mvua ilikuwa ikiusukuma kwenye kisima.Na maji yalikuwa, kwa kuwa ni mengi, hayaathiriwi na kuingiliwa na vitu hivyo na wala hayabadiliki.

## Pili: Maji Najisi

Nayo ni maji yaliyoingia ndani yake kitu chochote cha najisi kama mkojo na mfu, kikabadilisha mojawapo ya sifa tatu za hayo maji: harufu yake, tamu yake au rangi yake. Maji haya ni najisi kulingana na maoni ya wanavyuoni kwa umoja wao, na haifai kuyatumia.



Mfu usiobadilisha maji



Mfu aliebadilisha maji

Maelezo

1.Asili ya maji ni utwahara. Kukiwa na maji yasiyojulikana kama ni najisi au ni twahara, basi yatazingatiwa ni twahara kulingana na asili yake, na haifai kujilazimisha, na kujitia wasiwasi.
2.Inafaa kutawadhia maji ya Zamzam, kwa kuwa imethubutu kutoka kwa Mtume (s.a.w) aliitisha ndoo ya maji ya Zamzam akanywa kutoka kwenye hiyo ndoo na akatawadhia

# Hukumu za Najisi

## Maelezo ya Najisi

### Najisi kilugha

Uchafu

Najisi kisheria

Uchafu ambao Sheria imeamuru uondolewe

## Sampuli ya vitu Najisi

### 1. Mkojo wa binadamu na choo chake

Kwa Hadithi ya Mbedui aliyekojoa msikitini, Mtume (s.a.w) akamwambia (Hii misikiti haifai ikojolewe au ichafuliwe. Linalopasa ni kutajwa Mwenyezi Mungu, kuswaliwa na kusomwa Qur'ani) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim].

### 2. Damu ya Hedhi

Kwa ilivyothubutu kuwa Khaulah binti Yasaar alimjia Mtume (s.a.w) akasema: « Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi sina isipokuwa nguo moja, na ninaingia hedhini nikiwa nimeivaa. Mtume (s.a.w) akasema: (Ukitwahirika osha pale mahali pa damu kisha uswali ukiwa na hiyo nguo) [Imepokewa na Abu Daud] .

Na damu isiyokuwa ya hedhi ni twahara, iwe ni damu inayotiririka au isiyotiririka, kwa hadithi iliyothubutu kuwa mmoja wa washirikina alimfuma mmoja wa Waislamu kwa mshale naye yuwaswali ukampata, akaushopoa na akaendelea kwenye Swala yake na damu ikimtiririka.

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
Ghuslu - Nifaas Na Hedhi

### 3. Mkojo na choo cha wanyama wasio liwa

Kwa hadithi iliyosimuliwa na Ibn Mas›uud t kwamba Mtume (SAW) alienda chooni akaniamuru nimletee mawe matatu. Nikapata mawe mawili, nikatafuta la tatu nisipate, nikachukua choo kikavu cha mnyama nikamletea. Akachukua mawe mawili na kile choo akakitupa na akasema "Hiki ni najisi [ Riks: najisi.] " [ Imepokewa na Bukhari.].

Ni hukmu gani ya Mkojo na choo cha wanyama wanaoliwa ?

Mkojo wa mnyama anayeliwa na choo chake ni twahara, kwa kuwa ilithubutu kutoka kwa Anas bin Malik kwamba kuna watu walikuja Madina, na hewa yake isiwafae - yaani walishikwa na ugonjwa huko -. Mtume(s.a.w) akawapeleka kwenye ngamia wa Zaka wapate kunywa mikojo na maziwa ya hao ngamia [Imepokewa na Bukhari.].

### 4. Mfu

Naye ni aliyekufa mwenyewe bila kuchinjwa kisheria, kwa kuwa Mwenyezi Mungu U Aliyetukuka Alisema: {Sema: Sioni katika yale niliyo funuliwa mimi kitu kilicho haramishwa kwa mja kukila isipokuwa kiwe ni nyamafu au damu inayo mwagika au nyama ya nguruwe kwani hiyo ni uchafu} [6: 145].

Na kinaingia katika maana ya mfu kile kilichokatwa kutoka kwa mnyama aliye hai kabla hajachinjwa.

Na vinavyovuliwa katika mfu ni:

### 1. Mfu wa Samaki na Parare

Kwa neno lake Mtume (s.a.w): (Tumehalalishiwa mfu aina mbili, na damu aina mbili. Ama aina mbili za mfu, ni samaki na parare, na ama aina mbili za damu, ni ini na wengo) [Imepokewa na Ahmad]

### 2.Mfu asiye na Damu inayotiririka kama vile Nzi:

Kwa kuwa Mtume (s.a.w) alisema: (Anapoingia nzi kwenye chombo cha mmoja wenu, basi na amzamishe kisha amtoe na kumtupa, kwani kwenye mojawapo ya mabawa yake kuna ponyesho na katika lingine kuna ugonjwa) [ Imepokewa na Bukhari.].



Mfu



Samaki



Parare



Nzi

## 5. Nyama ya Nguruwe

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu U Aliyetukuka Amesema: {Sema: Sioni katika yale niliyo funuliwa mimi kitu kilicho haramishwa kwa mja kukila isipokuwa kiwe ni nyamafu au damu inayo mwagika au nyama ya nguruwe kwani hiyo ni uchmfu } [6: 145].



Nguruwe

## 6. Ute wa Mbwa

Mbwa ni najisi yeye mzima. Na unajisi wa ute wake umefanywa mzito, kwa kuwa Mtume (s.a.w) alisema: (Kutwahirika kwa chombo cha mmoja wenu iwapo mbwa amekiramba ni kukiosha mara saba, mara mojawapo kwa mchanga) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim].

Na kuramba ni atiapo mbwa ulimi wake ndani ya chombo na kuutikisa, anywe au asinywe.



Ute wa mbwa

## 7. Madhii

Nayo ni maji meupe mapesi yenye kunata, yanayotoka wakati wa kucheza na mke au kufikiria kuundama, si kwa matamanio ya nguvu wala hayatoki kwa kasi, na hayafuatiwi na hali ya kulegea,

na wakati mwingine mtu hahisi kamwe kuwa yametoka. Hii ni kwa kuwa Mtume (s.a.w) katika hadithi iliyopokelewa na Ali bin Abi Twalib t alipomuuliza mtume s.a.w kuhusu madhii, alisema: (Tawadha na uoshe dhakari yako) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim].

### 8. Wadii

Nayo ni maji meupe mazito yanayotoka baada ya kukojoa.

twahara wa Manii

Manii: ni maji meupe, mazito, yanayotoka kwa matamanio ya nguvu kwa kasi, na yanafuatiwa na ulegevu, na yana harufu inayofanana na yai lililoharibika.

Nayo ni twahara, kwani lau yangekuwa najisi Mtume (s.a.w) angeamrisha yaoshwe.

Na inatosheleza, katika kuondoa manii, kuyaosha yakiwa majimaji, na kuyakangura yakiwa makavu, kwa hadithi ya Aishah t kuwa alisema: (Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akiosha manii kisha akitoka kwenda kuswali kwa nguo hiyo na mimi nikiona athari yamuosho katika ile nguo) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na katika riwaya ya Muslim: (Nilikuwa nikiyakangura manii kwenye nguo ya Mtume (s.a.w) kisha akiswalia) [ Imepokewa na Muslim.].



Kuyaosha yakiwa majimaji



Kuyakangura yakiwa makavu

# Njia za Kutwahirisha Najisi

## 1. Kutwahirisha Ardhi Iliyonajisika

Ardhi ikinajisika, najisi hiyo huondolewa iwe ni kwa maji au kinginecho. Katika hadithi ya mbedui aliyekojoa msikitini, Mtume (s.a.w): (Muwacheni na mwageni kwenye mkojo wake ndoo ya maji) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na iwapo najisi ni majimaji ya kutiririka kisha ikakauka basi kwa hivyo huwa ishatwahirika kulingana na hadithi ya Abuu Qilaabah t kuwa alisema: “Ardhi ikikauka huwa imetwahirika” [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].



Najisi majimaji kinachomiminika ardhini



Kutwahirisha Ardhi Iliyonajisika



Kukauka kwa najisi majimaji

Pombe

Pombe ni twahara kinje ingawa kimaana ni najisi na kuwa kulinywa ni miongoni mwa dhambi kubwa, isipokuwa ya kwamba hakuna dalili kuwa ni najisi.

Ama neno lake Mwenyezi Mungu U {Enyi mlio amin!bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya shetani basi jiepusheni navyo } [5: 90]

Lililokusudiwa ni uchafu wa kimaana na sio uchafu wa kidhahiri, kama ilivyo kamari na masanamu. Hukumu inayochukuliwa hapa ni kuwa utumiaji wa mafuta mazuri yenye alkoholi unafaa, kwa kuwa alkoholi inatolewa kwenye pombe.




Pombe

## 2. Kuyatwahirisha Maji Yaliyonajisika

Yanatwahirika kwa kuongeza maji mengi ndani yake mapaka athari ya najisi iondoke. Pia yanatwahirika kwa kuyasafisha kwa njia za kiteknolojia za kisasa.




Kutwahirisha kwa vitu vya kisasa



Kutwahirisha kwa kuongeza maji

## 3.Kuitwahirisha Nguo Iliyonajisika

Huoshwa kwa maji, ikangurwe ikamuliwe mpaka Najisi Iondoke



Kutwahirisha nguo iliyonajisika

### 4.Kuyatwahirisha matandiko

Huoshwa kwa maji au kwa visafishaji vya kisasa, Na hukangurwa mpaka najisi iondoke.



Kutwahirisha matandiko

### 5. Kuitwahirisha Ngozi ya Mfu

### 1. Ngozi ya mfu wa mnyama anaeliwa

Hutwahirishwa kwa kuitia rangi kwa kauli yake Mtume (s.a.w): (Ngozi ikitiwa rangi huwa imetwahirika) [ Imepokewa na Muslim.].

Na dibaagh ni kutengeneza ngozi kwa baadhi ya madawa mpaka zilainike na uvundo wake uondoke. Ama mnyama anayeliwa awapo si mfu na akawa amechinjwa kwa njia ya kisheria, basi ngozi yake ni twahara

### 2. Ngozi ya Mfu wa Mnyama Asieliwa

Kwa Yule mnyama ambae haiwi halali kuchinjwa kwake ngozi yake haitotwahirika kwa kukaushwa hata kama katika uhai wake alikuwa twahara



Mnyama anayeliwa



Kupaka rangi ngozi



Mnyama asiyeliwa

### 6. Kutwahirisha mkojo wa mtoto wa kike na mkojo wa mtoto wa kiume ambaye hajala chakula

Mkojo wa mtoto wa kike huoshwa. Ama mkojo wa mtoto wa kiume, inatosha kunyunyiza maji juu yake, kwa kauli yake Mtume (s.a.w): (Mkojo wa mtoto wa kike huoshwa, na mkojo wa mtoto wa kiume hunyunyizwa maji) [Imepokewa na Abu Daud.]



Kunyunyiza Maji mkojo wa Mtoto wa Kiume



Kuuosha Mkojo wa Mtoto wa Kike

### 7. Kukitwahirisha kilichorambwa na Mbwa

Huoshwa mara saba, mara ya kwanza yake ni kwa mchanga, kwa kauli yake Mtume (s.a.w): (Utwahara wa chombo cha mmoja wenu iwapo mbwa amekiramba ni kukiosha mara saba, mara ya kwanza yake ni kwa mchanga) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim].




### 8. Kuyatwahirisha Madhii na Wadii

Ataosha dhakari yake na atatawadha, kwa kauli yake Mtume (s.a.w) katika hadithi ya Ali bin Abii Twalib: (Tawadha na uoshe dhakari yako) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Ama kuitwahirisha nguo, inatosha kunyunyiza maji mahali palipo na madhii au wadii, kwa hadithi ya Sahl bin Hanif kuwa yeye alimuuliza mtume (s.a.w): “Nilisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nguo yangu ikiiingiwa na chochote katika vitu hivyo itakuwaje?” Akasema: (Inakutosheleza utie maji kwenye kitanga cha mkono uyamimine nguoni mwako mpaka uone kwamba yameviondoa) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## 9. Kutwahirisha Damu ya Hedhi

Ni kuiosha kwa maji. Na haidhuru ikisalia athari yake, kwa kauli yake Mtume (s.a.w): (Yanakutosheleza maji, na athari yake haikudhuru) [Imepokewa na Abu Daud.]

## 10. Kuvitwahirisha Viatu

Husuguliwa chini mpaka iondoke athari ya najisi, kwa kauli yake Mtume (s.a.w): (Mmoja wenu anapokanyaga uchafu kwa kiatu chake, basi mchanga unakitwahirisha) [ Imepokewa na Abu Daud.].



Kutwahirisha viatu kwa kuvisugua kwenye Ardhi

## 11. Kuitwahirisha Nguo ndefu ya Mwanamke

Najisi ikipakana na ukingo wa nguo ya mwanamke, basi inamtosheleza yeye atembee mahali twahara na ardhi itaitwahirisha, kwa kauli yake Mtume (s.a.w) (Kitaitwahirisha kilicho baada yake) [ Imepokewa na Abu Daud.].



Kuitwahirisha Ardhi nguo ya mwanamke

## 12. Kuvitwahirisha Vyakula Vikavu

Vinatwahirika kwa kuiondoa najisi na zile sehemu zilizo pambizoni mwa hivyo vyakula, na kinachosalia kitakuwa twahara, kwa ilivyothubutu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) aliulizwa kuhusu panya aliyeingia ndani ya samli, akasema: (Vitupeni! Na vile vilivyo pambizoni mwakeviondoeni namule samli yenu). [ Imepokewa na Bukhari.]



Samli iliyoingia Panya Aliyekufa

## 13- Kutwahirisha Vitu Vigumu kama Viyoo na Gilasi

Itapanguswa mpaka athari ya najisi iondoke.`



Kutwahirisha Ukoa kwa Kuupangusa

Maelezo kuhusu Najisi

1- Asili ya vitu ni twahara isipokuwa vile ambavyo kuna dalili ya unajisi wake.
2- Najisi ikiingia kwenye kitu na isijulikane ilipo, basi chote kitaoshwa.
3- Najisi ikigeuka ikawa kitu kingine, kama vile kikichomwa choo cha punda kikawa jivu, basi itakuwa twahara.



Kugeuka choo kuwa jivu kunakukifanya kitwahirike

# Makombo

## Maelezo ya Makombo

### Makombo

Nayo ni yanayosalia chomboni baada ya kunywewa.
Asili makombo ni utwahara isipokuwa yale ambayo kuna dalili ya kuwa ni najisi, kama yanayofuata:

## 1. Makombo ambayo ni twahara

### a. Makombo ya mwanadamu:

Kwa hadithi iliyoyhibiti kwamba Mtume (s.a.w) alikuwa akinywa makombo ya Aishah na hali Aishah yuko katika hedhi, na akiweka kinywa chake mahali Aishah alipoweka kinywa chake [Imepokewa na Muslim.].



## b. Makombo ya paka

Kwa kauli yake Mtume (s.a.w) kuhusu paka aliyekunywa kutoka kwenye chombo: (Yeye si najisi, yeye ni miongoni mwa Wanaowazunguka na kuwa nanyi, wa kiume na wa kike) [ Imepokewa na Tirmidh.].




Makombo ya paka

## c. Makombo ya mnyama anayeliwa, mbagaa, punda, wanyama wakali na ndege wakali na mfano wa hao:

Ni utwahara, kwa kuwa asili ya vitu ni utwahara, na hakuna dalili ya kuwa ni najisi, na kwa kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akipanda punda na walikuwa wanapandwa wakati wake.




Makombo ya wanyama wambuaji



Makombo ya ndege wambuaji



Makombo ya mnyama aliwaye



Makombo ya punda

## 2. Makombo yaliyo najisi

### a. Makombo ya mbwa

Kwa kauli yake Mtume (s.a.w) Kutwahirisha kwa chombo cha mmoja wenu, kikirambwa na mbwa, ni akioshe mara saba, ya kwanza yake iwe kwa mchanga [Imepokewa na Bukhari na Muslim].

### b. Makombo ya nguruwe

Makombo ya nguruwe ni najisi kwa neno lake mwenyezi mugnu au nyama ya nguruwe kwani hiyo ni uchmfu} [6: 145]. Yaani najisi, nachochoe kinacho tokama na nguruwe ni najisi



Makombo ya nguruwe



Makombo ya mbwa

twahara wa mwanadamu

Mwanadamu ni utwahara, sawa awe ni muislamu, kwa neno lake mtume (s.a.w) {Hakika mu'min hanijisiki} [ Imepokewa na Bukhari na Muslim]

ao kafiri, kwa ilivo thubutu kuwa Mtume (s.a.w) alitawadha kwa chombo cha mushrik, ama neno lake mwenyezi Mungu { Hakika mushrikina ni najisi} [9: 28]

makusudio ni najisi ya

# Vyombo

## Maelezo kuhusu Vyombo

Vyombo
Vyombo vya kuhifadhia maji na vinginevyo

## Kutumia vyombo vya dhahabu na fedha

### 1. katika kula na kunywa

Ni haramu kuvitumia kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Msinywe kwenye vyombo vya dhahabu na fedha, na msile kwenye sahani zake. Kwani hivyo ni vyao wao ulimwenguni na ni vyetu kesho Akhera) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.]
Na kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Yule anayekunywa kwenye chombo cha fedha, kwa hakika anaingiza tumboni mwake moto wa Jahanamu) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

### 2. Kutumia vyombo vya dhahabu na fedha kwa matumizi yasiyokuwa ya kula na kunywa

Inafaa kuvitumia kwa matumizi mengine yasiyokuwa kula na kunywa, kama kutawadhia na mengineo kwa hadithi ilio tangulia kuwa imekaza kuvitumia kwa ajili ya kula na kunywa, na imethubu kwa hadithi ya Ummu Salamah t alikuwa na chombo (juljul) la fedha ambayo ndani yake kulikuwa na baadhi ya nywele za mtume ﷺ.



Kula kenye chombo cha dhahabu



Kula kwenye chombo cha fedha

## Kutumia vyombo vilivyolihimiwa kwafedha

Inafaa kutumia vyombo vilivyolihimiwa kwa fedha kidogo kuwapo na haja, kwa kuwa imethubutu kwamba kopo la Mtume ﷺ lilivunjika akapafunga pale palipopasuka kwa silsila ya fedha. [Imepokewa na Bukhari].



Birika ya fedha kwa ajili ya kutawadhia



Kutumia chombo kilcholihimiwa kwa fedha

Uvaaji dhahabu kwa wanaume

Haifai kwa mwanamume kuvaa dhahabu, kwa hadithi iliyothubutu kutoka kwa Abu Musa al-Ash›ari kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: (Limeharimishwa vazi la hariri na dhahabu kwa wanaume wa umma wangu na limehalalishwa kwa wanawake wao) [Imepokewa na Tirmidhi].

# Hukumu za kwenda haja

## Yanayopasa wakati wa kwenda haja

1.Kufunika uchi usionekane na watu wakati wa kwenda haja, kwa neno lake Mtume ﷺ: (Kuweka kizuizi baina ya macho ya majini na uchi wa binadamu angiapo chooni mmoja wenu ni aseme "Bismillah") [Imepokewa na Tirmidh.].

2.Kujiepusha asiingiwe na najisi nguoni mwake au mwilini mwake, na akiingiwa na najisi yoyote aioshe. Kwa hadithi iliyothubutu kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alipita kwenye kaburi mbili na akasema: (Hawa wawili wanaadhibiwa.

Na hawaadhibiwi kwa jambo kubwa. Ama huyu hakuwa akijihifadhi na mkojo) [Imepokewa na Abu Daud].

3.Kujiosha kwa maji au kujipangusa kwa mawe, kwa hadithi ya Anas bin Malik t kuwa alisema: (Mtume ﷺ alikuwa akiingia chooni, na mimi nikimbebea, pamoja na mtoto kama mimi, chombo cha maji na bakora, akachukua maji akajisafishia nayo) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Yanayoharamishwa wakati wa kwenda haja

1.Kuelekea kibla au kukipa mgongo wakati wa kwenda haja jangwani. Ama kwenye majengo, lililo bora zaidi ni kuacha kujilazimisha na hilo, kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Mkienda haja kubwa msielekee kibula, na msikipe mgongo kwa kukojoa wala kwa haja kubwa, lakini elekeeni mashariki au magharibi) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

2.Kuingia haja kwenye njia ya watu kupita au kwenye kiuvuli na sehemu za wao kukaa. Mtume ﷺ amesema: (Ogopeni vitu viwili vinavyosababisha mtu kulaniwa. Wakasema: ni vitu gani hivyo ewe mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: “Ni(kitendo cha) yule anayeingia haja kwenye njia ya watu kupita au kwenye kivuli cha watu kukaa) [Imepokewa na Muslim.].

3.Kuingia na Msahafu chooni, kwa kuwa kitendo hiko kinaonesha dharau kwa Kitabu cha Mwenyezi Mungu Aliyetukuka.



Kuingia chooni kwenye njia inayopitwa na watu




Kukidhi haja jangwani

Kukujoa kwenye maji yaliyotulia

Imethubutu kwamba kukojoa kwenye maji yaliyotulia kunapelekea kupatikana ugonjwa wa Bilharzia ambayo yanatokea yakisababishwa na aina ya vijidudu vinvyopasua mwili na kutoa damu kwenye kibofu cha mkojo,

## Yanaopendekezwa wakati wa kwenda haja

1.Kujiepusha na watu wakati wa kwenda haja jangwani

2.Aseme angiapo chooni: “Kwa jina la Mwenyezi Mungu. Ewe Mwenyezi Mungu! Mimi najilinda kwako kutokana na Mashetani wa kiume na wa kike” [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

3.Kutanguliza mguu wa kushoto angiapo chooni na mguu wa kulia atokapo.

4.Aseme anapotoka “Naomba msamaha wako” [Imepokewa na Abu Daud.].



kuingia kwa mguu wa kulia



kuingia kwa mguu wa kushoto

## Yanao chukiza kufanya wakati wa kwenda haja

1.Kusema wakati wa kwenda haja (chooni) au kuzungumza na watu isipokuwa kwa haja (dharura), kwa hadithi ya Ibn Umar kwamba (mtu mmoja alipita kwa Mtume ﷺ naye yuwakojoa, akamsalimia Mtume, asimrudishie salamu) [Imepokewa na Muslim.].

2.Kuingia chooni na kitu chochote chenye utajo wa Mwenyezi Mungu, U isipokuwa akichelea kuwa kitaibwa na mfano wake, kwa kuwa Mtume ﷺ alikuwa akiingia chooni akiiweka pete yake.

3.Kushika tupu kwa mkono wa kulia au kutamba au kupangusa kwa mawe kutumia huo mkono, kwa kauli ya Mtume ﷺ:
(Asishike mmoja wenu dhakari (tupu ya mbele) yake kwa mkono wa kulia wake akiwa yuwakojoa wala asijipanguse kwa mkono wake wa kulia baada ya kwenda haja)
[ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

4.Kukojoa kwenye mpasuko na pango ili asidhuriwe na wadudu wanaotembea au adhuriwe na wao.



Kuzungumza wakati wa kukidhi haja



Kuingia chooni pamoja na kitu chenye utajo wa Mwenyezi Mungu



Kukojoa kwenye tundu



Kuingia na mswahafu kwenye choo cha kuoga.

Kukojoa kwa kusimama

Mtume ﷺ alikataza kukojoa kwa kusimama. Lakini akijiaminisha kuwa tatuko za mkojo hazitamfikia inafaa afanye hivyo, kwa hadithi ya Hudhaifah kuwa Mtume ﷺ alikwenda kwenye taka za watu akakojoa kwa kusimama” [Imepokewa na Bukhari.].

## Kutamba kwa maji na kwa mawe

Kutamba ( KUSTANJI )

Kuondoa athari ya chenye kutoka kwenye tupu ya mbele na ya nyuma kwa maji yenye kutwahirisha.

### Kutamba kwa mawe

Kuondoa athari ya chenye kutoka kwenye tupu ya mbele au ya nyuma kwa mawe na mfano wake

## Hukumu ya kutamba kwa maji na kwa mawe

Kutamba kumewekwa na sheria kwa hadithi ya Anas bin Malik t kwamba yeye alisema: (Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akiingia chooni, na mimi nikibeba, na mvulana mwingine pamoja na mimi, chombo cha maji na bakora, akajisafisha na maji) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na inafaa kutamba kwa mawe peke yake kwa masharti mawili:

1.Mkojo au choo visipite zaidi ya mahali vinapotoka, vikipita basi itabidii atumie maji.

2.Kutamba kwa mawe kuwe ni kwa kufuta mafuto matatu mpaka kusafishika kwa tupu ya mbele au ya nyuma na iondoke athari ya najisi.

## Hekima ya kutamba kwa maji na kwa mawe

1.Kujitwahirisha na kuondoa najisi.

2.Kuwa msafi na kujiepusha na visababisho vya magonjwa

### Faida

Haihitajii kutamba kwa kutokwa na upepo.

Kutamba kwa maji ni bora kuliko kufuta kwa mawe, kwa kuwa huko kunatakasa zaidi na kutwahirisha zaidi

## Masharti ya kitu kifutio (jiwe au mfanowake)

1.Kiwe twahara. Kwani haifai kwa kitu najisi.

2.Kiwe chafaa kutumiwa, kwani haifai kwa kitu kilicho haramu.

3.Kiwe ni chenye kusafisha mahali pa najisi.

4.Kisiwe ni mfupa au choo.imepokewa na Salman al- Farisi t asema: (Alitukataza Mtume ﷺ kuelekea upande wa kibla kwa kwenda haja kubwa au ndogo, kutamba kwa mkono wa kulia, au

kutamba kwa mawe yasofikia matatu na kutamba kwa choo au mfupa).
5.Kisiwe ni kitu kinachoheshimiwa kama chakula au karatasi iliyoandikwa vitu vinavyohishimiwa.



Kutamba kwa mfupa



Kutamba kwa kitambaa



Kutamba kwa chakula



Kutamba kwa hanchifu



Kutamba kwa karatasi inayoheshimika



Kutamba kwa mawe

Kutamba kwa mkono wa kulia

Haifai kutamba kwa mkono wa kulia kwa kauli ya Mtume ﷺ aliyesema: (Na asishike mmoja wenu dhakari yake (tupu ya mbele) kwa mkono wake wa kulia na asijifute choo kwa mkono wake wa kulia) [ Imepokewa na Muslim.].

## Sunna za kimaumbile

## Kuzieleza sunna za kimaumbile

Sunna za maumbile

Mambo mazuri ambayo Mwenyezi Mungu aliwaumbia watu nayo, ni ambayo yanamfanya mtu akamilike mpaka afikie daraja ya sifa bora na pambo zuri.

Imepokewa kutoka kwa Aishah t kuwa alisema kwamba Mtume ﷺ alisema: (Mambo matano ni katika sifa za kimaumbile: kupunguza masharubu, kufuga ndevu, kupiga mswaki, kupuliza maji, kukata kucha, kusafisha makunjo viungoni, kusumua nywele za makapwa kunyoa nywele sehemu za siri, na kutamba kwa maji na kusukutua) [Imepokewa na Muslim.].

## 1.Kupiga mswaki

Mswaki

Ni kipande cha mti wa mpilipili – au mfano wake- kinachotumiwa kusafisha meno na chakula kilichogandamana na kuondosha harufu mbaya

Na Kupiga mswaki kumesuniwa nyakati zote, kwa kauli ya Mtume ﷺ: (Kupiga mswaki kunatwahirisha kinywa, kunamridhisha Mola) [Imepokewa na Ahmad].

Lakini imetiliwa mkazo kupiga mswaki katika sehemu zifuatazo: -

1. wakati wa kutawadha

Kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Lau si kwa kuwaonea uzito umma wangu ningaliwaamrisha kupiga mswaki kila wanapotawadha) [Imepokewa na Ahmad].

2. Wakati wa kuswali

Kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Lau si kwa kuwaonea uzito umma wangu ningaliwaamrisha kupiga mswaki kila wanapotaka kuswali) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

### 3. Wakati wa kuingia nyumbani

Imepokewa kwa al- Miqdad kumpokea babake t alisema: (Nilimuuliza Aishah t kuhusu kitu ambacho Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akikianzia akiingia nyumbani kwake. Akasema "Mswaki" [Imepokewa na Muslim.].

### 4. Wakati wa kuamka kutoka usingizini

Amepokewa Hudhaifah (RA) akisema: Mtume ﷺ alikuwa akiinuka usiku akisafisha kinywa chake kw a mswaki) [Imepokewa na Bukhari.].

### 5. Wakati wa kusoma Qur›ani:

Alipokewa Ali t akiamuru mswaki na akasema kwamba Mtume ﷺ alisema: (Hakika mja akipiga mswaki, kisha akasimama kuswali, Malika husimama nyuma yake akisikiliza kisomo chake, na humkaribia- au neno mfano wa hilo- mpaka kuweka kinywa chake juu ya kinywa yule, ikawa hakuna chochote cha qur'ani kitokacho kwake isipokuwa huingia kwa yule Malaika, basi twaharisheni vinywa vyenu kwa ajili ya qur'ani) [ Imepokewa na Bazzar].



Faida za mswaki

Miongoni mwa faida za mswaki ni kuwa unasafisha kinywa duniani, na unamridhi Mwenyezi Mungu akhera. Nao unatia nguvu meno,

unayashikanisha masinye, unatakasa sauti na unamchangamsha mja.

## 2.Kusukutua na kupuliza maji puani

### Kusukutua

Kutia maji kinyawani na kuyatikisa.

### Kupaliza puani

Kuyavuta maji puani kwa pumzi



Kusukutua



Kupaliza puani

## 3. Kutamba

### Kutamba

Kuondoa athari ya kilichotoka kwenye tupu ya mbele au ya nyuma kwa maji yenye kutwahirisha.

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:


Ghuslu - MAANA YA KUSTANJI NA HUKMU YAKE

## 4. Kupunguza masharubu na kuyafanya madogo

Makusudio ni kuyapunguza sana, kwa kufanya hivyo kunapatikana uzuri na usafi na kuenda kinyume na makafiri.

## 5. Kufuga ndevu

Nako ni kuziacha na kutozigusa




### Kunyoa ndevu

Ni haramu kunyoa ndevu, kwa amri iliyokuja ya kuzifuga na kuziacha.

Mtume ﷺ amesema: (Kateni masharubu na fugeni ndevu, wakhalifuni Majusi) [Imepokewa na Muslim.].

## 6.Kunyoa nywele sehemu za siri

### Kunyoa nywele sehemu za siri (istihdad)

Kunyoa nywele zinazomea kandoni mwa tupu

### Faida ya kunyoa nywele sehemu za siri

Imethubutu kielimu kwamba kunyoa sehemu hizo kunatunza afya ya mwili, nguvu zake na usalama wake, kwa kuwa kule kuwa na nywele nyingi sehemu hii kunasababisha vijipu kwenye ngozi ambazo hudhuru mwili.

## 7. Kutahiri na kupasha tohara

### Kumtahiri mwanamume

Ni kuondoa kigozi kinachofunika kichwa cha dhakari kwa mwanamume.

### Kumpasha tohara mwanamke

Ni kukata kinyama kilichozidi kilichoko juu ya sehemu ya kuingiza dhakari ya mwanamume.

Kutahiri ni kwa mwanamume, na kupasha tohara ni kwa mwanamke kwa kuwa mtume ﷺ alimwambia Ummu Atiyyah:

(Kata kidogo wala usifeke, kwani kufanya hivyo kunakufanya hapo mahali pawe na maangalizi mazuri na kunamfurahisha mume ) [ Imepokewa na Hakim].

Na kutahiri ni lazima kwa wanaume, ni sunna kwa wanawake.

Na hekima ya mwanamume kutahiriwa ni kuitwahirisha dhakari na najisi iliyopo kwenye kigozi kinachofunika kichwa cha dhakari. Ama kwa mwanamke ni kule kung’ara kwa uso wake

## 8. Kukata kucha

Nako ni kuzikata ili zisiwe ndefu



Kukata kucha

## 9. Kusumua nywele za makapwa

Yaani Kuondoa nywele zinazoota makapwani, kwa kuwa kuziondoa ni katika usafi na kuondoa harufu mbaya zinazokusanyika kwa kuwako nywele hizi.



Kusumua nywele za makapwa

## 10. Kuosha makunjo kwenye viungo

Makunjo viungoni

Viungo vya vidole

Baadhi ya wanavyuoni wameyaweka pamoja hayo makunjo na uchafu unaokusanyika masikioni na shingoni na baadhi ya sehemu za mwili.



Makunjo viungoni

Siku arubaini

Ni karaha kwa mtu kuacha kucha, pia nywele za makapwa, nywele sehemu za siri na masharubu zaidi ya siku arubaini. Imepokewa na Anas bin Malik t akisema: (Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alituwekea wakati wa kupunguza masharubu, kukata kucha, kunyoa nywele sehemu za siri na kusumua nywele za makapwa kuwa visiachwe zaidi ya siku arubaini) [Imepokewa na Muslim.].

# Kutawadha

## Maana ya Kutawadha

### Udhu katika lugha

Uzuri na usafi

### Udhu katika Sheria

Kutumia maji kwenye viungo maalumu kwa nia ya kujitwahirisha

## Hukumu ya kutawadha

Kutawadha: ima ni lazima na ima inapendekezwa:

### a. Ni lazima kutawadha kwa mambo matatu

### 1. Kuswali

Mwenyezi Mungu U Anasema: {Enyi Mlioamini! Mnapo simama kwa ajili ya swala basi osheni nyuso zenu, na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu, na osheni miguu yenu mpaka vifundoni} [5: 6]

### 2. Kutufu Alkaba:

Kwa kauli yake Mtume ﷺ kumwambia mwanamke aliye katika hedhi: (Usitufu mpaka utwahirike) [ Imepokewa na Bukhari.].

### 3. Kushika Msahafu:

Kwa neno lake Mwenyezi Mungu U: {Hawaigusi isipokuwa wale waliotwahiriwa} [56: 79]



Kutawadha kwa ajili ya kuswali



Kutawadha kwa ajili ya kutufu



Kutawadha kwa ajili ya kushika Msahafu


## b. Kutawadha kunasuniwa katika mambo mengine yasiyokuwa hayo

Kwa neno lake Mtume ﷺ aliposema: (Hajilazimishi na udhu isipokuwa mwenye Imani) [ Imepokewa na Ahmad].

Na kunapendekezwa zaidi kutawadha wakati wa kujadidisha udhu kwa kila Swala, kutawadha kwa kumtaja Mwenyezi Mungu na kuomba, wakati wa kusoma Qur'ani, kabla ya kulala, kabla ya kuoga, na kutokana na kumbeba maiti na baada ya kila tukio la kutangua udhu, hata kama hataki kuswali.


Kutawadha kwa ajili ya kumtaja Mwenyezi Mungu


Kutawadha wakati wa kulala


Kutawadha wakati wa kusoma Qur›ani


Kutawadha kwa ajili ya kubeba maiti

## Fadhila za kutawadha

1. Ni sababu ya kupendwa na Mwenyezi Mungu

Mwenyezi Mungu aliyetukuka Anasema:{Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wenye kutubia na anawapenda wenye kujitwahirisha} [2: 222].

2. Ni alama ya umma wa Mtume Muhammad ﷺ kwa kuwa watakuja Siku ya Kiyama wakiwa weupe wa nyuso na viungo vya kutawadha

Amesema Mtume ﷺ (Hakika ya umma wangu watakuja Siku ya Kiyama wakiwa weupe nyuso na viungo kutokana na athari ya kutawadha, basi yoyote miongoni mwenu anayeweza kurefusha weupe wake na afanye) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

3. Kunafuta dhambi na makosa

Amesema Mtume ﷺ alisema (Mwenye kutawadha akautengeza udhu wake, basi dhambi zake hutoka mwilini mwake mpaka hutoka chini ya kucha zake) [Imepokewa na Muslim.].

4.Huinua daraja

Amesema Mtume ﷺ (Je, siwaonyeshi nyinyi kile ambacho kwacho Mwenyezi Mungu hufuta dhambi na huinua daraja? Wakasema “Ndio, tuonyeshe” akasema: “Ni kueneza maji ya udhu kwenye viungo, na kukithirisha hatua za kwenga misikitini na kungojea Swala baada ya Swala. Hiyo ndiyo jihadi) [Imepokewa na Muslim.].

## Namna ya kutawadha

1.Kuhudhurisha nia moyoni.
2.Kutaja jina la Mwenyezi Mungu kwa kusema “bismillah”
3.Kuosha vitanga viwili vya mikono (mara tatu)
4.Kupiga mswaki: na mahali pake ni wakati kusukutua.
5.Kusukutua na kupaliza maji puani na kuyatoa.(mara tatu)
Madhmadhah: kutia maji kinywani na kuyageuza.

Istinshaaq: kuvuta maji puani kwa pumzi.
Kusukutua na kupaliza puani huwa kwa teko moja.
Istinthaar: ni kuyatoa maji puani.
6.Kuosha uso (mara tatu) pamoja na kupitisha maji ndani ya ndevu.
Na mpaka wa uso kiurefu ni kuanzia mameleo ya nywele za kichwa mpaka chini ya kidevu, na kiupana ni kuanzia sikio mpaka sikio.
7.Kuosha mkono wa kulia kuanzia ncha za vidole mpaka kifundoni (mara tatu), kisha mkono wa kushoto kama hivyo.
8.Kupangusa kichwa kwa kuupasha maji mkono kisha kupukusa mwanzo wa kichwa mpaka kwenye kishogo chake kisha kuurudisha mwanzo wake mara nyingine (mara moja).
9.kupangusa katikati mwasikio kwa kidole cha shahada, na inje yake kwa kidole cha gumba (mara moja)
10.Kuosha mguu wa kulia hadi kwenye vifundo (mara tatu) kisha mguu wa kushoto hivyohivyo.
11.Dua baada ya kumaliza kutawadha kwa kusema:
“ Nashuhudia kuwa hakuna mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika. Na nashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na mjumbe wake” “Ewe Mola! Nijaalie mimi ni kati ya wenye kutubia, na unijaalie mimi ni kati ya wenye kujitwahirisha” “Kutakasika ni kwako, ewe Mola! na shukrani ni zako. Nashuhudia kuwa hakuna Mola isipokuwa Wewe. na kuomba msamaha na natubia kwako” [Imepokewa na Nasai.].




Kuosha vitanga viwili vya mkono.(mara tatu)




Kusukutua (mara tatu)




Istinshaaq: (mara tatu)




Istinthaar: (mara tatu)




Kuosha uso (mara tatu)




Kutoa mwanya kwenye ndevu




Kuosha mikono kuanzia ncha za vidole mpaka vifundoni (mara tatu, )




Kupangusa kichwa




Kupangusa masikio mawili (mara moja)




Kuosha miguu hadi kwenye vifundo (mara tatu)

## Masharti ya kutawadha

1.Maji yawe twahara.
2.Maji yawe yafaa kutumiwa, yasiwe ya kuiba, kwa mfano.
3.Kuondoa chochote chenye kuzuia maji kufika kwenye ugozi, kama vile mafuta ya mshumaa na mfano wake.
4.Kutoeneza maji katika kutawadha,



Kuondosha rangi

## Faradhi za udhu

1.Kutia nia. Na mahali pake ni moyoni, wala haitamkwi. Na lau mtu afanya matendo ya kutawadha kwa lengo la kujiburudisha au kujinadhifisha, bila ya nia ya kutawadha, basi hilo halimtoshelezi.
2.Kuosha uso. Na miongoni mwa huko ni kusukutua na kupaliza puani.
3.Kuosha mikono miwili pamoja na vifundo viwili.
4.Kupangusa kichwa chote, pamoja na masikio mawili
5.Kuosha miguu miwili pamoja na vifundo viwili.

6.Kufuatanisha beina ya viungo

## Sunna za udhu

1.Kuosha vitanga viwili vya mikono mara tatu mwanzo wa kutawadha.
2.Kupiga mswaki.
3.Kuosha viungo mara tatu tatu, isipokuwa kichwa na masikio mawili, kwani hivyo havioshwi isipokuwa mara moja.
4.Kuanzia kuliani: nako ni kuanza upande wa kulia katika kuosha viungo vya udhu.
5.Kurefusha vingaja: yaani kupitisha zaidi ya vifundo vya mikono katika kuosha.
6.Kutoa mwanya kwenye ndevu ili kufikisha maji kwenye ngozi ya uso.
6.Kufikisha maji baina ya vidole vya mikono na miguu.
8.Kusugua viungo kwa mkono, na haitoshi kunyunyiza maji.
9.Kutumia maji kwa kiasi, kwa kuwa mtume ﷺ: amesema (Kutakuwa na watu katika umma huu watakaopitisha kiasi katika kujitwahirisha) [Imepokewa na Abu Daud.] Yaani watatumia maji ya kutawadhia kwa kupita kiasi
10.Dua baada ya kutawadha. Mtume ﷺ alisema: (Hakuna yoyote miongoni mwenu atakayetawadha, akaeneza maji ya kutawadhia kwenye viungo, kisha akasema "Nakiri kwa moyo kibaini kwa ulimi kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa mungu moja na Muhammad ni mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Ewe Mola! Nijaalie niwe miongoni mwa wenye kutubia na unijaalie ni miongoni mwa wenye kujitwahirisha" isipokuwa atafunguliwa milango ya pepo minane, auingie autakao) [Imepokewa na Tirmidhi.].
11.Kuswali rakaa mbili baada ya kutawadha. Mtume ﷺ alisema: (Mwenye kutawadha kama hivi ninavyotawadha, kisha akainuka akaswali rakaa mbili bila kusema na nafsi yake,

atasamehewa dhambi zake zilizotangulia) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].


Kupiga mswaki



Kurefusha viungo vya kutawadha


Kufikisha maji baina ya vidole

## Vitanguaji udhu

1. Kila chenye kutoka kwenye mojawapo ya njia mbili, mfano wa mkojo, choo, upepo (kushuta) kwa kauli yake Mtume ﷺ

(Mwenyezi Mungu hakubali Swala ya mmoja wenu akitokwa na hadathi mpaka atawadhe) [Imepokewa na Muslim.].

2. kulala usingizi mzito ambao mtu hafahamu chochote. Na hi inaingia hapa, kama kukosa fahamu, na kupotezwa fahamu kikamilifu.

3. Kula nyama ya ngamia, kwa hadithi ya Jabir bin samurah kwamba mtu alimuuliza Mtume ﷺ: (Je, tutawadhe kwa kula nyama za ngamia? Akasema: (Ndio) [Imepokewa na Muslim.]

4. kugusa tupu kwa mkono bila ya kizuizi, kwa hadithi iliyo pokelewa na busra binti swafawan (RA) kuwa alimsikia mtume ﷺ akisema (mwenye kugusa tupu yake na atawadhe) [ Imepokewa na Abu Daud.]



Kula nyama ya ngamia



Usingizi mzito

## Maelezo

1. Muislamu akiinuka kutoka usingizini na akataka kutawadha kwenye chombo, basi asichote humo kwa mikono yake mpaka aioshe mara tatu, kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Akiamka mmoja wenu kutoka kwenye usingizi, basi na asiuvike mkono wake

chomboni mpaka auoshe mara tatu, kwani hujui mkono wake ulilala wapi) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

2. Inapasa mtu awe na pupa la kuyafikisha maji kwenye kila kiungo kinacholazimu kuoshwa, hasahasa kwenye sehemu za baina ya vidole vya mikono na miguu, na baina ya ndevu na mashikio, pia visukusuku, vifundo na visiginyo kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Ole wa motoni kwa visiginyo) [Imepokewa na Muslim.].

3. Asili ni kujengea yakini. Lau mtu alikuwa na yakini kuwa alitawadha kisha akafanya shaka kuwa udhu wake umetanguka, basi atajengea yakini yake nayo ni kuwa ana udhu. Na lau alikuwa na yakini kuwa hana udhu, kisha akafanya shaka: ametawadha au la? Basi yakini ni kuwa yeye hakuwa naudhu.

4. Muislamu anapotawadha, akaosha viungo vinavotakikana kuoshwa kwa mwenye kutawadha, mara mojamoja au mara mbilimbili, au vingine mara moja na vingine mara mbili au mara tatu, udhu wake ni sahihi.

5. Mtu akiswali bila ya udhu kwa kusahau, itamlazimu kurudia Swala anapokumbuka.

6. Mtu akitawadha kisha akaingiwa na njisi, basi ataiondoa najisi wala harudii kutawadha, kwa kuwa kuingiwa na najisi hakutangui udhu.



Kutia mkono chomboni baada ya kuinuka kutoka usingizini



Baina ya ndevu na masikio



Kisiginyo



Kufikisha maji kwenye vidole vya miguu

Udhu na afya kwa jumla

Kwenye makala yaliyotolewa kwenye jarida la Source Linalotolewa na Umoja wa Mtaifa kuna maneno haya “Hakika kule kuoga kimpango na kutawadha kwa ajili ya kuswali katika jamii za Kiislamu kumesaidia sana kupunguza ueneaji ugonjwa wa trakoma ambao unaonekana kuwa ni sababu msingi ya upofu katika nchi za ulimwengu wa tatu..Na kuna watu wanaokaribia milioni mia tano wenye ugonjwa huu katika sehemu mbalimbali za ulimwengu ambao inawezekanakwao kujiepusha na upofu lau

wafuata njia ya Uislamu katika usafi unaompasa kila Muislamu kabla ya kuswali. Na imetazamwa na kuonekana kwamba kwenye jamii za Kiislamu zenye kushikamana na Dini kupungua kiwango cha kupatikana na ugonjwa huu, bali imefikia daraja ya kukosekana” [ Utabibu wa kimtume ukiangaziwa na elimu ya kisasa (Ghiyath al-Ahmad).].

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
Ghuslu - Wudhuu Unatenguka Akimgusa Mkewe?

## Makatazo

1. Kuleta nia kwa sauti wakati wa kutawadha.
2. Kutumia maji kwa kupita kiasi.
3. Kuzidisha maosho matatu katika kutawadha, kwa riwaya iliyopokewa kuwa mbedui alikuja kwa Mtume ﷺ kumuuliza juu ya kutawadha, akamuonesha udhu mara tatutatu kisha akasema: (Kutawadha ni namna hii. Na mwenye kuzidisha hapo amekosea, amepita mpaka na amedhulumu) [Imepokewa na Abu Daud.].

Lakini inafaa kuongeza zaidi ya maosho matatu iwapo atakuwa hakukisafisha kiungo kwa maosho matatu, kama mtu aliyeingiwa na mafuta au kitu kingine mkononi.

4. Kutoeneza maji katika kutawadha, kwa riwaya iliyopokewa kuwa mtu alitawadha, akaacha paku kadiri ya ukucha kwenye nyayo, Mtume ﷺ akaliona na aksema: (Rudi utawadhe kwa uzuri)[ Imepokewa na Muslim.] akarudi kisha akaswali.

Na inaingia kwenye kukosa kueneza maji ya udhu:

a- kutoosha vifundo viwili vya miguu
b- kutoosha visukusuku kwa sababu ya wembamba wa mikono ya kanzu.
c- kutoosha weupe ulioko baina ya masikio na ndevu.
d- Kutoosha kitanga cha mkono wa kushoto pamoja na mkono wa kushoto.
e- mwenye kutawadha naye una mapaku ya mafuta.

f- kutawadha kwa mwanamke na juu ya vidole vyake pana pambo lenye kuzuia maji kufika kwenye ngozi.
g- kutofikisha maji kwenye vidole vya miguu iwapo maji hayapiti baina ya vdole.
5. Kupangusa shingo:
Si miongoni mwa matendo ya kutawadha,
6. kuleta dhikiri ambazo hazikuja katika Sheria, mfano:
a- kuomba dua maalumu katika kuosha kila kiungo.
b- kumwambia “zamzam” mwenye kutawadha.



Utumizi wa maji wa kupita kiasi

# Kupukusa khofu mbili, soksi mbili, utata, bendegi na mfano wa hivyo

## Kwanza: kupukusa khofu mbili na soksi mbili

### Maana ya Khofu na Soksi

Khofu

Ngozi inayovaliwa miguuni

Soksi

Kinachovaliwa miguuni cha pamba na mfano wake

## Hukumu ya kupangusa khofu mbili na soksi mbili

Sheria imeweka upangusaji wa khofu mbili na soksi mbili, kwa hadithi nyingi mikongoni mwazo ni riwaya iliyopokewa na Anas bin Malik t alipoulizwa kuhusu upangusaji wa khofu mbili, alisema: Mtume ﷺ alikuwa akipukusa juu ya hivyo)

[ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Masharti ya kupangusa khofu mbili na soksi mbili

1.Kuzivaa baada kujitwahirisha kikamilifu. Mughirah amepokewa akisema: (Nilikuwa na Mtume ﷺ safarini, nikafanya haraka kumvua khofu zake, akasema: “Ziache, kwa kuwa mimi nilizivaa katika hali ya utwahara” akapukusa juu yake)
[ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

2.Ziwe ni zenye kusitiri miguu mpaka kwenye vifundo, zikiwa chini ya vifundo viwili hazipukuswi, kwa kuwa vifundo si katika nyayo.

3.ziwe zimetengezwa kwa vitu vilivyo twahara.

4.Ziwe zinafaa kutumiwa na zisiwe ni miongoni mwa vitu haramu kama hariri kwa wanaume.

5.Kule kupukusa kuwe ndani ya muda uliowekwa. Kwani Mtum ﷺ aliweka muda maalumu wa kupukusa (usiku na mcha kwa mkazi na siku tatu kwa msafiri). Haifai kupitisha muda huo.

6.Kupukusa kuwe kwenye kujitwahirisha kutokana na kutangukiwa na udhu na sio tukio kubwa la ukosefu wa twahara. Imepokewa na Swafwan bin Assal (R.A.) kuwa alisema (Alikuwa Mtume ﷺ akituamrisha tukiwa safarini tupukuse khofu zetu, na tusizifue siku tatu, kwa kwenda haja, kukojoa na kulala isipokuwa kutokana na janaba) [ Imepokewa na Bukhari.], yaani mwenye janaba ni juu yake azivue khofu mbili kwa kuoga kisha azivae mara nyingine.

## Namna ya kupangusa khofu mbili na soksi mbili

Atapukusa juu ya khofu kwa mikono yake miwili ikiwa majimaji, kuanzia kwenye vidole vya miguu yake mpaka kwenye muundi wake mara moja. Atapukusa mguu wakulia kwa mkono wa kulia na mguu wa kushoto kwa mkono wa kushoto.

Wala hapukusi chini ya khofu wala kisiginyo chake. Ali t amesema: (Lau Dini ilikuwa ni kwa maoni ingekuwa kupukusa chini ya khofu ni bora kuliko juu yake. Na kwa hakika nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu akipukusa juu ya khofo zake) [ Imepokewa na Abu Daud.].




Kupangusa kwa mikono yake miwili

## Muda wa kupangusa khofu mbili na soksi mbili:

Usiku na mchana kwa mkazi na siku tatu pamoja na masiku yake kwa msafiri.

Dalili yake ni neno la Ali (Mtume amemwekea msafiri siku tatu na masiku yake, na amemwekea mkazi wa mji usiku mmoja na mchana wake) [ Imepokewa na Nasai].




## Hesabu ya muda wa kupangusa

Muda unaanzia mwanzo wa kupangusa baada ya kutangukiwa na udhu. Avaapo soksi mbili akiwa kwenye hali ya utwahara, kisha akaukosa twahara kwa mara ya kwanza, basi kuanzia kupangusa huku kutahesabiwa usiku na mchana (masaa ishirini na nne). Mfano wake ni mtu aliyetawadha, akaosha miguu yake kisha akavaa soksi zake, akaswali alfajiri, na wakati wa saa nne asubuhi alitokewa na vitanguo, na udhu wake ukatanguka. Ilipofika saa tano asubuhi alitawadha na akaswali Dhuha na akapukusa soksi zake. Hapa yafaa kwake yeye kuendelea kuvaa soksi mbili na kupukusa juu yake mpaka saa tano asubuhi ya siku ya pili.
Hayo ni kwa mkazi ama msafiri ni kwa muda wa siku tatu na masiku yake



## Venye kutangua upangusaji wa khofu mbili na soksi mbili

1.Kumalizika muda wa kupukusa.
2.kuzivua soksi mbili au mojawapo.
3.kupatikana na tukio kubwa la kutangua twahara. Imepokewa kutoka kwa Swafwan bin Assaal t: (Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akituamrisha tukiwa safarini tusivue

khofu zetu kwa siku tatu na masiku yake isipokuwa kutokana na janaba, lakini kutokana na choo, mkojo na kulala) [ Imepokewa na Tirmidhi].



Kupangusa chini ya khofu



Kupangusa kisiginyo



Kuvua soksi kunatangua upangusaji

# Pili: Kupukusa juu ya kitata, bendeji na plasta

## Maana ya utata, bendeji na plasta

### Kitata

Ni kile kinachofungwa mahali palipovunjika kiwe ni tambara zito au vipande vya mti au mfano wake

Bendeji
Ni kitu kinachotatiwa kwenye jaraha au mahali palipochomeka au kinginecho kwa kitambaa au mfano wake ili kujitibu nacho.
Plasta
Ni kile kinachobandikwa kwenye jaraha na mfano wake kwa kujitibu.







## Dalili ya kusihi kupangusa juu ya vitata kisheria

Amepokewa Jabir t alisema: (Tulitoka kwenda safari, na mmoja wetu akagongwa na jiwe kichwani mwake likampasua. Kisha akaota (usingizini). Akawauliza wenzake: “Je mnanipatia ruhusa yoyote kisheria ya mimi kutayamam?” Wakasema “Hatukupatii madamu wewe

unaweza kutumia maji”. Akaoga na akafa. Tiliporudi kwa Mtume ﷺ alielezwa habari hiyona akasema: “Wamemuua! Mwenyezi Mungu Awaue. Si wangeuliza ikiwa hawajui? Kwani dawa ya kutojua ni kuuliza.” Hakika ingalimtosha yeye kutayamamu na kufunga kitamba kwenye jaraha lake, kisha akapukusa juu yake, na kuosha sehemu zisaliezo za mwili wake) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## Masharti ya kupangusa juu ya vitata, bendeji na plasta

1.Imesharutishwa katika bendeji au vitata visizidi sehemu inayotakikana kutibu pamoja na sehemu za kandokando yake zinazohitajika kuthibitisha vitu hivi.
2.Haisharutishwi katika kufunga bendeji au vitata awe mtu yuko kwenye twahara, vilevile haisharutishwi muda maalumu, madamu vinahitajika kusalia basi yafaa kupukusa juu yake wakati wakujitwahirisha na tukio kubwa na dogo la ukosefu wa utwahara. Na wakati wowote ule mahitaji yake yameondoka ni lazima kuvivua na kukiosha kiungo husika wakati wa kujitwahirisha.
3.Kuhusu mabendeji na vitata na mfano wahivyo ambavyo ni rahisi kuzirudisha itatazamwa:
a. Ikiwa kuvitoa na kuosha sehemu za chini yake ni sahali bila madhara au kusababisha jaraha kuchelewa kupoa, basi atavitoa aoshe sehemu za chini yake, kisha avirudishe.
b. Iwapo si rahisi kuvitoa na kuosha sehemu za chini yake bila kudhurika au kuchelewa kupoa, atapukusa juu yake wakati wa kuosha kiungo kile ambacho vitu hivyo viko juu yake.

## Namna ya kuhisabu muda wa kupangusa



Namna ya Kupangusa juu ya vitata




Namna ya kupangusa juu ya bendeji




Namna ya kupangusa juu ya bendeji

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
Swalah Kwa Khofu Ya Kuweko Najasa Ya Mbwa

# Kuoga

## Maana ya Kuoga

### Kuoga kilugha

Kueneza maji juu kitu

### Kuoga kisheria

Kueneza maji mwilini kwa namna maalumu kwa kusudia kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu U

# Yenye kuwajibisha kuoga

## 1. Kutokwa na manii

Na manii ni maji meupe, mazito yanatoka kwa kasi wakati wa matamanio, na yana harufu inayofanana na yai lililoharibika, kwa neno lake Mwenyezi Mungu : {Na mkiwa na janaba jitwahirisheni} [5: 6]

na neno lake Mtume ﷺ kumwambia Ali (RA). (Ukimwaga maji oga) [ Imepokewa na Abu Daud.].

Fadh'h almaa': kutoka maji kwa kasi, na makusudio yake ni manii

- Maelezo

1. Lau mtu aota na asitokwe na manii, basi haimpasi kuoga. Na yanapotoka baada ya kuamka itamlazimu kuoga.

2. Akikuta manii na asikumbuke kuwa ameota itamlazimu aoge kwa ajili ya kutokwa na manii. Mtume ﷺ amesema: (Hakika Ulazimu wa kutumia maji unasababishwa na kutokwa na maji) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.], yaani: Kuoga kunalazimu kwa kutokwa na manii.

3.Lau ahisi kuwa manii yanataka kutoka kisha yasitoke, basi haimlazimu kuoga.

4.Lau atokwa na manii kwa hitilafu fulani mwilini mwake au ugonjwa bila ya matamanio, basi hana ulazima wa kuoga.

5.Akiwa na janaba akaoga, kisha akatokwa na manii baada ya kuoga, haimlazimu kuoga tena, kwa kuwa hayo kwa kawaida hutoka bila matamanio. Na kutoka shakani ni kutawadha.

6.Aamkapo usingizini mwenye kulala akapata urutuba(maji maji ya manii) ambao hajui sababu yake, huwa ni moja kati ya hali tatu:

a. Akate kuwa ni manii, na hapo itampasa kuoga, awe akumbuka kuwa ameota au hakumbuki.

b. Akate kuwa si manii, hapo haimpasi kuoga, na hukumu yake ni hukumu ya mkojo.

c. Awe na shaka baina ya kuwa ni manii au si manii. Hapo ni juu yake ajitahidi, akikumbuka chenye kutilia nguvu kuwa ni manii, basi ni manii. Na akikumba chenye kutilia nguvu kuwa ni madhii, basi ni madhii. Na akitokumbuka chochote itamlazimu kuoga kwa kuondoa shaka.

7.Aonapo manii na asikumbuke aliota lini, basi itamlazimu kuoga na kuzirudia Swala usingizi wa mwisho aliyoulala.

### 2.Kuundama

Nako ni kukutana tupu ya mwanamume na tupu ya mwanamke, kwa kuingia sehemu ya mbele yote ya dhakari kwenye tupu, hata bila ya kushusha manii, kwa kauli ya Mtume ﷺ: (Tupu ikishapita kwenye tupu, basi kuoga huwa kumeshalazimu) [ Imepokewa na Tirmidhi].

### 3. Kafiri kusilimu

Kwa kuwa Mtume ﷺ alimuamuru Qais bin 'Aswim aliposilimu kuoga [ Imepokewa na Abu Daud.].

### 4. Kukatika damu ya hedhi na nifasi

Kwa hadithi ya ‹Aishah kwamba Mtume ﷺ alimwambia Fatimah binti Abi Hubaish (Hedhi ikija acha kuswali, na ikiondoka oga na uswali) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na nifasi ni kama hedhi kulingana na maoni ya wanavyuoni kwa umoja wao.

### 5. Kifo

Kwa kauli yake Mtume ﷺ katika hadithi ya kumuosha binti yake zainab alipokufa: (Muosheni mara tatu, au tano, au zaidi ya hapo mkiona hivyo) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Namna ya kuoga

Linalolazimu katika kuoga ni kueneza maji kwenye mwili kwa namna yoyote ile. Lakini inapendekezwa afuate vile Mtume ﷺ alivyooga, nayo ni kama ilivyoelezwa na Maimunah, Mama wa Waumini  aliposema (Mtume aliweka chombo cha maji ya


kujitwahirishia na janaba, akajimiminia maji kwenye kitanga cha mkono wa kushoto akitumia kitanga cha mkono wake wa kulia mara mbili au tatu, kisha akaosha tupu yake, kisha akapiga mkono wake kwenye ardhi au ukuta mara mbili au tatu, kisha akasukutua na akapaliza puani, akaosha uso wake na mikono yake, kisha akajimiminia maji kichwani mwake, kisha akaosha mwili wake, kisha akajiweka kando akaosha miguu yake) [ Imepokewa na Bukhari].

Asema Maimunah: (Nikamletea kitambaa, hakukitaka, akawa ajifukuta kwa mkono wake).

Hivyo basi namna ya kuoga ni:

1. Aoshe vitanga vyake vya mikono, mara mbili au tatu.
2. Aoshe tupu yake.
3. Apige mkono wake kwenye ardhi au ukutani, mara mbili au tatu.
4. Atawadhe kama vile anavyotawadha kuswali, bila ya kupukusa kichwa chake na kuosha miguu yake.
5. ajimiminie maji kichwani.
6. Aoshe mwili wake wote.
7. Ajiweke kando na aoshe miguu yake.






FAIDA

- Si lazima kwa mwanamke kufunguwa nywele zake anapo taka kuoga janaba au hedhi, Itamtosheleza kujimiminia maji na kuhakikisha kuwa maji yamefika kwenye ngozi ya kichwa.

- inapendekezwa kwa mwanamke anapo oga hedhi au nifasi achukuwe pamba au mfano wake na aiweke misk kisha ajiondoshe athari ya damu.
- Mtu anapo oga janaba inasihi kwake kuswali kwa josho hilo, sawa alitia nia ya kutawadha ama hakutia

## Yanayoharamishwa kwa mwenye janaba

### 1. Kuswali:

Kwa neno lake Aliyetukuka: {Enyi mlioamini! Msikaribie Swala hali mmelewa, mpaka myajue mnayo sema, wala hali mna janaba isipo kuwa mmo safarini mpaka muoge}.[ Al-Nisaa 43]

### 2. Kuitufu Nyumba Tukufu (Alkaba):

Kwa neno lake Mtume ﷺ: (Kutufu Alkaba ni kama kuswali) [ Imepokewa na Nasai.].

### 3. Kugusa Msahafu:

Kwa neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Hawaigusi isipokuwa waliotwahirishwa} [56: 9].

Na neno la Mtume ﷺ (Haugusi Msahafu isipokuwa aliye twahara) [ Imeipokewa na Malik katika Muwatta'.].

### 4. Kusoma Qur›ani:

Imepokelewa kutoka kwa Sayyidna Ali(RA) akisema (alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akitoka chooni na akitusomea Qur'ani, na akila nyama pamoja na sisi. Na hakuwa akizuiliwa na kitu chochote kusoma Qur'ani isipokuwa janaba) [ Imepokewa na Tirmidhi].

### 5. Kukaa msikitini isipokuwa kwa mpita njia:

Kwa neno lake Aliyetukuka: {Enyi mlioamini! Msikaribie Swala hali mmelewa, mpaka myajue mnayo sema, wala hali mna janaba isipo kuwa mmo safarini mpaka muoge}. [ Al-Nisaa 43]



Kuswali




Kutufu Alkaba



Kushika Msahafu



Kusoma Qur›ani




Kukaa msikitini

## Kuoga kunakopendekezwa

### 1. Kuoga kwa Ijumaa

Kwa kauli ya Mtume ﷺ: (Mwenye kutawadha kwa ajili ya kwenda Ijumaa, hilo ni jambo zuri, na mwenye kuoga, basi kuoga ni bora) [ Imepokewa na Abu Daud.]

### 2. Kuoga wakati wa kuhirimia kwa Umra au Hija:

Imepokewa kutoka kwa Zaid bin Thabit  kwamba yeye alimuona Mtume ﷺ akijiondoa na nguo za kawaida kwa ibada ya Hija na akaoga [ Imepokewa na Tirmidhi]

### 3. Kuoga baada ya kuosha maiti:

Kwa neno la Mtume ﷺ: (Mwenye kuosha maiti aoge) [ Imepokewa na Ibn Majah.]

### 4. Kuoga baada ya kila tendo la ndoa

imepokewa na Abu Rafi›  kwamba Mtume (SAW.) siku moja aliwapitia wake zake, na alikuwa akioga baada ya kumaliza kwa huyu na kwa yule. Mpokeaji asema: (Nikamwambia"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! usiuoge mara moja? Akasema (SAW " Hili ni safi zaidi, bora zaidi na twahara zaidi) [ Imepokewa na Abu Daud.].

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:

Ghuslu - Je, Inapasa Kufanya Ghuslu Baada Ya Kutokwa Na Manii Bila Ya Kujimai?

Makatazo

1- kuchelewesha kuoga janaba mpaka utoke wakati wa Swala.

2- kwa mwanamke aliyetwahirika na hedhi kuacha Swala ya wajibu. Na lau atwahirika kabla ya kutoka wakati wa adhuhuri kwa kadiri ya rakaa moja, basi itampasa aoge na aswali adhuhuri. Mtume ﷺ amesema (Mwenye kuwahi rakaa moja ya asubuhu kabla ya kuchomoza jua, basi amewahi Swala ya asubuhi. Na mwenye kuwahi rakaa moja ya alasiri kabla ya jua kuzama, basi amewahi Swala ya alasiri) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

# Kutayamamu

4.3

11044

## Maana ya Kutayamamu

Kutayamamu kilugha
Kukikusudia kitu na kukielekea
Kutayamamu kisheria
Kupukusa uso na mikono miwili kwa ardhi twahara kwa nia ya kujitwahirisha

## Hukumu ya kutayamamu

Inapasa kutayamamu yakikosekana maji au ikawa haiwezikani kuyatumia kwa jambo linalolazimu utwahara kama vile Swala. na kutayamamu kunapendekezwa katika kufanya jambo linalopendekezwa kama vile kusoma Qur›ani.

## Dalili za kutayamamu kisheria

1. Mwenyezi Mungu U Anasema: {Mkitopata maji kusudieni ardhi nzuri, mpanguse nyuso zenu na mikono yenu kwa hiyo} [5: 6]

2. Amesema Mtume ﷺ: (Nimepewa mambo matano hakuna aliyepewa kabla yangu: Nimenusuriwa kwa kitisho masafa ya mwezi, nimefanyiwa ardhi kuwa ni mahali pa kuswali na pa kujitwahirishia: kwani yoyote katika umma wangu atakayeingiliwa na kipindi cha Swala na aswali) [ Imepokewa na Bukhari.].

## Hekima ya Sheria kuweka kutayamamu

1. Kuwasahilishia umma wa Mtume Muhammad ﷺ

2. Kuepusha madhara yanayosababishwa na utumiaji maji katika hali ya ugonjwa, na baridi kali na mfano wa hayo.

3. Kudumisha mafungamano ya ibada yasikatike kwa kukosekana maji, au kutoweza kuyatumia

## Niwakati gani mtu anafaa kutayamamu

### 1. Yanapokosekana maji

Kwa neno lake Mwenyezi Mungu aliyetukuka: {Na mkitopata maji tayamamuni} [5: 6].

Na mtu haambiwi kuwa amekosa maji iwapo hakuyatafuta.

### 2. kushindwa kuyatumia maji

Kama mgonjwa au mkongwe asiyeweza kutembea, na akawa hana wa kumsaidia kutawadha.



Mgonjwa



Mtu mzima

### 3. Wakati wa kuchelea madhara kwa kutumia maji

Miongoni mwa hayo:

a. Mgonjwa ambaye angeyatumia maji ugonjwa wake utazidi.

b. Mtu aliye mahali penye baridi kali na asiwe na kitu cha kupasha maji moto na akawa na yakini lau ataoga atapatikana na ugonjwa. Hii ni kwa hadithi iliyothubutu kuwa Mtume ﷺ alimkubalia ‘Amr bin al-’Asw alipowaswalisha wenzake hali akiwa ametayamamu kwa sababu ya baridi kali [ Imepokewa na Abu Daud.].

c. Awapo mahali mbali na hana maji isipokuwa kidogo ambayo anayahitajia kwa kunywa na hawezi kuleta mengine.

## Namna ya kutayamamu

1. Aupige mchanga kwa mikono yake pigo moja.
2. Kisha aipulize kupunguza vumbi.
3. Kisha apanguse uso wake kwa hiyo mikono mara moja.
4. Kisha apanguse upande wa nje wa wa vitanga vya mikono.

Apanguse sehemu ya nje ya kitanga cha mkono wa kulia kwa sehemu ya ndani ya kitanga cha mkono wa kushoto, kisha nje ya kitanga cha mkono wa kushoto kwa sehemu ya

Na dalili ya namna ya kutayamamu ni hadithi ya Ammar t kwamba Mtume ﷺ alipiga ardhi kwa vitanga vyake viwili vya mkono, akavipuliza kisha akapangusa uso wake na vitanga vyake kwavyo) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].




Kupiga mchanga kwa mikono miwili




Kupuliza mikono miwili




Kupangusa uso




Kupangusa mkono wa kulia kwa wa kushoto



Kupangusa mkono wa kushoto kwa wa kulia

## Faradhi za kutayamamu

1. Kutia nia.
2. Kupangusa uso.
3. Kupangusa vitanga vya mikono.
4. Kufuatanisha: aanze kupangusa uso kisha vitanga viwili vya mikono.
5. Kufulililiza: Apanguse mikono miwili baada ya kupangusa uso papo kwa papo.

## Vitanguo vya kutayamamu

1. pakipatikana maji.
2. kutukiwa mojawapo ya vitanguo vya udhu.
3. Kutukiwa na chenye kupasisha kuoga kama kuota.
4. Kuondokewa na udhuru wa kutayamamu uliowekwa na Sheria, kama ugonjwa na mfano wake.



pakipatikana maji

Kwamba mchanga wa ardhi unakusanya kwenye chembechembe zake mada ya kutakasa. Mada hii inaweza kumaliza aina zote za vijidudu, na inaweza kumaliza virusi.

## Maelezo

1. Kuswali kwa kutayamamu, iwapo haiwezekani kutumia maji, ni bora kuliko mtu kuswali na huku amejizuia mkojo au choo.
2. Inafaa kutayamamu kwenye ukuta au mswala na mfano wa hivyo, iwapo kuna mchanga au vumbi juu yake.
3. Yafaa kwa mwenye kutayamamu kuswali, kwa tayamamu moja, swala atakazo za faradhi na za sunna, iwapo bado hajatangukwa na tayamumu yake.
4. Yafaa kwa mwenye kutawadha kumfuata mwenye kutayamamu, kwa kuwa Mtume ﷺ alimkubalia 'Amr bin al-'Asw t alipowaswalisha wenzake hali ya kuwa ametayamamu kwa ajili ya baridi kali [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
5. Mwenye kutayamamu na akaswali, kisha akapata maji kabla ya wakati kutoka, hatairudia ile swala. Abu Said al-Khudri t amepokewa akisema: (Walitoka watu wawili safarini, wakati wa Swala ukaingia na wao hawana maji, wakakusudia ardhi nzuri wakatayamamu na wakaswli, kisha wakapata maji ndani ya wakati, mmoja wao akarudia swala na udhu, na yule mwingine asirudie. Kisha wakamjia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ wakamuelza hayo, akasema kumwambia yule ambaye hakurudia "Umepata Sunna na Swala yako imekutosheleza" na akmwambia yule aliyetawadha na akarudia "Wewe una thawabu mara mbili") [ Imepokewa na Abu Daud.].
6. Mwenye kutayamamu kisha akapata maji kabla ya kuswali au katikati ya Swala, itamlazimu kujitwahirisha kwa maji, kwa kauli ya Mtume ﷺ: (Hakika ardhi nzuri ni twahirisho kwa Muislamu, hata kama hatapata maji miaka kumi.

Atakapopata maji basi ayatumie kwenye ngozi yake ya mwili, kwani hilo ni kheri) [ Imwpokewa na Tirmidhi].

7. Hakuna cha kumfunga Muislamu na Swala wala kuichelewesha wakati wake. Akitoweza kutumia maji au asipoyapata, atatayamamu, akielemewa na kutayamamu pia, basi ataswali bila twahara.

8. Mwenye kukosa vitwahirisho viwili (maji na mchanga) ataswali wakati ukiingia bila ya twahara wala haimlazimu kurudia, kwa kuwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Amesema: {Mcheni Mwenyezi Mungu mnavyoweza}

# Hedhi, inayofanana na hedhi na nifasi

## Hedhi

### Maana ya hedhi

#### Hedhi kilugha

Ni kitu kutiririka na kupita

#### Hedhi kisheria

Ni damu inayotoka kwenye uzao wa mwanamke katika muda maalumu bila yasababu

### Namna ya damu ya hedhi ilivyo

Ni nyeusi kama kwamba imechomeka kwa weusi wake mwingi, yaumiza, ina harufu mbaya, mwanamke akiwa nayo huhisi joto lingi

### Miaka ya hedhi

Hakuna miaka maalumu ya kuanzia hedhi, kwani inatafautiana kulingana na tabia ya mwanamke, na mazingira yake na hewa yake, wakati wowote mwanamke aonapo damu ya hedhi, basi yeye ameingia hedhini

## Muda wa hedhi

Hedhi haina muda maalumu. Miongoni mwa wanawake kuna anayeingia hedhini kwa muda wa siku tatu, na miongoni mwa wanawake kuna anayeingia hedhini siku nne. Na muda wa hedhi kwa wanawake wengi ni siku sita au saba, kwa neno lake Mtume ﷺ kumwambia Hamnah binti Jahsh, na alikuwa akiingia hedhini kwa siku nyingi: (Zingatia kile kinachokutoka, kwa siku sita au saba, kuwa ni hedhi, ujuzi wa kikamilifu uko kwa Mwenyezi Mungu, kisha oga) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## Maelezo

1. Asili ni kuwa mwenye mimba hapati hedhi, basi aonapo damu kabla ya kuzaa kwa muda mchache na ukafuatiwa na uchungu wa kuzaa, basi hiyo ni damu ya nifasi. Na ikitofuatana na uchungu wa kuzaa, au ikawa kabla ya kuzaa kwa muda mrefu, basi hiyo ni damu ya hedhi.

2. Ikitangulia au ikachelewa hedhi na wakati wake wa kawaida kwa mwanamke, kama wakati wake uwe ni mwanzo wa mwezi aione mwisho wake, au muda wake wa kawaida ukazidi au ukapungua, kwa mfano: iwe ada yake ni siku sita zikazidi zikawa saba. Basi na asijishughulishe na hilo, kwani popote aonapo damu, hiyo ni hedhi, na popote aonapo kuwa ametwahirika basi huo ni utwahara.

3. unajulikana kutwahirika kwa mwanamke, kwa kutokwa na Qassatul baydhaa nayo ni mtiririko mweupe unaotoka hedhi inapo simama, isipotoka, alama ya kutwahirika kwake ni kule kukauka, kwa kuweka pamba nyeupe kwa tupu yake na kisitoke chochote

## Miongoni mwa hukumu za hedhi

### 1. Hukumu ya uvindu na umanjano

#### Maana ya uvindu na umanjano

### Al-sufrah:
umanjano ni damu inayotoka kwa mwanamke.

### Al-kudrah:
ni damu iliyochafuka iliyo baina ya umanjano na weusi

## Hukumu ya uvindu na umanjano

Mwanamke akiona damu ya manjano au iliyochanganyika baina ya umanjano na weusi, au akaona umajimaji tu, huwa ni moja ya hali mbili:

1. Ima aione wakati wa hedhi au imeungana na hedhi kabla ya utwahara:

Katika hali hii itapewa hukumu ya hedhi, kwa hadithi ya Aishah t kwamba wanawake walikuwa wakimtumia kibakuli ambacho ndani yake kuna pamba yenye dowa rangi ya manjano, na yeye akiwambia: « musifanye haraka mpaka muone paku leupe" akikusudia kwa hilo kutwahirika na hedhi

2. Ima aione wakati wa twahara:

Katika hali hii huwa haizingatiwi kuwa ni kitu chochote, na haimpasi udhu wala kuoga, kwa hadithi ya Ummu ‹Atiyyah kwamba alisema: "Hatukuwa tukiizingatia damu iliyochafuka au iliyo manjano baada ya kujitwahirisha kuwa ni chochote) [ Imepokewa na Abu Daud.].



Alama ya kutwahirika



Namna ya umanjano



Namna ya mvurunduko

### 2. Hukumu ya kukatika katika kwa hedhi:

Mwanamke aonapo damu siku moja na kukatika siku moja na mfano wake, basi yeye ni mojawapo wa hali mbili

### 1. Hali hiyo iendelee na yeye kila wakati:

Basi hiyo ni damu ya istihadhah

### 2. Iwe yakatikakatika:

Kwa namna ya kwamba ikawa yamjia wakati mwingine na atwahirika wakati mwingine. Basi hukumu yake ni kama ifuatayo:

a. Kukatika damu kukipungua kwa siku moja, basi kipindi hiko kitahesabiwa kuwa ni katika kipindi cha hedhi.

b. Na akioona katika kipindi cha utwahara dalili za damu, kama kuona paku leupe, basi kipindi hiki ni cha utwahara, liwe ni dogo au kubwa, au liwe chini ya siku moja au zaidi.

## Damu ya istihadhah

### Maana ya istihadhah

## Istihadhah

Ni kutiririka damu kutoka kwenye tupu ya mwanamke ikawa haikomi kabisa au ikatike kwa kipindi kichache.

### Tofauti baina ya damu ya hedhi na ya istihadhah

| Damu ya istihadhah | Damu ya hedhi |
|---|---|
| Nyekundu nyepesi | Nyeusi nzito |
| Haina harufu | Ina harufu mbaya yenye kuchukiza |
| Inaganda (inashikana) | Haigandi (haishikani) |
| Inatoka kwenye kishipa cha uzao cha karibu | Inatoka mwisho wa uzao |
| Damu ya kuashiria kasoro, ugonjwa na uharibikaji | Damu ya afya na ya kawaida |
| Haina wakati maalumu | Inatoka wakati maalumu |

### Hali za ailye kwenye istihadhah

### Hali ya kwanza: awe na ada inayojulikana ya siku zake za hedhi kabla ya kujiwa na istihadhah:

Huyo atahesabu siku za kadiri ya ada yake kuwa ni hedhi na zinazosalia katika mwezi ni istihadhah, kwa hadithi ya ‘Aishah t kwamba Fatimah binti Abi Hubaish t alisema: (Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi sitwahiriki, je niache kuswali? Mtume akamwambia “La, hiko ni kishipa. Lakini acha kuswali kadiri ya siku zako za kuingia hedhini, kisha oga na uswali”) [ Imepokewa na Bukhari.].

### Hali ya pili: Asiwe na ada inayojulikana, lakini anaweza kupambanua baina ya damu ya hedhi na damu ya istuhadhah:

Basi huyu atatumia upambanuzi wake, kwa ilivyothubutu kwamba Fatimah binti Hubaish t alikuwa kwenye damu ya istihadha, Mtume akamwambia: (Ikiwa ni damu ya hedhi, basi hiyo ni

damu nyeusi inayojulikana. ikija, acha kuswali, na ikija ile nyingine tawadha na uswali, kwani damu hiyo ni kishipa) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## Hali ya tatu: Asiwe na ada maalumu na asiweze kupambanua:

Basi huyo atatumia ada za wengi wa wanawake, hivyo basi hedhi itakuwa ni siku sita au saba katika kila mwezi, ataanzia mwanzo wa kipindi anapoona damu, na siku zilizosalia zitahesabiwa ni istihadha. Hii ni kwa kauli yake Mtume ﷺ kumwambia Hamnah binti Jahsh t: (Basi hesabu kuwa wewe uko hedhini kwa siku sita au siku saba, uhakika unajulikana na Mwenyezi Mungu, mpaka ukiona kuwa umetwahirika na umetakasika, swali kwa masiku ishirini na tatu au masiku ishirini na nne na michana yake, na ufunge, kwani hilo linakutosheleza. Na ufanye hivyo katika kila mwezi, kama wanavyohidhi wanawake na kama wanavyotwahirika wanawake wengine, kulingana na nyakati zao za hedhi na utwahara) [ Imepokewa na Abu Daud.]

## Hali ya nne: Awe na ada maalumu na aweze kupambanua:

Huyu atazingatia ada na siyo kupambanua, kwa kuwa ada ina udhibiti zaidi kwa mwanamke. Na anaposahau ada yake basi atatumia upambanuzi.

## Maelezo

1. Iwapo mwanamke anajua wakati wa hedhi yake, lakini akawa amesahau idadi ya siku zake za hedhi, basi atashika hesabu ya ada ya wengi wa wanawake.
2. Iwapo mwanamke anajua idadi ya siku zake za hedhi, lakini akawa amesahau wakati wa hedhi yake, iwapo ni mwanzo wa mwezi au ni mwisho wake, atahesabu mwanzo wa mwezi idadi ya siku zake za hedhi. Akisema kuwa yamjia mwanzo wa mwezi lakini hawezi kujuwa ni lini wakati wake, atashika hesabu kuanzia

mwanzo wa nusu idadi ya siku ilipokuwa hedhi yake ikimjia, kwa kuwa nusu ya mwezi ndio kadiri iliyo karibu zaidi ya kudhibiti wakati wake.

3. Kikipita kipindi cha hedhi, na mwanamke yuko kwenye istihadhah basi ataoga kisha atafunga kitambaa kwenye tupu yake. Na hukumu yake itakuwa ni ile ya twahara, ataswali na atafunga, na haitamdhuru damu itakayomtoka baada ya kutawadha kwa kuwa ana udhuru, na atafanya mojawapo ya mambo matatu katika twahara:

a. Atawadhe kwa kila Swala baada ya wakati kuingia. Hilo ni baada ya kuosha tupu yake na kuifunga kitambaa, kwa kauli ya Mtume ﷺ kumwambia Fatimah binti Hubaish t: (Kisha tawadha kwa kila Swala na uswali) [ Imepokewa na Abu Daud.].

b. Aicheleweshe Adhuhuri mpaka kabla ya Alasiri, kisha aoge na aswali Adhuhuri na Alasiri, na atafanya hivi katika Swala nyingine. Hii ni kwa neno lake Mtume ﷺ kumwambia Hamnah binti Jahsh t: (Na ukiweza kuchelewesha Adhuhuri na kuitanguliza Alasiri, ukaoga na ukakusanya baina ya Swala mbili: Adhuhuri na Alasiri, na ukachelewesha Magharibi na akaianguliza Swala ya Isha, kisha uoge na ukusanye Swala mbili, basi fanya hivyo. Na ukiweza kuoga wakati wa wa swala ya Alfajiri basi fanya hivyo, na ufunge, kama waeza kufunga) [ Imepokewa na Abu Daud.].

4. Mwanamke akitokwa na damu kwa sababu yoyote ile, kama operesheni, na ikatiririka, basi yeye ni mojawapo wa hali mbili:

a. Ijulikane kuwa hatapata hedhi. Huyu hazipitishwi kwake hukumu za istihadhah, wala haachi kuswali wakati wowote, na ile damu ni ya ugonjwa na kuharibika kwa kitu, na atatawadha kwa kila Swala.

b. Ijulikane kuwa yeye inamkinika kuingia hedhini. Huyu hukumu yake ni ya istihadhah.

5. nafaa kumuingilia mwanamke aliye kwenye istihadhah.kwa kuwa Sheria haikumkataza.

# Nifasi

## Maana ya Nifasi

Nifasi

Ni damu inayotoka kwenye uzao wa mwanamke kwa sababu ya kuzaa

## Muda wa Nifasi

Hakuna mpaka wa uchache wa nifasi. Ama wingi wake kwa kawaida ya wengi ni siku arubaini, isipokuwa akiona utwahara kabla ya hapo, Basi ataoga na aswali.

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
Ghuslu - Muda Wa Kutwaharika Na Damu Ya Nifasi

## Miongoni mwa hukumu za nifasi

1. Mwanamke akizaa na asione damu- na hii ni hali ya nadra sana- atatawadha na ataswali, na halazimiki kuoga.
2. Damu ikipita siku arubaini, na ikawa ada yake ni kukatika kwa kumalizika siku ya arubaini, au zikadhihiri alama za kukaribia kukatika, atangojea mpaka ikatike. Iwapo damu itaendelea, basi yeye ana istihadhah na itamthibitikia yeye hukumu za istihadhah.
3. Akitwahirika kabla ya siku ya arubaini, kisha damu ikamrudia ndani ya siku arubaini itamlazimu aangalie: .
a. Akijua kuwa ni damu ya nifasi, basi ni damu ya nifasi.
b. Na akijua kuwa si damu ya nifasi, basi hukumu yake ni kuwa yuko katika twahara.
4. Haithubutu damu kuwa ni ya nifasi isipokuwa akiwa amezaa kitu chenye umbo la binadamu, akiwa amezaa tisha- naye ni mtoto aliyetoka kwenye uzao wa mwanamke kabla ya umbo lake kukamilika- ambalo halijafafanuka kwake umbile la binadamu. Nalo lina hali tatu:
a. Iwe ni kabla ya siku arubaini za kwanza (za kushika mimba). Bila ya hivyo, hii itakuwa ni damu iliyoharibika, hivyo basi ataswali na atafunga.
b. Iwe ni baada ya siku thamanini. Na hii ni damu ya nifasi.

c. Iwe muda wake wa kukaa matumboni ni baina ya siku arubaini na thamanini. Na hii itatazamwa: Iwapo imeonesha alama ya kuwa ni kiumbe, basi hiyo ni damu ya nifasi. ikitokuwa hivyo, basi ni damu iliyoharibika

## Yanayoharamishwa kwa ajili ya hedhi na nifasi

## 1. Kujamiana

Kwa neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Na wanakuuliza juu ya hedhi. Waambie, huo ni uchafu basi jitengeni na wanawake wakati wa hedhi.wala msiwaingilie mpaka watahirike. Wakisha twahirika basi waendeni alivyo kuamrisheni mwenyezi mugnu.} [2: 222]

Na kwa kauli ya Mtume ﷺ ilipoteremka aya hii: (Fanyeni kila kitu isipokuwa kuundama) [ Imepokewa na Muslim.].

## Maelezo

1. Mwenye kumuingilia mkewe na hali yuko katika hedhi hupata dhambi na itamlazimu kafara na huyo mke pia atoe kafara iwapo aliridhia.

Na kafara ni kutoa sadaka kadiri ya dinari moja au nusu dinari ya dhahabu, kwa hadithi ya Ibnu Abbas kumpokea Mtume ﷺ juu ya mtu anayemuingilia mkewe na hali yuko kwenye hedhi kuwa alisema: (Atatoa sadaka Dinari moja au nusu dinari) [ Imepokewa na Muslim.].

Dinari moja ni grama nne na robo za dhahabu.

2. Aliyoko hedhini akiingia twaharani, haifai kwa mumewe kumuundama (kumuingilia) mpaka aoge, kwa neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka {Na msiwakaribie mpaka watwahirike} yaani: kutokana na damu.

Kisha akasema: {wakijitwahirisha} yaani: wakaoga.

Kisha akasema {Wajieni kupitia pale alipowaamrisha nyinyi Mwenyezi Mungu} [2: 222], yaani: kuundama.

## 2.Kuswali

Kwa neno lake Mtume ﷺ: (Ikija hedhi acha kuswali, na ikiondoka Safisha damu kwa kuoga kisha uswali) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## Maelezo

1. Mwanamke haimlazimu kulipa swala akitwahirika, Kwa hadithi iliyothubutu kutoka kwa ‹Aishaah t kuwa aliulizwa juu ya aliyekuwa na hedhi kulipa Saumu na kutolipa Swala, akasema: (Tulikuwa tukipatikana na hilo tukiamrishwa kulipa saumu na hatukuwa tukiamrishwa kulipa Swala) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

2. Iwapo mwenye hedhi atawahi rakaa nzima ya wakati wa Swala, itamlazimu aswali, iwe ni rakaa ya mwanzo ya wakati au ya mwisho wake. Ikiwa atawahi sehemu ya wakati ambayo haikundukii rakaa moja, basi haimlazimu kuswali, kwa kauli ya Mtume ﷺ: (Mwenye kuwahi rakaa moja ya Swala amewahi swala) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

### 3. Kufunga Saumu

Kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Kwani akiingia katika hedhi si ataacha kuswali na kufunga? Wakasema (wanawake): “Ndiyo”) [ Imepokewa na Bukhari.].

## Maelezo

Akitwahirika mwenye hedhi kabla ya Alfajiri na akafunga, basi Saumu yake itakuwa sahihi, ingawa hakuoga mpaka baada ya Alfajiri

### 4. Kushika Msahafu

Kwaneno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Hawaigusi isipokuwa walitwahirishwa} [56: 79]

Na kwa neno lake Mtume (Hawagusi Mswahafu ila aliye twahara) [ Imepokewa na Malik katika Muwatta’].

### 5. Kutufu Alkaaba

Kwa neno la Mtume ﷺ kumwambia ‹Aishah t: (Fanya kile anachokifanya mwenye kuhiji isipokuwa usitufu Alkaaba mpaka uwe twahara) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.]
na kwa haditi ya Ibn ‘Abbas t alisema: (Wameamrishwa watu iwe mwisho wa kukutana kwao na Alkaaba ni kutufu, isipokuwa mwanamke mwenye hedhi amehafifishiwa hilo) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

## 6. Kukaa msikitini isipokuwa mpita njia

Kwa neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Enyi mlioamini! Msikaribie swala hali mmelewa, mpaka myajue mnayo yasema, wala hali mna janaba isipo kuwa mmo safarini mpaka muoge} [4: 43]
na kwa neno la Mtume ﷺ (Mimi simhalalishii msikiti mwenye hedhi wala mwenye janaba)

## Maelezo

1. Si makosa kwa mwenye hedhi kupita msikitini akijihifadhi na asichelee kuuchafua msikiti, kwa ujumla wa maneno ya Mwenyezi Mungu Aliyetuka: {Isipokuwa wapita njia} [4: 43]
2. Ni haramu kwa mwenye hedhi kukaa kwenye eneo la kuswalia Idi, kwa neno lake Mtume ﷺ (Na wajiepushe na kuhudhuria mahali pa kuswali Idi) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## 7.Talaka

Ni haramu kwa mume kumuacha mkewe akiwa na hedhi, kwa neno lake mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Ewe Nabii mkiwataliki wanawake, watalikini mkizingatia eda lao } [65: 1].
Yaani waelekee kwenye eda maalumu wakati wa kuachwa.
Na talaka ya mwenye hedhi inapita ingawa ni haramu na ni uzushi katika Dini.
Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
Ghuslu - Vipi Kukoga Janabah, Nifaas Na Hedhi

# SWALAH

## Cheo cha Swala na Hukumu Yake

### Maana ya Swalah

Swalah kilugha

Maombi

Swala kisheria

Ni kumuabudu Mwenyezi Mungu U kwa maneno na vitendo maalumu, vinavyoanzia kwa takbiri na vinavyomalizikia kwa kupiga salamu.

### Hadhi ya Swalah katika Uislamu

1. Swalah ni nguzo ya pili katika nguzo za Uislamu.

Amesema Mtume ﷺ: (Uislamu Umejengwa juu ya nguzo tano: kukiri kwa moyo na kubaini kwa ulimi kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni mja Wake na mtume Wake, na kusimamisha Swala…) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

2. Swalah ndio amali bora kimatendo.

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ: (Amali bora kuswali mwanzo wa wakati wake). [Imepokewa na Tirmidhi]

3. Swalah ni upambanuzi baina ya Uislamu na ukafiri.

Mtume ﷺ amesema: (Baina ya mtu na ushirikina na ukafiri ni kuacha Swala) [ Imepokewa na Muslim.].

4. Swalah ni nguzo ya Uislamu. Juu yake – baada ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu ndio yajenga Uislamu.
Mtume ﷺ: (Kichwa cha jambo hili ni Uislamu na nguzo yake ni Swala) [ Imepokewa na Ahmad].

## Fadhila za Swala

1. Swala ni nuru kwa mwenye kuswali. Mtume ﷺ amesema: (Na Swalah ni Nuru) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
2. Swala ni kafara ya dhambi. Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Amesema: {Na simamisha Swala ncha mbili za mchana na nyakati za usiku zinazokaribiana na mchana. Hakika mema yanafuta maovu. Hayo ni makumbusho kwa wenye kukumbuka} [11: 114].
Na amesema Mtume ﷺ: ( Mnaonaje, lau kuna mto mlangoni mwa mmoja wenu ambao anaoga ndani yake kila siku mara tano, je kutasalia chochote cha uchafu mwilini mwakeWakasema: Hakutasalia uchafu wowote katika mwili wake. Akasema Mtume ﷺ: Huo ndio mfano wa Swala tano,. Mwenyezi Mungu kwa hizo Swalah anayafuta madhambi) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
3. Swala ni sababu ya mtu kuingia Peponi. Mtume ﷺ alimwambia Rabi’ah bin Ka’ab, alipomtaka wasuhubiane naye Peponi,: Mtume akamjibu: (Nisaidie kwa kuishughulisha nafsi yako kwa kusujudu sana) [ Imepokewa na Muslim.].

## Hukumu ya Swala

Swala tano ni wajibu kulingana na Qur›ani, Sunna na umoja wa wanavyuoni:
1. Qur’ani:

Anasema Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Na simamisheni Swala na toeni Zaka na rukuuni pamoja na wenye kurukuu} [2: 43].

2. Sunna:

Amesema ﷺ: (Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: kushuhudia kuwa hapana mola isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni mja Wake na mtume wake, na kusimamisha Swala, nakutoa Zaka, nakuhiji Alkaba na kufunga mwezi wa Ramadhani) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

- Na imepokewa kutoka kwa Twalhah bin 'Ubeidillah kwamba mtu mmoja alimuuliza Mtume ﷺ kuhusu Uislamu, akasema ﷺ: (Ni Swala tano mchana na usiku. Akasema: "Je, kuna nyingine zinazonilazimu sizizokuwa hizo?" Akasema: La, isipokuwa ukijitolea) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

3. Umoja wa wanavyuoni:

Umma kwa umoja wao wamekubaliana juu ya uwajibu wa Swala tano kipindi cha mchana na usiku.

## Swala inamlazimu nani?

Swala inamlazimu kila Muislamu, aliyebaleghe, mwenye akili, awe mwanamume au mwanamke.

Kulipa Swala

Kafiri haamrishwi kulipa Swala zilizompita kabla ya kusilimu, kwa kuwa uislamu unafuta yale yaliyo kabla yake.

## Hukumu ya mwenye kuacha Swala

### 1. Mwenye kuacha Swala kwa kukanusha uwajibu wake:

Atafahamishwa akiwa hajui. Akiendelea kukanusha kwake, basi yeye ni kafiri, mkanushaji wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na umoja wa Waislamu.

### 2. Mwenye kuacha Swala kwa uvivu:

Mwenye kuacha Swala kwa kukusudia na uvivu atakuwa amekufuru. Na ni juu ya kiongozi amlinganie kuswali na amuorodheshee toba kwa muda wa siku tatu. Basi akitubia ni sawa, na akitotubia atamuua kwa kuwa ameritadi. Hii ni kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Ahadi iliyoko baina ya sisi na wao ni Swala. Yoyote yule atakayeiacha basi atakuwa amekufuru ) [ Imepokewa na Tirmidhi.], na kauli yake ﷺ: (Hakika baina ya mtu na ushirikina na ukafiri ni kuacha Swala) [ Imepokewa na Muslim.].

Swala ya mtoto

Mtoto anaamrishwa kuswali akifika miaka saba, kwa kumzoeza, na anapigwa kwa kuiacha afikapo miaka kumi kipigo kisichoumiza. Amesema Mtume ﷺ: (Waamrisheni watoto wenu kuswali wakiwa ni vijana wa miaka saba, na wapigeni kwa kuiacha swala wakiwa ni vijana wa miaka kumi)) [ Imepokewa na Abu Daud.].



# Adhana na ikama

## Maana ya Adhana na Ikama

### Kuadhini

Ni kujulisha kuingia wakati wa Swala kwa kuleta maneno maalumu ya dhikiri.

### Kukimu

Ni kujulisha kuanza kuswaliwa kwa kuleta maneno maalumu ya dhikiri.

## Hukumu ya kuadhini na kukimu

### 1. Katika Swalah za jamaa:

Ni faradhi ya kutosheleza, kwa Swalah tano za faradhi peke yake, safarini na mjini, kwa kuwa hizo mbili ni miongoni mwa alama za Uislamu za waziwazi, hivyo basi haifai kuziacha. Amesema Mtume ﷺ: (Ufikapo Wakati wa Swala, basi awaadhinie mmoja wenu, kisha awaswalishe mkubwa wenu) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

### 2. Katika Swalah ya anayeswali peke yake:

Ni sunna. Amepokewa ‹Uqbah bin ‹Amir akisema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akisema: (Anamuonea ajabu Mola wako mchunga mbuzi aliye juu ya kilele [ Shadhiyyah: Ni kipande kilichoinuka kilichoko kwenye kilele cha jabali.] cha jabali, anayeadhini kwa Swala kisha akaswali, hapo aseme Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: “Mwangalieni mja wangu huyu, anaadhini kisha anakimu Swala, ananiogopa! Nishamsamehe mja wangu na nitamuingiza Peponi”) [ Imepokewa na Annasai.].

Hikma ya kuadhini

1. Kujulisha kuwa wakati wa swala umeingia.
2. Kuhimiza juu ya Swalah ya jamaa.
3. Kuwazindusha walioghafilika na kuwakumbusha waliosahau watekeleze Swalah ambayo ni miongoni mwa neema tukufu zaidi.

## Adhana imewekwa lini na sharia na ni kwa sababu gani?

Adhana iliwekwa na Sheria mwaka wa kwanza wa Hijria. Na sababu yake ni kuwa ilipotokea haja ya kuweka alama ambayo kwayo watu wote watajua kuwa wakati wa Swala umeingia Waislamu walishauriana juu ya hilo. Ulipokuja usiku Abdullah bin Said aliota usingizini kuwa amemuona mwanamume amebeba kengele[ Naaquus: kengele.], Akamwambia: " je, unauza kengele hii?" Yule mwanamume akasema: "Wataka kufanyia nini?". Abdullah akasema: "Tuwaitie watu kwenye Swala". Yule mwanamume akasema: "Je, sikupi ushauri wa kitu bora kuliko hiki?" [ Imepokewa na Daarimi.].

Abdullah akasema: "kwani? Nipe". Hapo akamfundisha adhana hii ijulikanayo, kisha akamfundisha ikama. Abdullah alisema: Nilipopambaukiwa nilimwendea Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ nikampa habari ya kile nilichokiona usingizini. Akasema ﷺ: (Hiyo ni ndoto ya kweli, Mwenyezi Mungu Akitaka, basi inuka pamoja na Bilali umfudishe hayo maneno, kwani yeye ana sauti kubwa zaidi kuliko wewe) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## Fadhla za kuadhini

1. Kinamtolea ushahidi mwadhini kwa Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka, Siku ya Kiyama, kila kilichofikiwa na sauti yake. Amesema Mtume ﷺ: (Hakuna jini wala binadamu wala kitu chochote kinachofikiwa na sauti ya mwadhini isipokuwa humshuhudilia Siku ya Kiyama) [ Imepokewa na Bukhari.].

2. Lau watu wangejua ubora wa kuadhini wangalishindaniana kwa hilo. Amesema Mtume ﷺ: (Lau watu wanajua ubora ulioko kwenye adhana na safu ya mbele, kisha wasipate suluhisho isipokuwa wapige kura [ Isthaam: Kupiga kura ili apatikane anaestahiki kutangulizwa.], basi wangepiga kura kushindania hayo) [ Imepokewa na Bukhari.]

## Masharti ya kuswihi kwa adhana

1. Muadhini awe ni Muislamu, mwanamume, mwenye akili.
2. Adhana ilingane na mpango uliowekwa.
3. Iwe ni yenye kufuatanishwa, kusiwe na mwanya mrefu baina ya maneno yake.
4. Iwe ni pale unapoingia wakati wa Swala.

## Sunnah za kuadhini

1. Kuelekea Kibla.
2. Kutwahirika kwa mwadhini kutokana na hadathi mbili.
3. Kuzunguka katika ha-yaa Ala(Swala/Falaa) mbili, nazo ni anaposema: Ha-yaa Ala Swalat. Ha-yaa Alal Falah, kuliani na kushotoni.
4. Mwadhini aweke vidole vyake viwili vya shahada masikioni mwake.
5. Mwadhini awe na sauti nzuri ya nguvu.
6. Adhana itolewe kwa ufafanuzi na utulivu.



## Namna ya kuadhini na kukimu

1. Namna ya kuadhini: (Allaahu Akbar, Allaahu Akbar, Allaahu Akbar, Allaahu akbar. Ash'hadu an laa ilaaha illa Allah, Ash'hadu an laa ilaaha illa Allah.Ash'hadu anna Muhammadan Rasuulu-Allah, Ash'hadu anna Muhammadan Rasuulu-Allah, Hayya 'ala ssalaah, Hayya 'ala ssalaah. Hayya 'ala l falaah, Hayya 'ala l falaah. Allaahu Akbar, Allaahu Akbar. Laa ilaaha illa Llaah) [ Imepokewa na Muslim].

2. Namna ya kukimu: (Allaahu Akbar, Allaahu Akbar. Ash'hadu an laa ilaaha illa Llaah. Ash'hadu anna Muhammadan Rasuulu Laah. Hayya 'ala l falaah. Allaahu Akbar, Allaahu Akbar. Laa ilaaha illa Llaah).

## Yanayopendekezwa kwa anayesikia adhana

1. Asema kama vile anavyosema mwadhini, isipokuwa anaposema: (Haya njooni mswali! Haya njooni kwenye kufaulu !) hapo atasema (Hapana hila zozote za kufanyia mambo ya utiifu wala nguvu zozote za kuyaepuka maasia isipokuwa ni kwa msaada wa Mwenyezi Mungu) [ Imepokewa na Bukhari.].

2. Asema baada ya adhana: (Nashuhudilia kwamba hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu, Peke Yake, Hana mshirika, na kwamba Muhammad ni mja wake na Mtume Wake. Nimeridhika kwamba Mwenyezi Mungu ndie Mola, na kwamba Muhammad ﷺ, ni mtume na kwamba Uislamu ni Dini) [ Imepokewa na Muslim.].

3. Amswalie Mtume ﷺ baada ya adhana, kisha aseme: (Ewe Mola! Bwana wa ulinganizi huu uliotimia, na Swala hii iliyosimama! Mpe Muhammad njia za kheri na utukufu, na umfikishe kwenye Cheo chenye kusifiwa ulichomuahidi) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## Miongoni mwa hukumu za Adhana na Ikama

1. Adhana peke yake inatosha wakati wa kukusanya Swala mbili, kama vile Adhuhuri na Alasiri, Na hapo kutakimiwa kwa kila Swala.

2. Swala ikikimiwa, kisha kukachelewa kuswaliwa, basi hakuna haja ya kukimiwa mara ya pili.

3. Ni juu ya mwadhini ajihadhari na kukosea katika matamshi ya adhana, na miongoni mwayo ni:

a. kusema “Aallaahu Akbar?” kwa kuuliza swali.

b. Kusema: “Allaahu akbaar” kwa kuivuta Baa.
c. kusema: “Allaahu wa akbar” kwa kuzidisha Waw.
4. Swalah ikikimiwa, haifai kuswali swalah ya sunnah. Ama ikiwa itakimiwa na mtu ashaanza kuswali Sunna, ataikamilisha iwapo imesalia kidogo kumalizika, na ikitokuwa hivyo, ataikata, bila ya kutoa Salamu, na ataingia kwenye Swala ya faradhi pamoja na imamu.
5. Adhana ya mtoto anayefahamu inakubalika
6. Sheria imeweka adhana na ikama kwa Swala iliyompita mtu kwa sababu ya kulala au kusahau, kwa hadithi iliyothubutu kwa Mtume ﷺ walipolala Maswahaba wakapitwa na Swala ya Asubuhi mpaka jua likachomoza, kwamba alimuamuru Bilali akaadhini, kisha wakatawadha na wakaswali rakaa mbili za Alfajiri, kisha akamuamuru Bilali akimu Swala, akakimu Swala na Mtume akawaswalisha Swala ya Asubuhi ) [ Imepokewa na Ahmad.].
7. Aliye msikitini baada ya kuadhiniwa hafai kutoka isipokuwa kwa dharura, kwa hadithi iliyopokewa na Abu Hurairah t alisema: ( Alituamrisha Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kwamba mkiwa msikitini na mwadhini ukaadhiniwa, asitoke mmoja wenu mpaka aswali) [ Imepokewa na Ahmad.]
8. Mwadhini anatakiwa na Sheria ateremshe sauti yake katika shahada mbili, kisha arudie kuongeza sauti, kwa kuwa hilo limethubutu katika Sunna. [ Imepokewa na Abu Daud.]

Yasiofaa

1. kuleta adhana kwa mahadhi na kuimba kwa namna inayopelekea kugeuza herufi, haraka, sakna, kupunguza na kuzidisha.
2. kuinua sauti kwa kumswalia Mtume ﷺ baada ya adhana.
3. Kusema, baada ya kusikia: QAD QAAMATU SWALAAT “Swala imesimama”: “Mwenyezi Mungu Aisimamishe na Aidumshe”, bali atalirudia neno hilo kama lilivyo.
- Adhana ya Swala ya Alfajiri

Alfajiri imewekewa adhana mbili: ya kwanza ni kabla ya kuingia wakati, na ya pili ni ya kujulisha kuwa wakati umeingia ili watu wahudhurie kuswali. Katika adhana ya kwanza, mwadhini anatakiwa aseme: “Swala ni bora kuliko kulala” mara mbili, kwa kuwa Mtume ﷺ alisema: Ukiadhini adhana ya kwanza ya Alfjiri, sema: “Swala ni bora kuliko kulala “ [ Imepokewa na Abu Daud.]

Adhana Humfukuza Shetani

Kutoka kwa Abuu hurera (RA) amesema: Amesema Mtume ﷺ (Inapo Nadiwa kwa ajili ya swala shetani hukumbia na huku akishuta, ili asisikie Adhana inapo malizika Adhana hurudi, inapo kimiwa hukimbia inapo malizika hurudi na kuingia kati ya mtu na nafsi yake, na kumwabia: kumbuka kitu Fulani na Fulani, jambo ambalo alikuwa halikumbuki, mpaka mtu akawa hajui ameswali ngapi, asipojuwa mmoja wenu ameswali rakaa ngapi, tatu au nne, basi asujudu sijida mbili na hali yakuwa amekaa) [ Imepokewa na Bukhari.]

Faida

1. Haifai kutoka Msikitini baada ya kuadhiniwa na kabla ya kukimiwa kwa hadithi ya Abuu Hureyra (RA) Alipo muona mtu ametoka Msikitini baada ya kuadhiniwa, akasema: ama huyu amemuasi babake Qaasim (SWA)
2. Hakuadhiniwi wala hakukimiwi kwa Swala ya sunna, wala Swala ya Iddi Mbili, wala Swala ya Jeneza, ila katika Swala ya Kupata kwa jua kutanadiwa Swalatu Jaamia
3. wakati wa Mvua nyingi au ubaridi kali atesema Muadhini bada ya hayyalal falah Alaa Swalluu fi Rihalikum (Swalini majumbani mwenu)

## Masharti ya kufanya Swala iwe sahihi


## Kwanza: kuingia wakati

Swala ya faradhi ina wakati ambao haiswihi kabla yake, wala baada yake isipokuwa kwa dharura. Asema Mwenyezi Mungu aliyetukuka: { Hakika Swala kwa Waumini ni faradhi iliyo wekewa nyakati maalum} [4: 103],
yaani imefaradhiwa katika vipindi maalumu.
Nyakati za Swala ni: .
1. Wakati wa Alfajiri:
Ni kuanzia kutoka alfajiri ya kweli, nao ni ule weupe unaokuwa kwenye pambizo upande wa Mashariki, mpaka kuchomoza jua.
2. Wakati wa Adhuhuri:
Ni kuanzia kupinduka jua mpaka kivuli cha kitu kiwe mfano wake, baada ya kile kivuli cha kupinduka jua. Hivyo ni kwamba jua likichomoza kitu kinachosimama huwa na kivuli upande wa magharibi, kisha kivuli hiko huenda kikipungua kila jua likipanda mpaka kivuli kisimame. Kisha kivuli kinaanza kuongezeka, na ongezeko hili lianzapo hua ndio wakati wa kupinduka.
3. Wakati wa Alasiri:
Ni kuanzia wakati wa Adhuhuri kuisha mpaka kivuli cha kitu kiwe ni mara mbili yake baada ya kivuli cha kupinduka jua.
4. Wakati wa Magharibi:
Ni kuanzia jua linapozama mpaka yapotee mawingu mekundu, nayo ni ule mwangaza mwekundu unaokuwa kwenye pembe za mbingu pale jua linapozama.
5. Wakati wa Isha:
Ni kuanzia kipindi cha Magharibi mpaka nusu ya usiku, kwa neno lake ﷺ: (Wakati wa Swala ya Isha ni mpaka usiku wa kati)
[ Imepokewa na Muslim.].

Na katika zama hizi, inawezekana kujua nyakati za Swala kwa urahisi kwa njia ya kuweka jaduali za kujulisha nyakati.



Swala ya Alfajiri



Swala ya Adhuhuri



Swala ya Alasiri



Swala ya Magharibi



Swala ya Isha

Yasiofaa

- Kuswali na nguo ya kubana yenye kusifu uchi wa mtu, au nguo nyembamba yenye kuonyesha, au kuswali na huku akiwa tupu yake inaonekana, au na isbaal nao ni mtu kuswali na nguo yake imevuka vi fundoni.
- Kuswali na nguo yenye picha, au kuswali sehemu zilowekwa picha za roho, au kuswalia mswala wenye picha na michoro.
- Kuswali katika Msikiti wenye Makaburi, kwa neno lake Mtume ﷺ (Jueni kuwa watu walio kuwa kabla yenu wakiyafanya makaburi ya manabii wao na watuwema wao misikiti, basi musiyafanye makaburi yeni misikiti mimi nawakataza hilo) [ Imepokewa na Muslim.]

Faida


1. Mwenye kuwahi rakaa moja kabla ya kutoka wakati huwa amewahi Swala, kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Mwenye kuwahi rakaa moja ya Swala huwa amewahi Swala) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
2. Ni lazima kutekeleza Swala kwa haraka iwapo wakati wake umepita kwa kulala au kwa kusahau, kwa neno lake Mtume ﷺ: (Mwenye kuisahau Swala basi ni juu yake aiswali anapoikumbuka, hakuna kafara yake isipokuwa hiyo) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

## Pili: Kutwahirika na hadathi

### 1. Kutwahirika na hadathi ndogo (tukio la kutokuwa na udhu):

Nako kunapatikana kwa kutawadha. Mtume ﷺ anasema:

(Mwenyezi Mungu hatakubali Swala ya mmoja wenu akitokewa na tukio la kutokuwa na udhu mpaka atawadhe) [ Imepokewa na Bukhari].



### 2. Kutwahirika na hadathi kubwa:

nako kunapatikana kwa kuoga, kwa neno la mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Na mkiwa na janaba jitwahirisheni} [5: 6].

Na yoyote atakayekumbuka akiwa katika Swala kuwa hana udhu au ametokewa na jambo la kuharibu udhu katikati ya Swala, basi Swala yake itatanguka Na itamlazimu ajitoe Swalani ili ajitwahirishe na bila ya kutoa Salamu, kwa kuwa swala ishatanguka na bado haijamalizika, na utoaji salamu ndio mwisho wa Swala.



## Tatu: Utwahara wa Nguo, mwili na mahali

### 1. Utwahara wa nguo,

kwa neno lake Mwenyezoi Mungu aliyetukuka: {Na nguo zako twahirisha} [74: 4].



Utwahara wa nguo

## 2. Utwahara wa mwili,

kwa ilivyothubutu kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliipita kwenye kaburi mbili akasema: (Hakika wawili hawa wanaadhibiwa. Na hawaadhibiwi kwa jambo kubwa. Ama huyu alikuwahajiepushi [ Laa yastanzihu min al-baul: hajiepushi na hajikingi na mkojo.] na mkojo usimuingie) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## 3. Utwahara wa mahali,

kwa hadithi ya mbedui aliyekojoa msikitini. Mtume ﷺ alisema: (Muacheni na umwagieni [ Hariiqu: mwageni.] mkojo wake ndoo [ Dhanuub: ndoo kubwa iliyojaa maji.] ya maji) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].



Utwahara wa Mahali pa kuswali

## Swala na Najisi

Mwenye kuswali naye ana najisi bila ya kuijua au akaisahau, basi Swala yake ni sahihi. Kwa kuwa ilithubutu kwamba Mtume wa

Mwenyezi Mungu ﷺ aliswali akavua viatu vyake, na watu wakavua viatu vyao. Alipoondoka alisema ﷺ: (kwa nini mlivua viatu vyenu? Wakasema: “Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Tulikuona ukivua viatu vyako na sisi tukavua”. Mtume akasema: “Jibrili alinijia akanipasha habari kwamba viatu vina uchafu. Basi anapokuja mmoja wenu msikitini, avigeuze viatu vyake avitazame. Akiona kuwa vina uchafu, basi na avisugue chini kisha aswali navyo) [ Imepokewa na Abu Daud.].

Yoyote atakayejua kuwa ana najisi akiwa katikati ya Swala, itamlazimu kuiondoa, kisha aendelee na Swala yake na ajengee juu ya kile alichokiswali, kwa hadithi iliyotangulia. Akitoweza kuiondoa, swala yake itatanguka.

## Ardhi yote ni Msikiti

Ardhi yote ni msikiti, kwa kuwa kuswali hapo inafaa. Mtume ﷺ amesema: (Nimefanyiwa ardhi kuwa ni mahali pa kuswali na mahali pakujitwahirishia. Basi mtu yoyote miongoni mwa umma wangu aliyeingiliwa na kipindi cha Swala na aswali) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Kinachovuliwa hapo ni kuswali kwenye sehemu zilizokatazwa, kama vile kuswali makaburini (Kinachovuliwa hapo ni Swala ya maiti.) na chooni, kwa kuwa Mtume ﷺ alisema: (Ardhi yote ni mahali pa kuswali, isipokuwa makaburini na chooni) [ Imepokewa na Tirmidhi.].

Na pia sehemu ya malazi ya ngamia kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Musiswali katika malazi ya ngamia) [ Imepokewa na Tirmidhi.]. Na hapo ni mahali pa ngamia kulala na kukusanyika.



Kuswali makaburini



Kuswali chooni

## Nne: Kusitiri tupu

Tupu ya mwanamume: ni kuanzia kitovuni hadi gotini.
Tupu ya mwanamke: ni mwili wake wote isipokuwa uso na vitanga vya mikono.






Kufinika mabega

Inamlazimu mwenye kuswali avae nguo yenye kufinika mabega yake na shingo yake, kwa kuwa Mtume alisema: (Asiswali mmoja wenu kwa nguo moja bila ya kuwa imefinika mabega yake) [ Imepokewa na Tirmidhi.].
isipokuwa yeye hakuwa akiswali juu yake Swala za faradhi) [ Imepokewa na Tirmidhi.].

## Tano: Kuelekea Kibla

Na kibla ni alkaaba tukufu
Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Amesemna: { Elekeza uso wako upande wa msikiti wa Haram. Na popote mlipo, elekezeni nyuso zenu upande wake} {Al-Baqara: 144}.
Na inalazimu kuchunga baadhi ya mambo:
1. La wajibu kwa mwenye kuswali ndani ya msikiti wa Haram aielekee alkaba yenyewe. Ama yule anayeswali akiwa mbali na Alkaaba, basi ataelekea upande wa hiyo Alkaba na sio kuielekea yenyewe, kwa kuwa hawezi kuielekea yenyewe. Kwa hivyo, Mtume ﷺ alisema: (baina ya mashariki na magharibi ni kibla) [ Imepokewa na Tirmidhi].
2. Swala ya Sunna kwa aliyepanda mnyama, kibla chake ni ule upande ambao kile kipando kinaelekea, kwa kuwa ilithubutu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akiswali [ Yusabbihu: anaswali Swala ya Sunna.] juu ya kipando chake akielekea popote pale kile kipando kinapoelekea, na

alikiswali witri juu yake, isipokuwa yeye hakuwa akiswali juu yake Swala za faradhi) [ Imepokewa na Abu Daud.].

- Asiyejua Kibla Atafanya Nini?

Asiyejua kibla akiwa kwenye jengo au mahali penye watu walio karibu, atauliza au atajijulisha kibla kwa vibla vya misikiti au dira au jua au mwezi au vinginevyo. Akitoweza kujua basi atajitahidi na atafuata lile lenye nguvu katika dhana yake, kwa neno lake Mwenyezi Mungu: {Muogopeni Mwenyezi Mungu vile mnavyoweza} [64: 16].



Mwenye kuswali ndani ya msikiti wa Haram
Mwenye kuswali akiwa mbali na Alkaba

# Miongoni mwa adabu za kuswali

Swalah ni ibada kuu. Muislamu katika ibada hiyo anaelelekea kwa moyo wake na mwili wake kwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka. Hivyo basi inatakikana itanguliwe na matayarisho ya kiroho na ya kimwili, ili aingie katika swala akiwa hana kitu cha kumshughulisha na aitekeleze kwa njia sahihi, na kwa hivyo imewekewa mambo yafuatayo:

## 1. Ikhlasi (kumtakasia Mwenyezi Mungu)

Mwenyezi Mungu U Anasema: {Na hawakuamrishwa isipokuwa wamuabudu Mwenyezi mungu hali ya kumtakasia Yeye Dini, hali ya kuwa na msimamo thabiti, na wasimamishe Swala na watoe Zaka, na hiyo ndiyo Dini ya mila iliyolingana sawa} [Al-Bayinah: 5].

Na Mwenyezi Mungu hakubali amali njema yoyote isipokuwa ibada ya kutakasiwa Yeye, isiyokua na kujionyesha wala kutaka sifa wala aina yoyote ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu.

## 2. Kueneza maji kwenye viungo vya kutawadha

Nako ni kutawadha vizuri kwa njia kamilifu.

Abu Huraira (RA) alipokewa akisema kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: (Je, siwajulishi nyinyi kitu ambacho kwacho Mwenyezi Mungu hufuta dhambi na hupandisha daraja? Wakasema: “ kwani? Tujulishe, ewe Mtume wa Mwenyezi mungu!” Akasema: Ni kueneza maji kwenye viungo vile itakikanavyo katika kutawadha [ Al-makarih: ni vile vinavyomsumbua mtu kama baridi na mfano wake.] , kukithirisha hatua za kwenda misikitini, na kungojea Swala baada ya Swala, kwani huko ndiko kujifunga kwenye utiifu wa Mwenyezi Mungu [ Ribatw: Kujifunga nafsi juu ya utiifu wa Mwenyezi Mungu.]) [Imepokewa na Muslim.].

## 3.Kutoka mapema kwa ajili ya Swalah

Nako ni kutoka mapema ili kupata fadhila za kungojea Swala. Abu Huraira ﷺ amepokewa akisema kwamba Mtume wa Mwenyezi mungu ﷺ amsema: (Mmoja wenu huzingatiwa anaendelea kuwa kwenye Swala kwa mda ambao anasubiri swala) [ Imepokewa na Bukhari.].

## 4. Kumtaja Mwenyezi Mungu

- Amtaje Mwenyezi Mungu anapotoka nyumbani kwa kusema: (Kwa jina la Mwenyezi Mungu, nimetegemea kwa Mwenyezi Mungu, Hapana hila za kujiepusha na maasia wala nguvu za kufanya mambo ya utiifu isipokuwa ni kwa msaada wa Mwenyezi Mungu) [ Imepokewa na Abu Daud.], (Ewe Mola! Mimi najilinda kwako ni sipotee au nipoteze, au niteleze au niwafanye watu wateleze, au nidhulumu au nidhulumiwe, au nikosee au nikosewe) [ Imepokewa na Abu Daud.].

- Na amtaje Mwenyezi Mungu anapokwenda msikitini kwa kusema: (Ewe Mola! Nijaalie nuru moyoni mwangu, na nuru kwenye ulimi wangu, na nuru kwenye masikizi yangu, na nuru kwenye maangalizi yangu, na ujaalie nuru nyuma yangu, na nuru mbele yangu, na ujaalie nuru juu yangu na nuru chini yangu. Ewe Mola! Nipe nuru) [ Imepokewa na Muslim.].

## 5. Kwenda msikitini kwa utulivu na upole

Kwa kauli yake Mtume ﷺ: (mkisikia swala inakimiwa, nendeni kuswali, na kuweni na utulivu [ Sakinah: Utulivu na upole katika kwenda.] na umakini [ Waqaar: Umakini, utulivu, uinamishaji macho na uchache wa kuzungukazunguka.], na msiende haraka, mnachokipata kiswalini na kinachowapita kitimizeni) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## 6. Kumtaja Mwenyezi Mungu wakati wa kuingia na kutoka msikitini

- Atangulize mguu wake wakulia wakati wakuingia msikitini na aseme: (Najilinda kwa Mwenyezi Mungu Mkubwa, na kwa uso wake mtukufu na mamlaka yake ya tangu na tangu, kutokana na Shetani aliyefukuzwa kwenye rehema ya Mwenyezo Mungu) [Imepokewa na Abu Daud.], (Na ingia kwa

jina la Mwenyezi Mungu na kumuombea rehema na amani Mtume wa Mwenyezi mungu) [Imepokewa na Muslim.]. ( Ewe Mola! Nifungulie milango ya rehema zako) [Imepokewa na Muslim.].

- Na atangulize mguu wake wakushoto wakati wa kutoka msikitini na aseme: ( Natoka kwa jina la Mwenyezi Mungu na kumuombea rehema na amani Mtume wa Mwenyezi Mungu. Ewe Mola! Mimi nakuomba fadhila zako. Ewe Mola! Nilinde mimi kutokana na Shetani ) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## 7. Asikae mpaka aswali rakaa mbili

Kwa kauli yake Mtume ﷺ: ( Anapoingia mmoja wenu msikitini, aswali rakaa mbili kabla hajakaa) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## 8. Kujiepusha na kushikanisha vidole

Kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Anapotawadha mmoja wenu vizuri kisha akatoka kukusudia msikitini, basi na asivishikanishe vidole vyake kwakuwa yeye yuko katika Swala) [Imepokewa na Abu Daud.]

## 9. Kujishughulisha na kumtaja Mwenyezi Mungu

Kujishughulisha kumtaja Mwenyezi Mungu, kuomba dua na kusoma Qur›ani wakati wa kungojea Swala bila kuwafanyia fujo wenye kuswali.

## 10.Kuwa mnyenyekevu katika Swala

Unyenyekevu ndio kiini cha Swala na roho yake. Swala bila ya unyenyekevu wala kuhudhurisha moyo ni kama mwili uliokufa. Ibnu Rajab, Mwenyezi Mungu amrehemu, alisema: “ Asili ya unyenyekevu ni moyo kulainika na kuwa nyororo, kutulia, kuwa mnyonge, kujivunjavunja na kupishika. Basi moyo ukinyenyekea

viungo vyote huufuata moyo, kwa kuwa hivyo vinauandama na kuufuata moyo” [ Al-Khushuu’ cha ibnu Rajab.].
Basi unyenyekevu mahali pake ni moyo, na ulimi wake wenye kueleza ni viungo.

## 11. Kujilazimisha na Sunna ya Mtume ﷺ katika swala yake yote

Swala ni ibada ambayo ni lazima kufuata, kusifanywe chochote wala kusisemwe lolote katika Swala ambalo Mtume ﷺ hakulifanya wala hakulisema, kwa neno lake Mtume ﷺ: (Swalini kama vile mlivyoniona nikiswali) [Imepokewa na Bukhari. ]

# Kizuizi cha mwenye kuswali

## Kukieleza kizuizi cha mwenye kuswali

### Kizuizi cha mwenye kuswali

Ni kitu anachokiweka mwenye kuswali mbele yake, baina yake yeye na mwenye kupita mbele yake

## Sharia ya kuweka kizuizi kwa mwenye kuswali

Kuweka kizuizi kumeamrishwa na Sheria, mjini na safarini, kwa Swala ya faradhi na swala ya Sunna, msikitini na mahali penginepo, kwa hadithi iliyothubutu kwa Mtume ﷺ kwamba yeye alisema: ( Anaposwali mmoja wenu aelekee kwenye kizuizi na awe karibu nacho) [ Imepokewa na Abu Daud.].

Amepokewa Wahb (R.A.) kuwa alisema: (Mtume alituongoza katika Swalah hapo Mina, akaisimamisha fimbo yake ﷺ – nayo ni kipande cha mti kidogo- mbele yake, akatuswalisha rakaa mbili) [ Imepokewa na Ahmad.].

## Hukuma ya kuweka kizuizi cha mwenye kuswali

Kuweka kizuizi ni lazima, kwa kuwa Mtume ﷺ ameamrisha kuweka kizuizi kwa imamu na pia mwenye kuswali peke yake na amehimiza hilo. Kwa hivyo inatakikana kwa Muislamu aweke kizuizi mbele yake aswalipo na amzuie mwenye kupita baina yake yeye na kile kizuizi alichokiweka, kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Usiswali isipokuwa uwe umeelekea chenye kukuzibia, na usimuache yoyote kupita mbele yako, na akikataa basi pigana naye) [ Imepokewa na Ibnu Khuzaimah.].

## Hekima ya kuweka kizuizi kwa mwenye kuswali

Mwenye kuswali ametakiwa na Sheria aweke kizuizi kwa hekima nyingi miongoni mwazo:

1. Kumzuia mtu asipite mbele ya mwenye kuswali akamkatia unyenyekevu wake.
2. Kummakinisha mwenye kuswali aishughulishe akili yake kwenye lile jambo la Swala na sio jambo lingine.
3. Ajihifadhi na kukatikiwa na swala yake kwa kupita mwanamke au mbwa au punda mbele yake, kwa hadithi iliyopokewa na Abu Dharr t kuwa alisema kwamba mtume ﷺ alisema: (Mmoja wenu akiinuka kuswali, kinatosha kuwa ni kizuizi chake iwapo mbele yake pana mfano wa kiwekea miguu kwa mwenye kupanda mnyama. Iwapo hakuna mbele yake mfano wa kiwekea miguu, basi Swala yake huharibiwa na punda, mwanamke na mbwa mweusi”. Nikasema: Ewe Abu Dharr! Kuna tofauti gani ya Mbwa mweusi na mbwa mwekundu na mbwa manjano? Akasema: Ewe mtoto wa ndugu yangu!

Nilimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ kama ulivyoniuliza, akasema: “Mbwa mweusi ni Shetani”) [ Imepokewa na Muslim.].

## Miongoni mwa Hukumu za kuweka Kizuizi

1. Kuweka kizuizi ni kwa imamu na mwenye kuswali peke yake. Ama maamuma, kizuizi cha imamu ni kizuizi chake. Amepokewa Ibnu Abbas t akisema: (Nilikuja nimepanda punda [ Ataan: punda jike.], na mimi siku hiyo nimekaribia umri wa kubaleghe na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ yuwaswalisha watu hapo Mina, nikapita mbele ya sehemu ya safu, nikashuka na nikamuacha punda kulisha, nikaingia safuni na hakuna mtu yoyote aliyepinga) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].



2. Haifai kupita mbele ya mwenye kuswali, kwani hilo ni miongoni mwa dhambi kubwa, kwa neno lake Mtume ﷺ: (Lau anajua dhambi alizonazo mpitaji mbele ya mwenye kuswali, ingalikuwa ni bora kwake kungojea siku arubaini kuliko kupita mbele yake). Abunnadhr anasema: ” Sijui kama alisema “siku arubaini” au “miezi” au “miaka” [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
Isipokuwa iwapo kule kupita ni kando ya pale mahali pa kusujudu kwake ikiwa mwenye kuswali ameweka kizuizi.



3. Ni lazima kwa mwenye kuswali amzuie anayepita mbele yake. Abu Said al- Khudri t alipokewa akisema: Nilimsikia Nabii ﷺ akisema: (Anaposwali mmoja wenu kuelekea kitu alichokifanya ni kizuizi chake cha kumzuia na watu, akaja mtu kutaka kupita mbele yake basi amzuie kupita, na akikataa, basi apigane naye, kwani yeye ni Shetani) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

4. Kuna jopo la wanavyuoni waliyouvua Msikiti wa Haram, wakawaruhusu watu kupita mbele ya mwenye kuswali, kwa dalili ya kutomtia mtu makosani, kwa kuwa kuwazuia watu. kupita mbele ya mwenye kuswali kwenye Msikiti wa Haram ni kumtia mtu madhambini na mashakani mara nyingi.

5. Na kizuizi cha Swala hupatikana kwa kuswali kuelekea ukutani au kwenye nguzo miongoni mwa nguzo za msikiti au kabati au aweke kitu mbele yake kama vile fimbo na mfano wake.

6. Masafa baina ya mwenye kuswali na kizuizi yanakadiriwa kwa nafasi ya kupita mbuzi, kwa hadithi iliyopokewa na Sahl  akisema: ( Baina ya mahali mtume wa Mwenyezi Mungu alipokuwa akiswali na baina ya ukuta ni kiasi cha kupita mbuzi) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Mwanamke kuharibia watu Swalah

Hakuna, katika hadithi iliyopita kuwa kupita mwanamke humuharibia mtu Swala, kumfananisha mwanamke na punda na mbwa mweusi. Vitu vitatu kutajwa kwenye mfumo mmoja haina maana kuwa sababu zake za kuharibu Swala zinafanana. Yaani haimaanishi kuwa sababu ya kuwa mbwa mweusi anamuharibia

mtu Swala kuwa ni sababu hiyohiyo inayofanya punda na mwanamke wamuharibie mtu Swala.
Hivyo basi, kule kuwa mbwa mweusi ni Shetani, kama hadithi ilivyosimulia, haina maana kuwa punda au mwanamke ni Shetani. Huenda zikawa sababu ya hivi vitatu ni tafauti ingawa vimekusanywa kwenye mfumo mmoja, ingawa sababu ya mbwa imeelezwa wazi kwenye tamko la hadithi, na sio vingine vilivyosalia. Hii inaonyesha kuwa sababu yake ni tofauti na sababu za vile visalievyo na haifanani nazo.
Na inamkinika kutoa sababu ya kuwa mwanamke anamkatia mwenye kuswali Swala yake kwa kupita mbele yake, au karibu yake , ni kuwa hilo huenda likambabaisha mwanamume moyo wake na huenda likamshughulisha na Swala. Kwa ujumla, kupita kwa mwanamke kunaushughulisha zaidi moyo wa mwanamume kuliko kupita mwanamume mwingine. Hivyo basi, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi zaidi, amri ya Sheria imekuja kuwa yeye ni miongoini mwa vitu vinavyoharibu Swalah ya mtu, ili kuhifadhi unyenyekevu wa Swala.

## Namna ya kuswali

Amesema Mtume ﷺ (Swalini kama munavoniona mimi nikiswali) [ Imepokewa na Bukhari]
Aisha alipokewa kwamba alisema: (Mtume ﷺ alikuwa akifungua Swalah kwa Takbiri na kisomo cha “Alhamdu lillaahi Rabbil ‘aalamiin”, na alikuwa akirukuu hakiinamishi kichwa chake na wala hakisimamishi sawa, bali alikikiweka baina ya hali hizo mbili. Na alikuwa akiinua kichwa chake

kutoka kwenye rukuu, hasujudu mpaka alingane katika kusimama. Na alikuwa akisoma Atahiyatu katika kila rakaa mbili, na alikuwa akikalia mguu wake wa kushoto na akiusimamisha mguu wake wa kulia. Na alikuwa akikataza mkao wa Shetani (kukaa kama shetani) na alikikataza mtu kuiweka chini mikono yake katika kukaa kama vile mnyama wa kuwinda, na alikuwa akihitimisha Swala yake kwa kupiga Salamu) [ Imepokewa na Muslim.].

## Kuelekea Kibla na Takbiri ya kufungia Swalah

- Anayetaka kuswali atasimama hali ya kuelekea Kibla na kujihisi kuwa amesimama mbele ya Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, hali ya kuwa ni mnyenyekevu katika kuswali kwake.
- Kisha anuilia kuswali moyoni mwake.na nia pahali pake ni moyoni, na haifai kuitemka nia kwani kufanya hivyo ni uzushi.Amesema Mtume (Hakika amali zote ni kwa nia na kila mtu hulipwa kwa alilo nuiliya) [Imepokewa na Bukhari.na muslim. ]
- Kisha ainue mikono yake mkabala wa mabega yake au masikio yake na aseme: ALLAHU AKBAR (Mwenyezi Mungu ni Mkubwa) [ Imepokewa na Muslim.].
- Kisha aweke mkono wake wa kulia juu ya wa kushoto kifuani mwake au aushike mkono wa kushoto kwa wa kulia [ Imepokewa na Ahmad.].



## Dua ya kufungulia Swalah na kusoma Fatiha

- Mwenye kuswali ainamishe kichwa chake, atazame mahali pa kusujudia, kisha aseme: SUB'HANAKA ALLAHUMMA WABIHAMDIKA, TABAARAKA IS'MUKA WATA'AALA JADDUKA WALAA ILAAHA GHAY'RUKA (Kutakasika ni kwako na sifa njema ni zako. Lina baraka jina lako na uko juu utukufu wako, na hakuna mola asiyekuwa Wewe) [ Imepokewa na Muslim.].

Kisha aseme baada ya hapo: A'UDHU BILLAHI MINA SHEYTWANI RAJIIM (Najilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na Shetani aliyefukuzwa kutoka kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu) BIS'MILLAHI ARRAH'MAANI ARRAHIIM (Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu) kwa siri [ Imepokewa na Muslim.].

Baada ya hapo asome Fatiha [ Imepokewa na Bukhari.], kisha aseme "Aamiin", yaani: Ewe Mola! Takabali.

. Kisha, huyo mwenye kuswali, asome Sura au baadhi ya aya za Qur'ani zilizo sahali kwake kuzisoma katika rakaa mbili za mwanzo, na asome kwa sauti katika Swala ya alfajiri na katika rakaa mbili za mwanzo za Magharibi na Isha.



## Kurukuu na kuinuka kotoka kwenye rukuu

- Mwenye kuswali atainua mikono yake na alete takbiri hali ya kuinama kwende kwenye rukuu, aiweke mikono yake juu ya magoti yake, huku amekunjua vidole vyake kama kwamba anayashika magoti, asawazishe mgongo wake na kichwa chake katika hali ya kuinama kisha aseme: SUBHANA RABIYAL

ADHIIM (Kutakasika ni kwa Mola wangu Aliye Mkubwa) (mara tatu ) [ Imepokewa na Tirmidhi.].

- Kisha ainuke na aseme (awe ni imamu au mwenye kuswali peke yake): SAMI'A LLAHU LIMAN HAMIDAH (Mwenyezi Mungu Anamsikia yule anayemsifu) [ Imepokewa na Tirmidhi.], na hapo wote waseme RABANA WALAKAL HAMDUH (Mola wetu! Sifa njema zote ni zako, kujaa kwa mbingu na kujaa kwa ardhi na kujaa vilivyoko baina hizo na kujaa kwa vinginvyo baada ya hizo ) [ Imepokewa na Tirmidhi.].

Na imependekezwa kuweka mikono juu ya kifua kama alivyofanya katika kusimama kabla ya kurukuu.



## Kusujudu na kuinuka kutoka kwenye kusujudu

- Atatoa takbiri kisha apomoke hali ya kusujudu, na kitu cha kwanza cha kugusa ardhi kiwe ni magoti yake kisha mikono yake [ Imepokewa na Abuu Daud.] kisha paja lake la uso na pua yake, Na akunjue vitanga vyake vya mikono juu ya ardhi mkabala wa mashikio yake na mabega yake.

Na avielekeze vidole vyake upande wa kibla na ainue mikono yake [ Saa'id: ni sehemu iliyo baina ya kiwiko na kifundo.] isiguse chini na aiepushe sehemu ya juu ya mikono iwe kando na mbavu zake ['Adhud: ni sehemu iliyo baina ya kiwiko na bega.], na pia matumbo yake [ Imepokewa na Bukhari] ayaepushe na mapaja yake, na aseme: SUBHANA RABIYAL A'ALAA (Kutakasika ni kwa Mola wangu Aliye juu kabisa) [ Imepokewa na Muslim.] (mara tatu), na akithirishe dua katika kusujudu kwake..

- Kisha atainua kichwa chake huku akileta Takbiri, na hatainua mikono yake na atakaa kwa kukalia mguu wake wa kushoto [ Imepokewa na Muslim.], na kusimamisha mguu wake wa kulia hali ya kuvielekeza vidole vyake upande wa Kibla, aiweke mikono yake juu ya mapaja yake ikiwa imekunjuliwa na vidole vyake vimeelekezwa Kibula na aseme: (Mola wangu! Nisamehe, unirehemu, uniungeunge, uniongoze na uniruzuku) [ Imepokewa na Tirmidhi.].



- Kisha atapiga takbiri na asujudu mara ya pili, kisha ainue kichwa chake hali ya kupiga takbiri na akae kikao kidogo kinachoitwa "kikao cha kujipumzisha" kwa hadithi iliyopokewa na Harith bin al-Huwairith (R.A.) katika kueleza namna ya Swala ya Mtume ﷺ kuwa yeye (alikuwa hainuki mpaka akilingana katika kukaa ) [Imepokewa na Bukhari.].
- Kisha ainuke huku akipiga Takbiri ya rakaa ya pili akijisaidia kwa mikono yake. [ Imepokewa na Bukhari.].
- Kisha ataswali rakaa ya pili kama vile ya kwanza, lakini hatasoma dua ya kufungulia Swala.

## Kikao cha Atahiyatu

Amalizapo mwenye kuswali rakaa mbili za kwanza atakaa kikao cha Atahiyatu ya kwanza, akikalia mguu wake wa kushoto hali ya kusimamisha mguu wake wa kulia na kuiweka mikono yake juu ya mapaja yake, na aukunjue mkono wake wa kushoto na akikunje kidole chake kidogo[ Al-Khinswar: ni kidole cha mwisho cha mkono.

Al-Binswar: ni kidole kinachofuatia kidole cha kwanza. - Al-wustwaa: kidole kinachofuatia kidole kidoge.- Al-Sabbaabah: Ni kidole chaShahada nacho ni kile kinachofuatia kidole cha kati. - Al-ibhaam: kidole kinachofuatia kidole cha shahada.] na kile kinachokifuatia vya mkono wa kulia, na akikunje kile cha kati pamoja na gumba, na akiinue kidole cha shahada na aashirie kwa kidole chake cha shahada wakati wa kikao cha Atahiyatu, na akitazame kwa macho yake na aseme: (Kila jinsi ya maamkuzi mema ni ya Mwenyezi Mungu, na rehema na mazuri yote. Amani ikushukie wewe, ewe Nabii, na rehema ya Mwenyezi Mungu na baraka Zake. Amani itushukie sisi na iwashukie waja wema wa Mwenyezi Munjgu. Ninaakiri kwamba hapana mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa mwenyezi Mungu, na ninakiri kwamba Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake) [Imepokewa na Bukhari.].

- Kisha atainuka huku akipiga Takbiri, iwapo Swala ni zaidi ya rakaa mbili, na ainue mikono yake apigapo Takbiri, na hatosoma katika rakaa zisaliezo isipokuwa Fatiha.

- Na atakaa kikao. cha tawarruk [ Imepokewa na Abu Daud.] katika Atahiyatu ya mwisho. Na tawarruk ni kuutoa mguu wa kushoto upande wa kulia na kuutaza na akalie matako yake, na mguu wa kulia usimamishwe. Na aseme matamko yaliyokuja kwenye Atahiyatu ya kwanza na azidishe juu yake: (Ewe Mola! Mrehemu Muhammad na jamaa za Muhammad, kama ulivyomrehemu Ibrahim na jamaa za Ibrahim, wewe ni Mwingi wa kuhimidiwa, ni Mwingi wa kusifiwa na kutukuzwa. Ewe Mola Mbarikie Muhammad na jamaa za Muhammad kama ulivyombarikia Ibrahim na jamaa za ibrahim, hakika wewe ni Mwingi wa kuhimidiwa, ni Mwingi wa kusifiwa na kutukuzwa) [ Imepokewa na Bukhari.].

- Kisha aseme: (Ewe Mola! Mimi najilinda kwako na adhabu ya Jahanamu na adhabu ya kaburi na maonjo ya uhai na

umaiti na shari ya fitna za Al-Masih Al-Dajjal) [ Imepokewa na Bukhari.].

## Kutoa Salamu

Mwisho wa Swala atatoa Salamu upande wake wa kulia na aseme: (Amani iwe juu yenu na rehema ya Mwenyezi Mungu) [ Imepokewa na Muslim.], na upande wa kushoto kadhalika.



Takbiri ya kufungia Swala



Kusoma suratul Fatiha



Kurukuu na kutoka kwenye Rukuu



Kusujudu na kutoka kwenye Sijida



Kukaa kitako baina ya sijida mbili







Kukaa kitako cha Atahiyatu ya Mwisho





Kutoa Salamu

## Miongoni mwa dua baada ya Swala

- ASTAGHFIRU LLAH (Namuomba Mwenyezi Mungu msamaha) (mara tatu), ALLAHUMMA ANTASSALAAM WAMINKA SSALAAM TABAARAKTA YAA DHAL’JALAALI WAL’IKRAAM (Ewe Mola! Wewe ni Amani, na amani inatoka kwako, Umetukuka, ewe Mwenye utisho na utukufu) [ Imepokewa na Muslim.].

(Hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu Peke Yake Asiye na mshirika. Ni Wake Yeye ufalme na Zake yeye sifa njema. Na Yeye

kwa kila kitu ni muweza. Ewe Mola! Hakuna mwenye kukizuia ulichokitoa, na hakuna mwenye kukitoa ulichokizuia, na haimnufaishi bahati ya mwenye bahati kukimbia) [ Imepokewa na Bukhari.].

(Hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu, Peke Yake, Asiye na mshirika. Ufalme ni Wake na sifa njema ni Zake, na Yeye kwa kila jambo ni muweza. Hapana hila wala nguvu isipokuwa kwa msaada wa Mwenyezi Mungu. Hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hatumuabudu isipokuwa yeye. Neema ni Zak na wema ni Wake, na ni Zake Yeye sifa njema, hapana Mola isipokuwa Mwenyezi mungu, hali ya kuwa sisi tunamtakasia Dini, ingawa makafiri wanachukia).

(Kutakasika ni kwa Mwenyezi Mungu, na sifa njema zote ni Zake, na Mwenyezi Mungu ni Mkubwa) (mara 33) (Hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu, Peke Yake, Asiye na mshirika. Ufalme ni Wake na sifa njema ni Zake, na Yeye kwa kila jambo ni muweza) [ Imepokewa na Muslim.]

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
NAMNA YA SWALAH YA IJUMAA

- (Ewe Mola! Nisaidie nikutaje, nikushukuru na nikuabudu vizuri) [ Imepokewa na Abu Daud.]
- Kusoma Ayatul Kursi, na sura ya Ikhlaas, na AL-Falaq na Al-Naas [ Imepokewa na Nasai.].
- Aseme: (Ewe Mola! Mimi nakuomba elimu yenye manufaa, riziki nzuri na matendo mema yenye kutakabaliwa) [ Imepokewa na Ibnu Majah.], baada ya kupiga Salamu ya Swala ya Alfajiri.

Maelezo:

Mwanamke ni kama mwanamume, sawa sawa, katika namna ya kuswali

# Hukumu za Swala

## 1. Swalah ya mwenye kukaa

### a. Katika Swalah ya Sunna:

Swala ya mwenye kukaa ni sahihi na thawabu zake ni nusu ya zile za mwenye kuswali kwa kusimama, kwa kuwa Mtume (S.A.W) alisema: (Akiswali kwa kusimama, basi hivyo ni bora. Na mwenye kuswali kwa kukaa basi thawabu zake ni nusu ya thawabu za mwenye kusimama. Na mwenye kuswali kwa kulala, basi thawabu zake ni nusu ya thawabu mwenye kukaa) [ Imepokewa na Bukhari.].

Na akiswali kwa kukaa kwa dharura, basi atapata thawabu kamili, kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Mja akiwa Mgonjwa au akiwa safarini, basi ataandikiwa thawabu mfano wa thawabu ya yale mema ambayo alikuwa akiyafanaya alipokuwa mjini na kuwa mzima) [ Imepokewa na Bukhari.].

### b. Katika Swalah ya Faradhi:

Mwenye kuswi kwa kukaa hali yakuwa anaweza kusimama swala yake haikubaliwi





## 2. Kutia nia

Miongoni mwa hukumu za nia:

1. Haifai kuikata nia katikati ya Swala. Yoyote mwenye kutia nia ya kukata Swala, basi Swala yake huharibika na analazimika kuianza upya.
2. Mwenye kufunga Swala ya Sunna haitafaa kuigeuza katikati yake kuifanya Swala ya faradhi.
3. Mwenye kufunga Swala ya fardhi akiwa ana swali peke yake kisha ikakimiwa Swala ya jamaa, inafaa aigeuze nia yake kuifanya ni Swala ya sunna na akamilishe rakaa mbili kisha apige Salamu na aswali pamoja na jamaa.

## 3. Kusoma Suratul Fatiha

Ni lazima kwa mwenye kuswali kusoma Fatiha, katika Swala ya kujihirisha (kusoma kwa sauti), hata kama ni maamuma. Ubadah bin Swamit  alisema: (Tulikuwa nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ katika Swala ya Alfajiri, akasoma Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, na kisomo kikawa kizito kwake. Alipomaliza Mtume ﷺ, alisema: (Huenda nyinyi mnasoma nyuma ya imamu wenu? Wakasema: 'Ndio, tunafanya hivyo, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu'. Akasema ﷺ: "Msifanye hivyo isipokuwa kwa Ufunguzi wa Qur'ani (Fatiha), kwani asiyeisoma huwa hana Swala) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## 4. Kusema ‹Aamiin›

Kusema ‹Aamiin' ni sunna kwa kila mwenye kuswali, awe ni imamu au maamuma au mwenye kuswali peke yake au mwenye kuswali faradhi au mwenye kuswali Swala ya sunna, ziwe ni katika swala za kusoma kwa siri au za kusoma kwa sauti.
Dalili yake ni neno la Mtume ﷺ: (Imamu akisema 'Aamiin', basi na nyinyi semeni 'Aamiin'. Kwani yoyote yule ambaye Amina yake imeafikiana na Amina ya Malaika, atasamehewa dhambi zake zilizotangulia) [Imepokewa na Bukhari.]

## 5. Vinyamazo vya imamu

1. Kinyamazo baina ya takbiri na kisomo kwa ajili ya dua ya kufungia Swala.
2. Kinyamazo baina ya Fatiha na Sura. Maamuma atasoma Fatiha katika vinyamazo vya imamu.
3. Kinyamazo baada kumaliza kisomo kabla ya kurukuu.

## 6. Kusoma kwa sauti wakati wa kukidhi Swala ya Faradhi, na Swala za sunna

Ikimpita Swala na akataka kuilipa: je, atasoma kwa siri au atasoma kwa sauti?
Linalozingatiwa ni ile Swala yenyewe, na sio wakati wa kuilipa, kwani lau anailipa Swala ya kusoma kwa sauti katika kipindi cha mchana, atatakiwa asome kwa sauti.
Sunna ni kusoma kwa siri katika Swala za sunna isipokuwa kunapokuwako dalili ya kusoma kwa sauti, kama vile Swala ya Tarawehe na Swala ya kupatwa kwa mwezi.

## 7. Kuinua mikono

Mikono huinuliwa katika sehemu zifuatazo:
1. Takbiri ya kufungia Swala.
2. Takbiri ya kurukuu.
3. Wakati wa kuinuka kutoka kwenye rukuu.
4. Wakati wa kuinuka baada ya kikao cha Atahiyatu ya kwanza.

## 8. Kuipata rakaa

Maamuma anapoiwahi rukuu pamoja na imamu, basi huwa ameipata rakaa, kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Mwenye kuwahi Rukuu, basi huyo ameipata Rakaa) [ Imepokewa na Abu Daud.].

## 9. Kujituliza

Kujituliza katika nguzo zote za Swala ni mojawapo ya nguzo za hiyo Swala ambayo bila hiyo Swala haiwi sahihi. Hii ni kwa hadithi iliyopokewa na Abu Hurairah kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ aliingia msikitini. Kisha akaja mtu akaingia akaswali, kisha akaja akampigia Salamu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ, na Mtume wa Mwenyezi Mungu

ﷺ akamrudishia salamu. Akasema kumwambia: “Rudi uswali kwani wewe hukuswali”. Yule mtu akarudi akaswali kama alivyoswali. Kisha akaja kwa Mtume ﷺ akampigia salamu. Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akasema kumjibu: “Na wewe salamu zikushukie” kisha akasema: “Rudi uswali kwani wewe hukuswali” [ Imepokewa na Bukhari.].

## 10. Kutingisha ulimi

Haitoshi katika kusoma Qur, ani, na kupiga takbiri na kutoa dhikri, kisomo cha moyoni, bali hapana budi kutamka. Na uchache wake ni kutikisa ulimi na mdomo kwa kisomo.

## 11. Namna ya kusujudu

Kusujudu kunakuwa kwa viungo saba kwa neno lake Mtume ﷺ: (Mja anaposujudu vinasujudu pamoja naye viungo saba: uso wake, vitanga vyake viwili vya mkono, magoti mawili yake na nyayo mbili zake) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].



## 12. Kuashiria kwa kidole

Sunna ni kuashiria kidole katika kikao cha Atahiyatu., kwa hadithi ya Waail bin Hujr: (Kisha akainua kidole chake nikamuona akikitingisha, akiomba dua kwacho) [Imepokewa na Nasai.].

Yasiofaa

- Kutowa sauti wakati wa kutia nia na kulazimisha kufuata nia wakati wa kupiga takbiri ya kufungia swala.

- Kuzidisha neno (Washukru) wakati wakusema (Rabbanaa walakal Hamdu) na ziada hii haikupokewa kutoka kwa Mtume (SAW)
- Kuzidisha neno la (Sayyidnaa) katika Attahiyatu, au katika kumswalia Mtume (SAW) Katika Swala
- Kuashiria kwa mkono wa kulia upande wa kulia na kwa mkono wa kushoto upande wa kushoto wakati wa kutoa salamu
- Kupeana mikono baada ya kuswali,na kusema Haram,na mwengine kusema Jama'an na Mfano wake
- Wanavo fanya baadhi ya wenye kuswali kusoma mmoja wao Ayatul kursi kisha kusema: Subhana llah na wao wakaleta nyuma yake Tasbihi
- Kupangusa Uso baada ya Dua na Dhikri

# Nguzo za Swala na Wajibu wake na Sunna zake

4.2

38031

Nguzo za Swalah

Ni sehemu zake za kimsingi ambazo Swala inatokana nazo, kwa namna isiyofaa kuziacha kwa hali yoyote ile. Hazipomoki kwa kukusudia wala kwa kusahau isipokuwa katika hali ya kutoweza.

1. Kutia nia
2. Kusimama katika swala ya faradhi pamoja na kuweza
3. Takbiri ya kufungia Swala
4. Kusoma Fatiha
5. Kurukuu
6. Kuitadili kwa kulingana sawa baada ya kurukuu
7. Kusujudu kwa viungo saba
8. Kukaa baina ya sijida mbili
9. Kukaa kwa Atahiyatu ya mwisho.
10. Kusoma Atahiyatu
11. Kumswalia Mtume ﷺ katika Atahiyatu ya mwisho.
12. Kutoa salamu
13. Kujituliza katika nguzo zote
14. Kutungamanisha baina ya nguzo

### Atafanya nini mwenye kuacha nguzo moja miongoni mwa nguzo za Swalah?

### 1. Mwenye kuacha nguzo kwa kusudi Swala yake inabatilika na inamlazimu kuirudia.

### 2. Mwenye kuacha kwa kusahau, basi ni moja wa hali mbili:

a. Asikumbuke kuwa yeye ameiacha nguzo hii mpaka baada ya kuifika pale mahali pake katika rakaa iliyofuatia. Basi hapa ile rakaa iliyopita ambayo aliiacha nguzo hiyo haitahesabiwa, na ataifanya rakaa hii ndiyo badala ya rakaa aliyoisahau, kisha atasujudu sijida ya kusahau118.

- Mfano wake: Mtu alikumbuka katika rakaa ya pili katika kusoma Fatiha kuwa yeye alisahau kusoma Fatiha katika rakaa ya kwanza. Hapa ataifanya rakaa yake hii kuwa ndio rakaa yake ya kwanza na ile iliyotangulia ataipuuzwa.

b. akumbuke kuwa alisahau nguzo kwenye rakaa, kabla hajafika kwenye mahali pa nguzo hiyo katika rakaa inayofuata. Hapa itamlazimu kurudia nguzo hiyo kwa haraka pale anapokumbuka.

- Mfano wake: Mtu alisahau kurukuu kisha akasujudu alipomaliza kisomo chake, kisha akakumbuka alipokuwa hali ya kusujudu kuwa bado hajarukuu. Basi huyu itamlazimu asimame arukuu kisha akamilishe Swala yake.

## Pili: Mambo ya wajibu katika swalah

### Mambo ya wajibu katika swala

Ni yale yanayoungwaungwa kwa sijida ya sahau na yanapomoka kwa kuyasahau

1. Takbiri za kuhamia kutoka kwenye kitendo kwenda kwenye kingine.
2. Kusema SUBHANA RABIYAL ADHIIM "Kutakasika ni kwa Mola wangu Mkubwa".
3. Kusema SAMI'A LLAHU LIMAN HAMIDA "Mwenyezi Mungu Amemsikia mwenye kumsifu" kwa imamu na kwa mswali pweke, ama maamuma hakuwekewa na Sheria kusema neno hilo.
4. Kusema RABBANAA LAKAL HAMDU "Mola wetu! Na sifa njema zote ni zako" katika kuitadili kutoka kwenye rukuu.
5. Kusema SUBHANA RABBIYAL A'LAA "Kutakasika ni kwa Mola wangu Aliye juu" katika sijida.
6. Kusema RABBIGH FIRLIY "Mola wangu ! nighufirie" baina ya sijida mbili.
7. Kukaa kikao cha Atahiyatu ya kwanza.
8. Kuleta Atahiyatu ya kwanza

### Atafanya nini mwenye kuacha jambo la wajibu miongoni mwa wajibu wa swalah ?

1. Mwenye kuiacha kwa kukusudia Swala yake inabatilika na itamlazimu kuirudia.
2. Mwenye kuiacha kwa kusahau, basi Swala yake ni sahihi, na atasujudu sijida mbili za sahau kabla hajapiga salamu.

## Tatu: Sunna za Swalah

Na kila kisichokuwa ni miongoni mwa masharti ya Swala, nguzo zake na mambo yake ya wajibu katika vile vilivyotajwa juu ya Namna ya Kuswali, basi hicho ni sunna ambao kuiacha hakuathiri katika usahihi wa Swala wala hailazimu kwa kuacha kusujudu sijida sahau.

Na sunna za Swala ni aina mbili:

### Kwanza: Sunnah za maneno

1. Dua ya ufunguzi wa Swala: Nayo ni dua inayosomwa kabla ya kusoma Fatiha.
2. Kuleta Audhu: nako ni kusema A'UDHU BILLAHI MINA SHETWANI RAJIIM (Najilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na Shetani aliyefukuzwa kwenye rehema ya mwenyezi Mungu).
3. Kuleta bismillahi nako ni kusema BISMILLAHI RRAHMANI RRAHIM (Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu).
4. Tasbihi iliyo zaidi ya moja katika kurukuu na kusujudu.
5. Maneno ya ziada baada ya kusema RABBIGH FIRLIY (Mola wangu nighufirie) baina ya sijida mbili.
6. Kisomo cha ziada baada ya RABBANAA LAKAL HAMDU (Mola wetu! Na sifa njema zote ni zako) baada ya kuinuka kutoka kwenye rukuu.
7. Kisomo cha ziada baada ya Suratul Faatiha

### Pili: Sunnah za vitendo

Nazo ni nyingi miongoni mwazo ni:

1. kuinua mikono pamoja na takbiri ya kufungia Swala, wakati wa kurukuu, kuinuka kutoka kwenye rukuu wakati wa kuinuka kwenda kwenye rakaa ya tatu.
2. Kuweka mkono wa kulia juu ya wa kushoto wakati wa kusimama kabla ya kurukuu na baada yake.
3. Kuangalia mahali pa kusujudu.

4. Kuiepusha mikono iwe kando na tumbo na mbavu wakati wa kusujudu.
5. Kukaa kikao cha iftiraash: nacho ni kukaa hali ya kuinua nyayo za mguu wa kulia na kuvielekeza vidole vyake kibla, hali ya kuweka mguu wa kushoto chini na kuukalia. Kikao hiki kimesunniwa katika vikao vyote vya Swala isipokuwa kikao cha Atahiyatu ya mwisho ya Swala ambayo rakaa zake zinapita mbili.
6. kikao cha tawarruk: nacho ni kukaa hali ya kusimamisha nyayo za mguu wa kulia na kuzielekeza vidole vyake kibla, na kuziweka nyayo za mguu wa kushoto chini ya muundi wa mguu wa kulia na kuzitoa nyayo upande wa kulia na kukalia kitako kwa kujitegemeza kalio la upande wa kushoto. Kikao hiki ni sunna kwa Attahiyatu ya mwisho ya Swala inayozidi rakaa mbili.
Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
Swalaah Za Sunnah Zinaswaliwa Rakaa Ngapi Ngapi?



Kiako cha iftiraash



Kikao cha tawarruk

# Yanayo faa, na yanayo chukiza, na yale yanayo vunja Swalah

## Kwanza: Yanayo faa katika Swalah

1. Kutembea katika Swala kwa tukio muhimu kwa sharti ya kutogeuka upande wa kibla kama kufunguwa mlango
2. Kubeba mtoto katika Swalah
3. Kuuwa nyoka na n'nge katika Swalah
4. Kuzunguka katika Swalah kwa dharura
5. Kulia katika Swalah
6. Kuleta tasbihi kwa wanaume na kupiga makofi kwa wanawake
7. Kumfunguza Imamu
8. Kuashiria kwa kidole kwa ajili ya kurudisha salamu au kwa mkono
9. Kutoa ishara ya kufahamisha kwa anae swali wakati akitokewa na haja
10. Kumshukuru Mwenyezi Mungu anapoona linalo kupelekea kufanya hivyo
11. Kutema mate na kohozi katika Swala upande wakushoto
12. Kumzuia anaepita mbele ya mwenye kuswali

## Pili: Yanayo chukiza katika Swalah

1. Mtu kuswali akiwa na mawazo mengi yenye kumshawishi, ama mbele yake kuna jambo la kushugulisha na swala yake, kama kujizua na haja ndogo ama kubwa ama upepo, au akiwa na njaa au kiyu ama kuwa mbele yake chakula anacho kipenda, au kutazama kitu kinacho mshughulisha na swala yake

2. Kufanya jambo lenye kukutowa kwenye unyenyekevu na utulivu katika swala, mfano kufanya harakati nyingi bila ya haja, na kuchezacheza na ndevu na nguo na kilemba na saa na kuvialisha vidole na kuvishikanisha na mfano wa hayo
3. Kuzunguka kwa uso katika Swala bila ya haja kwa sharti mwili uwe umeelekea kibla, lakini mwili ukitoelekea kibla swala itaharibika
4. Nakushika kiuno kwenye swala kama wanavofanya mayahudi
5. kuufunga mdomo na pua katika swala
6. Kukunja nguo kama mikono ya kanzu na mfano wake
7. Kuzifunga nywele kwa anaekuwa na nywele nyingi ili anapo sujudu zi sisujudu pamoja na yeye
8. Kutema mate ama kohozi mbele ya kibla au upande wake wa kulia
9. Kutizima mbingu
10. Kufumba macho bila ya haja
11. Kunyosha mikono wakati wakusujudu.

## Tatu: Mambo yanayo Haribu Swala

1. Kufanya jambo linalo pingana na sharti miongoni mwa sharti za swala kama kufanya jambo lenye kutenguwa twahara, au kukusudia kufunguwa uchi, au Kuzunguka upande wakibla, kwa mwili wake, au kuvunja nia
2. kukusudia kuacha nguzo au wajibu wa swala.
3. kujishughulisha na vitendo vingi kwa kitendo nje ya swala bila ya dharura kama kutembea na haraka nyingi
4. Kucheka na kujikohoza
5. Kuzungumza ndani ya Swala kwa kusudi
6. Kula na kunywa kwa kusudi.
7. Kuzidisha Rakaa au Nguzo kusudi
8. Maamuma kutoa salamu kabla ya imamu wake

# Sijida ya kusahau, kushukuru na kisomo

## Kwanza: Sijida ya sahau

### Maelezo kuhusu sijida ya kusahau

#### Sijida ya sahau

Ni sijida mbili ambzo mwenye kuswali anasujudu ili kuungaunga kasoro iliyopatikana katika Swala yake kwa ajili ya kusahau.

### Sababu za sijida ya kusahau

Sababu za kusujudu sijida ya kusahau ni tatu: kuwa na shaka, kuongeza na kupunguza.

### 1- Kufanya shaka

#### Kufanya shaka

Nako ni kuwa na shaka baina ya vitu viwili, ni kipi kilichotokea.
Kufanya shaka katika Swala kuna gawanyika mara mbili:

#### 1. Kufanya shaka baada ya kuswali:

Shaka hii haishughulukiwi.
- Mfano wake: Mtu alifanya shaka baada ya kuswali Alfajiri, Ameiswali rakaa mbili au tatu? Shaka hii haishughulikiwi, mpaka awe na yakini, hapo atafanya kulingana na yakini yake.

#### 2. Kufanya shaka akiwa ndani ya Swala:

Shaka hii ina hali mojawapo ya hali mbili:
a. Liwe na nguvu kwake yeye mojawapo ya mambo mawili:
Na hapa atafanya kile kilicho na nguvu kwake na atasujudu kwa kusahau baada Salamu.

Mfano wake: Mtu anaswali adhuhuri na akaifanyia shaka rakaa: je ni ya pili au ni ya tatu, lakini lililo na nguvu kwake ni kuwa ni ya tatu, hili litaifanya hiyo rakaa kuwa ni ya tatu na ataitimiza Swala yake, kisha atasujudu kwa kusahau baada ya Salamu.

Na dalili ya hilo ni kauli ya Mtume ﷺ: (Akifanya shaka mmoja wenu na ajitahidi kujuwa la sawa ni lipi, kisha atowe Salamu, kisha asujudu sijida mbili) [Imepokewa na Ibnu Hibbaan.].



Anatowa Salamu kisha Atasujudu sijida ya kusahau

b. Lisimdhihirikie katika mambo mawili, ni lipi lenye nguvu: Huyu atajengea juu ya kichache, hivyo basi atatimiza Swala yake na atasujudu sijida ya kusahau kabla ya Salamu.

Mfano wake: Mtu anaswali Adhuhuru akaifanyia shaka ile rakaa anayoiswali: ni ya pili au ya tatu? Kusiwe na uzito wa jambo lolote kati ya haya mawili. Basi huyu atajengea juu ya uchache na ataihesabu kuwa ni ya pili, na atatimiza Swala yake na atasujudu sijida ya kusahau kabla ya Salamu.

Na dalili ya hilo ni kauli ya Mtume ﷺ: (Akifanya shaka mmoja wenu katika Swala yake, asijue ameswali ngapi, tatu au nne, basi aitupilie mbali shaka yake na ajengee juu ya yakini yake kisha asujudu sijida mbili kabla hajapiga Salamu) [Imepokewa na Muslim.].



Anatowa Salamu kisha Atasujudu sijida ya kusahau

## 2. Kuzidisha

Nako ni kule kuongeza Rukuu au Sijida kwa mwenye kuswali… Na kuzidisha kuko namna mbili

### a. Awe mwenye kuswali ataikumbuka pale wakati wa kuzidisha.

Na hapo itamlazimu aiache ile ziada na atimize Swala yake kisha asujudu sijida ya kusahau baada ya kupiga Salamu.

- Mfano wake: Mtu anaswali Adhuhuri, akasimama kuleta rakaa ya tano kisha akakumbuka katikati. Hapa itamlazimu akae haraka na atimize Swala, kisha asujudu sijida ya kusahau baada ya kupiga Salamu.

### b. Awe mwenye kuswali akakumbuka baada ya kuifanya.

Huyu atatimiza Swala yake kisha atasujudu sijida ya kusahau baada ya kutowa Salamu. Na dalili yake ni hadithi ya Ibnu Mas›ud t kwamba Mtume ﷺ aliswali Adhuhuri rakaa tano.

Akaambiwa: “Je Swala imeongezwa?” Akasema: “Kwani kuna nini?” akaambiwa: “Umeswali rakaa tano”, akasujudu sijida mbili baada ya kuwa ashatowa Salamu ) [Imepokewa na Bukhari.].

## 3. Kupunguza

Nako ni kupunguza mwenye kuswali nguzo au wajibu miongoni mwa nguzo au wajibu za Swala.

## 1. Kupunguza nguzo

Iwapo nguzo hiyo ni takbiri ya kufungia Swala, basi Swala inabatilika, kwa kuwa itakuwa haikufungika tangu mwanzo. Na iwapo nguzo hiyo si takbiri ya kufungia Swala, basi hapo pana mojawapo ya hali mbili:

a. Ni aikumbuke mwenye kuswali baada ya kufikia mahali pa hiyo nguzo kwenye rakaa ifuatayo:

Hii inafuta ile rakaa ambayo nguzo hii iliachwa na inasimamisha rakaa ifuatayo mahali pake.

- Mfano wake: Mtu aliyesahau kurukuu katika rakaa ya kwanza, kisha akakumbuka naye yuko kwenye rukuu ya rakaa ya pili kuwa alisahau kurukuu kwenye rakaa ya kwanza.Mtu huyu ataizingatia rakaa ile kuwa ni rakaa ya kwanza na hataizingatia ile rakaa iliyotangulia, na atakamilisha Swala yake, kisha atasujudu kwa kusahau baada ya kutowa Salamu.



Anatowa Salamu kisha Atasujudu sijida ya kusahau

b. Aikumbuke mwenye kuswali kabla hajafikia mahali pa nguzo hiyo kwenye rakaa ifuatayo:

Hapa itamlazimu airudie ile nguzo iliyoachwa ailete na zile za baada yake, na ataikamilisha Swala yake, kisha atasujudu kwa kusahau baada ya Salamu.

- Mfano wake: Mtu alisahau sijida ya pili na kikao cha kabla yake katika rakaa ya kwanza, akakumbuka hilo baada kuinuka kutoka kwenye rukuu katika rakaa ya pili. Yeye atarudi kukaa na kusujudu, kisha ataikamilisha Swala yake, kisha atasujudu kwa kusahau baada ya Salamu.

## 2. Kupunguza jambo la wajibu:

Akisahau mwenye kuswali jambo moja la wajibu miongoni mwa mambo ya Swala ya wajibu basi hapo pana hali tatu tu:
a. Aikumbuke kabla hajaondoka pale mahali pa wajibu huo katika Swalah.
Na hapa ataileta huo wajubu na hatolazimika na jambo lolote.
b. Aikumbuke baada ya kuondoka pale mahali pa nguzo hiyo katika Swala kabla hajafika kwenye nguzo ifuatayo.
Na hapa atarudi aifanye nguzo hiyo na asujudu sijida ya kusahau baada ya kutoa Salamu.
c. Aikumbuke baada ya kufikia kwenye nguzo inayoifuatia.
Na hapa ataendelea na Swala yake na hatairudia na atasujudu kwa kusahau kabla ya kutoa Salamu.
Mfano wake: mtu aliinuka kutoka kwenye sijida ya pili ya rakaa ya pili ili ainuke kwenda kwenye rakaa ya tatu hali ya kusahau kikao cha Atahiyatu ya kwanza. Kisha akakumbuka kabla ya kusimama kuwa yeye amesahau kikao cha Atahiyatu. Basi huyu atajituliza akae kwa kikao cha Atahiyatu, kisha ataikamilisha Swala yake, na hatolazimiwa na jambo lolote.
Akiwa atakumbuka baada ya kuinuka na kabla ya kulingana sawa katika kusimama, atarudi akae na asome Atahiyatu, kisha akamilishe Swala yake, na asujudu kwa kusahau kabla ya kutoa Salamu.
Akikumbuka baada ya kulingana katika kusimama, kikao cha Atahiyatu hakimlazimu na kwa hivyo hatakirudia, atakamilisha Swala yake na atasujudu sijida ya kusahau kabla ya kutoa Salamu.
Na dalili ya hilo ni hadithi ya Abdullah bin Buhainah t kwamba Mtume ﷺ aliwaswalisha Adhuhuri akainuka katika rakaa mbili za kwanza bila ya kukaa, na watu wakainuka pamoja naye. Hata alipomaliza kuswali na watu wakamngojea kupiga Salamu, alipiga takbiri na hali yeye amekaa, akasujudu sijida mbili kabla ya kutoa Salamu, kisha akatoa Salamu) [Imepokewa na Bukhari].

Kwa yaliyotangulia inabainika kwetu sisi kwamba sijida ya kusahau inakuwa kabla ya kutoa Salamu na pia baada ya kutoa Salamu.




## Namna ya kusujudu sijda ya kusahau

Sijida ya kusahau ni kama sijida ya Swala, atapiga takbiri wakati wa kusujudu, na wakati wa kuinuka kutoka kwenye sijida, na atasema yale yanayo semwa katika sijida na kati ya sijida mbili.

## Maelezo

1- Akipiga Salamu mwenye kuswali kabla ya Swala kukamilika na asikumbuke isipokuwa baada ya kipindi kirefu, basi atairudia Swala upya, na akikumbuka baada ya kipindi kifupi kama dakika mbili tatu, ataikamilisha Swala yake na atasujudu kwa kusahau baada ya Swala.

2- Inamlazimu maamuma kumfuata imamu katika sijida ya kusahau hata kama alimfuata baada kusahau.

3- Ikikusanyika kwa mwenye kuswli sahau mbili, mahali pa mojawapo ni kabla ya Salamu na mahali pa pili ni baada ya Salamu, basi yeye atasujudu sijida ya kusahau mara moja kabla ya kuleta Salamu.



Takbiri ya kufungia Swala



Atasujudu sijida ya kusahau

## Pili: Sijida ya kushukuru

### Sijida ya kushukuru

Ni kusujudu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata neema au jambo la furaha au kuepukwa na jambo kuchukiza na mfano wake.

Na dalili ya kuwa Sijida ya kushukuru imewekwa na Sheria ni hadithi iliyopokewa na Abu Bakrah t kwamba Mtume ﷺ alikuwa likimjia jambo la furaha au akabashiriwa nalo hupomoka hali ya kusujudu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu [Imepokewa na Abuu Daud.].

### Namna ya sijida ya kushukuru

Ataleta takbiri hali ya kusujudu na aseme SUBHANA RABBIYAL A'ALAA (Kutakasika ni kwa Mola wangu Aliye juu kabisa) na amsifu Mwenyezi Mungu na amshukuru kwa neema Alizompa yeye, kisha ainuke kutoka kwenye sijida yake na asilete takbiri wala asipige Salamu.

## Tatu: Sijida ya kisomo

### Sijida ya kisomo

Ni sijida ambayo mwenye kusoma husujudu anapofika kwenye aya yenye Sijida.

Dalili ya kuwa Sijida ya kisomo imewekwa na Sheria ni hadithi iliyothubutu kutoka kwa Ibnu ‹Umar t kuwa alisema: (Mtume

alikuwa akitusomea sura yenye sijida na yeye akasujudu na sisi tukasujudu) [ Imepokewa na Bukhari.].

Kusujudu kunakuwa pale mwenye kusoma anapopita kwenye aya yenye sijida ndani ya Swala, iwe ni ya siri au ya dhahiri, au nje ya Swala. Na sijida yenyewe haishurutiswi kuwa na udhu.

## Namna ya kusujudu kwa kisomo

- Mwenye kusoma au kusikiliza Qur›ani atapiga takbiri kwa ajili ya kusujudu na aseme: (Kutakasika ni kwa Mola wangu Aliye juu kabisa), na aombe kwa kusema: (Uso wangu umemsujudia Yule Aliyeuumba, akapasua masikizi yake na maoni yake kwa uwezo Wake na nguvu Zake) [ Imepokewa na Tirmidhi.].

(Ewe Mola! niandikie kwa sijida hii malipo yaliyoko Kwako, na uniondolee kwayo dhambi, uijaalie ni akiba yangu kwako wewe, na uikubali kutoka kwangu mimi kama ulivyoikubali kutoka kwa mja wako Daud) [ Imepokewa na Tirmidhi.].

- Kisha apige takbiri na ainuke kutoka kwenye sijida, akiwa yuko katika Swala, na akiwa hayuko katika Swala, atainuka bila takbiri wala Salamu.

Aya zinazokusanya sijida za kisomo

| | |
|---|---|
| AL-A’raaf Aya (206) | Al-Furqaan Aya (60) |
| Ar-Raa’d A ya (15) | An-Naml Aya (25) |
| An-Nah’l Aya (49) | Assajda Aya (15) |
| Al-Israa Aya (107) | S’aad Aya (24) |
| Maryam Aya (58) | Fuss’ilat Aya (37) |
| Al- Hajj Aya (18) | Annajm Aya (62) |

| | |
|---|---|
| Al- Hajj Aya (77) | Al-Inshiqaaq |
| Al-A’laq | |

### Maelezo

1- Msafiri juu ya kipando akisoma aya ya Sijida, atashuka kwenye kipando chake na asujudu kwa kisomo. Likitomsahilikia hilo ataashiria kwa kichwa chake kusujudu.
2- Msomaji akiirudia aya ya sijida, inamtosheleza yeye kusujudu mara moja.
3. Si makosa kusujudu kwa ajili ya kisomo katika nyakati ambazo zimekatazwa kuswaliwa.
4- Iwapo msomaji hakusujudu, basi msikilizaji hatasujudu kwa kuwa yeye ni mfuasi wake na ni mwenye kumfuata katika kisomo.
5- Mwenye kumsikia msomaji bila kukusudia kumsikiliza, kama akiwa ni mpita njia au ameshughulika na jambo lingine, basi hatamfuata kwenye kusujudu kwa kuwa hakuwa akimfuata katika kisomo.

# Swala ya jamaa na Fadhla zake

## Hukumu ya Swala ya jamaa

Sheria imeamrisha Swala ya jamaa kwa wanaume wanaoweza na imemuonya mwenye kuiwacha. Na Mtume ﷺ alidhamiria kuwachoma wale wasioihudhuria. Alafu Mtume ﷺ hakumruhusu kipofu kuacha jamaa, na dalili ya hilo ni: ya

1. Neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka kuhusu Swalah ya Hofu: {Na ukiwa na wao na ukawasimamishia Swala, basi na lisimame jopo miongoni mwao..} (4: 102).
Mwenyezi Mungu Aliyetukuka hapa Ameamrisha kusimamisha jamaa katika hali ya hofu ya kivita na safari, basi katika hali ya amani na ukazi ni aula zaidi.
2. Hadithi iliyopokewa na Abu Hurarah t kwamba Mtume ﷺ alisema: (Swala nzito zaidi kwa wanafiki ni Swala ya Isha na Swala ya Alfajiri. Na lau wao walijua Yaliyomo kwenye Swala mbili hizo, wangaliziendea japo kwa kujikokota [ Habwan: kujikokota kwa kitako.]. Na mimi nilidhamiria kutoa amri Swala kukimiwa, kisha nimuamrishe mtu awaswalishe watu, kisha nitoke na watu wakiwa na matita ya kuni niwaendee wale watu wasiohudhuria Swala niwachomee nyumba zao kwa moto) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
Na Mtume ﷺ hadhamirii kuwachoma wale wasiohudhuria jamaa isipokuwa hiyo jamaa ni wajibu. Pia hawasifiwi wale wanaoacha kuhudhuria kwa unafiki, isipokuwa ni kwa uajibu wake.
3. Hadithii ya kipofu aliyemtaka ruhusa Mtume ﷺ aswali nyumbani kwake – na hana mtu wa kumuongoza njia-, na Mtume ﷺ akamwambia: (Je unasikia mwito wa Swala?) Akasema: ” Ndio”. Akasema: (Basi itikia) [Imepokewa na Muslim.].
4. Hadithi iliyothubutu kutoka kwa Ibnu Mas’ud t kwamba yeye alisema: (Mwenye kufurahika kukutana na Mwenyezi Mungu Kesho hali ya kuwa ni Muislamu, basi ajilazimishe na hizi Swala. Kwani zitatangwazwa. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Amemfaradhia Nabii wenu ﷺ nyendo za uongofu, na hakika hizi Swala ni miongoni mwa nyendo za uongofu. Na lau nyinyi mkiswali kwenye nyumba zenu kama anavyoswali nyumbani kwake huyu asiyehudhuria mgaliacha mwendo wa Nabii wenu, na lau mnaacha mwendo wa Nabii wenu

mgalipotea. Na hakuna mtu yoyote anayejitwahirisha vizuri Kisha akaukusudia msikiti mmoja kati ya hii misikiti isipokuwa Mwenyezi Mungu Atamuandikia, kwa kila hatua anayoipiga, jema moja, Anampandisha daraja moja na Anampomoshea dhambi moja. Hakika niliona vile tulivyokuwa hakuna anayeacha kuihudhuria jamaa isipokuwa mnafiki anayejulikana unafiki wake. Na alikuwa mtu akiletwa na huku ameshikiliwa baina ya watu wawili- yaani akijishikiliza na wao- mpaka akasimamishwa kwenye safu) [ Imepokewa na Muslim.].

## Hekima ya Swalah ya jamaa na Fadhla zake

1. Kujuana kwa ndugu na wanaopendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wao kwa wao na kutilia nguvu ushikano wa mapenzi baina yao, mambo ambayo imani haiwi isipokuwa kwa hayo. Kwani hakuna njia ya Imani wala ya Peponi isipokuwa kwa kupendana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Aliyetukuka.
2. Kuepukana mja na unafiki na Moto kwa aliyewahi takbiri ya kufungia Swala siku arubaini mfululizo, kwa hadithi aliyoipokea Anas kutoka kwa Mtume ﷺ: (Mwenye kuswali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu siku arubaini kwa jamaa, akawa anawahi takbiri ya kwanza, ataandikiwa kuwa mbali na Moto na kuwa mbali na unafiki) [ Imepokewa na Tirmidhi.].
3. Kukusanyika waislamu walio huku na kule na kuzizoweza nyoyo zao kheri na utengefu.
4. Kushikamana Waislamu na kusaidiana kwao baina yao.
5. Kudhihirisha ibada za Dini na nguvu yake.
6. Kuziunganisha nyoyo za Waislamu, kwa kumfanya mweupe na mweusi, Mwarabu na asiyekuwa Mwarabu, mkuu na mdogo, tajiri na masikini, wote wakawa pamoja ndani ya msikiti mmoja, nyuma ya imamu mmoja na katika wakati mmoja, wote wanaekelea kibla kimoja na muelekeo mmoja.

7. kuwatia hasira maadui wa Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa Waislamu bado wana nguvu iwapo wataendelea kutunza utekelezaji Swala misikitini.
8. Kufutiwa dhambi na kupandishwa daraja. Imepokewa na Abu Huraira t kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: (Je si niwajulishe kitu kinacho sababisha kufutiwa dhambi na Mwenyezi Mungu na kupandishwa daraja? Wakasema: "Kwani? Tujulishe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu" Akasema: "Nikueneza maji ya kutawadhia kwenye viungo, na kuwa na hatua nyingi za kwenda msikitini, na kungoja Swala baada ya Swala. Kwani huko ndiko kujitolea katika kusimamisha Dini) [ Imepokewa na Muslim.].
9. Swala ya jamaa ni bora kuliko Swala ya mwenye kuswali peke yake kwa daraja ishirini na saba. Ibnu 'Umar t amepokewa kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: (Swala ya jamaa ni bora kuliko Swalah ya mwenye kuswali peke yake kwa daraja ishirini na saba) [ Imepokewa na Bukhari.]

# Uimamu na Umaamuma

## Anayestahiki zaidi uimamu

Kwa mpango:
Kwanza: Msomi zaidi wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu: naye ni aliyekihifadhi zaidi na kuuzifahamu zaidi hukumu zake.

Pili: Mjuzi zaidi wa Sunna (mafundisho ya Mtume ﷺ: naye ni yule anayejua zaidi ya maana za hadithi zake na hukumu zilizomo ndani ya hizo hadithi.

Tatu: Mwenye kutangulia kugura (Hijra): Mwenye kutangulia kugura kutoka nchi ya kikafiri na kuenda nchi ya kisalmu. Naikiwa Hakuna hijra basi Mwenye kuhama machafu nakurudi kwa Mwenyezi Mungu

Nne: Mkuu zaidi wa miaka: Hapa ni iwapo kuna kulingana katika hayo yaliyopita.

Na dalili ya haya yaliyotangulia ni hadithi iliyopokewa na Ibnu Mas'ud al-Answari t kuwa alisema kwamba Mtume ﷺ alisema: (Atawaongoza watu katika Swala msomi zaidi wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Wakiwa wamelingana katika usomi, basi mjuzi zaidi wa Sunna miongoni mwao. Wakiwa wamelingana katika ujuzi wa Sunna ni yule aliyewatangulia katika hijra (kugura), na iwapo wamelingana katika kugura, basi ni yule aliyewatangulia katika Uislamu[ Silman: yaani Uislamu. Na katika riwaya nyingine: "sinnan"]) [Imepokewa na Muslim.].

Na unazingatiwa mpango huu itakikanapo kumuweka imamu wa msikiti au katika jamaa ya watu wasiokuwa na imamu ratibu (naye ni imamu maalumu wa kuswalisha katika msikiti). Ama msikiti ukiwa na imamu ratibu au imamu akawa ni mwenye nyumba, au akawa ni mtawala, [ Takrimah: kile kinachoandaliwa mgeni kukalia.], basi yeye atangulizwa mbele ya mwengine, kwa neno lake Mtume ﷺ: (Na mtu asiwe imamu wa mtu mwingine kwenye mamlaka yake, na aiskaye nyumbani kwake kwenye maandalizi yake isipokuwa kwa ruhusa yake) [Imepokewa na Muslim.].

## Kisimamo cha imamu na maamuma katika Swalah

1. Maamuma akiwa mmoja: Sunna ni asimame upande wa kulia wa imamu akiwa amekaribiana naye, kwa hadithi iliyopokewa na Ibnu ‘Abbas  kuwa alisema: (Niliswali pamoja na mtume ﷺ usiku mmoja nikasimama upande wake wa kushoto, na Mtume akashika kichwa changu kwa nyuma yangu akaniweka upande wake wa kulia) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

2. Jamaa iwapo ni ya watu wawili na zaidi: Imamu husimama mbele yao kati ya safu, kwa hadithi iliyopokewa na Jabir na Jabaar t kwamba mmoja wao alisimama upande wa kulia wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na mwingine upande wake wa kushoto. Jabir alisema: (Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akatushika mikono yetu pamoja akatusukuma mpaka akatusimamisha nyuma yake) [Imepokewa na Muslim.].

## Kisimamo cha mwanamke

1. Wanaposwali wanawake kwa jamaa, lililo sunna ni asimame imamu wao kati ya safu yao na asiwatangulie.

2. Mwanamke husimama nyuma ya mwanamume iwapo mwanamume ni imamu wake. Na akiswali na wanaume basi atasimama nyuma ya safu.

3. Iwapo wanaume na wanawake wanaswali jamaa, sunna ni wawe nyuma ya wanaume. Na safu zao huwa ni kama safu za wanaume. Abu Hurairah t amepokewa akisema kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: (Bora ya safu za wanawake ni zile zilizo nyuma ya safu, na shari ya safu za wanawake ni zile za mwanzo wake) [Imepokewa na Ibnu Majah.]



Swala ya wanawake




Mwanamke kuwa karibu ya mwanamume

## Miongoni mwa hukumu za kumfuata imamu

1. Haisihi kwa mtu aliye nyumbani kwake kumfuata imamu kupitia kusikia sauti yake kwa kipaza sauti au kupitia kusikiliza redio.
2. Inafaa kumfuata imamu kutoka nje ya msikiti iwapo safu zimeungana.
3. Inasihi kwa maamuma kumfuata imamu hata kama wako juu ya sakafu ya msikiti au wakawa chini ya imamu iwapo wanasikia sauti yake.
4. inafaa kwa mwenye kuswali faradhi kumfuata mwenye kuswali sunna au kinyume chake, mfano wa mwenye kuswali swala ya Isha nyuma ya mwenye kuswali Tarawehe, au kuswali pamoja na aliyepitwa na Swala ili apate thawabu ya Swala ya jamaa. Jabir bin Abdillaht amepokewa akisema kwamba Mu'aadh alikuwa akiswali pamoja na Mtume ﷺ kisha akiwajia watu wake akiwaswalisha) [Imepokewa na Bukhari.].



Kufuata kutoka nje ya msikiti

## Kumtangulia imamu

1. Amri ya Sheria ni kuwa maamuma amfuate imamu wake kwa kufanya kitendo anachofanya imamu wake papo kwa papo, kwa kauli ya Mtume ﷺ: (Imamu amewekwa afuatwe: akipiga takbri, na nyinyi pigeni takbiri, akirukuu na nyinyi rukuuni na akisujudu, na nyinyi sujuduni) [ Imepokewa na Bukhari na M.uslim.].

2. Imeharamishwa kumtangulia imamu, na Mtume alilitilia hilo makazo mkubwa kwa kusema: (Kwani haogopi mmoja wenu, anapoinua kichwa chake kabla ya imamu, Mwenyezi Mungu amgeuze kichwa chake akifanye kichwa cha punda au azifanye sura zake kuwa sura za punda) [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

3. Mwenye kumtangulia imamu wake kwa kusahau itamlazimu arudi amfuate.

Kuswali nyuma ya asiye na twahara

Swala Haisihi nyuma ya asiye na twahara [ Al-muhdith: ni asye na twahara.]., isipokuwa iwapo hakujulishwa kuwa hana udhu mpaka baada ya kumalizika Swala. Na katika hali hii inasihi swala ya maamuma, na ni juu ya imamu arudie Swala.

# Swala ya wenye nyudhuru (wasiojiweza)

## Maelezo kuhusu Nyudhuru

Nyudhuru
Ugonjwa, Safari na Hofu

## 1. Swala ya mgonjwa

Inamlazimu mngonjwa kutekeleza Swala kwa kadiri ya uwezo wake. Akiwa ataweza kuilipa kama mwenye afya itamlazimu afanye hivyo. Na akiwa hawezi, basi ataitekeleza kulingana na uwezo wake.
Mgonjwa anapaswa aswali kwa kusimama akiwa anaweza kusimama. Akiwa hawezi kusimama, basi ataswali kwa kukaa. Akitoweza kukaa, ataswali kwa ubavu na uso wake uwe umeelekea Kibla. Akitoweza kuswali kwa ubavu wake, ataswali kwa kulala kwa mgongo, na miguu yake iwe imeelekea kibla iwapo hilo ni sahali kwake, akitoweza kufanya hivyo basi ataswali kulingana na hali yake ilivyo.
Na dalili ya hayo yaliyotangulia ni neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Muogopeni Mwenyezi Mungu vile mnvyoweza} [64: 16].
Na neno lake Mtume ﷺ kumwambia ‘Imraan bin Huswain t:

(Swali kwa kusimama. Ukitoweza swali kwa kukaa. Na ukitoweza, swali kwa ubavu) [Imepokewa na Bukhari.].

### Miongoni mwa hukumu za Swala ya mngonjwa

1. Mgonjwa akiswali kwa kukaa na akawa anaweza kusujudu, itamlazimu kusujudu.

2. Akiswali kwa kukaa na asiweze kusujudu, basi ataashiria kwa mwili wake kwa kurukuu na kusujudu, na sijida yake iwe chini zaidi kuliko rukuu yake. Iwapo ni uzito kwake yeye kuashiria kwa mwili wake, basi ataashiria kwa kichwa chake.
3. Iwapo ni tabu kwa mngonjwa kujitwahirisha kwa kila Swala, au ikawa ni shida kuziswali Swala katika nyakati zake, basi inafaa akusanye baina ya Swala ya Adhuhuri na ya Alasiri, na baina ya Swala ya Magharibi na ya Isha katika wakati wa Swala ya kwanza au ya pili, kulingana na lile analoliona kuwa sahali zaidi kwake.
4. Mgonjwa harusiwi kuacha Swala kabisa madamu ana akili yake. Haifai kwa mngonjwa kudharau Swala, kwa hoja kuwa yeye ni mngonjwa, na ajitahidi awezavyo kutekeleza Swala.
5. Iwapo mgonjwa anakosa fahamu kwa siku kadha kisha anazinduka, ataswali anapozundukana kulingana na uwezo wake. Na haitamlazimu kuzilipa swala zilizompita akiwa hana fahamu. Lakini iwapo kukosa fahamu kwake ni kuchache kama vile siku moja au mbili – kwa mfano-, basi itamlazimu kulipa popote an anapopata nafasi kufanya hivyo.

Kurukuu
Kusujudu
Kupiga Takbiri
Kisomo

## 2. Swalah ya msafiri

Msafiri ameruhusiwa na Sheria kupunguza Swala za rakaa nne-nne (Adhuhuri, Alasiri na isha) kuzifanya rakaa mbili-mbili, pia kukusanya Swala ya Adhuhuri pamoja na Alasiri na ya Magharibi pamoja na Isha, kwa neno la Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka: {Na mkisafiri kwenye safari, si makosa kwenu nyinyi kufupisha Swala, mkiogopa kufitiniwa na makafiri, kwani makafiri kwenu nyinyi ni maadui walio wazi} [4: 101]
Na kwa hadithi iliyothubutu kutoka kwa Anas bin Malik t kwamba alisema: (Tulitoka pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu

ﷺ kutoka Madina hadi Makka, na akawa akatuswalisha rakaa mbili-mbili mpaka tukarudi) [Imepokewa na Nasai.].

## Makusudio ya Safari

Kila kinachoitwa safari kikawaida, basi hiyo ni safari ya kufaa kupunguza Swala





## Kupunguza Swala

1. Msafiri ataanza kupunguza Swalah baada ya kupita makazi ya mji anaokaa. Na haruhusiwi kupunguza Swala na hali yeye yuko kwenye mahali pa makao yake, kwa kuwa haikuthibiti kuwa Mtume ﷺ alipunguza swala isipokuwa baada ya kutoka kwake.

2. Msafiri anapowasili kwenye mji na akanuilia kukaa hapo siku nne au zaidi, basi itamlazimu kutimiza. Na akinuilia kukaa chini ya siku nne, ataruhusiwa kupunguza. Na iwapo hakunuilia kukaa muda maalumu, lakini akawa na lengo ambalo akilimaliza atarudi, basi huyo anafaa kupunguza, hata kama muda utapita siku nne.

3. Inamlazimu msafiri kutimiza anaposwali nyuma ya imamu ambaye ni mkazi wa mji, hata kama hakuwahi kuswali na yeye isipokuwa rakaa moja.

4. Anaposwali mkazi wa mji nyuma ya msafiri anayepunguza Swala, itamlazimu kutimiza Swala yake baada ya imamu kupiga Salamu.

## Kukusanya Swala mbili

1. Inafaa kwa msafiri na mgonjwa kukusanya baina ya Adhuhuri na Alasiri katika wakati wa Swala mojawapo. Akizikusanya katika wakati wa Swala ya kwanza itakuwa ni mkusanyo wa kutanguliza, na akizikusanya katika wakati wa Swala ya pili itakuwa ni mkusanyo wa kuahirisha.
2. Inafaa kwa anayeswali msikitini kujumuisha kukiwa na mvua yenye kusababisha usumbufu na matatizo. Ama anayeswali nyumbani kama vile wanawake, haruhusiwi kujumuisha.
3. Si lazima kujumuisha na kupunguza kuwe pamoja, kwani huenda akajumuisha na akafupisha, na huenda akajumuisha na asifupishe.

## Swala ya msafiri akiwa garini

## 1. Iwapo ni swala ya sunna:

Swala itakuwa sahihi, awe na udhuru au asiwe na udhuru, kwa hadithi iliyothubutu kwamba Mtume ﷺ alikuwa akiswali sunna juu ya mnyama popote anapoelekea) [ Imepokewa na Bukhari.].

## 2- Iwapo ni swala ya faradhi:

Swala itakuwa sahihi iwapo hawezi kushuka kuswali chini, au akawa atashindwa kupanda akishuka, au akawa anaogopa adui au mfano wake. Na kuswali juu ya kipando kuna namna kadha, miongoni mwazo ni:

a. kuwa anaweza kuelekea Kibla na anaweza kurukuu na kusujudu, kama akiwa ndani ya jahazi. Hapo itamlazimu kuswali kwa namna yake inayojulikana, kwa kuwa anaweza.

b. aweze kuelekea Kibla na asiweze kurukuu na kusujudu. Hapo itamlazimu kuelekea Kibla wakati wa kupiga takbiri ya kufungia Swala, kisha ataswali vile gari litakavyomuelekeza na ataashiria kwa kurukuu na kusujudu.



## 3. Swala ya hofu

Swala ya Hofu imewekwa na Sheria katika kila mapigano ya halali, mjini au safarini, Na dalili ya kuwa imewekwa na Sheria ni Qur›ani na Sunna:

1. Katika Qur'ani ni neno lake Aliyetukuka: {Na unapo kuwa pamoja nao, ukawasalisha, basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawe na wachukue silaha zao, na watakapo maliza sijida zao, basi na wende nyuma yenu, na lije kundi jengine ambalo halijasali, lisali pamoja nawe. Nao wachukue hadhari yao na silaha zao.} [4: 102].

2. Na katika Sunna ni kitendo cha Mtume ﷺ kwa kuwa yeye aliswali na maswahaba zake, pia waliiswali Swala hiyo baada yake.

### Namana ya kuswali Swala ya Hofu

Hofu ya vita haina athari yoyote juu upunguzaji idadi ya rakaa, Swala ikiswaliwa mjini huswaliwa kama ilivyo, na ikiswaliwa safarini hupunguzwa, isipokuwa namna yake ina tofauti. Na kuhusu namna ya kuiswali kuna njia kadhaa ambazo zote zinafaa.

### Na hofu yenye kupasisha Swala hii ina mojawapo ya hali mbili:

### Hali ya Kwanza: Hali ya kuogopa kushambuliwa na adui:

Inaswaliwa kwa namna mojawapo ya namna zilizokuja kutoka kwa Mtume ﷺ. Na namna iliyotangaa zaidi ni ile iliyokuja kwenye hadithi iliyopokewa na Sahl bin Abi Hathmah t. Nayo ni

kuwa imamu awagawanye makundi mawili. Kundi moja lisimame upande wa adui ili kulinda, na Kundi lingine litaswali pamoja na yeye rakaa moja. Anaposimama imamu kwenda kwenye rakaa ya pili, lile Kundi litanuilia kutomfuata imam na litajitimizia Swala yake na litatoa Salamu, kisha litakwenda upande wa adui kulinda. Hapo litakuja Kundi la kwanza, litaswali pamoja na imamu rakaa ya pili. Na imamu anapokaa kwa kikao cha Atahiyatu, watu wa Kundi lile watainuka na wajiswalie wenyewe, hali ya kuwa imamu anawangojea, na wanapomaliza kukaa kikao cha Atahiyatu imamu atapiga Salamu na wao.

### Hali ya pili: ni pale hali ya hofu ikizidi na ikitowezekana kuswaliwa kwa namna ya kawaida iliyowekwa na Sheria:

Katika hali hii wataswali wakiwa wanatembea kwa miguu au wanapanda wanyama na kuelekea Kibla ikiwezekana, na ikitowezekana, basi wataelekea upande wowote ule, kama alivyosema Ibnu ‹Umar t: (Kukiwa na hofu kubwa zaidi wataswali wakiwa wanatembnea kwa miguu au wanapanda, wawe wameelekea Kibla au hawakuelekea) [ Imepokewa na Bukhari.], na wataashiria katika kurukuu na kusujudu. Ataswali naye anatembea au amepanda ndege yake au kifaru chake kwa hali inayomkinika, kama ilivyo katika hali ya vita na mapambano au katika hali nyiginezo ambazo mtu hua hamakiniki kuswali kwa namna yake ya kawaida. Na inaashiria hukumu hiyo neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: (Mkiwa katika hali ya hofu, basi swalini mkiwa mnatembea kwa miguu au mko juu ya vipando) [2: 239].



Ataswali ndani ya kifaru



Ataswali ndani ya jahazi



Ataswali ndani ya ndege

Usahali na wepesi wa Sheria

Miongoni mwa sifa za Sheria Ya Uislamu za kipekee ni usahali na upesi na kuondoa dhiki. Na huu ni msingi ulioenea katika Sheria "Shida zinaleta usahali".

# NAMNA YA SWALAH YA IJUMAA

## Hukumu ya Swalah ya Ijumaa

Swalah ya Ijumaa ni wajibu kwa kila Muislamu, aliyebaleghe, asiye na udhuru wa kuiacha.
Dalili ya hilo:

1. Neno la Aliyetukuka: {Enyi mlioamini! Kukinadiwa Swala kwa siku ya Ijumaa, endeni kwa haraka kwenye utajo wa Mwenyezi Mungu, na muache biashara} [62: 9].

2. Neno la Mtume ﷺ: ( Hawatoacha watu kuhudhuria Ijumaa, au Mwenyezi Mungu Atapiga mihuri juu ya nyoyo zao, kisha wawe ni miongoni wa walioghafilika) [Imepokewa na Muslim].

## Wale ambao Ijumaa si lazima kwao

Swala ya Ijumaa haimlazimu mwanamke, mtoto mdogo, msafiri na mgonjwa ambaye atadhurika akiihudhuria, lakini inasihi kwa wote hao. Wakihudhuria pamoja na wengine itawatosheleza na wakitohudhuria, wataswali Adhuhuri.



Mwanamke



Mtoto mdogo



Mgonjwa



Msafiri

## Ubora wa siku ya Ijumaa

Siku ya Ijumaa ni bora ya siku za wiki ambayo Mwenyezi Mungu Amewahusu nayo Waislamu baada ya umma wengine kuwapotea. Na zimekuja hadithi nyingi kuhusu ubora wake, miongoni mwazo:

1. Neno lake Mtume ﷺ: ( Siku bora iliyotokewa na jua ni siku ya Ijumaa. Katika siku hiyo aliumbwa Adam, na katika siku hiyo alitiwa Peponi, na katika siku hiyo alitolewa humo) [Imepokewa na Muslim].


2. Amepokewa Abu Huraira t akisema kwamba Nabii ﷺ alisema: (Mwenye kuoga siku ya Ijumaa, akaswali alichokadiriwa kuswali, kisha akakaa kimya mpaka imamu akamaliza hutuba yake, kisha akaswali pamoja naye, atasamehewa dhambi zilizo baina ya siku ile na Ijumaa nyingine na nyongeza ya siku tatu) [Imepokewa na Muslim].

3. Amepokewa Abu Huraira t akisema kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alikuwa akisema: (Swala tano, na Ijumaa

mpaka Ijumaa, na Ramadhani mpaka Ramadhani vinafuta dhambi zilizo baina yake, iwapo mtu atajiepusha na dhambi kubwa) [Imepokewa na Muslim].

## Masharti ya kusihi Swalah ya Ijumaa

1. Wakati: Ijumaa haisihi kabla ya kuingia wakati wake wala baada ya kutoka wakati wake kama ilivyo kwa Swala nyinginezo. Na wakati wake ni wakati wa Swala ya Adhuhuri.
2. Ihudhuriwe na kundi la watu: Kwani haisihi kwa mtu mmoja. Na uchache wa jamaa ya Ijumaa ni watu watatu.
3. Kuwa mkazi: nako ni kuwa mtu ni mkazi wa kijiji kilichojengwa kwa mawe na vinginevyo miongoni mwa vitu vya kawaida vinavyotumiwa katika ujenzi wa makao, kisichohamwa kipindi cha kaskazi wala kusi. Ama watu wanaokaa majangwani na mahemani wanaohama mara kwa mara, Ijumaa inaswihi kwao lakini haiwalazimu.
4. Itanguliwe na hutuba mbili: kwa kuwa Mtume ﷺ alidumu nazo hutuba hizo.



Wakati wa Ijumaa



Inaswaliwa kwa jamaa



Watu wa majangwani

## Namna ya kuswali Swalah ya Ijumaa

Swala ya Ijumaa ni rakaa mbili na kisomo katika rakaa hizo husomwa kwa sauti.Na ni sunna kusoma katika rakaa ya kwanza- baada ya Fatiha- sura ya Al-Jum'ah, na katika rakaa ya pili – baada ya Fatiha- kusoma sura ya Al- Munaafiquun, au asome katika rakaa ya kwanza sura ya Al-A'laa na katika ya rakaa ya pili asome sura ya Al-Ghaashiah. [ Imepokewa na Muslim.].

## Hutuba mbili

### Hukumu ya hutuba mbili

Hutuba mbili ni wajibu, nazo ni mojawapo ya masharti ya kusihi Ijumaa. Na zitolewa kwa lugha ya Kiarabu, iwapo wengi wa waliohudhuria wanafahamu Kiarabu na waelewa maana yake kwa ujumla, ili kuhimiza kujifunza Kiarabu na kutoenda kinyume na uongofu wa Mtume ﷺ.

Na iwapo wengi waliohudhuria hawafahamu lugha ya Kiarabu, basi hapana makosa kuitoa kwa lugha nyiginezo, kwani la msingi katika hutuba ni kufundisha na kuongoza, si utoaji hutuba tu, lakini iwe pamoja na kuchunga uletaji aya za Qur›ani kwa lugha ya Kiarabu- ikimkinika- kisha kufasiri maana yake.

### Vikamilisho vya hutuba

Hutuba ya Ijumaa haina nguzo, isipokuwa hutuba inakuwa kwa kile kinachoitwa hutuba kikawaida. Lakini miongoni mwa vitu vinavyoifanya hutuba ikamilike ni vifuatavyo:

1. Kumsifu Mwenyezi Mungu.
2. Kuleta shahada mbili.
3. Kumswalia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ.
4. Kuusia watu kumcha Mwenyezi Mungu.
5. Kusoma sehemu ya Qur›ani.
6. Kuwaidhia.

### Sunna za hutuba mbili

1. Kuhutubu juu ya mimbari.
2. Kuwatolea watu salamu anapopanda mimbari.
3. Kupambanua baina ya hutuba mbili kwa mwanya mdogo.
4. Kuzifupisha hizo hutuba mbili.
5. Kuwaombea Waumini dua.

## Yanayokatazwa katika Swalah ya Ijumaa

1. Ni haramu kusema na imamu yuwahutubu siku ya Ijumaa, kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Ukimwambia mwenzako siku ya Ijumaa "Nyamaza" na imamu yuwahutubu, basi umecheza) [ Imepokewa na Bukhari.].
2. Ni karaha kuruka shingo za watu, isipokuwa awapo ni imamu au mtu awaruke watu kuenda kwenye mahali penye nafasi hawezi kuifikia isipokuwa kwa kufanya hivyo.

## Kuipata Ijumaa

Ni juu ya Muislamu afanye haraka kwenda Ijumaa mapema. Akichelewa kuhudhuria Swala na akaiwahi rukuu katika rakaa ya pili pamoja na imamu ataitimiza Swala kama ya Ijumaa. Na akitoiwahi rakaa ya pili. Basi ataitimiza kama Adhuhuri. Hivyo hivyo, mwenye kupitwa na Swala ya Ijumaa kwa sababu ya kulala au nyingine, basi ataiswali adhuhuri – yaani, ataiswali rakaa nne-

## Yanayo pendekezwa siku ya Ijumaa

1. Kusoma sura ya Al-Kahf siku ya Ijumaa, kwa kauli ya Mtume ﷺ: (Mwenye kusoma sura ya Al-Kahf siku ya Ijumaa

atapata mwangaza wa nuru baina ya Ijumaa mbili)
[ Imepokewa na Haakim.].

2. Kumswalia Mtume ﷺ kwa wingi. Alipokewa Abu Ms'ud al-Answari t kuwa Mtume ﷺ alisema: (Niswalieni kwa wingi siku ya Ijumaa, kwani hakuna yoyote atakayeniswalia isipokuwa nitaorodheshewa Swala yake) [Imepokewa na Haakim.].

Kuoga na kujipaka manukato, kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Mtu yoyote anayeoga siku ya Ijumaa, akajitwahirisha anavyoweza kujitwahirisha, akajipaka mafuta aliyonayo, au akajitia manukato ya nyumbani kwake, kisha akatoka asitie uhasama baina ya wawili, kisha akaswali kile alichoandikiwa kuswali, kisha akanyamaza kimya imamu anaposema, basi huyo atasamehewa dhambi zilizo baina ya Ijumaa ile na Ijumaa nyingine) [Imepokewa na Bukhari.].

## Maelezo kuhusu Ijumaa

1. Lililo sunna kuhusu mimbari iwe ni daraja tatu, kwa kumfuata Mtume ﷺ.



Minbari yenye daraja tatu

2. Si katika sunna kile kinachoitwa "suratul Jumu'ah" ambapo wenye kuswali wanakaa kumsikiliza msomaji kuwasomea baadhi ya aya za Qur'ani mpaka kuadhiniwa Swala ya ijumaa au kutoa nashidi na dhikri kwa pamoja kupitia vipazasauti.

3. Mwenye kuswali akihudhuria na imamu anahutubu, basi na aswali rakaa mbili fupi kabla hajakaa, kwa kauli ya Mtume ﷺ:

(Anapokuja mmoja wenu Ijumaa, basi na aswali rakaa mbili na azifupishe) [Imepokewa Ibn khuzema.].

4. Mweye kuhutubu ataomba akitumia kidole chake cha shahada, na hatainua mikono yake wakati wa kuomba dua isipokuwa katika kuomba mvua au kuomba mvua ikome. Huswain bin Abdurrahman t alipokewa akisema: (Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na yeye yuwahutubu, akiomba akisema hivi- akiaashiria kwa kidole chake cha shahada-) [Imepokewa na Ahmad.].



Ataashiria kwa kidole chake

5. Swala ya Ijumaa haina sunna ya kabla yake, lakini inapendekezwa aswali sunna ya kawaida kabla ya adhana, kwa kuwa Mtume ﷺ alisema: (Mwenye kuoga siku ya Ijumaa akajitwahirisha kwa anachoweza cha kujitwahirisha kisha akajipaka mafuta yake au akajitia manukato ya nyumnbani kwake, kisha akatoka kwenda Ijumaa, asiwafarakanishe baina ya watu wawili, na akaswali kile alichojaaliwa kuswali, na akanyamaza kimya imamu alipotoka kuja kuhutubu, basi atasamehewa dhambi baina ya Ijumaa ile na wiki nyingine) [Imepokewa na Daarimi.].

6. Sunna ya baada ya Ijumaa inaswaliwa rakaa mbili kwa hadithi iliyopokewa na Ibnu ‘Umar t kuwa alisema: (Alikuwa Mtume wa Mwenyezi ungu ﷺ akiswali rakaa mbili baada ya Ijumaa nyumbani kwake) [Imepokewa na Jamaa.],

au nne, kwa neno la Mtume ﷺ: (Atakayekuwa ni mwenye kuswali miongoni mwenu baada ya ijumaa, aswali rakaa nne) [Imepokewa na Muslim].
na lililo bora ni aziswali nyumbani kwake.
7. Idi na Ijumaa zinapokusanyika, kwa kutoka shakani ni aswali Idi na Ijumaa. Na akiswali Idi ni lazima, kwa uchache, aswali Adhuhuri. Na inaruhusiwa kwa watu wanaokaa mbali, wakiswali Idi, wasirudi kuswali Ijumaa. Amepokewa Iyaas bin Ramlah al-Shaami akisema: (Nilimshuhudia Mu'awia akimuuliza Zaid bin Arqam: "Je uliwahi kushuhudia pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ Idi mbili pamoja? Akasema: "Ndio. Aliswali Idi mwanzo wa mchana, kisha akatoa ruhusa kuhusu Ijumaa, akasema: 'Atakaye kukusanya, basi na akusanye) [Imepokewa na Ahmad.].

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:
Hukmu Ya Anayeswali Ijumaa Pekee Na Kuacha Swalaah Zilizobaki

# Swala ya Sunna

## Maana ya Swala ya Sunna (kujitolea)

Swalah ya Sunna
Swalah iliyowekwa na Sheria isiyokuwa ya lazima

## Fadhla za Swalah ya Sunnah

1. Swala ya sunna ni sababu ya mja kupendwa na Mwenyezi Mungu. Imekuja kwenye hadithi Alqudusiy kwamba Mwenyezi Mungu Aliyetukuka ansema: (Haachi mja wangu kuendelea

kujikurubisha kwangu kwa sunna mpaka nimpende, na ninapompenda nitakuwa ni masikizi yake ya kusikia na maangalizi yake ya kuonea na mkono wake wa kushikia na mguu wake wa kuendea, na akiniomba nitampa, na akijilinda kwangu nitamlinda) [Imepokewa na Bukhari.]

2. Swala ya sunna inaunga kasoro za faradhi. Mtume (s.a.w) amesema: (Kitu cha kwanza wanachohesabiwa kwacho Siku ya Kiyama miongoni mwa matendo ni Swala. Mwenyezi Mungu aliyetukuka, Atawaambia Malaika wake- na yeye ni mjuzi zaidi-: "Itizameni Swala ya mja wangu, je ameikamilisha au ameipunguza?" Iwapo imekamilika inaandikwa kuwa imekamilika, na ikiwa ina upungufu wa kitu, Atasema: "Tizameni, je mja wangu huyu ana sunna alizoziswali? Akiwa ana sunna, Atasema: Mkamilishieni mja wangu faradhi yake kutoka kwa sunna zake" ) [Imepokewa na Abu Daud.].

3. Swala ya sunna nyumbani ni bora zaidi

Swala ya sunna majumbani ni bora kushinda misikitini isipokuwa katika Swala ziliwekewa jamaa na Sheria kama Swala ya Tarawehe katika mwezi wa Ramadhani. Mtume (s.a.w) amesema: (Bora zaidi wa Swala ya mtu ni ile anayoiswali nyumbani kwake isipokuwa Swala ya faradhi) [Imepokewa na Bukhari.].

## Aina za Swala ya sunnah

Swala ya sunna ni aina nyingi: Muhimu zaidi ya hizo ni zifuatazo:

### Kwanza: Sunna za ratiba

Nazo ni sunna zenye kufuata Swala za faradhi

Na jumla ya sunna za ratiba ni rakaa kumi au rakaa kumi na mbili, nazo ni:

- Rakaa mbili kabla ya Alfajiri.
- Rakaa mbili kabla ya Adhuhuri au nne na rakaa mbili baada yake.

. Rakaa mbili baada ya Magharibi.

- Rakaa mbili baada ya Isha. Ibnu ‹Umar amepokewa akisema: (Nimehifadhi kutoka kwa Mtume (s.a.w) rakaa kumi: Rakaa mbili kabla ya Adhuhuri na rakaa mbili baada yake, rakaa mbili baada ya Magharibi nyumbani kwake, rakaa mbili baada ya Isha nyumbani kwake na rakaa mbili kabla ya Swala ya Asubuhi) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na imethubutu hadithi kama hii kutoka kwa ‘Aishah t isipokuwa yeye alitaja rakaa nne kabla ya Adhuhuri [Imepokewa na Muslim.].

| Sunna ya Qabliya | Swala za faradhi | Sunna ya Baadiya |
|---|---|---|
| Rakaa 2 | Alfajiri | —— |
| Rakaa 4 | Adhuhuri | Rakaa 2 |
| —— | Alasiri | —— |
| —— | Magharibi | Rakaa 2 |
| —— | Ishaa | Rakaa 2 |

Na bora wa sunna za ratiba ni ambazo Mtume (s.a.w) alidumu nazo mjini na safarini ni rakaa mbili za Alfajiri, kwa hadithi ya ‹Aishah t kwamba alisema: (Mtume ﷺ hakuwa akidumu na kitu chochote miongoni mwa sunna isipokuwa rakaa mbili za Alfajiri) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na imesunniwa kuzifanya fupi rakaa zake bila kuziharibu wajibu wake, kwa ilivyothubutu kutoka kwa Aishah t kuwa alisema: (Alikuwa Mtume (s.a.w) akizifupisha zile rakaa mbili za kabla ya Swala ya Asubuhi kwa kiasi kwamba nilikuwa nikisema: “Je amesoma Fatiha?”) [Imepokewa na Bukhari.].

Pia inafaa kuilipa Swala hiyo, kwa neno lake Mtume (s.a.w) : ( Asiyeswali rakaa mbili za Alfajiri, basi aziswali baada ya jua kuchomoza). [ Imepokewa na Tirmidhi.]

Maelezo

Imethubutu Ubora wa kuswali rakaa nne baada ya swala ya adhuhuri, kwa neno lake Mtume (s.a.w) : ( Mwenye kuswali kabla ya Adhuhuri rakaa nne na baada yake rakaa nne

Mwenyezi mungu atamuharamishia moto) [Imepokewa na Abu Daud.]
- Na katika Swala za Sunna zisizo tiliwa mkazo, ni kuswali rakaa nne kabla ya Alasiri, kwa neno lake Mtume (s.a.w) (Mwenyezi Mungu amrehemu mja alie Swali kabla ya Alasiri Rakaa nne) [ Imepokewa na Abu Daud.]
-Inafaa kuswali sunna zisizo kutiliwa mkazo, kabla ya Alasiri na Magharibi na ishaa, kwa neno lake Mtume (s.a.w) (Kati ya kila Adhana mbili kuna swala, alisema mara tatu na alisema mara ya tatu kwa anaetaka) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.]
Na makusudio ya Adhana mbili: ni Adhana na Ikama.
-Inafaa kukidhi swala ya sunna akitomakinika kuiswali kwa sababu ya usingizi ama kwa kusahau, hata kama ni wakati ulio katazwa kuswali, kwa ilivyo thubutu kutoka kwa Mtume (s.a.w) Aliposhughulishwa aliswali Sunna baadiya ya Adhuhuri baada ya swala ya Alasiri.

## Pili: Swala ya Witr

## Hukumu ya Swala ya Witri na Fadhla zake

Witri ni sunna iliyotiliwa mkazo. Mtume (s.a.w) anasema: (Hakika Mwenyezi Mungu ni Mmoja, Anapenda Swala ya Witri basi Swalini Witri enyi watu wa Qur'ani ) [Imepokewa na Abu Daud.].
Na alikuwa Mtume (s.a.w) akidumu nayo akiwa mjini na akiwa safarini

## Namna ya kuswali Witri

1. Uchache wa Swala ya Witri ni rakaa moja na wingi wake ni rakaa kumi na moja au kumi na tatu, anaziswali mbilimbili kisha anaswali moja ya kufanyia witri.
2. Na uchache wa ukamilifu ni rakaa tatu, ataswali rakaa mbili kisha atowe Salamu, kisha ataswali rakaa moja na atowe Salamu. Pia inafaa kwa mtu kuziswali hizo rakaa tatu kwa kikao cha Atahiyatu kimoja. Na inapendekezwa asome katika rakaa ya

kwanza baada ya Fatiha sura ya Al-A'laa na katika rakaa ya pili sura ya Al-Kaafiruun, na katika rakaa ya tatu sura ya Al-Ikhlas, kwa hadithi iliyothubutu kutoka kwa ubayy bin Ka'b t kuwa alisema: (Alikuwa Mtume ﷺ akisoma katika rakaa ya kwanza ya witri 'Sabbihisma Rabbikal A'laa', na katika ya pili 'Qul yaa ayyuhal kaafiruun', na katika ya tatu 'Qul Huwallaahu Ahad') [Imepokewa na Nasaai.].

## Wakati wa Witri:

Ni baada ya Swala ya Isha mpaka kutokea wakati wa Alfajiri. Na kuiswali kipindi cha theluthi ya mwisho ya usiku ni bora zaidi, kwa Hadithi ya Jaabir (RA) kuwa Mtume (s.a.w) alisema: (Atakaechele kutoamka mwisho wa usiku basi aswali witr mwanzo wake) [ Imepokewa na Muslim.], wala hatoswali tena witr, kwa neno lake Mtume (s.a.w) (Hakuna witri mbili katika usiku mmoja) [ Imepokewa na Abu Daud.].

Na Amesema tena (Atakae kuwa nahamu yakuamka mwisho wa usiku, basi aiswali witr mwisho wake, hakika Swala ya mwisho wa usiku inashuhudiliwa, na hilo ni bora) [Imepokewa na Muslim.].

## Dua Katika Witri:

Sheria imeweka dua katika rakaa ya mwisho ya Witri kabla ya kurukuu [ Imepokewa na Abuu Daaud.] au baada ya kuinuka kutoka kwenye rukuu [Imepokewa na Bukhari.].

Atainua mikono yake na aombe dua zilizopokewa, na miongoni mwa dua hizo ni: (Ewe Mola! Niongoze niwe miongoni mwa wale uliowaongoza, Unipe afya niwe miongoni mwa wale uliowapa afya, Uninusuru niwe miongoni mwa wale uliowanusuru, Unibarikie katika kile ulichonipa, Uniepushie shari ya kile ulichokadiria. Hakika Wewe unaamua na huamuliwi. Hakika hadhaliliki uliyemfanya rafiki wala hatukuki unaeteta naye. Zimekithiri kheri Zako, ewe Mola wetu, na Umetukuka) [Imepokewa na Tirmidhi.].

Na imamu aletapo kunuti wataitikia maamuma Aamin katika dua ya maombi, ama katika dua yakumsifu Mwenyezi Mungu watanyamaza kama asemapo Hakika Wewe unaamua na huamuliwi

## Maelezo

1. Sunna ni kusema baada ya Swala ya Witri: (Kutakasika ni kwa Mfalme Mtakatifu) [ Imepokewa na Ahmad.], mara tatu. Aivute sauti yake na aiinue juu mara ya tatu. Pia inafaa kuzidisha: (Mola wa Malaika na Jibrili) [Imepokewa na Tirmidhi.].
2. Kupangusa uso baada ya kuomba dua hakukuwekwa na Sheria, si katika Witri wala penginepo kwa kuwa hilo halikupokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w)
3. Nakunuti inafaa kwa mwaka mzima, wala haikhusishwi katika nusu ya mwisho wa mwezi wa ramadhani, na nisunna kukunutiwa katika swala za faradhi kunapo tokea majanga na kadhalika
4. Dua ya kukhitisha Dua ya kukhitimisha Qur’ani katika Swala haikuwekwa na sharia

Kuilipa Swala ya Witri mchana

Inafaa kulingana na Sheria kuilipa swala ya Witri kipindi cha mchana. Na inalipwa Rakaa mbilimbili, kwa hadithi iliyothubutu kutoka kwa ‹Aishah kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alikuwa ikimpita Swala ya usiku kwa sababu ya kuumwa au sababu nyigine, akiswali mchana rakaa kumi na mbili [ Imepokewa na Muslim.].

## Tatu: Swala ya Tarawehe

Tarawehe ni Swala ya usiku katika mwezi wa Ramadhani.
Na imeitwa Tarawehe kwa kuwa wao walikuwa wakipumzika baada ya kila rakaa nne kwa sababu ya urefu wa Swala

## Hukumu za Swala ya Tarawehe:

Tarawehe ni sunna iliyotiliwa mkazo, iliwekwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) katika mwezi wa Ramadhani tukufu, kwa kuwa Nabii (s.a.w) aliiswali na swahaba zake msikitini masiku kadha, kisha akaacha kuiswali kwa kuogopa isifaradhiwe

juu yao. Na maswahaba waliifanya baada yake ﷺ [Imepokewa na Muslim.].

## Idadi ya rakaa za Swala ya Tarawehe:

Lililo bora zaidi ni rakaa kumi na moja, kwa kuwa hiko ndicho kitendo alichokuwa Mtume (s.a.w) akikifanya zaidi, Kwa kauli ya ‘Aishah t alipoulizwa: “Ilikuwa namna gani Swala ya Mtume?” Akasema: (Hakuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akizidisha katika Ramadhani au miezi mingine kupita rakaa kumi na moja) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Maelezo

1. Swala ya usiku ni Sunna iliyotiliwa mkazo katika mwaka Mzima, Imekirihishwa kwa anayeswali usiku kuacha ada yake. Abdullah bin ‹Amr bin Al-›Aasw t alipokwea akisema kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema: (Ewe Abdullah! Usiwe kama fulani aliyekuwa akiinuka usiku kuswali kisha akaacha kuinuka usiku) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
2. Imependekezwa kwa mtu akizundukana kwa kuswali usiku amuamshe mke wake, kadhalika mwanamke amuamshe mumewe, kwa kauli yake Mtume (s.a.w) : ( Mtu akimwamsha mke wake usiku wakaswali rakaa mbili pamoja, wataandikwa kuwa ni miongoni mwa wanaume na wanawake wenye kumtaja Mwenyezi Mungu) [Imepokewa na Abuu Daaud].
3. Mwenye kushindwa na usingizi katika Swala ya usiku, basi aiache Swala na alale mpaka usingizi umuondokee. ‘Aishah t alipokewa akisema kwamba Nabii (s.a.w) alisema: (Akisinzia mmoja wenu katika Swala, basi na alale mpaka usingizi wake umuondokee) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].



Kuamka kwa ajili ya Swala

4. Imependekezwa kuleta istighfari na kuomba dua katika theluthi ya mwisho ya usiku, kwa hadithi iliyopokewa na Abu Huraira t kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) amesema: (Anateremka mwenyezi Mungu kwenye uwingu wa karibu katika kipindi cha theluthi ya usiku ya mwisho na Anasema: “Ni nani aniombae nimkubalie? Ni nani anayeniomba msamaha nimsamehe?) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Kuswali Tarawehe kwa nia ya Ishaa

Mwenye kuchelewa kuswali Ishaa, alipohudhuria akawakuta watu wanaswali Tarawehe, basi ataswali pamoja nao kwa nia ya Ishaa, na imamu akipiga Salamu atainuka kutimiza Swala yake.

## Nne: Swala ya Dhuha

Nayo ni Swala iliyowekwa na sheria kuswaliwa kipindi cha mwanzo wa mchana.

## Wakati wa Swala ya Dhuha

Na Wakati wa Swala ya Dhuha: Ni kuanzia pale jua linapochomoza na kuangatika kadiri ya uti wa mkuki. Kuangatika huku kunakuwa ni kiasi cha theluthi ya saa mpaka kipindi cha kabla ya jua kupinduka kwa uchache, wa robo saa au theluthi yake, na ubora wawakati ni pale jua linapokuwa kali zaidi.

## Ubora wa Swala ya Dhuha:

Amesema Mwenyezi Mungu katika Hdithi qudsi (takatifu): (Ewe mwanadamu! Swali kwa ajili yangu rakaa nne mwanzo wa

mchana, nipate kukutosheleza mwisho wake) [Imepokewa na Muslim.].

## Idadi ya rakaa za Swala ya Dhuha:

Yafaa kuswaliwa rakaa mbili au Nne au Sita au Nane, kwa kuwa Mtume (s.a.w) alifanya hivyo.

Na mwenye kuswali rakaa Nne Mwenyezi mungu atamtosheleza siku yake, Amepokea Nuaym bin Hammazi Al-ghatwafaniy kutoka kwa Mtume (s.a.w) Kutoka kwa Mola wake alietukuka kwamba yeye amesema (Ewe mwanadamu Swali kwa ajili yangu rakaa nne mwanzo wa mchana nitakutosheleza mwisho wake) [ [ Imepokewa na Ahmad.]

Na mwenye kuiswali baada ya kuswali Alfajiri kwa jamaa na akakaa kumtaja Mwenyezi Mungu mpaka jua likachomoza basi ataandikiwa ujira wa hijja na umra iliyo timia Amesema Mtume (s.a.w) (Mwenye kuswali swala ya asubuhi kwa jamaa kisha akakaa kumtaja mwenyezi mungu mpaka jua likachomoza kisha akswali rakaa mbili basi huandikiwa ujira wa hijja na umra ) akasema Mtume (iliyotimia iliyotimia iliyotimia) [Imepokewa na Tirmidhi na imeswahihiswa na Albaani katika Swahihul Jaami'i]

## Tano: Swala ya Kuamkia Msikiti

Nayo ni rakaa mbili imewekewa yule aliyeingia msikitini kabla hajakaa.

## Na hukmu yake

Na hukmu yake ni sunna iliyo tiliwa mkazo sana.

Na Dalili yake ni kauli ya Mtume (s.a.w) : (Akiingia mmoja wenu msikitini, basi aswali rakaa mbili kabla hajakaa) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na inatosheleza badala yake sunna inayofuatana na faradhi. Mwenye kuingia msikitini kwa kuswali adhuhuri- kwa mfano- akaswali sunna ya adhuhuri itamtosheleza, na hatatakiwa kuswali Swala ya kuuamkia msikiti.

## Sita: Swala ya Kutaka Ushauri(swalatul istikharah)

Nayo ni rakaa mbili ambazo mtu ataziswali anapokuwa katika hali ya kutoamua katika jambo, kabla ya kuchukua uamuzi juu yake, na huombwa Dua baada yake Na Mtume (s.a.w) alikuwa akiwafundisha Maswahaba Swala hiyo kama alivyokuwa akiwafundisha sura ya Qur›ani.

## Dua ya Swala ya Kutaka Shauri

## (swalatul istikharah):

Amesema Mtume(s.a.w) (Akiwa na nia mmoja wenu ya kufanya jambo, basi na aswali rakaa mbili zisizokuwa za faradhi, kasha aseme: "Ewe Mola! Hakika mimi nakutaka shauri kwa ujuzi wako, nakuomba kwa uwezo wako na ninakuomba fadhila zako zilizo kubwa. Kwa hakika wewe unaweza na mimi siwezi, na unajua na mimi sijui, na wewe Ndiye Mjuzi wa ghaibu zote. Ewe Mola! Iwapo kwenye ujuzi wako wewe, jambo hili lina kheri na mimi katika dini yangu, maisha yangu na mwisho wa jambo langu, au alisema 'mambo yangu ya sasa na ya baadae' basi nikadiria na unifanyie sahali kisha unitilie baraka katika jambo hili. Na ikiwa kwenye ujuzi wako jambo hili lina shari na mimi katika Dini yangu, maisha yangu na mwisho wa jambo langu, au alisema 'katika mambo yangu ya sasa na ya baadae' niepushe nalo na liepushe na mimi. Na unikadirie kheri yote mahali iliyopo, kisha niridhishe nalo". asema 'Kisha aitaje haja yake') [ Imepokewa na Bukhari.].

Alama ya Swala yakutaka Ushauri

Si makosa kukariri Utakaji ushauri, na sio sharti kwa mtaka shauri aone ndoto ya kumbainishia jambo alilolitakia Shauri. Litakikanalo ni kwamba afuate jambo alilolichagua na ambalo alimtaka Shauri Mwenyezi Mungu kwalo, lisiwe ni jambo la dhambi na la kukata kizazi. Likitimia, basi ndio kheri, na lisipotimia hiyo pia ndio kheri.

## Saba: Kuswali Rakaa mbili baada ya Kutawadha

Kwa kuwa ilithubutu kutoka kwa Abu Huraira t kwamba Mtume (s.a.w) alimwambia Bilal wakati wa Swala ya Alfajiri: (Ewe Bilal! Nihadithie juu ya tendo jema ulilolifanya katika Uislamu unalolitarajia zaidi, kwani mimi nilisikia mchakato wa viatu vyako [ Daff na'laika: sauti ya viatu vyako.] Peponi) Akasema: (Sikufanya tendo jema lolote ninalolitarajia zaidi isipokuwa mimi wakati wowote ninapojitwahirisha ninaswali kwa utwahara huo vile ninavyokadiriwa, iwe ni kipindi cha mchana au usiku) [Imepokewa na Bukhari.].

### Nane: Swala ya Sunna Huru

Nayo ni Swala isiyofungamana na wakati wala sababu.

Na Swala ya sunna iliyoachiliwa inaruhusiwa kuswaliwa wakati wowote isipokuwa kwenye nyakati ambazo kuswali kumekatazwa.

### Mifano ya Sunna Iliyoachiliwa (Swala ya usiku) Qiyaamul-Layl

Mtume (s.a.w) alisema: (Bora wa Swala baada ya faradhi ni Swala ya Usiku) [ Imepokewa na Muslim.].

Na pia alisema (s.a.w) : (Hakika Peponi kuna Vyumba huonekana nje kutoka ndani yake, na ndani yake kutoka nje yake). Akainuka Mbedui akasema "Ni vya nani hivyo?" Akasema: (Ni vya anayesema maneno mazuri, na akalisha chakula, na akadumu kufunga na akaswali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu usiku na ilhali watu wamelala) [ Imepokewa na Tirmidhi.].

Kuinuka usiku kuswali katika utabibu

Kuinuka usiku kuswali kunapelekea kupunguza utoaji wa homoni ya kotisoni (cortisone)- nayo ni kotisoni ya kitabia ya mwili- hasa kabla ya kuamka kwa masaa kadha, kipindi hicho kinalingana na wakati wa kula daku (theluthi ya mwisho ya usiku). Homoni hiyo inazuia kuongezeka kighafula kiasi cha sukari ya damu, jambo ambalo linaleta hatari kwa wagonjwa kisukari.

## Nyakati Ambazo zimekatazwa Kuswali

1. Kuanzia baada ya Swala ya Alfajiri mpaka kuchomoza jua na kuangatika kiasi cha urefu wa mkuki, ambao kwa kawaida inakuwa ni kiasi cha theluthi ya saa
2. kuanzia kipindi cha jua kuwa limesimama katikati mpaka lipinduke.
3. Kuanzia baada Swala ya Alasiri mpaka jua lizame.

Na dalili yake ni hadithi iliyopokewa na ‹Uqbah bin ‹Amir kuwa alisema: (Nyakati tatu, alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu akitukataza kuswali, au kuzika[ Naqbura: twazika.] maiti zetu: wakati jua likichomoza [ Baazighah: wazi.] hadi liangatuke, wakati wa katikati ya mchana mpaka jua lipinduke na wakati jua linapopindukia[ Tudhayyafu: linapindukia.] kuchwa mpaka lizame) [ Imepokewa na Muslim.].

Swala zenye Sababu Katika Nyakati za Makatazo

Inafaa kuswali Swala zenye sababu – iwe ni sababu yoyote, kama vile Swala ya kuuamkia msikiti, na Swala ya Jeneza- hata kama ni katika nyakati za makatazo.



# Swala ya Kuomba Mvua

## Maana ya Swala ya kuomba Mvua

### Kuomba Mvua

Ni kuomba kunyeshe mvua, kutoka kwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, kipindi cha ukame na uchache wa mvua.

## Dalili ya Usheria wa Swalah ya Kuomba Mvua

Swalah ya kuomba mvua ni sunnah iliyotiliwa mkazo kwa kitendo cha Mtume ﷺ, kama ilivyo kwenye hadithi iliyopokelewa na Abdullah bin Zaid t kwamba Mtume ﷺ alitoka kwenda kwenye kiwanja cha kuswali akaomba mvua, akaelekea Kibla, akageuza kishali chake na akaswali rakaa mbili) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Wakati wa Swala ya Kuomba Mvua

Wakati uliowekwa na Sheria wa Swala ya kuomba mvua ni ardhi inapokuwa kavu na mvua kutonyesha, au yanapokuwa machache maji ya chemchemi na visima, au mito ikakauka na mfano wake. Inapendekezwa ifanyike baada ya jua kuchomoza na kufikia kadiri ya mkuki na wakati huo kwa kiasi ni baada ya kuchomoza jua kwa dakika ishirini kama vile Swala ya Idi.

## Mahali pa kuswali Swalah ya Kuomba Mvua

Lililo la sunna ni iswaliwe uwanjani na sio msikitini, kwa hivyo ndivyo alivofanya Mtume ﷺ isipokuwa kwa dharura.

## Namna ya kuswali Swala ya Kuomba Mvua

1. Swala ya Kuomba Mvua ni rakaa mbili, bila ya kuadhini wala kukimu, na kisomo katika rakaa mbili hizo huwa ni kwa sauti.
2. Mwenye kuswali katika rakaa ya kwanza atapiga takbiri saba baada ya ile takbiri ya kufungia Swala. Na katika rakaa ya pili atapiga takbiri tano, mbali ya ile takbiri ya kuinuka kutoka kwenye sijida.
3. Mwenye kuswali atainua mikono yake katika kila takibiri, atamhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifu na atamswalia Mtume ﷺ baina hizo takbiri.
4. Baada ya kuswali imamu atahutubu hutuba moja, atakithirisha kuomba msamaha na kusoma Qur›ani katika hiyo hutuba. Kisha ataomba kwa wingi dua zilizopokewa, pamoja na kukariri na kurudia maombi na kuonyesha unyonge, uhitaji na umasikini kwa

Mwenyezi Mungu aliyetukuka, na ainuwe mikono yake upeo wa kuinua.

5. Imamu ataelekea Kibla, atageuza kishali chake, kilicho kuliani akiweke kushotoni na kilicho kushotoni akiweke kuliani, na ataendelea kuomba baina yake yeye na Mola wake.

## Miongoni mwa hukumu za Swalah ya Kuomba Mvua

1. Itanguliwe na mawaidha na kuwakumbusha watu yale yatakayolainisha nyoyo zao kwa kutaja kutubia kutokana na maaswia na kujisafisha na dhuluma kwa kuwarudishia watu haki zao, kwani maaswia ni sababu ya kuzuiliwa mvua, na kutubia, kuomba msamaha na kumcha Mwenyezi Mungu ni sababu ya kukubaliwa dua na ni sababu ya kupata kheri na baraka. Awahimize wao kutoa sadaka, kwani utoaji sadaka ni sababu ya kupata rehema.

2. Imamu aiweke siku ya kutoka kwenda kuswali, ili watu wajitayarishe kwa hiyo Swala.

3. Imesunniwa kutoka kwenda kuswali kwa unyenyekevu, utiifu, unyoge na kujidhalilisha pamoja na kuonyesha uhitaji kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo Swala hiyo haikuwekewa kujitengeza na kujitia manukato kwa ajili yake. Ibnu 'Abbas t amesema katika kusifu kutoka kwa Mtume ﷺ kwenda kuomba mvua: (Hakia Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alitoka akiwa amevaa nguo takavu [ Almutabadhdhil: Anayeacha pambo na vazi zuri], hali ya kunyenyekea na kujidhalilisha mpaka akafika mahali pa kuswali) [ Imepokewa na Abu Daud.]

4. Kutaka msamaha na kuomba dua kwa wingi pamoja na kuinua mikono katika hutuba ya Kuomba Mvua.

## Linalopendekezwa wakati mvua inaponyesaha

Inapendekezwa, mvua inaponyesha kwa mara ya kwanza, kusimama na kujitia mvuani, kwa kuwa Mtume ﷺ alifanya hivyo

katika hadithi iliyopokewa na Anas t akisema: (Tulinyeshewa na mvua na sisi tuko na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ. Asema: Mtume ﷺ akafunua nguo yake mpaka mvua ikampiga. Tukasema: ”Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwa nini umefanya hivo?” Akasema ﷺ kwa kuwa imepitiwa na muda mchache kutoka kwa Mola wake”) [Imepokewa na Muslim.].

Mvua ni kheri inayotoka kwa Mwenyezi Mungu Peke Yake

Muislamu ni lazima aamini kwamba mvua inateremka kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na rehema Zake kwa waja Wake, na sio kama baadhi ya watu wanaosema: «Tumeteremshiwa mvua kwa sababu ya nyota kadha wa kadha» Huu ni ushirikina, tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu nao.

# Swalah ya kupatwa Jua na kupatwa Mwezi

## Maana ya kupatwa jua na Mwezi

Kupatwa Jua

Kuondoka mwangaza wa jua au baadhi yake mchana

Kupatwa Mwezi

Kuondoka nuru ya mwezi au baadhi yake Usiku

## Hekima ya Kupatwa Jua na kupatwa Mwezi

Jua na Mwezi ni alama mbili miongoni mwa alama za Mwenyezi Mungu, Anawatisha kwavyo waja wake mpaka warudi Kwake.

Mtume ﷺ Alisema: (Hakika jua na mwezi havipatwi kwa kufa mtu wala kwa kuishi kwake, lakini hivyo ni alama mbili miongoni mwa alama za Mwenyezi Mungu, huwatishia kwavyo waja Wake, basi vinapopatwa kimbilieni kuswali). [ Imepokewa na Abu Daud.]

## Hukumu ya Swalah ya kupatwa jua na ya kupatwa mwezi

Ni sunna iliyokokotezwa (iliyotiliwamkazo) kwa kauli ya Mtume ﷺ: (Hakika jua na mwezi ni alama mbili miongoni mwa alama za Mwenyezi mungu, havipatwi kwa kufa mtu wala kuhuika kwake. Basi mkiona hilo muombeni Mwenyezi Mungu. Mpige takbiri, mswali na mtoe sadaka) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Wakati wa Swalah ya kupatwa jua na kupatwa mwezi

- Wakati wa Swalah ni kuanzia kupatwa jua au mwezi mpaka kumalizika kwake.
- Na mwenye kuswali atatimiza swala yake hata kama kupatwa kwa jua au kwa mwezi kumemalizika. Na hatorudia Swala akiwa amemaliza kuswali na kupatwa kwa jua au kwa mwezi hakujamalizika, bali Waislamu wataendelea kuomba dua na kuleta istighfari.

## Namna ya Swalah ya kupatwa Jua na kupatwa Mwezi

Amepokewa ‹Aisha t akisema: (Lilipatwa jua wakati wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ na Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akawaswalisha watu. Akasimama na akakirefusha kisimamo. Kisha akarukuu na akairefusha rukuu. Kisha akainuka kusimama akakirefusha kisimamo lakini kikawa


chini ya kisimamo cha kwanza. Kisha akarukuu na akairefusha rukuu lakini ikawa chini ya rukuu ya kwanza. Kisha akasujudu na akairefusha sijida. Kisha akafanya katika rakaa ya pili kama alivyofanya katika ya kwanza. Kisha akamaliza na hali jua lishaachwa. Hapo akawahutubia watu, akamhimidi Mwenyezi Mungu na akamsifu kisha akasema: 'Jua na mwezi ni miongoni mwa alama za Mwenyewzi mungu. Havipatwi kwa kufa yoyote wala kuhuika kwake. Basi mkiona hilo, Muombeni Mwenyezi Mungu, mpige takbiri, mswali na mtoe sadaka') [Imepokewa na Bukhari.].

Na kulingana na hayo, itokeapo kupatwa kwa jua au kupatwa kwa mwezi:

1. Kutaitwa kuswaliwa kwa kusema: SWALAATU JAAMI'A "Haya imesimama Swala ya jamaa"
2. Watu wakikusanyikana, imamu atawaswalisha rakaa mbili ndefu, atainua sauti kwa kisomo, asome katika rakaa ya kwanza Fatiha, kisha asome sura ndefu. Kisha atarukuu na airefushe hiyo rukuu. Kisha ainuke na aseme: SAMI'ALLAHU LIMAN HAMIDA (Mwenyezi Mungu Amemsikia Aliyemsifu. Mola wetu! Sifa njema ni zako). Kisha asome Fatiha na sura ndefu, lakini fupi kuliko ile ya mwanzo. Kisha arukuu na airefushe rukuu hiyo, lakini fupi kuliko ya kwanza. Kisha ainuke na huku yuwasema: SAMI'ALLAHU LIMAN HAMIDA (Mwenyezi Mungu Amemsikia Aliyemsifu. Mola wetu! Sifa njema ni zako) kisha atasujudu sijida mbili ndefu, na atakaa baina ya sijida mbili wala asirefushe kikao, kisha atasimama kutoka sijida ya pili kwa Takbiri na ataswali rakaa ya pili sawa na rakaa ya kwanza kwa kisimamo chake na rukuu zake na sijida zake lakini sio ndefu kama rakaa ya kwanza, kisha atakaa tashahud nakusoma attahiyatu kisha atatowa salamu

## Sunna za Swalah ya kupatwa Jua na Mwezi

1. Iswaliwe kwa jamaa, na akiswali kila mmoja peke yake si makosa.
2. Iswaliwe msikitini, na si makosa kwa wanawake kutoka kwenda kuswali.
3. Kuirefusha Swala, kwa kisimamo, rukuu na sijida, isipokuwa iwapo jua limeachwa au mwezi basi hapo itatimizwa kwa kufupishwa.
4. Rakaa ya pili itakuwa fupi kulingana na ya kwanza, kwa kisimamo chake, rukuu yake na sijida yake.
5. Kutolewa mawaidha baada yake, na kuwakumbusha watu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, na kueleza hekima ya kupatwa mwezi na jua, na kuwahimiza watu kufanya mambo ya utwiifu na kuacha mambo mabaya.
6. kuomba dua kwa wingi, kunyenyekea, kuomba msamaha, kutoa sadaka na mengineyo miongoni mwa matendo mema, mpaka Mwenyezi Mungu Awaondolee watu yale waliyo nayo.
7. Inafaa kuinua mikono katika dua kwenye Swala ya kupatwa jua au mwezi, kwa hadithi ya Abdurrahman bin Samurah t aliyesema: (Nikamjia Mtume ﷺ na yeye amesimama katika Swala na huku ameinua mikono yake) [Imepokewa na Muslim.]




Maelekezo

1. Swala ya kupatwa jua au mwezi hailipwi iwapo kupatwa kwa jua au mwezi hakukujulikana isipokuwa baada ya kuachwa.
2. Kuwa elimu ya kisasa imejua sababu ya kupatwa Jua na mwezi haifuti kuwa viwili hivyo ni miongoni mwa alama za Mwenyezi Mungu. Basi Muislamu atakikana ajishughulishe kwa ibada na

kunyenyekea kwa Mwenyezi Mungu, na sio ajishughulishe na kuangalia na kuchunguza kupatwa kwa mwezi au jua. Abu Bakrah t amepokewa akisema: (Lilipatwa jua wakati wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ akatoka na huku anakokota kishali chake). Hii inaonyesha vile anavyoogopa ﷺ.

3. Kupata rakaa kunakuwa kwa kupata rukuu ya kwanza pamoja na imamu. Basi aliyekosa rukuu ya kwanza na akapata ya pili, rakaa huwa ameikosa, na atailipa kwa namna zake baada ya imamu kutowa Salamu.
4. Swala ya kupatwa jua au mwezi huswaliwa hata katika nyakati zilizokatazwa kuswaliwa.
5. Haitoshi kuthibiti Swala ya kupatwa mwezi au jua kwa habari, bali ni mpaka kupatwa kuonekane waziwazi.

# Swala ya Idd mbili

## Tamasha za idd

Idi za Waislamu ni mbili: Idi ya Fitri baada ya mwezi wa Ramadhani na Idi ya Adh›ha baada ya siku ya Arafa. Na Mwenyezi Mungu Ametupa Idi hizo ziwe ni badala ya Idi za kijahilia na kila idi yenye kuzuliwa. Anas bin Malik t amepokewa akisema: «Watu wa Jahilia (kabla ya Uislamu) walikuwa na siku mbili kila mwaka, wakisherehekea idi hizo. Mtume ﷺ alipokuja Madina alisema: (Mlikuwa na siku mbili mkizisherehekea, na Mwenyezi Mungu Amewabadilishia idi bora kuliko hizo: Idi ya Fitri na Idi ya Adh’ha) [Imepokewa na Nisaa.].
Na haifai kusherehekea wala kushiriki kwenye idi za makafiri. Kwani hizo idi ni alama zenye nguvu zaidi za kila dini na alama

zilizojitokeza zaidi za sheria na njia zake. Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Anasema: {Na usifuate mapenzi yao ukaacha haki iliyokujia. Kwani kila mmoja miongoni mwenu tumemuwekea sheria na njia} [5: 48]

Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Ameweka Swala katika Idi mbili hizi inayoitwa Swala ya Idi, nayo ni tukio miongoni mwa matukio yake muhimu zaidi.

## Hukumu ya Swalah ya Idi mbili

Ni faradhi ya kutosheleza ambayo wakisimama kuifanya watu wanaotosheleza, wengine wasaliao hupomokewa na dhambi ya kutoifanya- na ingawa amri ya kuifanya imetiliwa mkazo sana- Kwani Mtume ﷺ ameamrisha kuitekeleza. Bali aliamrisha kuwatoa wasichana na kina mama, hata wale walioko hedhini (aada ya mwezi) miongoni mwao ingawa hawatoswali. Hii inaonesha ubora wa Swala ya Idi na kuitilia mkazo. Na dalili ya ulazima wake ni yafuatayo:

1. Neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Mswalie Mola wako na uchinje} [108: 2].

2. Mtume ﷺ Ameamrisha iswaliwe, mpaka amewaamrisha wanawake waiswali, kwa hadithi iliyopokewa na Ummu ‘Atwiyyah t kuwa alisema: (Ametuamrisha Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ tuwatoe wanawake kwa Swala ya Idi: wadogo wanaoanza kubaleghe [’Awaatiq: ni wingi wa ‘aatiq naye ni msichana mwanzo wa kubaleghe.], waliomo hedhini [ Huyyadh (walio na hedhi): ni wingi wa haaidh (aliye na hedhi).] na wanawali walio paziani [ Dhawaat al- khduur: wanawali (Msichana bikira).]. Ama wenye hedhi watajiepusha na kuswali na watahudhuria kwenye kheri na dua ya Waislamu) [ Imepokewa na Bukhari.].

## Wakati wa Swalah za idd mbili

Unaanza wakati wa Swala ya idd pale jua linapochomoza na kuangatika kadiri ya uti wa mkuki. Kuangatika huku kunakuwa ni kiasi cha robo saa kuanzia kuchomoza kwa jua mpaka kupinduka. Na sunna ni kuichanguliza Swala ya Iddul Adh'ha ili waislamu wapate wakati wa kuchinja, na kuichelewesha swala ya iddul Fitr ili waapate nafasi ya kutoa Zaka za Fitri.

## Namna ya kuswali Swala ya Idd mbili

Swalah ya Idi mbili ni rakaa mbili bila ya kuadhini wala kukimu. Na kisomo kinasomwa kwa sauti, na namna yake ni kama inayofuata:

1. Atapiga takbiri saba katika rakaa ya kwanza baada ya takbiri ya kufungia Swala na dua ya Ufunguzi na kabla ya kuleta Audhu na kusoma.
2. Ataleta Audhu na apige bismillahi na aanze kusoma Fatiha na sura baada yake. Ni sunna asome katika rakaa mbili hizo sura ya Al-A'laa katika rakaa ya kwanza na sura ya Al-Ghaashiah katika rakaa ya pili, au sura ya Qaaf katika rakaa ya kwanza na sura ya Al-Qamar katika rakaa ya pili.
3. Atapiga takbiri tano katika rakaa ya pili baada ya takbiri ya kuhama (kutoka kwenye sijida ya pili ya rakaa ya kwanza) na atainua mikono yake katika kila takbiri.
4. Atamhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifu, na amsalie Mtume ﷺ baina ya hizo takbiri.
5. Akitoa Salamu kutoka kwenye Swala atapanda mimbari na atahutubu hutuba mbili, atakaa baina ya hutuba mbili hizo kikao kichache. Ataanza hutuba ya kwanza kwa kupiga takbiri tisa, na hutuba ya pili kwa kupiga takbiri saba.
6. Inapendekezwa katika Idd ya Fitri awakumbushe watu hukumu za Zaka za Fitri, na katika idi ya Adh, haa awakumbushe hukumu za kudhahi (kuchinja).

## Mahali pa kuswali Swala ya idd

Sunna ni kusimamisha Swala ya Idd mbili katika muswallaa (uwanjani), na ikiswaliwa msikitini si makosa –iwapo kuna dharura ya kufanya hivyo.

## Yanayo pendeza katika Swala ya idd

1. Mwanamume ajipambe kwa kuvaa nguo zake nzuri zaidi. Ama wanawake, watatoka kwenda kwenye kuswali bila ya kujipamba wala kujitia manukato.
2. Maamuma ahudhurie mapema na atangulie kwenye safu za mwanzo.
3. Aende kuswali kwa miguu kupitia njia na arudi kupitia njia nyingine. Jabir t amepokewa akisema: (Alikuwa Mtume ﷺ, ikiwa siku ya Idi, akibadilisha njia ) [Imepokewa na Bukhari.].
4. Ale tende idadi ya witiri (tatu au tano) kabla hajatoka kwenda kuswali Swala Idd ya Fitri, na asile chochote katika Idd ya Adh’ha mpaka arudi.
5. Inapendekezwa kuchelewesha Swala ya Idd ya Fitri ili Muislamu apate nafasi ya kutoa Zaka za Fitri na kuzifikisha kwa wanaostahiki. Ama Swala ya Idd ya Adh’ha inapenkezwa iswaliwe mapema.

## Miongoni mwa hukumu za Swala ya Idd mbili

1. Ni karaha kuswali sunna kabla ya Swala ya Idd na baada yake mahali palepale, isipokuwa iwapo imetekelezwa msikitini, basi itaswaliwa swala ya kuuamkia msikiti wakati wa kuingia.
2. Ni sunna kwa aliyeikosa Swala ya Idd au sehemu ya hiyo Swala: ailipe kwa namna ile ile inavyoswaliwa, nayo ni kuiswali rakaa mbili kwa takbiri zake. Na ile sehemu ya Swala hiyo iliyompita ataitimiza kwa namna yake.
3. Mwenyezi Mungu Amewaamrisha waja wake mwisho wa Ramadhani wamtukuze. Anasema Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Na ili mkamilishe idadi na mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa kile alichowaongoza} [2: 185].

(Tukabbiru llaha): Yaani mumtukuze kwa nyoyo zenu na ndimi zenu. Nako ni kusema" Allahu Akbar, Allah Akbar, Laa ilaaha illallah wa Allahu Akbar wa Lillaahil-hamd"

4. Ni sunna kuinua sauti kwa takbiri kwa wanaume. Ama wanawake watapiga takbiri kwa siri, kwa kuwa mwanamke ameamrishwa aifanye chini sauti yake.

5. Takbiri ya Idi ya Fitri inaanza tangu wakati wa kuzama jua usiku wa Idi - ikijulikana kuwa mwezi umeingia kabla ya jua kuzama-. Ama ikijulikana kuingia mwezi kabla ya jua kuzama, kama iwapo watu walikamilisha kufunga siku thelethini, au kuanzia kuthibiti kuonekana mwezi wa Mfungo mosi. Na inakoma hiyo takbiri pale watu waanzapo kuswali Idi. Ama Idi ya Adh'ha, takbiri inaanza baada ya Swala ya Alfajiri ya siku ya Arafa mpaka Swala ya Alasiri ya siku ya tatu katika siku za Tashriq.

## Maelekezo

1. Ni sunna kwa waislamu kupongezana kwa Idd.
2. Ni sunna kuifurahia Idd na kuonyesha hiyo furaha, na Muislamu awapongeze jamaa zake na vipenzi vyake na ndugu zake Waislamu.
3. Idi ni fursa ambayo yapasa kuichukua katika kuunga vizazi vilivyo katika na kuwapatanisha watu walioteta.
4. Kuzuru makaburi siku ya Idi hakukuwekwa na Sheria, bali hilo ni jambo linaloenda kinyume na kile kinachotakiwa katika Idi cha kuonyesha furaha na teremo.
5. Sheria imeweka kuwakunjulia watoto katika mavazi na chakula kuwafurahisha siku ya Idi mbili kwa vitu vilivyohalalishwa na Mwenyezi Mungu. Idi mbili ni siku za furaha na buraha na teremo. Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Anasema: {Sema: Kwa nyongeza za menyezi Mungu na rehema Zake, basi kwa hilo na wafurahike. Hilo ni bora kuliko vile wanavyovikusanya}[10: 58]
6. Haifai kusherehekea kwa Masia, nay ale yanayo mkasirisha Mwenyezi mungu kwa kusikiliza miziki na kwa kuchanganyikana

baina ya wanaume na wanawake, na kuacha Swala, na kupoteza wakati kwa mambo ya upuzi na yaharamu na kadhalika

# Swalah ya Janeza

## Kumtayarisha Maiti

Inapendekezwa kuhudhuria pale penye mtu ambaye alama za kifo zimedhihiri kwake, na kumkumbusha kusema «Laa ilaaha illa-llah» kwa kauli yake Mtume ﷺ (Walakinini maiti zenu "Laa ilaaha illa- llaah") [Imepokewa na Muslim.].
Akifa atafumbwa macho yake na afinikwe nguo na kufanywe haraka kumtayarisha kwa mazishi na kumswalia na kumzika.

### Hukumu ya kumuosha maiti na kumtayarisha na kumzika

Kumuosha maiti, kumkafini, kumbeba, kumswalia, na kumzika ni katika faradhi inayotosheleza. Wakifanya baadhi ya waislamu inapomoka madhambi kwa waliobakia.

### Hukumu ya kumuosha maiti

1. Yatakikana achaguliwe mtu mwaminifu wa kuosha maiti, pai awe mjuzi wa hukumu za kuosha.
2. Hutangulizwa kuosha yule mtu ambaye maiti mwenyewe alikuwa ameusia aoshwe na yeye. Kisha yule aliye karibu zaidi na maiti, iwapo ana ujuzi wa hukumu za kuosha. Akitokuwa hivyo, basi atatangulizwa mwenye ujuzi wa hilo.
3. Mwanamume huoshwa na wanaume, na mwanamke huoshwa na wanawake. Na kila mmoja miongoni mume na mke anafaa kumuosha mwenzake, kwa kauli ya Mtume ﷺ kumwambia›Aishah t: (Hakuna cha kukudhuru, lau wafa kabla

yangu nikakuosha, nikakukafini na nikakuswalia kisha nikakuzika) [Imepokewa na Ibn Maajah.].

Pia inafaa kwa wanaume na wanawake kuwaosha watoto walio chini miaka saba. Na haifai kwa Muislamu - awe mwanamume au mwanamke- kumuosha kafiri, walakubeba jeneza yake wala kumkafini wala kumswalia, hata kama ni jama yake wa karibu kama vile baba.

4. Shahidi aliyekufa vitani haoshwi wala hakafiniwi wala haswaliwi, bali huzikwa na nguo zake.

5. Afikapo tisha- naye ni mwana aliyetoka kwenye tumbo la mamake kabla ya kutimia umbo lake, awe ni mwanamume au ni mwanamke- miezi minne, ataoshwa, akafiniwe na aswaliwe. Kwani yeye baada ya miezi minne huwa ashakuwa na umbo la binadamu kamili.

6. Maji ya kuoshea maiti ni sharti yawe ni maji yanayofaa kujitwahirishia na yawe ni ya halali, na aoshwe mahali pa sitara, na haifai kuhudhuria asiyekuwa na mafungamano yoyote na kumuosha maiti.

## Namna ya kumuosha maiti

1. Maiti awekwe juu ya kitanda cha kuoshewa, kisha afinikwe uchi wake, kisha avuliwe nguo zake, afichwe na macho ya watu ndani ya chumba au mfano wake.

2. Inapendekezwa kwa muoshaji atatie kitambaa mkononi mwake wakati wa kuosha.

3. Muoshaji atakiinuwa kichwa cha maiti akaribie kumkalisha, kisha apitishe mkono wake kwenye tumbo lake na alikamue, kisha aisafishe tupu yake ya mbele na ya nyuma kwa kuosha najisi yoyote iliyopo.

4. Muoshaji atanuilia kuosha na atapiga bismillahi.

5. Muoshaji atamtawadhisha maiti kama udhu wa Swala, isipokuwa katika kusukutua na kupaliza puani, huwa inatosha kumpukusa kinywa na pua.

6. Atakiosha kichwa cha maiti na ndevu zake kwa maji ya mkunazi au sabuni au kinginecho.


7. Ataosha sehemu ya kulia kisha sehemu ya kushoto, kisha atakamilisha sehemu ya mwili iliyosalia.
8. Inapendekezwa atie kafuri katika osho la mwisho.
9. Atampangusa maiti.
10. Amuondolee maiti vitu vinavyotakikana kuviondoa kama kucha, nywele za kinena (nywele za sehemu ya siri) na makapwa.
11. Atazisuka mkili nywele za mwanamke aziweke nyuma yake




Atamuinuwa muoshaji ichwa cha maiti




Atatie muoshaji kitambaa mkononi mwake




Atawekwa maiti juu yakitanda cha kuoshewa




Muoshaji atabonyeza kwa mkono wake tumbo la maiti na kumkamua kwa upole




Muoshaji atamtawadhisha maiti kama udhu waswala




Atamuosha kichwa cha Maiti na ndevu zake kwa maji na mkunazi




Atamuosha upande wakulia kisha upande wakushoto



Atampanguswa maiti

## Faida

- Lawajibu ni osho moja iwapo litatosha kumsafisha, na linalopendekezwa ni kumuosho mara matatu, hata kama ashasafishika.
- Ikitowezekana kumuosha maiti kwa kukosekana maji au ukiwa mwili umekatikakatika kwa moto au mfano wake, atatayamamishwa kwa mchanga.
- Inapendekezwa kwa mwenye kumuosha maiti aoge baada ya kumaliza kuosha.

## Kumkafini maiti

1. Sunnah ni kumkafini mwanamume katika lifafa tatu nyeupe za pamba, zisizoonyesha ngozi ya mwili, yenye kusitiri mwili wake wote, wala zisiwe ni za ghali.

Na mwanamke anakafiniwa ndani ya nguo tano za pamba: nguo ya chini, msuani, kanzu na lifafa mbili.

Na mtoto wa kiume anakafiniwa kwenye nguo moja, na inafaa pia kukafiniwa kwa nguo tatu, na mtoto wa kike anakafiniwa kwenye kanzu lifafa mbili za nguo.

2. Lifafa tatu zinaletwa na zinafukizwa kwa udi, kwa kauli yake Mtume ﷺ: (Mkifukiza [ Jammara: yaani kufukiza kwa udi] maiti basi fanyeni witiri (mara tatu)) [ Imepokewa na Ibnu Hibbaan].

3. Lifafa hizi zitatengwa kila lifafa juu ya nyingine, na baina ya kila lifafa kutatiwa mafuta mazuri kama vile ambari, kafuri, miski na mfano wake. Isipokuwa akiwa maiti yuko kwenye ihramu,

hapo nguo yake haitafukizwa kwa udi wala haitatiwa manukato kwa kauli ya Mtume ﷺ: (Wala msimgusishe mafuta mazuri) [Imepokewa na Bukhari.].

4. Atawekwa maiti akiwa amelala kwa mgongo juu ya hizi lifafa, kisha itavutwa ile ncha ya lifafa ya juu ya upande wa kushoto kwenye upande wake wa kulia, kisha itapelekwa ncha yake ya kulia kwenye upande wa kushoto, kisha ile ya pili, kisha ya tatu, kisha ile sehemu iliyozidi huwekwa usoni mwake, kisha hufungwa fundo kwa ufita wa kufungia ili isifunguke, na wakati wa kuzikwa hufunguliwa.

5. La wajibu ni kusitiri mwili wote. Iwapo hakuna ila nguo moja tu haitoshi kuenea mwili mzima, basi atafinikiwa kichwa chake, na katika miguu yake yatawekwa majani ya idhkhir[ Idhkhir: mmea wenye harufu nzuri.], kwa kauli ya Mtume ﷺ kumwambia Khabbaab katika kisa cha kukafiniwa Mus'ab bin 'Umair: (Akatuamrisha Nabii ﷺ tukifinike kichwa chake na tuweke kwenye miguu yake majani ya idhkhir) [Imepokewa na Bukhari.].

6. Aliyekufa katika hali ya ihramu atakafiniwa kwenye nguo zake mbili alizohirimia, wala hafunikwi kichwa mwanamume aliyekufa katika hali ya ihramu, kwa neno lake Mtume ﷺ: (Muosheni kwa maji na mkunazi. Na mkafinini kwenye nguo mbili, na msimpake manukato [ Hanuutw: Manukato yaliyochanganywa ya kutiwa kwenye kafani za maiti.], wala msimfunike kichwa chake [ Laa tukhammiuu ra'sahu: msimfunike kichwa chake.], kwani atafufuliwa siku ya Kiyama akiwa analeta talbiah (Labbaika llaahumma labbaika..)[ Mulabbiya: analeta talbiah: (Labbaika llaahumma labbaika).]) [ Imepokewa na Bukhari.].



Kuweka manukato katika lifafa (sanda)



Atawekwa maiti kwa kulala kwatani



Kusitiri mwili mzima



## Swalah ya Maiti

## Nguzo za Swala ya maiti

1. Kusimama kwa anayeweza.
2. Takbiri nne..
3. Kusoma Fatiha.
4. Kumswalia Mtume ﷺ.
5. Kumuombea Maiti Dua
6. Kutugamanisha (kutaratibisha).
7. Kutoa Salamu.

## Sunnah za Swalah ya Maiti

1. Kuleta A›udhu..kabla ya kusoma.
2. Kujiombea dua mwenye kuswali na kuwaombea Waislamu.
3. Kusoma kwa siri.
4. Kuzifanya safu ziwe nyingi, ziwe tatu au zaidi.

## Namna ya kuswalia maiti(jeneza)

Atasimama imamu kwenye kichwa cha maiti iwapo ni mwanamume, na katikati ya maiti iwapo ni mwanamke. Na maamuma watasimama nyuma yake kama ilivyo kwenye Swala nyingine, kisha atapiga takbiri nne kama ifuatavyo:

1. Atapiga takbiri ya kwanza, nayo ni takbiri ya kufungia Swala, na ataleta Audhu.. na apige bismillahi.. na asisome dua ya kufungulia Swala, kisha asome Fatiha.
2. Atapiga takbiri ya pili, na atamswalia Mtume ﷺ kama ilivyo namna ya kumswalia Mtume katika kikao cha Atahiyatu ya mwisho.
3. Atapiga takbiri ya tatu, na atamuombea maiti. Na miongoni mwa dua ni kusema: (Ewe Mola! Mghufirie na umrehemu, umpe afya na umsamehe, ukirimu mashukizi yake na umpanulie njia yake kuingilia (Peponi), Umsafishe kwa maji, theluji na barafu, umtakase kutokana na dhambi kama inavyo takaswa nguo nyeupe na uchafu, Umbadilishie nyumba umpe nyumba ya kheri kuliko nyumba yake alokuwa nayo, na watu wa kheri zaidi kuliko watu alokuwa

nao, na mke wa kheri kuliko yule alokuwa naye, Umtie peponi na umlinde na adhabu ya kaburi, au adhabu ya Moto)[ Imepokewa na Muslim.].
Na iwapo maiti ni mwanamke kutatumika dhamiri za kike (dua isomwapo kwa Kiarabu)
Na maiti akiwa ni mtoto mdogo au ni tisha [ Siqtw: mwana wa matumboni anayezaliwa kabla ya kukamilika.] atasema: (Ewe Mola! Mjaalie ni akiba ya wazazi wake na kitangulizi chema [ Faratw: aliyetanguliwa na kuwa wa mwanzo.] na ni thawabu kwao na kiombezi mwenye kukubaliwa dua) [ Imepokewa na Bukhari.].
4. Atapiga takbiri ya nne, na atanyamaza kidogo, kisha atatowa Salamu moja upande wake wa kulia au salamu mbili.




## Kumbeba maiti na kumshindikiza na kumzika

Kunapomalizika kumswalia maiti, sunna ni kufanya haraka kumbeba kumpeleka kwenye kaburi lake. Na imesunniwa kwa anayefuata jeneza kushiriki kulibeba. Na imesunniwa kwa anayemuingiza maiti kaburini aseme: BISMILLAH WA'ALAA MILLATI RASULILLAH (Kwa jina la Mwenyezi Mungu, na kwa mila ya Mtume wa Mwenyezi Mungu) [Imepokewa na Tirmadhi.],
na amuweke ufukoni [ Lahd: ni kufukuliwa kwenye ardhi ngumu shimo lenye urefu na kuengeza kufukuwa upande wake wa Kibla.] kwa ubavu wake wa kulia na uso wake uelekee Kibla, kisha alifunguwe fundo la kafani, kisha uzibwe mwanya wa ufuko kwa udongo.

Na ni sunna kwa aliyehudhuria mazishi ajaze mchanga vitanga vyake vya mikono na aurushe kaburini mara tatu.Kisha kaburi ifinikwe kwa mchanga, na iinuliwe juu ya ardhi kadiri ya shubiri moja, na viwekwe juu yake vijiwe na mawe, na inyunyizwe maji. Na si makosa kuweka jiwe kubwa kwenye ncha moja ya kaburi au ncha zote mbili liwe ni alama yake.



Kushiriki katika kubeba jeneza



Ufuko



Atajaza mchanga kwenye vitanga vyake vya mikono na aurushe kaburini



Alama juu ya kaburi

### Kutaazii

Inapendekezwa kuwataazii waliofiliwa, kwa kuwa hilo linakunjua nafsi zao na linapunguzia msiba wao, na kuwahimiza wasubiri.

Na taazia inafaa kwa neno lolote lenye kutimiza lengo la kutaazii, kama vile kusema: (Ni cha Mwenyezi Mungu alichokichukua, na ni chake alichotoa, na kila kitu, kwa Mwenyezi Mungu, kina muda wake uliyoandikwa) [ Imepokewa na Bukhari.].

Na mfano wa maneno haya.

Wanawake kutoka kufauata jeneza

wanawake Kutoka kufuata jeneza ni jambo lisiloambatana na Sheria, kwa hadithi iliyothubutu kutoka kwa Ummu ‹Atwiyyah t kuwa alisema: (Tulikatazwa kubeba jeneza na hatukuwekewa mkazo) [Imepokewa na Ibnu Maajah].

## Kuzuru makaburi

Ni sunna kuzuru makaburi kwa wanaume kwa lengo la kuwaidhika na kuwaombea wafu, kwa kuwa Mtume ﷺ alisema: (Niliwakataza kuzuru makaburi, basi sasa yazuruni, kwani hayo yanawakumbusha Akhera) [Imepokewa na Muslim.].

Miongoni mwa dua zilizokuja za kuombwa wakati wa kuyazuru makaburi ni: (Amani iwafikie nyinyi, enyi mlio kwenye nyumba ya watu Waumini! Na sisi pale atakapo Mwenyezi Mungu ni wenye kukutana nanyi) [Imepokewa na Muslim.].

Au (Amani iwashukie watu wa nyumba hizi kati ya walioamini na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu. Na

Mwenyezi Mungu Awarehemu waliotangulia na waliokuja nyuma. Na sisi atakapo Mwenyezi Mungu ni wenye kukukutana nanyi) [Imepokewa na Muslim.].

(Namuomba Mwenyezi Mungu Atuafu sisi na nyinyi) [Imepokewa na Muslim.].

Na lau atawaombea rehema na msamaha na mfano wake, basi hilo linafaa.

## Makatazo yanayo ambatana na jeneza

1. Kuomboleza na kulia kwa makelele [ Nadb: Kutaja mema ya maiti pamoja na kulia - Niyaahah: Kumlilia maiti kwa kelele.], kuonyesha papatiko na hasira juu ya uamuzi wa Mwenyezi Mungu na kadara Yake.

Anasema Mtume ﷺ: (Mwanamke anayelia kwa makelele kwa kufiwa, iwapo hatatubia kabla hajafa, atasimamishwa siku ya Kiyama akiwa amevaa nguo ya shaba [ Qatwiraan: Kanzu ya shaba iliyoyayushwa.]) [Imepokewa na Muslim.].

2. Kupasua nguo, kujipiga makofi, kupiga kelele, kusumua nywele au kunyoa.

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu: ﷺ: (Si miongoni mwetu mwenye kujipiga makofi au akapasua nguo au akaita mwito wa kijahilia (wa kuomboleza)) [Imepokewa na Muslim.]

3. Kuwasha taa makaburini:

Ibnu ‘Abbas t amepokewa akisema: (Mtume wa mwenyezi Mungu amewalaani wanawake wenye kuzuru makaburi na watu wenye kufanya misikiti juu yake na kuwasha taa [ Suruj: taa.]) [Imepokewa na Muslim.].



Haifai kuyangarisha makaburi kwa taa wala kuyakandika

4. Kukaa juu ya makaburi au kuyakandika au kuyajengea.

Jabir t amepokewa akisema: (Alikataza Mtume wa Mwenyezi Mungu kaburi isikandikwe [ Yujasswaswu: kukandikwa.], isikaliwe na isijengewe) [Imepokewa na Muslim.].

5. Kutabaruku kwa makaburi na kuyazunguka na kuwaomba wafu.

Haya ni miongoni mwa ushirikina iwapo mtu ataitakidi kuwa hivyo vinamnufaisha au kumdhuru, kwani hakuna mwenye kunufaisha au kudhuru isipokuwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Anasema U: {Sema: Siimilikii nafsi yangu manufaa wala madhara, ila apendavyo Mwenzi Mungu.} [7: 188]



Haifai kuyazunguka makaburi

6. Kuzika ndani ya misikiti, au kujenga misikiti juu ya makaburi au kuswali kuelekea kaburi.

Mtume wa mwenyezi Mungu ﷺ alisema: (Mwenyezi Mungu Amewalaani Mayahudi na Manaswara, waliyafanya makaburi ya manabii wao kuwa ni misikiti) [Imepokewa na Bukhari.].

## Miongoni mwa hukumu za Swalah ya jeneza

1. Mwenye kukosa Swala ya maiti atamswalia kaburini kabla ya kuzikwa au baada yake, kwa hadithi iliyothubutu kwa Mtume ﷺ katika kisa cha mwanamke aliyekuwa akisafisha msikiti alipo kufa na kuzikwa Mtume ﷺ alikwenda akamswalia kaburini
[ Imepokewa na Bukhari.].
2. Inapendekezwa kutayarishiwa watu waliofiliwa chakula, kwa kuwa wao wameshughulishwa na msiba na kutotayarisha chakula. Kwa ilivyopokewa kuwa jamii ya Jaafar walipofiliwa, Mtume ﷺ akasema: (Wafanyieni jamii ya Jaafar chakula, kwa kuwa wamejiwa na jambo la kuwashughulisha) [Imepokewa na Abuu Daud.].



Kuwafanyia chakula waliofiliwa

3. Kumlilia maiti, bila kujitia hasira wala kuinua sauti wala kuomboleza, kunafaa. Mtume ﷺ Amesema alipokufa mwanawe, Ibrahim: (Kwa hakika jicho linatokwa na machozi na moyo unasikitika, na hatusemi isipokuwa linalomridhisha Mola wetu. Na sisi, ewe Ibrahim!, tuna huzuni) [Imepokewa na Bukhari.].
4. Shahidi wa vitani atazikwa na nguo zake alizouawa nazo, na haoshwi wala haswaliwi, kwa haditi iliyothubutu kwamba Mtume ﷺ aliamrisha wazikwe mashahidi wa vita vya Uhud wazikwe wakiwa na damu zao na wasioshwe [Imepokewa na Bukhari.].



Shahidi huzikwa akiwa na nguo zake

5. Akifa aliye kwenye hali ya Ihramu ya Hija au ya Umra, ataoshwa na hatatiwa manukato, wala hatafinikwa kichwa chake na ataswaliwa.

Hii ni kwa iliyothubutu kwamba Mtume ﷺ alisema kuhusu mtu aliyekufa naye yuko kwenye Ihramu ya Hija: (Muosheni kwa maji na mkunazi, na mkafinini ndani ya nguo mbili, wala msimfinike kichwa chake, kwani yeye atafufuliwa Siku ya Kiyama katika hali ya kuleta Labeka) [Imepokewa na Bukhari.].

Ingia katika kiungo kifuatacho upate maelezo zaidi:

# SAUM

## Fadhili za swaumu na Hukumu zake

## Maana ya swaumu

### Saumu Katika Lugha

Ni kujizuia na kujiepusha kufanya jambo fulani.

### Saumu Kisheria

Ni kufanya ibada kwa ajili ya Mwenyezi Mungu U kwa kujizuia kula, kunywa na kufanya tendo la ndoa kuanzia kutokeza kwa alfajiri hadi kutwa kwa Jua.

## Fadhla za swaumu

Asema Mwenyezi Mungu { Enyi mlo Amini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andkikwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kucha mungu.(Mfunge) siku maalumu za kuhisabika.na atakaye kuwa miongoni mwenu mgonjwa au yumo safarini basi atimiza hisabu katika siku nyingine. Na wale wasio weza watoe fidiya kwa kumlisha masikini na atakaye fanya wema kwa kujitolea, Basi ni bora kwake na Mkifunga ni bora kwenu kama mnajua.} (Al-Baqarah- Aya 183: 185)

Saumu ina fadhila kubwa sana, na thawabu nyingi mno tena maradufu, na kwa hakika Mwenyezi Mungu ameinasibisha saumu kwake yeye kwa ajili ya kuipa utukufu na kuitukuza. Katika Hadithi Al-Qudsy iliyopokewa na swahaba Abu Hurayrah, t Anasema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw): “kila tendo la mwanadamu huongezwa malipo ya wema wake mara kumi ya mfano wa jema hilo alilolitenda mpaka hufikia kuongezwa (huku kwa malipo ya wema huo) hadi nyogeza mara sabiini. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Isipokuwa saumu, kwani hiyo saumu ni yangu mimi, na mimi ndiye mwenye kutoa malipo yake; (mja wangu) anaacha matamanio yake na chakula chake kwa ajili yangu. Katika kufunga saumu kuna furaha mbili: furaha (ya kwanza) ni pale anapofungua saumu aliyefunga, na furaha (ya pili) ni

wakati (aliyefunga) atakapokutana na Mola wake. Na harufu inayotoka kwenye kinywa cha aliyefunga ni nzuri sana mbele ya Mwenyezi Mungu kushinda harufu ya miski”. [Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

## Hekima za kufaradhishwa kufunga

1. Ni mja kupata ucha Mungu kwa kuitika amri ya Mola wake amri hii ya kufunga na kujitolea muhanga kuitekeleza sheria ya Mola wake. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Enyi mlioamini! Mmelazimishwa kufunga (saumu) kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu} (Al-Baqarah- Aya 183).
2. Kuipa nafsi mazoezi ya kusubiri, na kujipa nguvu ili kuweza kushinda matamanio.
3. Kujizoezesha mtu kufanya hisani, na kuwa na huruma kwa wanaohitaji masikini na mafukara; kwa sababu mtu anapoonja hisia ya njaa itampelekea mtu huyu kuwa na moyo laini na kuhisi jinsi wanavyohisi ndugu zake wahitaji wasio na chochote cha kula.
4. Kupata raha ya kiwiliwili na afya bora katika kufunga.

## Hukumu ya kufunga swaumu Imegawanyika saumu ambayo Mwenyezi Mungu ameiweka katika sheria vigawanyo vifuatavyo:

### 1. Saumu ya wajibu

Nayo iko sampuli mbili:
1. Saumu aliyoiwajibisha Mwenyezi Mungu U kuanzia mwanzo wake (mwanzo wa hii saumu – chanzo chake) kwa mja wake, nayo ni saumu ya kufunga mwezi wa ramadhani, na saumu hii ni nguzo moja wapo katika nguzo za Uislamu.
2. Saumu ambayo kwamba mja ndiye anayekuwa sababu ya kuwajibishwa yeye mwenyewe kuifunga, kama vile saumu ya nadhiri na saumu ya kafara.

### 2. Saumu za Sunna

Nayo ni kila saumu ambayo kwamba sheria ya kiislamu imependekeza saumu hiyo kufungwa, kama kufunga siku ya Jumatatu na Alhamisi, na kufunga siku tatu za kila mwezi, na kufunga siku ya A'shura, na kufunga masiku kumi ya mwanzo wa mwezi wa Dhilhijja, na kufunga siku ya A'rafah.

## Masharti ya mtu kuwajibika Kufunga

1. Uislamu: Haimlazimu kafiri kufunga.
2. Kubaleghe: Sio lazima kwa mtoto mdogo kufunga, lakini huamrishwa kufunga akiwa anaweza ili kumpa mazoezi ya saumu naye azoee.
3. Kuwa na akili: Sio wajibu kwa mwendawazimu kufunga.
4. Uwezo wa kufunga: Sio wajibu kufunga kwa mtu ambaye hawezi kufunga (labda amekuwa mzee sana ama afya yake haimruhusu kuhimili saumu).

## Kufunga Ramadhani

Kufunga mwezi wa Ramadhani ni nguzo mojawapo kati ya nguzo za Uislam, na ni lazima kufunga mwezi huu. Mwenyezi Mungu amewalazimisha waja wake kufunga.

Anasema Mwenyezi Mungu mtukufu: {Enyi mlioamini! Mmelazimishwa kufunga (Saumu) kama walivyolazimishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu} (Al-Baqarah –Aya 183).

Na amesema Mtume (saw): "Uislamu umejengwa kwa mambo matano" [Imepokewa na Bukhari.] na akataja miongoni mwa mambo hayo: "kufungu saumu ya mwezi wa Ramadhani".

## Fadhila za Mwezi wa Ramadhani

1. Kufunga na kusimama usiku katika mwezi wa Ramadhani hali ya kuwa mtu ana imani na kutaraji malipo basi husamehewa madhambi yake yote yaliyopita. Amesema Mtume Mtume (saw):

“Atakayefunga mwezi wa Ramadhani hali ya kuwa ana imani na kutaraji malipo husamehewa yote yaliyotangulia katika madhambi aliyoyafanya” [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na akasema Mtume Mtume (saw): “Atakayesimama (kuswali usiku) katika mwezi wa Ramadhani hali ya kuwa na imani na kuridhia atasamehewa yote yaliyotangulia katika madhambi aliyoyafanya” [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

2. Ndani ya mwezi wa Ramadhani kuna ‘Lailatu Al-Qadr’ – ‘Usiku wenye hishima kubwa’ ambao kwamba Mwenyezi Mungu. U amesema kuhusu usiku huu: <> (Al-Qadr – Aya 3). Atakayesimama usiku huu basi atasamehewa madhambi yake yote yaliyotangulia. Amesema Mtume Mtume (saw): “Yoyote atakayesimama usiku wa cheo hali ya kuwa na imani na kuridhia atasamehewa yote yaliyotangulia katika madhambi yake” [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

3. Kufanya U’mrah ndani ya mwezi wa Ramadhani ni sawa na kuhiji pamoja na Mtume Mtume (saw). Amesema Mtume Mtume (saw): “Kufanya U’mrah ndani ya Ramadhani ni sawa na kuhiji pamoja nami” [Imepokewa na Muslim.].

4. Mwezi wa Ramadhani hufunguliwa milango ya peponi, na hufungwa milango ya motoni, na hutiwa minyororo (hufungwa) mashetani, na nafsi huelekea katika kufanya mambo ya kheri. Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtume (saw): “Unapoingia mwezi wa Ramadhani hufunguliwa milango ya mbinguni, na hufungwa milango ya motoni, na hutiwa minyororo mashetani” [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

5. Mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa Qur’an, na ndiyo mwezi ulioteremshwa Qur’an, kwa hivyo inafaa kuzidisha kusoma Qur’an ndani ya mwezi huu, Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Mwezi wa Ramadhani ni mwezi ambao imeteremshwa Qur’an katika mwezi (huo)} [Al-Baqarah – Aya 185]

6. Mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa ukarimu na kutoa sana sadaka. Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas t akisema: "Alikuwa Mtume (saw) mkarimu sana kushinda watu wote katika kufanya mambo ya kheri, na alikuwa mkarimu zaidi wakati wa mwezi wa Ramadhani, hakika Jibril alikuwa akikutana na Mtume kila mwaka katika mwezi wa Ramadhani mpaka uishe mwezi, basi ikawa Jibril wakati kama huu anampitishia Mtume (anaregelea kusoma pamoja na Mtume) Qur'an, basi pindi Mtume anapokutana na Jibril alikuwa Mtume mkarimu sana katika mambo ya kheri kushinda upepo mkali uliotumwa" [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Kitu gani kitathibitishia kuingia kwa Mwezi wa Ramadhani?

Inathibiti kuingia mwezi wa Ramadhani kwa kuonekana kwa mwezi, utakapoonekana mwezi baada ya kuzama kwa jua siku ya ishirini na tisa katika mwezi wa shabani, basi itakuwa umeshaingia mwezi wa Ramadhani, na ikiwa haukuonekana mwezi baada ya kuzama kwa jua siku ya thelathini ya mwezi wa shabani, au hali ikatanda wingu bila kuonekana mwezi, au kukawa na vumbi kali, au kukawa na moshi (wa umande wa baridi), itakamilishwa mwezi wa shabani siku thelathini; kwa kauli ya Mtume Mtume (saw): "Fungeni kwa kuonekana kwa mwezi na fungueni kwa kuonekana kwa mwezi, na ikiwapitikieni kwamba hamuuoni mwezi basi hisabuni siku thelathini (kukamilika shabani)" [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Ruhusa za mtu kula ndani ya mwezi wa Ramadhani

Kula ndani ya mwezi wa Ramadhani (yaani nyakati za mchana) ni haramu na ni katika madhambi makubwa, na atakayefungua siku moja tu bila ya udhuru wowote na wala asitubie basi hatokubaliwa saumu ya mwaka mzima hata akifunga, kwa kauli ya Mtume

Mtume (saw): "Atakayekula siku moja katika mwezi wa Ramadhani bila ya ruhusa yoyote aliyoiruhusu Mwenyezi Mungu hatokubaliwa mtu huyu saumu ya mwaka mzima" [Imepokewa na Abuu Daud.].

Na dhambi la kula ndani ya mwezi wa Ramadhani ni kubwa sana, kutoka kwa Abi Umaamatu Albaahiliy amesema: "Nilimsikia Mtume Mtume (saw) yuwasema: Pindi mimi nilikuwa nimelala walinijiia watu wawili ….., kisha wakaniondokea, nikawa nimefika mahali pa watu ambao wamefungwa sehemu zao za nyuma ya magoti wametanuliwa sehemu za pambizoni mwa midomo yao, sehemu zao za pambizoni mwa midomo inatona damu. Akasema: Nikauliza: Ni kina nani watu hao?. Akasema: Hao ni wale ambao kwamba wanakula kabla ya kukamilika kwa saumu zao) [Imepokewa na Ibnu Hibbaan.]

## Hali ya watu wema katika mwezi wa Ramadhani

### Kielelezo cha watu wema ni Mtume Muhammad (saw)

Asema Ibnul-Qayyim Mungu amrehemu (Na alikuwa mtume (saw) Katika muongozo wake kwnye mwezi mtukufu wa Ramadhani huzidisha sampuli nyingi za Ibada, Alikuwa jibril (AS) Akimsomesha yeye Qur'ani katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani na Alikuwa anapo kutana na jibril ni mkarimu zaidi kwa mambo ya kheri kushinda upepo uliotumwa, na Alikuwa ni mtowaji zaidi wa kushinda watu na Ramadhani alikuwa zaidi akizidisha kutoa sadaka na kufanya wema na kusoma Qur'ani na kuswali na kumtaja Mwenyezi Mungu na kukaa Itikafu na alikuwa akiukhusisha mwezi wa Ramadhani kwa ibada Asiyo yakhusisha katika miezi mengine mpaka mara nyingine akiunganisha saumu ili akapate masaa mengi ya kufanya Ibada).

### Watu wema na kusoma Qur'ani katika mwezi wa Ramadhani

Imependekezwa katika nyakati bora kama Mwezi wa Ramadhani haswa katika masiku kuzidisha kusoma Qur'ani kwa ijili yakufaidika kwa Wakati.
Huyu hapa imamul –Bukhari mungu amrehemu alikuwa usiku wa kwanza wa mwezi wa Ramadhani Wakijikusanya kwake marafiki zake akiwaswalisha na akisoma kila rakaa aya ishirini, akifanya hivyo mpaka akimaliza Qur'ani. Na alikuwa wakati wa maladaku akisoma kati ya nusu na thuluthi ya Qur'ani, na akikhitimisha Qur'ani wakati wa kufunguwa saumu kila usiku na Akisema kila unapo maliza msahafu kuna dua isiyo rudishwa
Na imepokewa kuwa imamu shafi alikuwa akikhitisha Qur'ani mara sitini mbali na zile anazo soma katika Swala

# Nguzo za swaumu na ya kuharibu swaumu

## Nguzo za swaumu

### NGUZO YA KWANZA: Ni kujizuia kufanya mambo yatakayo Haribu swaumu kuanzia kutokeza kwa alfajiri hadi kuzama kwa jua kwa kuingia jioni

Dalili ni kauli yake Mwenyezi Mungu U: {…Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni saumu mpaka usiku…} (Al-Baqarah- Aya 187).

### NGUZO YA PILI: Ni kutia nia ya Kufunga

Nako ni kukusudia kwa anayefunga saumu ya kwamba huku kujizuia na vitu vinavyofungua saumu ni ibada kwa ajili ya

Mwenyezi Mungu Mtukufu; kwa dalili ya kauli ya Mtume (saw): ( Hakika kila jambo analolifanya (mwanadamu) ni kulingamana na nia yake, na hakika kila mtu atalipwa kulingana na alivyonuilia) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

## Mambo yanayofaa kufanya ndani ya swaumu

1. Kuoga, na kukaa mahali penye maji ili kupata baridi.
2. Kumeza mate na makohozi.
3. Kuonja chakula ili kujua kiwango cha sukari au chumvi yake kwa kutumia ulimi peke yake, kwa sharti asiingize chochote katika chakula hicho hadi kwenye koo.
4. Kunusa harufu ya manukato na visafisha hewa.

Matumizi ya mswaki kwa mtu aliyefunga

Yaruhusiwa kutumia mswaki kwa mtu aliyefunga wakati wowote ule, sawasawa iwe ni kabla ya kuzama kwa jua kwa kuingia jioni au baada ya hapo, na vilevile uwe mswaki wenyewe uko majimaji au mkavu, lakini anatahadharishwa aliyefunga ikiwa mswaki anaotumia uko majimaji kusije kukaingia chochote kooni wakati anapiga mswaki; kwa sababu kuingia kwa kitu kooni kunaharibu saumu yake.

## Mambo yanayopendekezwa kufanywa ndani ya saumu

### 1. Kula daku na kuchelewesha kula daku hadi karibu sana na kuadhiniwa alfajiri

Kwa kauli ya Mtume (saw): (Kuleni daku, hakika katika kula daku kuna Baraka) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.]
Na inahesabika kula daku kwa kupatikana chakula kingi au kidogo, hata kama ni tama la maji kwa kauli ya Mtume (saw): “Daku uchache wake ni baraka, basi msiache kula daku, hata kama atakunywa mmoja wenu tama la maji, kwani Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanawaswalia wenye kula daku” [Imepokewa na Ahmad.]

Na inapendekezwa kuchelewesha kula daku, kutoka kwa Zaid ibn Thaabit t Anasema: (Tulikula daku pamoja na Mtume ﷺ, kisha tukasimama kuswali (yaani swala ya alfajiri), anasema Anas ibn Malik: nikasema: ilikuwa ni kipindi cha mda gani kati ya kula kwenu hiyo daku na kuswali? Akasema: kiwango cha (kusoma) Aya hamsini) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

- Kunywa wakati adhana inapo adhiniwa

Mtu anaposikia adhana na kinywaji chake kipo mkononi mwake basi anaruhusiwa kunywa hadi amalize; kutoka kwa Abu Hureirah anasema: Amesema (saw): "Atakaposikia mmoja wenu adhana na hali ya kuwa chombo cha kunywea maji kipo mkononi mwake basi asikiweke kando mpaka amalize haja yake ya kutumia hicho chombo" [Imepokewa na Abuu Daud.]

Na wanazuoni wamesema kuhusu hadithi hii ni kwa Yule ambae ana shaka kutokeza kwa alfajiri, ama akihakikisha kuwa alfajiri imetokeza kwa huyu hafai kuendelea kula wala kunywa, na akiendelea kufanya hivyo Saumu yake imebatilika na itamlazimu Ailipe

## 2. Kufanya haraka katika kufungua saumu

Yapendekezwa kwa aliyefunga kufanya haraka kufungua saumu yake pindi tu anapohakikisha kwamba jua limezama na kuingia jioni.; kwa kauli ya Mtume (saw): (Watu wangali katika kheri pindi wanapoharakisha kufungua saumu zao) [Imepokewa na Abuu Daud.].

Na inapendekezwa mtu kufungua saumu kwa rutab (tende tosa), asipopata rutab basi afungue kwa tende, na hizo tende ziwe ni hesabu isiyogawanyika kwa mbili (kama vile tende moja, tatu, tano na mfano huu), asipopata tende basi na anywe matama ya maji; kulingana na hadithi ya Anas ibn Malik, anasema: "Alikuwa Mtume (saw) anafungua saumu kwa Rutab (Tende Tosa) kabla hajaswali, na ikiwa hakuna Rutab basi alikuwa akifungua kwa tende kidogo hivi, na ikiwa hakuna tende

alikuwa akinywa [ Hasaa: alikunywa.] matama ya maji” [Imepokewa na Tirmidhi.].

Na akiwa hakupata kitu chochote cha kufungulia saumu basi atanuia kufungua saumu kwa moyo wake, na hili litamtosheleza kwamba amefungua.

Atakae Funguwa kwa bahati mbaya

Atakapo kula mtu aliyefunga hali ya kudhania kwamba jua limezama na kuingia jioni, au kwa kutoelewa kutokeza kwa alfajiri, kisha ije kum’bainikia kinyume na alivyodhania, basi haimlazimu kwake kuilipa saumu hiyo; kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu U: { Wala si lawama juu yenu mkikosa, lakini (kuna lawama) katika yale ziliyoyafanya nyoyo zenu kwa kusudi } ( Al-Ahzab- Aya 5).

Na kauli yake Mtume (saw): “Hakika ya Mwenyezi Mungu amewaondoshea umma wangu (hawaandikiwi madhambi) kwa jambo watakalolikosea bila ya kukusudia na kwa watakayofanya kwa kusahau, na kwa watakayolazimishwa kufanya (hali ya kuwa wao wenyewe wanayachukia)” [ Imepokewa na Ibnu Maajah.]

### 3. kuomba Dua wakati wakufungua swaumu

Kwa ilivyo Thubutu kutoka kwa Mtume (saw) Alipokuwa akifunguwa Saumu Akisema: “Kiu imeondoka, na jasho limekuwa majimaji (limeanza kutokeza), na yamepatikana malipo (ya thawabu) apendapo Mwenyezi Mungu” [Imepokewa na Abuu Daud.].

Na amesema Mtume (saw): “Hakika kwa aliyefunga saumu wakati anapofungua kuna dua isiyorudi) [ Imepokewa na Ibnu Maajah.] yaani dua inayokubalika moja kwa moja mbele ya Mwenyezi Mungu U.

### 4. Kuacha mambo ya upuzi na mambo machafu

Kwa kauli ya Mtume (saw): “Ikiwa ni siku ambayo mmoja wenu amefunga, basi asifanye mambo machafu, [ Yarfuth Kufanya mambo machafu: yatokamana na neno uchafu,

nako ni kutamka matamshi mabaya, na vile vile hutumika neno hili kumaanisha tendo la ndoa na vitangulizi vya tendo hili.] wala asikemee wenziwe[ Yaskhab: Yuwakemea: yatokamana na neno kemea, nako ni kubishana na kupiga ukulele.], anapotukanwa na mtu, au anapopigwa vita basi na aseme: Mimi ni mtu niliyefunga" [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

(Yaani ajitahidi kujiepusha kupigana na kutukanana na watu).

Na kwa neno lake Mtume (saw) (Asie acha maneno machafu na kuyatumia basi Mwenyezi Mungu hana haja kwa mtu huyo kuacha chakula chake na kinywaji chake) [Imepokewa na Abuu Daud.]

### 5. Kuzidisha kwa wingi kufanya Ibada

Kama kusoma Qur'an, na kufanya adhkari kumtaja Mwenyezi Mungu, na kuswali swala ya Tarawehe, na visimamo vya usiku (swala za usiku wakati watu wamelala), na kufanya visimamo vya usiku wa Lailatul Qadri, na kuswali swala za sunnah, na kutoa sadaka, na kuwa mkarimu na kujitahidi katika kufanya mambo ya kheri, na kuwalisha waliofunga wakati wa kufungua saumu zao, na kwenda U'mrah, kwasababu matendo mema siku ya Ramadhani malipo yake yanaongezeka mara nyingi sana, kutoka kwa Ibn Abbas anasema: "Alikuwa Mtume (saw) ni mkarimu kushinda watu wote, na alikuwa mkarimu zaidi wakati wa Ramadhani pindi anapokutana na Jibril, na alikuwa Jibril akikutana na Mtume kila usiku wa mwezi wa Ramadhani, ikawa anamfundisha Qur'an (yaani Jibril anamfundisha Mtume Qur'an), basi Mtume (saw) pindi anapokutana na Jibril alikuwa mkarimu katika mambo ya kheri kushinda upepo mkali uliotumwa" [Imwpokewa na Bukhari.].

### 6. Kujitahidi kwa Ibada hasa kumi lamwisho katika Mwezi wa Ramadhani

Imepokewa na bibi A'isha t Amesema: (Alikuwa Mtume (saw) likingia kumi la mwisho akijifunga kibobwe [(Shadda

mi'zarah) Nikinaya cha mtu kujitihidi katika ibada zaidi kuliko ilivo zowewa. Na kumesemwa ni kinaya cha mtu kujiepusha na mkewe, Almi'zar: ni kikoi nacho nikile kinchovaliwa sehemu chini ya muili.] na akiuhuisha usiku na akiwamsha wakezake[(Ayqadha Ahlahu) akiwatanabahisha kwa ajili ya ibaada na akiwahimiza juu yake.]) [Imwpokewa na Bukhari.]

## Mambo yanayochukizwa kuyafanya ndani ya saumu

### 1. Kupitisha mpaka katika kusukutuwa na kupandisha maji puani

Na hii ni kwa ajili ya kuhofia maji yasije yakaingia tumboni mwake, kwa kauli ya Mtume (saw): "Na fanyeni sana katika kupandisha maji puani isipokuwa wakati mtu amefunga saumu" [Imwpokewa na Abuu Daud.].

### 2. Kumpiga busu kwa matamanio ya kimapenzi

Inachukizwa kwa aliyefunga saumu ikiwa anachelea nafsi yake kutokwa na manii au kusisimukwa kwa matamanio ya kimapenzi. Na ni juu ya aliyefunga kujiepusha na kila ambalo kwamba litampelekea kusisimukwa na kuleta harakati za kuibuka matamanio ya kimapenzi, na ikiwa anaamini nafsi yake kwamba haitompelekea katika hisia za matamanio ya kimapenzi basi hakuna kosa kwake kum'busu mkewe au mke kumbusu mumewe; kutoka kwa A'isha anasema: "Alikuwa Mtume(saw) akipiga busu na kubashiriana ( yaani akimshikashika mkewe), na alikuwa ni m'bora zaidi kuliko nyinyi katika kumiliki matamanio ya kimapenzi [ Irbihi: Haja yake.]" [Imwpokewa na Bukharin a Muslim.].

Na kwa ajili hii inachukizwa kubashiriana kimapenzi kwa kijana kinyume na mzee kwa kuwa kijana damu yake ni moto zaidi, kutoka kwa Abu Hureirah anasema: "Kwamba kuna mtu mmoja alimuuliza Mtume (saw) kuhusu kubashiriana mke na mume kwa aliyefunga, Mtume akampa ruhusa ya kufanya hivyo,

na akaja mwengine akauliza (swali hilo hilo), Mtume akamkataza, kwani yule aliyempa ruhusa alikuwa ni mzee, na yule aliyemkataza alikuwa ni kijana” [ Imwpokewa na Abuu Daud.].

## Mambo yanayoharibu Saumu

### 1. Kula na kunywa kwa kukusudia ndani ya mchana wa Ramadhani

Kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U: {Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku. Kisha timizeni saumu mpaka usiku} (Al-Baqarah – Aya 187).

Kula kwasababu ya kazi

Yoyote anayefanya kazi mahali pa mapishi ya mikate hivi na mahali pa kazi ngumungumu sio ruhusa kwao kutofunga (yaani hawafai kula mchana wa Ramadhani); kwasababu wamelazimika kama watu wengine kufunga Ramadhani.

- Maelezo
- Atakaye kula au kunywa kwa kusahau basi saumu yake imeswihi (iko sawa haina tatizo lolote), na inamlazimu kujizuia na vitu vinavyoharibu saumu pindi anapokumbuka; kwa kauli ya Mtume (saw): “Aliyesahau hali ya kuwa amefunga akala na kunywa, basi akamilishe saumu yake, kwani Mwenyezi Mungu amemlisha na kumnywesha (mtu huyo)” [Imwpokewa na Muslim.].
- Kinaharibu saumu chochote kile kinachoingia tumboni kwa njia ya mdomoni au puani, na chochote kinachofahamika kuwa chakula au kinywaji, kama vile sindano za lishe/chakula. Ama sindano ambazo si za chakula, kama penicillin na mfano wake, hazifunguzi saumu, kwasababu sio chakula wala kinywaji, wala sio kwa maana ya chakula.

- Chochote kinachoingizwa mdomoni kwa ajili ya kutizama kitu na vipuliza hewa vya kutibu pumu na mfano kama huu, hakiharibu saumu.
- Wanja, na matone ya kitu majimaji kutonezwa kwenye jicho na sikio na mfano wa hivi viwili havivunji saumu, kwasababu hakuna dalili ya vitu hivi kuharibu saumu, na kwasababu jicho sio sehemu inayotegemewa kwa kuingilia chakula na kinywaji, na vile vile matone ya kitu majimaji kwenye sikio na puani, lakini ubora kwa haya matone ni kujitenga nayo, kwa jinsi alivyokataza Mtume (saw) kuhusu kupita mpaka katika kupandisha maji puani kwa aliyefunga, [Imwpokewa na Tirmidhi.] na kwasababu ni sehemu inayopitisha chakula hadi tumboni.
- Anapotumia mtu kitu ambacho hakiliwi au kinadhuru, kama vile sigara basi atakuwa amefungua, kwasababu amekitumia kupitia sehemu inayotumika kwa chakula, nayo ni mdomo, kama nayo itakavyofahamika kuwa chakula ama kinywaji.
- Hakiharibu saumu kitu ambacho kwamba huwezi kukiepuka, kama vile vumbi la njiani, na mabaki ya chakula yaliosalia kati ya meno.



Dawa inayotumika kama chakula inaharibu saumu.



Sindano ya penicillin haiharibu saumu.(Hii ni sindano ya kukinga au kutibu madhara yanayosababishwa na bacteria).



Vipuliza hewa vya kutibu pumu haviharibu saumu.



Wanja haiharibu saumu.



Sigara zinaharibu saumu.



Mabaki ya chakula yaani katika meno hayaharibu saumu.

## 2. Kufanya Tendo la Ndoa

Kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U { Mmehalalishiwa usiku wa saumu kuingiliana na wake zenu} (Al-Baqarah – Aya 187). Na "Ar-Rafath" ni neno la kiarabu lililotumika katika Aya hii kumaanisha kuingiliana – yaani kufanya tendo la ndoa, basi yoyote atakaye ingiliana na mkewe au mumewe hali ya kuwa amefunga, saumu yake itakuwa imeharibika, na atalazimika ailipe siku hiyo, na pamoja na kuilipa ni juu yake kutoa kafara nzito, nayo ni kuacha huru mtumwa, akiwa hatopata mtumwa wa kumuacha huru, atalazimika kufunga miezi miwili mfululizo, na akiwa hawezi kufunga atalazimika kulisha masikini sitini, kama ilivyothibiti kutoka kwa Abu Hureiah t Anasema: " Alikuja mtu mmoja kwa Mtume (saw) akasema nimeangamia. Mtume akamuuliza: Una nini? Akajibu: Nimemuingilia mkewangu ndani ya Ramadhani. Mtume akamuuliza: Waweza kuacha mtumwa huru?. Akajibu: Siwezi.. Mtume akamuuliza: je waweza kufunga miezi miwli mfululizo? Akasema: Siwezi. Mtume akamuuliza: Basi waweza kulisha masikini sitini?. Akasema: Siwezi. Mtume akamwambia: Kaa. Akakaa. Mtume (saw) akaleta chombo ambacho ndani yake mna tende. Akasema: Chukua (hiki chombo) wende ukatolee sadaka. Akasema yule mtu: Je kuna fakiri zaidi yetu? (yaani maskini kuliko familia yake). Mtume akacheka mpaka yakaonekana magego ya meno yake, akasema: Lisha familia yako ( hizo tende)" [Imwpokewa na Bukharin a Muslim.]. Na inakuwa kafara inafuata mfumo huu, hivyo basi mtu asilishe maskini isipokuwa akiwa hawezi kufunga hiyo miezi miwili mfululizo, wala asifunge isipokuwa ikiwa hawezi kuacha huru mtumwa.

Na inamlazimu mwanamke kutoa kafara ikiwa ameridhiana na mumewe kufanya tendo la ndoa, na iwapo amelazimishwa na mumewe kuingiliana basi saumu yake imeharibika na itamlazimu

mwanamke huyo kuilipa saumu hiyo peke yake bila ya kutoa kafara.
Na ni katika maana ya jimai (tendo la ndoa) kujitoa manii kwa kukusudia, Mtu akitokwa na manii kwa kubusiana, au kwa kugusa au kwa kutumia mkono, basi saumu yake itaharibika, kwa sababu hiyo ni katika shahawa inao haribu saumu, na itakuwa ni juu yake kuilipa saumu yake wala hatolazimika kutoa kafara, kwa sababu kafara imekuja kwa tendo la ndoa peke yake.
Mtu akibusu au akigusa au akifikiria akatokwa na madhii saumu yake ni swahihi. kwa kutokuwa na dadili yakuharibu saumu kwa kutokwa na madhi
Mtu anapo lala akaota, au akatokwa na manii bila ya shahawa kama kuwa mgonjwa, saumu yake ni swahihi kwa sababu hayakutoka kwa hiyari yake.
Mtu anapo amka na janaba la tendo la ndoa kabla ya alfajiri au akaota, saumu yake ni swahihi na ni juu yake kuoga ili apate kuswali alfajiri na jamaa, imethubutu kutoka kwa bibi A'isha t Kwamba Mtume ﷺ Alikuwa akiingiliwa na Alfajiri na yeye akiwa na janaba la mkewe, kisha akioga na akifunga

### 3. kujitapisha kwa kusudi

Nao ni mtu kutoa kilichoko tumboni kutokana na chakula au kinywaji kwa njia ya mdomo kwa kusudi, ama akishindwa na akatoka bila ya khiyari yake haiathiri saumu yake kwa neno lake Mtume (saw) ( Mwenye kushindwa na matapishi basi hana haja ya kukidhi na mwenye kujitapisha kwa kusudi basi alipe)

### 4. Damu ya Heidhi na Nifasi

Wakati wowote mwanamke atakapo ona damu ya hedhi au nifasi japo kuwa ni wakati wa jioni kabla ya kutwa jua kwa mda mchache saumu yake itaharibika na atawajibika kuilipa

Faida

- Kauli yenye nguvu ni kuwa kuumika hakuvundi saumu kwa sababu Mtume (saw) Aliumika na hali yakuwa amefunga,

Amepokewa kutoka kwa said Al’khudriy t akisema (Aliruhusu Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ Kubusu kwa aliyefunga na kuumika, lakini inachukizwa kuumika kwa ajili ya kudhofika, Aliulizwa Anas bin Maalik t Mulikuwa mukichukiza kuumika kwa alie funga? Akasema la ila kwa ajili ya kudhofika.
- Haidhuru mtu kutokwa na damu katika jaraha, au kung’oa jino au kutokwa na damu za puwa, au kutoa damu kwa ajili ya kujipma, au kujitolea, yote haya hayaharibu swaumu.

# Nyudhuru/Ruhusa za mtu kula ndani ya mwezi wa Ramadhani

## Ruhusa za mtu kula ndani ya mwezi wa Ramadhani

### 1. Ugonjwa

Yaruhusiwa kwa mgonjwa kula ndani ya mwezi wa Ramadhani; kwa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: { Na atakaye kuwa mgonjwa katika nyinyi au katika safari (akafungua baadhi ya siku), basi (atimize) hisabu katika siku nyingine} (Al-Baqarah – Aya 184).
Na ugonjwa amabao waruhusiwa mtu kufungua ni ugonjwa unaosababisha dhiki kwa mgonjwa akifunga, au unaleta madhara kwa mgonjwa iwapo atafunga.
- Kula kwa mgonjwa
Atakapokula mgonjwa (ndani ya Ramadhani) - na ugonjwa wenyewe ni wenye kutarajiwa kupona – inamlazimu kulipa siku

alizokula pindi atakapopona; kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U: {….basi atimize hisabu katika siku nyingine} (Al-Baqarah –Aya 184).

Na ikiwa ugonjwa ni usiotarajiwa kupona – kama vile ugonjwa wa kudumu au ni mtu mzee sana asiyeweza kufunga kabisa, itabidi mtu kama huyu alishe kila siku maskini mmoja nusu kibaba cha mchele au mfano wake katika chakula kinachotumika eneo lake.

### 2. Safari

Inaruhusiwa kwa msafiri kula ndani ya Mwezi wa Ramadhani, na inamlazimu kuilipa saumu hiyo baadaye, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na atakayekuwa mgonjwa katika nyinyi au katika safari (akafungua baadhi ya siku), basi atimize hisabu katika siku nyingine} (Al-Baqarah –Aya 184).

Na safari inyoruhusiwa mtu kula ni ile ambayo kwamba mtu anaruhusiwa kufupisha swala, na ni ile safari ambayo ki-ada ya kwao inatambulika kuwa safari, kwa sharti iwe safari yenyewe inaruhusika kisheria, ikiwa ni safari ya maasi (iliyo kinyume na sheria), au safari ya malengo ya ujanja wa kutaka kufungua basi hairuhusiwi katika safari hiyo kufungua.

Na iwapo msafiri atafunga basi saumu yake inakubalika na atalipwa ujira, kwa hadithi ya Anas ibn Malik asema: “Tulikuwa tukisafiri pamoja na Mtume (saw) wala hakumkosoa aliyefunga kwa asiyefunga, wala ambaye hakufunga kwa aliyefunga” [Imepokewa na Bukhari.].

Lakini kwa sharti ya kwamba saumu hii isimpe shida katika safari yake, ikiwa itampa shida, au itamletea madhara, basi kula kwa msafiri kama huyu ni bora zaidi, kwasababu Mtume (saw) alimuona katika safari mtu aliyefunga amekuwa tabaani sana kwa joto jinsi lilivyokuwa kali, na watu wamemzunguka, akasema Mtume (saw): “ Si katika wema kufunga safarini “ [Imepokewa na Bukhari.].

### 3. Mimba na kunyonyesha

Mjamzito au mwenye kunyonyesha akiwa atakhofia nafsi yake kudhurika kwa kufunga basi anaruhusiwa kula, na atailipa saumu hiyo kama vile mgonjwa; kwa kauli ya Mtume (saw): “Hakika ya Mwenyezi Mungu amemuondoshea msafiri kufunga, na akamshurutisha kuswali, na akamuondoshea (akampa ruhusa ya kula) mjamzito na mwenye kunyonyesha saumu) [Imepokewa na Tirmidhi.].

Na iwapo atakhofia juu ya mtoto wake peke yake bila ya kukhofia nafsi yake anaweza kula, na akailipa baadaye, na anatakiwa alishe kila siku (atakayokula) maskini mmoja; kwa kauli ya Ibn Abbas: t (Na mwenye kunyonyesha na mjamzito watakapokhofia juu ya watoto wao wanaweza kula, na walishe maskini mmoja) [Imepokewa na Abuu Daud.].

4. Damu ya Heidhi na Nifasi

Mwanamke mwenye hedhi au nifasi ndani ya Ramadhani analazimika kula, na ni haramu kwake kufunga, na lau atafunga saumu yake haikubaliwi, na itamlazimu kuilipa tena saumu hiyo, kama ilivyothibiti kutoka kwa A’isha alipoulizwa kulipa kwa mwenye hedhi saumu bila ya kulipa swala – akasema: (Ilikuwa tukitokwa na damu ya hedhi, na tulikuwa tukiamrishwa kulipa saumu, wala hatukuamrishwa kulipa swala) [Imwpokewa na Bukharin a Muslim.]

## Kulipa swaumu

- Muislamu akila siku moja katika Mwezi wa Ramadhani bila ya dharura ni lazima atubie kwa Mwenyezi Mungu na aombe msamaha, kwa sababu kula bila ya sababu ni katika Madhambi makubwa, na ni lazima kulipa masiku aliyokula baada ya Ramadhani kwa haraka, na hii na kwa kauli ya wanachuoni, kwa sababu alikuwa haruhusiwi kula, na asili ni kutekeleza kwa wakati wake.
- Mtu anapokula kwa dharura kama vile mwanamke akiwa katika hedhi, au nifasi, au kwa ajili ya ugonjwa au safari au dharura nyingine aliyo ruhusiwa na sharia basi nilazima kulipa masiku

aliyo kula baada ya Ramadhani, ila akishindwa kufunga, na silazima kulipa kwa haraka bali anaruhusiwa kuchelewesha kwa sharti asiingiliwe na Ramadhani nyingine, kwa hadithi iliyopokelewa na bibi Aisha t Amesema (Nilikuwa na daiwa saumu ya ramadhani na nisiweze kuilipa ila mwezi wa shabani kwa kumshughulikia Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) [Imwpokewa na Bukharin a Muslim.] Lakini inapendekezwa kufanya haraka kukidhi saumu kwa sababu ni kujitoa kwenye dhima, na ni uzuri kwa mtu asije likamtokezea jambo asiweze kufunga baadae kama ugonjwa na mfano wake.

- Na mtu akichelewa kukidhi saumu kwa dharura mpaka akaingiliwa na ramadhani nyingine basi atalazimika kufunga baada ya Ramadhani ya pili.na hana kafara.
- Na akicheleweshा kukidhi bila ya dharura yoyote ile mpaka akaingiliwa na Ramadhani ya pili, basi ni juu yake kwa kauli ya jamhuri ya wanafiqihi, alipe saumu pamoja na kulisha masikini kila siku aliyo kula nusu ya pishi ya chakula cha watu wa mjini.
- Haisharutishwi katika kulipa saumu kufuatanisha, bali inasihi kufuatanisha na kufunga siku mbali mbali kwa neno lake Mwenyezi Mungu “Na atakayekuwa mgonjwa katika nyinyi au katika safari (akafungua baadhi ya siku), basi atimize hisabu katika siku nyingine” (Al-Baqarah –Aya 184).
- Na mwenyezi Mungu hakushurutisha kufuatanisha, na kama ingekuwa ni lazima Mwenyezi mungu angelibainisha.
- Na mtu akiwa anadaiwa na saumu ya Ramadhani, mwanzo atalipa deni la saumu kabla ya kufunga saumu ya sunna kwa sababu Faradhi ndio Asili na ndio inayo tangulizwa, lakini lau atafunga sunna kabla ya kukidhi inafaa, hasa ikiwa saumu yenyewe ina fadhila na asipo funga atakosa fadhila hizo kama siku kumi za fungo nne na saumu ya siku ya arafa na siku sita za mwezi wa mfungo mosi (shawwal) kwa sababu wakati wa kulipa ni mrefu, ingawa Ubora ni alipe kwanza.
- Mwenye kuacha kulipa saumu mpaka akafa, ikiwa alikwa na dharura kwa kutolipa kwake basi hana lolote, kwa sababu

hakukusudia, ama kama alikuwa hana dharura yoyote, basi atalishwa masikini kwa ajili yake, ikiwa ni saumu ya Ramadhani, ama ikiwa anadaiwa saumu ya Nadhiri atamfungia yeye walii wake, na baadhi ya wanachuoni wamesema Mtu anapokufa na akawa na deni la saumu basi atamfungia yeye walii wake sawa iwe ni deni la Ramadhani au Nadhiri kwa hadithi ya bibi Aisha t kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw)Amesema (Mwenye kufariki na Akawa anadaiwa Saumu basi atamfungia yeye walii wake) [ Imwpokewa na Bukharin a Muslim.]

- Na kwa hadithi ya Ibnu Abbas t Asema alikuja mtu kwa Mtume (saw)akasema ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu mama yangu amefariki na anadaiwa saumu ni mlipie? Akasema (Ndio: deni la Mwenyezi Mungu lina haki zaidi kulipwa) [Imwpokewa na Bukharin a Muslim.]

# swaumu za Sunna

## Maana ya saumu za swaumu

### swaumu za Sunna

Saumu yoyote amabayo sio ya lazima na mtu anaifunga ili kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu mungu

Na saumu ya sunna ina fadhila kubwa na malipo makubwa. Katika Hadithi Al-Qudsy kutoka kwa Abu Hureirah t Anasema: Amesema Mtume (saw): “Kila kitendo chema cha mwanadamu malipo yake huongezwa, jema moja hulipwa kwa kumi mfano wake mpaka kufikia mara sabini. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Isipokuwa saumu, kwani hiyo ni yangu mimi, na

mimi ndiye mwenye kuilipa” [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Siku ambazo kwamba ni sunna kufunga.

### 1. Siku sita katika mwezi wa Shawwaal (Mfungo mosi)

Kwa kauli ya Mtume (saw): (Atakayefunga Ramadhani, kisha akafuatiliza kwa kufunga siku sita za Shawwaal, itakuwa ni kama aliyefunga mwaka mzima) [Imepokewa na Muslim.].




Sawasawa awe amezifunga siku sita hizi kwa pamoja kufuatana au siku mbalimbali zisizofuatana.

### 2. Kufunga Siku Tisa za Mwanzo wa Mwezi wa Dhulhijjah. (Mfungo tatu)

Kwa kauli ya Mtume (saw): (Hakuna masiku ambayo matendo mema ni bora zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko masiku haya – yaani masiku kumi ya Dhulhijjah – wakasema (maswahaba): hata jihadi kwa njia ya Mwenyezi Mungu? Akema (Mtume): “Hata jihadi kwa njia ya Mwenyezi Mungu, isipokuwa mtu aliyetoka (kwenda jihadi) yeye mwenyewe na mali yake, wala asirudi na chochote (yaani akafa vitani)” [Imepokewa na Bukhari.].

Na masiku haya yakatiliwa nguvu zaidi na siku ya A’rafa kando na hajj – nayo ni siku ya tisa ya mwezi wa Dhulhijjah; kwa kauli ya Mtume (saw): (Kufunga siku ya A’rafa nataraji kwa Mwenyezi Mungu kusamehewa mtu madhambi ya mwaka kabla yake, na mwaka uliyo baada yake) [Imepokewa na Muslim.].




### 3. Kufunga siku ya A’shuura na siku iliyo kabla yake.

A’shuura

Ni siku ya kumi katika mwezi wa Muharam (Mfungo nne).

Kwa kauli ya Mtume (saw): (Na kufunga siku ya A’shuura nataraji kwa Mwenyezi Mungu kusamehewa kwa mtu madhambi ya mwaka uliyo kabla yake) [ Imepokewa na Muslim.].

Na sababu ya kufunga siku hii ni kama ilivyothibiti kutoka kwa Abdillahi ibn Abbas anasema: (Aliingia Madina Mtume (saw) akawaona Mayahudi wamefunga siku ya A’shuura, akasema Mtume: Ni nini hiki (mnachofanya)? Wakasema: Hii ni siku njema, siku hii ndiyo siku Mwenyezi Mungu aliyowaokoa wana israili kutokamana na maadui zao, basi akaifunga siku hii Nabii Musa. Akasema Mtume: Basi mimi nina haki zaidi kwa Musa kuliko nyinyi, akaifunga Mtume siku hiyo na akaamrisha watu kuifunga) [Imepokewa na Bukhari.].

Na inapendekezwa vile vile kufunga siku ya tisa, kwa ilivyo pokelewa kutoka kwa Mtume (saw) Alisema (Lau nitaishi mpaka Mwaka ujao nitafunga siku ya tisa) [ Imepokewa na Muslim.]

### 4. Kufunga Masiku meupe ya kila mwezi

Masiku meupe

Nayo ni tarehe kumi na tatu, na kumi na nne, na kumi na tano ya kila mwezi katika miezi ya kiislamu, na yameitwa meupe; kwasababu usiku wa masiku haya hunga’ra kwa mwangaza wa mwezi.

Kama ilivyothibiti kutoka kwa AbdulMalik ibn Minhal kutoka kwa babake: Kwamba (babake) alikuwa pamoja na Mtume (saw) akasema (kumwambia mwanaye – AbdulMalik): Alikuwa Mtume (saw) akiwaamrisha kufunga masiku meupe, na akisema: (Masiku) haya ni saumu za mwaka) [Imepokewa na Ibnu Hibbaan.]

5. kufunga siku mbili – jumatatu na alhamisi katika kila wiki.

Kama ilivyopokewa kutoka kwa Abu Hureira t kwamba Mtume ﷺ amesema: "Hupandishwa matendo (juu kwenda mbinguni) kila jumatatu na alhamisi, basi napenda matendo yangu yapandishwe hali ya kuwa nimefunga" [Imepokewa na Tirmidhi.].

6. Kufunga siku Moja na kula siku Nyingine

Bora katika funga za sunnah ni saumu ya Nabii Daud juu yake iwe amani – Alikuwa akifunga siku moja na kuacha siku moja; kutoka kwa Abdillahi ibn A'mru t Anasema: Amesema Mtume (saw): (Hakika saumu ya kupendeza sana mbele ya Mwenyezi Mungu ni saumu ya Daud, na alikuwa akifunga siku moja na kula siku moja) [Imepokewa na Nasaai.].

7. Kufunga Mwezi wa Muharam.

Kutoka kwa Abu Hureira t Anasema: Amesema Mtume (saw): (Saumu ilio bora baada ya Ramadhani ni saumu ya mwezi wa Muharam) [Imepokewa na Muslim.].

8. Kufunga Mwezi wa Shabani

Kutoka kwa Usama ibn Zaid t Asema: Nilisema: (Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, sijapata kukuona ukifunga mwezi wowote mfano wa unavyofunga Shabani. Akasema: Kwa sababu huo ndio mwezi ambao watu wanaghafilika kati ya Rajabu na Ramadhani, na ndio mwezi ambao matendo hupandishwa juu kwa Mola wa walimwengu, basi napenda matendo yangu yapandishwe hali ya kuwa nimefunga) [Imepokewa na Nasaai.].

Ama Katazo lililo kuja katika hadithi ya Mtume (saw) Inayo sema (Ifikapo nusu mwezi wa shabani Musifunge) [Imepokewa na Ibnu Khuzeymah.]
inachukuliwa ni kwa Yule anae khusisha nusu ya mwisho wa shabani kwa kufunga, au kutounganisha shabani na Ramadhani, ama Yule alifunga mwanzo wa shabani, wala asikhusishe mwisho wa shabani wala asiunganisha na ramadhani hapana ubaya kwa mtu huyu kufunga.

## Masiku yanayo haramishwa kufunga na yanayo chukiza

### Kwanza: Masiku yanayo haramishwa

1. Ni haramu kufunga siku za idd Mbili Amepokeya Abuu Hurayra t Kwamba Mtume (saw) (Amekataza kufunga siku mbili: Siku ya Adh'ha na Siku ya Fitr) [Imepokewa na Muslim.]
2. Ni haramu kufunga siku za Tashriiq, nazo nisiku tatu baada ya iddul'Adh'ha, Amesema Mtume (saw) (siku za tashriiq ni siku za kula na kunywa) [Imepokewa na Muslim.]
Lakini inafaa kwa mahujaji kufunga ikiwa hija yake ilikuwa ni kwania ya Tamattu na Qiran na asipate mnyama wa kuchinja kwa neno lake Mwenyezi Mungu (Basi mwenye kujistarehesha kwa kufanya umra kisha ndio akahiji, basi achinje mnyama aliye mwepesi kumpata.na asiye pata afunge siku tatu katika hija na siku saba mtakapo rudi) [Al-baqara: 196]
3. Niharamu kufunga Siku ya shaka, nayo nisiku ya thalathini ya mwezi wa Shabani, ikiwa usikuwake ni usiku wa mawingu au vumbi lakutowezekana kuonekana Mwezi, Kwa neno lake Ammaar t (Mwenye kufunga siku ya Shaka hakika amemuasi babake Qaasim (saw) [Imepokewa na Tirmidhi na akasema ni hadithi nzuri swahihi.]

### Pili: Masiku Ambayo ni makruhu kufunga

1. Ni makuruhu kupwekesha mwezi wa Rajabu kwa kufunga, kwa sababu alama za watu wa jahiliya ni kutukuza mwezi wa Rajab, na katika kuhusisha kuufunga ni katika kuhuisha alama zao

2. Ni makuruhu kufunga siku ya ijumaa kwa kukatazwa kufanya hivyo, Amepokeya Abuu Hureyra t Amesema: Amesema Mtume (saw) ( Asifunge mmoja wenu siku ya ijumaa ila afunge siku kabla yake au siku baada yake) [ Imepokewa na Muslim.]

Isipokuwa ikisadifu ada ya mtu basi atafunga wala si makuruhu kwake kufunga.

3. Ni Makruhu kuunganisha Saumu, nao ni mtu kufunga siku mbili mfululizo bila ya kufunguwa, kwa sababu Mtume alikataza kuunganisha Saumu, Amepokeya Abdullah bin Umar t Amesema Amekataza Mtume (saw) Kuunganisha wakasema kumuuliza wewe waunganisha akasema (mimi si kama nyinyi mimi nalishwa na kunyeshwa) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

Saumu kwa mtizamo wa ki-afya

Hakika ya saumu inasaidia katika kutibu magonjwa ya ngozi, na sababu ya hili ni kwamba saumu inapunguza kiwango cha maji ndani ya damu na kusababisha damu kupungua kiwango chake katika ngozi, ambapo jambo hili linapelekea kuongezeka kwa kinga za ngozi na kuweza kupambana dhidi ya viini hatari na magonjwa ya tumboni yanayosababishwa na bacteria.

## Maelezo

1. Muislamu nilazima kujilazimisha katika Ibaada zake na sharia ya Mwenyezi Mungu, asifunge siku zilizo katazwa na sharia kufunga, au kujikhusisishia masiku kufunga ambao sharia haikuhusisha kama kufunga siku ya ishirini na saba mwezi wa Rajab au kufunga Nusu Shabani, kwa kauli yake Mtume(saw) (Mwenye kuzusha katika dini yetu hii jambo ambalo halimo ataregeshewa mwenyewe) [ Imepokewa na Muslim.]

2. Muislamu ni lazima awe Mbali na kutukuza Alama za Makafiri, asihishimu Masiku wanayoyatukuza kwa kufunga au kwa Sampuli ya Ibaada aina yoyote ile.

# (Usiku wa cheo)Lailatu Al-qadr

## Kwanini ukaitwa usiku wa cheo (usiku waheshima)?

1. Kumesemwa: Ni kwasababu ya kuutukuza, kama ilivyo kaulu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na (Mayahudi ) hawakumhishimu Mwenyezi Mungu kama inavyotakiwa kumhishimu} (Al-An-a’m – Aya 91).
Na maana yake: Ni kwamba huu usiku ni wenye hishima; kwa kuteremshwa Qur’ani ndani yake na kupatika na kushuka malaika, na ni usiku wa baraka na rehema na msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu.
2. Inasemekana: Al-qadr kwa maana ya kubanika kwa kuwa ndogo sana, kama kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: { na yule ambaye amepungukiwa riziki yake (riziki yake imebanika kwa kuwa ndogo sana), atoe katika kile alichopewa na Mwenyezi Mungu} ( At-twalaq – Aya 7).
Na maana ya kubanika kwa kuwa ndogo sana: Ni kule kufichika katika elimu za watu kutambua hasa usiku huo ni usiku wa tarehe ngapi.

3. Na inasemekana: Al-qadr kumaanisha makadirio, kwa maana: katika usiku huu ndiyo kunakadiriwa hukumu za mwaka ulioko; kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U: { Katika (usiku) huu hubainishwa kila jambo la hikima} (Ad-Dukhan – Aya 4).

## Fadhla za Lailatul.Qadr na Hadhi yake

### 1. Katika usiku huu ndio Qur'ani iliteremshwa.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Hakika Tumeiteremsha (Qur'ani) katika Laylatu-Qadr (usiku wenye hishima kubwa)} (Al-qadr –Aya 1).

### 2. Usiku huu ni bora kuliko miezi elfu moja.

Mwenyezi Mungu U Amesema kuhusu usiku huu: {Huo usiku wa hishima ni bora kuliko miezi elfu }. (Al-qadr –Aya 3).

Yaani matendo ndani ya usiku huu ni bora kuliko matendo ya miezi elfu ambayo hayako katika usiku huu wa hishima.

### 3. Huteremka Malaika na Jibril katika Usiku huo.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Huteremka Malaika na roho katika usiku huo } [Al-qadr –Aya 4]. Na makusudio ya roho: Ni Jibril.

Kutoka kwa Abu Hureira t Anasema: Amesema Mtume (saw): (Lailatu Al-qadr ni tarehe ishirini na saba au ishirini na tisa, hakika Malaika usiku huo ni wengi sana katika ardhi kuliko idadi ya changarawe za mawe) [Fat-hul-Baary (4/255).].

### 4. Ni usiku wa amani.

Anasema Mwenyezi Mungu U: { Ni amani (usiku) huo mpaka mapambazuko ya alfajiri } (Al-qadr – Aya 5).

Yaani usiku wote huo ni kheri tupu, hakuna shari kutoka mwanzo wake hadi kupambazuka kwa alfajiri.

### 5. Ni usiku wenye baraka.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Kwa yakini tumeteremsha (Qur'ani) katika usiku uliobarikiwa – bila shaka Sisi ni waonyaji} (Ad-Dukhan – Aya 3).

Ibn Abbas t Asema: ”Yaani: Usiku wa Lailatu Al-qadr”.

6- Ndani ya usiku huu ndiyo yanakadiriwa makadirio ya mwaka mzima.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Katika (usiku) huu hubainishwa kila jambo la hikima} (Ad-Dukhan – Aya 4).

7. Atakayesimama kufanya ibada katika usiku huu hali ya kuamini na kutarajia malipo atasamehewa madhambi

Amesema Mtume (saw): (Atakayesimama (kufanya ibada) usiku wa Lailatu Al-qadr kwa imani na kutarajia malipo, basi atasamehewa yote yaliyotangulia katika madhambi yake) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Ni Usiku upi wa Laylatul Qadr ?

Mwenyezi Mungu U hakuuweka wazi usiku huu ili watu wapate kujitahidi katika kumi la mwisho wa mwezi wa Ramadhani na haswaa katika siku zisizogawanyika kwa mbili (katika kumi hili) nazo ni usiku wa tarehe 21, 23, 25, 27, na 29; kwa kauli ya Mtume (saw): “Kuweni na hamu (kujitahidi ili kuipata)) usiku wa Lailatu Al-qadr katika siku zisizogawanyika kwa mbili ndani ya kumi la mwisho wa mwezi wa Ramadhani” [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Mambo yanayo pendekezwa kufanywa ndani ya Laylatul.Qadr

1. Kufanya itikafu

Nayo ni katika kumi lote wala sio usiku wa Lailatu Al-qadr peke yake, kutoka wa A’isha t anasema: “Alikuwa Mtume (saw) akifanya itikafu katika kumi la mwisho wa mwezi wa Ramadhani” [ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

2. Kusimama usiku wake hali yakuamini na kutaraji malipo

Amesema Mtume (saw): (Atakayesimama usiku wa Lailatu Al-qadr hali ya kuwa na imani na kuridhia, husamehewa yote

yaliyotangulia katika madhambi yake) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

### 3- Kuomba Dua:

Kutoka kwa A'isha Allah awe naye radhi Anasema: (Nilisema: Ewe Mtume wa Allah, ikiniafikia Lailatu Al-qadr niombe kitu gani? Akasema: Sema: Ewe Mola! Hakika yako wewe ni mwenye kusamehe (madhambi) tena Mkarimu wapenda sana kusamehe, basi nisamehe (makosa yangu)" [Imepokewa na Tirmidhi.].

### 4. Kuwaamsha watu wa nymbani kwa ajiliya ibaada

Amepokeya bibi A'isha t Amesema: (Alikuwa Mtume (saw) likiingia kumi la mwisho akijifunga kibwebwe na akikesha usiku wake na akiamsha wake zake) [Imepokewa na Bukhari.]

## Alama za Laylatul.Qadr

### 1. Ni usiku ambao hauna joto wala baridi kali.

Kutoka kwa Jaabir ibn Abdillahi t Anasema: Amesema Mtume (saw): (Nilikuwa nimeoneshwa Lailatu Al-qadr, kisha nikasahaulishwa, nayo iko katika nyakati za usiku wa kumi la mwisho, nao ni usiku wenye bashasha [ Twalqat: ikiwa hakuna joto wala baridi ya kuudhi] unang'ara [ Baljah: yenyekung'ara] usio na joto wala baridi) [ Imepokewa na Ibnu Khuzeymah].

### 2. Jua linatokeza Asubuhi yake jeupe halina Miale.

Anasema Ubeyi ibn Ka'ab t alipoulizwa kuhusu dalili za Lailatu Al-qadr: "Kwa dalili aliyotueleza Mtume (saw) ni kwamba jua linachomoza siku hiyo halina miale". [Imepokewa na Tirmidhi]

Na katika upokezi wa Muslim: " Jeupe halina miale".

## Maelezo

1. Ni juu ya kila muislamu kuzidisha kufanaya ibada katika siku kumi za mwisho za mwezi wa ramadhani kwa sampuli ya ibada mbali mbali kwa sababu ni masiku bora ya mwaka.
2. Ni juu ya Muislamu asipoteze wakati wake katika masiku matukufu na msimu wa kheri kwa kufanya upuzi na mchezo na kuzurura masokoni, na kutembea sehemu zisizo kuwa nahaja.

# Itikafu(kukaa ndani ya msikiti)

## Maana ya Itikafu

### Itikafu ki-lugha.

Ni kujilazimisha na jambo fulani, na kujifunga nafsi yako juu ya kulifanya jambo hilo.

### Itikafu ki-sheria.

Ni kujilazimisha kukaa ndani ya msikiti kwa ajili ya kumuabudu Mwenyezi Mungu.

## Usharia wa Itikafu

Kufanya itikafu ni katika matendo yaliyo bora sana, na twa'a tukufu. Kutoka kwa A'isha Mungu awe naye radhi anasema: "Alikuwa Mtume (saw) akifanya itikafu (maisha yake) katika kumi la mwisho wa mwezi wa Ramadhani mpaka Mungu alipomkabidhi roho yake (Mtume alipokufa)" [Imepokewa na Bukhari.].
Na inaruhusiwa ki-sheria kwetu sisi na kwa waliokuja kabla yetu kufanya itikafu, Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ( Na

tulimusia Ibrahimu na Ismaili Itakaseni nyumba yangu kwa ajili ya wale wanaoizunguka kwa ajili ya kutufu na wanaokaa hapo na (kwa ajili ya) wanaorukuu na kusujudu hapo pia”) ( Al-Baqarah –Aya 125).

## Hukumu ya Kukaa Itikafu

Kufanya itikafu ni sunna wakati wowote ule, na ubora wake zaidi kuifanya ni katika kumi la mwisho wa mwezi wa Ramadhani; kwasababu Mtume ﷺ alidumu katika kufanya itikafu kwenye kumi la mwisho wa mwezi wa Ramadhani [Zaadul-Ma’ad.].

## Masharti ya Kukaa Itikafu

### 1. Kutia niya.

Mwenye kufanya itikafu anatia niya ya kujilazimisha kukaa ndani ya msikiti kwa lengo la kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na kumuabudu; kwa kauli ya Mtume (saw): ( Hakika kila Amali ni kwa niya ya mtu) [Imepokewa na Bukhari na Muslim].

### 2. Msikiti atakaofanyia Itikafu uwe ni msikiti wa kuswali swala ya jumaa.

Haifai kufanya Itikafu isipokuwa Msikitini kwa neno lake Mwenyezi Mungu ( Hali yakuwa mumekaa itikafu msikitini) [Al-baqara: 187]

Na kwa kitendo chake Mtume (saw) kwani hakufanya Itikafu isipokuwa Msikitini.

Na kufanya itikafu msikiti usio swaliwa Jamaa itampelekea Mwenye kufanya Itikafu kutoka mara kwa mara kuenda kuswali jamaa kwa sababu Swala ya jamaa kwake ni wajibu, na kule kutoka mara kwa mara hukosekana maana ya Itikafu, ama mwanamke husihi Itikafu yake msikiti wowote sawa uwe msikiti waswaliwa jamaa au hauswaliwi, na hii ni ikipelekea kutopatikana fitna katika kukaa kwake itikafu, ama ikipatikana fitna haifai na atakatazwa.

Na ubora uwe msikiti unaswaliwa swala ya ijumaa lakini hilo si katika masharti ya itikafu

### 3. Kuwa twahara kutokamana na hadathi kubwa.

Haifai kwa mwenye janaba kufanya Itikafu, wala mwenye damu ya heidhi, wala mwenye damu ya nifasi, kwa kule kukosekana kwao ruhusa ya kukaa ndani ya msikiti.

Kufunga sio Sharti ya Kukaa Itikafu.

Haizingatiwi kufunga kama ni sharti ya kukaa Itikafu. Kwasababu imepokewa kutoka kwa Ibn Umar kwamba Umar alimuuliza Mtume (saw) akisema: Niliweka nadhiri wakati wa Jahiliya (kabla ya kuwa Muislamu) kwamba nifanye Itikafu usiku mmoja ndani ya Masjid haram. Mtume (saw) akasema: ( Basi itekeleze nadhiri yako [Imepokewa na Bukhari.].

Lau ingekuwa kufunga ni sharti ya kufanya Itikafu basi isingekubalika Itikafu ya Umar kufanya usiku. kwasababu usiku watu hawafungi. Na imethibiti vile vile kwamba Mtume (saw) alifanya Itikafu katika kumi la kwanza la mwezi wa Shawwal [Imepokewa na Muslim.], na katika kumi hili kuna masiku ya Idi ambayo mtu hafai kufunga, kama vile vile (saumu na Itikafu) ni ibada mbili ambazo hazikuambatana pamoja, kwa hivyo sio lazima kufanya nyingine kwa kupatikana mojawapo.

## Wakati wa kukaa Itikafu

Yaruhusiwa kufanya Itikafu siku yoyote ile, na wakati wowote ule, isipokuwa ubora wake ni isipunguwe Itikafu mchana mzima au usiku mzima; kwasababu haijapokewa kutoka kwa Mtume (saw) wala kutoka kwa yoyote katika maswahaba zake ambaye alifanya chini ya hapo.

## Kukaa Itikafu katika kumi la Mwisho la Mwezi wa Ramadhani

- Nao ndio wakati bora zaidi wa mtu kufanya Itikafu, kama ilivyithibiti kutoka kwa A'isha t kwamba Mtume (saw) alikuwa akifanya Itikafu kwenye kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhani mpaka alipokufa [Imepokewa na Bukhari].
- Na yoyote atakayenuia kufanya Itikafu katika kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhani ataswali alafajiri ya kuamkia tarehe ishirini na moja katika msikiti atakaofanya Itikafu, kisha ndio aanze Itikafu yake. Imepokewa kutoka kwa A'isha Mungu awe naye radhi akisema: (Alikuwa Mtume (saw) akifanya Itikafu kila mwezi wa Ramadhani, na pindi anaposwali swala ya asubuhi alikuwa akienda mahali pake ambapo atafanyia Itikafu yake) [Imepokewa na Bukhari.].
- Na inamalizika Itikafu kwa kuzama kwa jua siku ya mwisho ya mwezi wa Ramadhani, na ubora ni kuondoka kutoka kwenye Itikafu mapema sana asubuhi ya siku ya Idd, na ndivyo ilivyothibiti kwa wengi watu wema waliotangulia.

## Hikima ya kufanya Itikafu.

Hikima iliyoko katika Itikafu ni kujikatisha na mambo ya kidunia na kutojishughulisha nayo na watu wake, na kujitengea mda maalumu kwa ajili ya ibada, basi inamlazimu mwenye kufanya Itikafu kuutengea moyo mambo haya.

## Mambo yanao ruhusiwa kufanywa ndani ya Itikafu

1. Kutoka msikitini pasipo na budi kufanya hivyo, kama kutoka kwa ajili ya kula na kunywa, ikiwa hana mtu wa kumletea chakula, na kutoka ili kukidhi haja zake (kwenda choo), kama ilivyothibiti kutoka kwa A'isha akisema: (Alikuwa Mtume (saw) pindi anapofanya Itikafu akiinamisha kichwa chake kuja kwangu nikimchana nywele, na alikuwa hatoki nje isipokuwa kwa haja ya kibinadamu) [Imepokewa na Muslim.].

2. Kutengeza nywele zake vizuri na kuzichana; kama ilivyopokewa kwa Hadithi iliyopita.
3. Kuzungumza na watu maneno yenye faida, na kuwajulia hali zao, lakini hairuhusiwi kuzidisha katika kujuliana hali, kwasababu ni kinyume cha makusudio ya Itikafu.
4. Watu wake na jamaa zake kumzuru, na kutoka mahali pake pa Itikafu ili kuwaaga jamaa zake. Imepokewa kutoka kwa Swafiya Binti Huyay – Mungu awe naye radhi anasema: “Alikuwa Mtume (saw) yuko kwenye Itikafu nikaenda kumtembelea siku moja nikamuinamia (kuongea naye) kisha nikasimama ili niende zangu, akasimama pamoja nami ili kunisindikiza” [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Mambo yenye kuharibu Itikafu

1. Kutoka msikitini bila ya dharura yoyote kwa kukusudia – hata kama kipindi ulichotoka ni kichache kiasi gani -;

Kama ilivyothibi kutoka kwa A’isha t akisema: (Na alikuwa (Mtume) haingii nyumbani isipokuwa kwa haja ya kibinadamu) [Imepokewa na Muslim.].

Na kwasababu kule kutoka kuna acha kipindi fulani kukosekana kwa mwenye kufanya Itikafu ndani ya msikiti, na huku kuwa ndani ya msikiti ni nguzo ya Itikafu.

2. Kufanya tendo la ndoa – hata kama kufanya huko kutakuwa ni usiku.

Kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U: {Wala msichanganyike nao, na hali mnakaa Itikafu misikitini} (Al-Baqarah – Aya 187).

Na hukumu hii ya tendo la ndoa pia inasimamia: Kuondosha matamanio bila ya kuingiliana kama kujitoa manii kwa kutumia mkono, na kumshikashika mkeo sehemu zisizo za siri.

3. Kuwa na niya ya kuivunja Itikafu.

Anaponuia Muislamu kufanya Itikafu siku maalumu, kisha akavunja kuifanya hiyo Itikafu yuwafaa ailipe, kama ilivyothibiti kutoka kwa A’isha – Mungu awe naye radhi asema: (Alikuwa

Mtume (saw) anapotaka kufanya Itikafu akiswali alfajiri kisha ndio aingie mahali pake pa itikafu [ Mahali pake pa Itikafu: Yaani sehemu anayokaa kufanyia Itikafu.]. Na hakika aliamrisha kufungwa khibai (hema) lake na likafungwa – Hali ya kutaka kufanya Itikafu kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhani -; Zainab naye aliamrisha kufungwa khibai lake na likafungwa. Na aliamrisha mwengine katika wake za Mtume (saw) kufungwa khibai lake na likafungwa. Mtume alipomaliza kuswali alfajiri akatizama, akaona makhibai (mahema). Akasema: Ni wema munataka? Akachukua khibai lake akalinyanyua [ Kulinyanyua: Yaani kulikunjakunja lile khibai.]. Na akaacha Itikafu katika Ramadhani mpaka kumi la kwanza la mwezi wa Shawwal" [Imepokewa na Bukhari na Muslim]. Na katika upokezi mwengine: (kumi la mwisho la mwezi wa Shawwal).

4. Mwenye kufanya Itikafu hatembelei mgonjwa wala hashindikizi jeneza.

Na yuwabaki kufanya ibada mahali pake pa Itikafu.

# ZAKAH

## Zaaka hukumu yake na masharti yake

## Maana ya zaka

### Zaka kilugha.

Ni kukua kwa kitu na kuzidi.

### Zaka kisheria.

Ni kiwango maalumu cha mali kinachotolewa wakati maalumu ili kupewa watu maalumu.

## Umuhimu wa zaka

Zaka ni faradhi katika faradhi za Dini ya Kislamu, na ni nguzo ya tatu katika nguzo za Uislamu, Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na simamisheni swala na toeni zaka} (Suratu An-Nur: 56),

Na akasema Mtume (saw): (Umejengwa Uislamu kwa mambo matano: Kushuhudia ya kwamba hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake, na kusimamisha Swala (tano za kila siku), na kutoa Zaka, na kuhiji nyumba tukufu (Al-ka'abah – ilioko Makkah), na kufunga Mwezi wa Ramadhani) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Hukumu ya anayekataa kutoa Zaka.

Anayekataa kutoa Zaka, ima amekataa kwa kupinga kwamba sio lazima kutoa [Juhuud: Ni kukataa kuwajibishwa kwake.], au kwa ubakhili.

### 1. Mwenye kukataa kutoa Zaka kwa kupinga.

Anayepinga wajibu wa Zaka basi amekufuru kwa makubaliano ya umma wote – ikiwa mtu huyu anajua vizuri wajibu wa Zaka; kwa sababu atakuwa amemzulia uwongo Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

### 2. Anayekataa kutoa Zaka kwa ubakhili.

Atakayekataa kutoa Zaka kwa ubakhili wake basi huchukuliwa kutoka kwake Zakaa kwa nguvu na wala hawi kafiri kwa kufanya hivyo kukataa kutowa Zaka kwa ubakhili.
Na atakuwa ametenda dhambi kubwa miongoni mwa madhambi makubwa na ni uovu mkubwa sana.

Kwa kauli ya Mtume (saw) kuhusu wanaokataa kutoa Zaka: “Mtu yeyote aliye na hazina ya dhahabu na fedha na wala haitolei Zaka basi atachomwa nayo katika moto wa Jahannam na itajaaliwa kama vinoo ambavyo atapigwa navyo kwenye migongo na vipaji kila akipata ubaridi (yakipoa makali ya moto) anaregelewa tena (kupigwa navyo), mpaka Allaah Amalize kuhukumu waja wake siku ambayo ni sawa na miaka elfu khamsini. Kisha ndio ataoneshwa njia yake ikiwa ni ya peponi au motoni” [ Imepokewa na Bukhari.]

Na lau atapigana na kukataa kutekeleza amri ya zaka basi mpigeni vita mpaka arudi katika kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu, na atoe zaka, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U: {Lakini wakitubu na wakasimamisha swala na wakatoa zaka, basi iacheni njia yao (waacheni} (Suratu At-tawbah: 5).

Na kwa kauli ya Mtume (saw): (Nimeamrishwa niwapige watu vita mpaka washuhudiye ya kwamba hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na wasimamishe Swala, na watoe Zaka, watakapofanya hivyo basi imeharamishwa kwangu damu yao na mali yao isipokuwa kwa haki ya Uislamu, na malipo yao yako kwa Mwenyezi Mungu) [Imepokewa na Muslim.].

Na Abubakar t alipiga vita mtu yoyote ambaye alipinga wajibu wa zaka, na akasema: (Naapa kwa Mungu ya kwamba nitampiga vita yoyote aliyetenganisha kati ya Swala na Zaka, kwa hakika hiyo Zaka ni haki ya mali, Wallaahi kama wakinizuilia hata kwa (kamba ya) kutiwa shemere (anayofungwa

mnyama kwenye pua zake) nitapambana nao madamu walikuwa wakiitoa kwa Mtume) [ Imepokewa na Bukhari.].

## Hekima ya watu kuwajibika kutoa Zaka.

1. Ni kuzisafisha nafsi na kuzitakasa kutokana na ubakhili, na madhambi, na makosa, Anasema Mwenyezi Mungu U: "Chukua sadaka(zaka) katika mali zao, na uwaombee (dua) safishe na kwatakasa kwa ajili ya hizo (sadaka zao)" (suratu At-Tawbah: 103).
2. Kusafisha mali na kuikuza, na kutia baraka ndani yake, kwa kauli ya Mtume (saw): "Sadaka haipunguzi chochote (inapotolewa) katika mali" [Imepokewa na Muslim.].
3. Ni mja kupewa mtihani katika kutekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu, na katika kutanguliza mapenzi yake kwa Mungu zaidi kuliko mapenzi yake ya kupenda mali.
4. Kuwaliwaza mafakiri na kuziba pengo la mahitaji ya wenye haja, jambo ambalo linaongeza mapenzi, na linatimiliza kiwango cha juu sana katika usaidizi wa kijamii baina ya waislamu wa eneo moja.
5. Kujizoezesha katika kutoa kwa njia ya Mwenyezi Mungu.

## Fadhla ya kutoa Zaka

1. Ni sababu ya kupata Rehema za Mwenyezi Mungu, Anasema Mwenyezi Mungu U: {Na rehema yangu inaweza kukienea kila kitu. Lakini nitawaandikia (kweli kweli kabisa) wale wanaojikinga na yale niliyowakataza, na wanaotoa Zaka na wanaoziamini Aya zetu} (Al-A'raf: 156).
2. Ni sharti ya kupatikana Nusra ya Mwenyezi Mungu, Anasema Mwenyezi Mungu U: {Na bila shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anayesaidia dini yake.Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kushinda. Wale ambao tukiwamakinisha, (tukiwaweka uzuri) katika ardhi husimamisha Swala na wakatoa Zaka} (Al-hajj 40-41).

3. Ni sababu ya kufutiwa madhambi, Amesema Mtume (saw): (Na sadaka hufuta madhambi kama vile maji yanavyozima moto” [Imepokewa na Tirmidhi.].

## Mali Yanayo wajibika jutolewa Zaka

| |
|---|
| 1-(vitu) vinavyotoka ndani ya ardhi |
| 2-Zaka za Dhahabu na Fedha |
| 3-Zaka ya Mali ya biashara |
| 4-wanyama wa mifugo |




## Masharti ya mtu kulazimika kutoa Zaka

### 1. Uislamu
Haikubaliwi Zaka kwa kafiri, kwasababu Mwenyezi Mungu U hakubali matendo yake.

### 2. Kuwa huru (muungwana).
Haikubaliwi kwa mtumwa kutoa Zaka, kwasababu mali yake ni milki ya bwana wake.

### 3. Kumiliki Nisabu.(kiwangu)

### Maana ya Nisabu.

Nisabu.
Ni kiwango maalumu cha mali ambacho kwamba kikifikiwa basi inalazimika mali hayo kutolewa Zaka.

### Masharti ya Nisabu.

1. Iwe Nisabu ni ziada ya mahitaji ya dharura ambayo kwamba mtu hatosheki kwa kuyapata mahitaji hayo, kama chakula, mavazi na makazi, kwasababu Zaka ni wajibu kwa lengo la kuwaliwaza mafukara. Hivyo basi inatakiwa mwenye kutoa hiyo mali asiwe ni mtu muhitaji.
2. Iwe Nisabu inamilikiwa na mtu maalumu umiliki wa kiukamilifu, basi haiwajibiki Zaka kwa mali ambayo haimilikiwi na mtu maalumu, kwa mfano: mali iliyokusanywa kwa lengo la kujenga msikiti, au mali iliyowekwa wakfu kwa maslahi ya ummah, au mali iliyoko kwenye hazina za jumuia za mambo ya kheri.

### 4. Mali kupitiwa na Mwaka

Mwaka

Ni mwaka wa kiislamu) uliyokamilika.
Na hii ni kwamba ipite miezi kumi na mbili ya kalenda ya mtizamo wa mwezi hali ya kuwa Nisabu iko kwenye miliki ya mwenye mali. Na sharti hili ni peke yake kwa pesa (dhahabu na fedha), na mapato ya biashara, na wanyama wa mifugo. Ama mazao ya kilimo na matunda, na madini, hazina iliyozikwa ardhini sio sharti kwa vitu hivi kupitiwa na mwaka.

# Zaaka ya (vitu) vinavyotoka ndani ya ardhi

## Maana ya Vinavyotoka kwenye Ardhi

Vinavyo toka Ardhini

Kila kinachotoka ndani ya ardhi, na kinawezekana kunufaika nacho.

Kinachotoka ndani Ardhini ni Sampuli mbili: ni Nafaka na Matunda na Madini, na Hazina iliyozikwa Ardhini

## Kwanza: Nafaka na Matunda

### Maana ya Nafaka na Matunda

#### Nafaka

Kila tembe (mbegu) inayohifadhiwa katika mtama, ngano na mfano wa hii.

#### Matunda

Kila tunda linalohifadhiwa kama tende, na zabibu, na lozi.

### Hukumu ya kutoa Zaka ya nafaka na matunda

Zaka ya nafaka na matunda ni wajibu, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U: {Na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake} (Al-An-am: 141);

na kwa kauli ya Mtume (saw): (Kwa yaliyo nyunyiziwa (maji) ya mbinguni (yaani mvua) au mito au kama yamemea yenyewe [ Yamemea yenyewe: Ni mavuno yaliyomea kwa kunywa maji bila ya kunyunyuziwa maji, ima ni kwa unywevu wa mizizi yake kuwa na umajimaji au kupitia kwa mvua na umajimaji (kama vile hali ya umande) na mito.] (inafaa mtu atoe) ushuri moja (yaani atoe sehemu moja kwa kumi ya mavuno atakayopata (1/10), na yaliyonyunyiziwa kwa kumwagiwa maji [ Yaliyonyunyiziwa kwa kumwagiwa maji (na mtu mwenyewe): Yaani amemwagia maji na akagharamika katika kuyatoa hayo mavuno.] nusu ushuri (yaani atoe sehemu moja kwa tano yamavuno atakayopata (1/20)" [ Imepokewa na Bukhari.].

### Masharti ya kuwajibika kwa Zaka ya nafaka na matunda

1.Iwe ni katika (mavuno) yanayohifadhika.

Ikiwa si mavuno ya kuhifadhika, na ni mavuno ya chakula chake cha siku basi hakuna Zaka ya kutolewa hapo; kwasababu sio ya kuhifadhiwa hayakuzidi mahitaji yake ya kula kwake kwa kila siku, hivyo basi hayamtoshelezi mahitaji yake; kwa kukosekana utulivu wa kunufaika (na yale mavuno).

### 2. Iwe ni (mavuno) yanayopimwa.

Na hii iwe ni katika (mavuno) yanayopimwa kwa mizani ili kulinganishwa na saaq, nayo ni kipimo (fulani), hii inaashiria kutambulika kwa mavuno hayo; kwa kauli ya Mtume (saw): (Hakuna katika nafaka, wala tende Zaka yoyote mpaka ifike saaq tano [Al - Wasaq: Ni Sawa na Pishi 60.] ) [Imepokewa na Muslim.].

Basi ikiwa sio mavuno yanayopimwa kama vile mboga, na mabogaboga, hakuna Zaka kwa vitu hivi.

### 3. Iwe imemea kwa kupandwa na mtu katika Ardhi yake.

Ama yaliyomea peke yake bila kupandwa na mtu Mavuno hayo hayana Zaka.

### 4. Mavuno yafikie Nisabu.

Nayo ni Makapu matano, kwa kauli ya Mtume (saw): (Hakuna katika nafaka wala tende Zaka yoyote mpaka ifike saaq tano) [Imepokewa na Muslim.],

na hii itakuwa ni swaa'(Pishi) mia tatu, nayo ni sawa na (612kg) katika ngano nzuri, na yanachanganywa matunda ya aina moja pamoja ya mwaka mzima ili kukamilisha nisabu; kama sampuli tofautitofauti za tende, kwa mfano tende za sukkari zinachanganywa na tende za barhy, kwasababu ni sampuli za mavuno aina moja, wala haifai kuchanganya aina tofauti ya mavuno kwa nyengine, hivyo basi haifai kuchanganya ngano kwa shayir, wala ngano kwa tende.

### Wakati wa kuwajibika kutoa Zaka ya Nafaka na Matunda.

Inawajibika utoaji wa Zaka katika nafaka pindi pale zitakapokomaa kuwa tayari, na katika matunda pale yatakapoanza

kuonesha uzuri wake, kwa hali ya kwamba yamefikia kuwa mazuri kulika, na atakayeuza matunda au nafaka baada ya wakati wake wa kuwajibika kutolewa Zaka basi Zaka itakuwa ni kwa aliyeuza, kwasababu alikuwa akimiliki mavuno hayo wakati ule wa kuwajibika kutolewa Zaka.

### Kiwango kinachowajibika kwa Zaka ya nafaka na matunda

1. Yalazimu kutoa ushuri (10%) Kwa (mavuno) ambayo kwamba hayakunyunyiziwa maji Kwa kuenezewa (na mtu) au kwa kugharamika (kwa mtu), kama vile yaliyonyunyiziwa kwa maji ya mvua au mito.
2. Yalazimu kutoa nusu ushuri (5%) kwa yaliyo nyunyiziwa kwa kuenezwa (na mtu) na kugharamika, kama yale yanayo nyunyiziwa kwa maji ya visima.
3. Yalazimu kutoa rubui tatu ya ushuri (7.5%) kwa yaliyo nyunyiziwa kutumia njia zote mbili, kama vile yanayo nyunyiziwa mara nyengine kwa maji ya mvua na mara nyengine kwa maji ya visima.

Na dalili ni kauli ya Mtume (saw): (Kwa yaliyo nyunyiziwa kwa maji ya mbinguni na mito, na maziwa (yatolewe Zaka) ushuri, na kwa yaliyo nyunyiziwa kwa kutumia saania [ Saania: Ni mnyama anayetumika kunyweshea] (yatolewe Zaka) nusu ushuri) [Imepokewa na Muslim.].

### Kuharibika kwa Nafaka na Matunda

Nafaka zikiharibika au matunda bila ya kuharibiwa na mtu au kushindwa kuzichunga vizuri, basi hakuna Zaka kwa mavuno hayo, ikiwa kuharibika kwake baada ya kupita mda wa kuwajibika kwake kwa kushindwa kuzichunga vizuri, au kuyaharibu mavuno kwa kusudi jambo hili halimuondoshei mtu jukumu la kutoa Zaka, atalazimika atekeleze jukumu hili hivyo hivyo.

### Zaka za Asali

Ameeleze Ibnu Abdulbar (R) kwamba Jumuhuri ya wanavyoni kwamba asali haitolewi zaka nahilo ndilo lililo wazi, kwa sababu hakuna dalili katika Qur’ani wala katika Hadithi ya kuwajibisha

kuitolewa zaka, na asili nikutowajibika lolote mpaka ipatikane dalili ya kuwajibisha

# Pili: Madini na hazina iliyozikwa Ardhini

## Maana ya Madini na hazina iliyozikwa ardhini

### Madini

Ni chochote kinachotolewa ndani ya ardhi ambacho kwamba sio sampuli ya ardhi kama vile dhahabu, fedha, vyuma, na vijiwe vya tunu kama vile almasi na rubi, na risasi, na vyenginevyo katika vitu asili vinavyotolewa ndani ya Ardhi.

### Hazina iliyozikwa ardhini

Ni Mali iliyozikwa ndani ya ardhi kwa kuekwa na mtu, kutokana na dhahabu, na fedha, na mfano wa vitu hivi.

## Hukumu ya zaka ya madini na hazina iliyozikwa ardhini

Ni lazima; kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U: {Enyi mlioamini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyokutoleeni katika ardhi} (Al-Baqarah: 267),


na kauli ya Mtume (saw): (Na katika hazina iliyozikwa ardhini (toeni) khumusi (1/5)) [Imepokewa na Bukharin a Muslim.].

## Masharti ya kutoa zaka ya hazina iliyozikwa ardhini

Hakuna masharti yoyote ya zaka ya hazina iliyozikwa ardhini, basi atakapomiliki mtu hio hazina iliyozikwa ardhini anafaa kutoa zaka yake moja kwa moja.

## Kiwango cha kuwajibika mtu kutoa zaka ya madini na hazina iliyozikwa ardhini

Ni wajibu mtu kutoa khumusu (1/5) kwa kichache au kingi atakachopata katika madini na hazina iliyozikwa ardhini, kwa jumla ya kauli ya Mtume (saw): (Na katika hazina iliyozikwa ardhini (toeni) khumusi) [Imepokewa na Bukharin a Muslim.].



Dhahabu



Fedha



Risasi



# Zaka za Dhahabu na Fedha

## Maana ya Dhahabu na Fedha

Dhahabu na Fedha
Dhahabu na fedha, na chochote kinachosimamia nafasi ya vitu hivi viwili miongoni mwa pesa za karatasi zinazotumiwa siku hizi.

## Hukumu ya Zaka ya Dhahabu na Fedha.

Ni lazima; kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U: {Na wale wanaokusanya dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Mwenyezi Mungu, wape habari za adhabu inayoumiza } (At-Tawbah 34)
na kwa kauli ya Mtume ﷺ: ( Mtu yeyote aliye na hazina ya dhahabu na fedha na wala haitolei Zaka basi atachomwa nayo katika moto wa Jahannam na itajaaliwa kama vinoo ambavyo atapigwa navyo kwenye migongo na vipaji kila akipata ubaridi (yakipoa makali ya moto) anaregelewa tena (kupigwa navyo), mpaka Allaah Amalize kuhukumu waja wake siku ambayo ni sawa na miaka elfu khamsini. Kisha ndio ataoneshwa njia yake ikiwa kama ni ya peponi au motoni" [Imepokewa na Muslim.].

## Masharti ya kuwajibika kutolewa kwa zaka ya Dhahabu na Fedha

1. Kupitiwa na mwaka.
2. Kuzimiliki kiukamilifu.

3. kufika nisabu ya zaka.

## Nisabu ya zaka ya Dhahabu na Fedha

1. Nisabu ya dhahabu ni Dinari ishirini (85gms)
2. Na Dinari moja ya dhahabu = (ina dhahabu) gramu nne na robo, hivyo basi inakuwa nisabu ya dhahabu kwa gramu 4.25 x 20 = 85gms za dhahabu safi (ambayo haikuchanganywa na kitu).
3. Nisabu ya fedha ni Dirham mia mbili (595 gms)

Na Dirham moja ya fedha = (ina fedha) 2.975gms, hivyo basi inakuwa nisabu ya fedha kwa gramu = 2.975 x 200 = 595gms za fedha safi.

Mfano: Ikiwa gramu moja ya dhahabu = inauzwa Dolari 30, basi inamlazimu mtu kutoa zaka ikiwa amefikisha 85 x 30 = Dolari 2550 dolari.



Dhahabu



Fedha



Pesa za karatasi

## Kiwango kinachofaa kutolewa zaka ya Dhahabu na Fedha

Kiwango kinachomlazimu mtu kutoa zaka katika dhahabu na fedha na stakabadhi za kiashirio cha pesa ni robo ushuri = 2.5%. Basi kwa kila Dinari ishirini ya dhahabu atatoa zaka nusu Dinari, na itakayozidi (zaidi ya Dinari ishirini) itapigiwa hisabu, iwe imezidi kidogo au sana.
Na kwa kila Dirhamu mia mbili za fedha atatoa zaka Dirhamu tano, na kitakachozidi atakipigia hisabu; kwa kauli ya Mtume ﷺ:
(Ikiwa unamiliki Dirhamu mia mbili, na zimekamilisha mwaka, basi yatakiwa utoe Dirhamu tano, na si juu yako kutoa chochote – yaani – katika dhahabu mpaka umiliki Dinari ishirini, basi ukiwa na Dinari ishirini, na umemaliza nazo mwaka, basi itakulazimu utoe nusu ya Dinari, na zitakazozidi utafanya kwa hisabu hii) [Imepokewa na Abu Daud.].
- Mfano wa kufahamisha:-
Mtu anamiliki Dolari 9000, na imepita mwaka mzima hali ya kuwa anazimiliki hizo pesa, je analazimika kutoa zaka?
Kwanza: Tutahisabu nisabu ya zaka kwa mtizamo wa dhahabu au fedha kama ifuatavyo:
Nisabu = Gramu thamanini na tano katika dhahabu safi = 85 x bei ya gramu moja ya dhahabu safi (inavyouzwa) siku ile ya

kulazimika kwake kutoa Zaka, na tukisie kwamba gramu moja yauzwa = Dolari 30.
= 85 x 30 = Dolari 2550.
Kwa hivyo Nisabu yake = Dolari 2550, hivyo basi itakuwa mali ya mtu huyu imefika nisabu, na imekamilisha mwaka mzima, kwa hivyo inamlazimu kutoa zaka.
Pili: Tutahisabu kiwango anachofaa kutoa zaka kama ifuatavyo: - Kiwango cha kutolewa zaka = 2.5%.
= 9000 x 2.5/100 = Dolari 225.
Kwa hivyo huyu mtu yafaa atoe kutoka kwa mali yake Dolari 225 kama zaka.




- Kukusanya Dhahabu na Fedha pamoja

Mtu anapo miliki dhahabu na fedha lakini zikawa hazifikii kiwango cha kutolewa zaka, kauli yenye nguvu ni kuwa hatowajibika kutoa zaka, wala hata zikikusanywa pamoja ili zifikiye kiwango, kwani uwajibu ni kutoa dhahabu pekeyake na fedha pekeyake kwa sababu ni vitu viwili tofauti, na hakuna dalili ya kuzikusanya pamoja ili ifikie kiwango, na kwa neno lake Mtume (Hakuna chini ya wakiya tano zaka) [Imepokewa na Bukharin a Muslim]
na atakae zikusanya dhahabu na fedha itakuwa amewajibisha zaka chini ya wakia tano

## Zaka ya mapambo ya wanawake

Mapambo ya wanawake yako sampuli mbili: Mapambo ya dhahabu na fedha, na mapambo yasiyokuwa ya dhahabu wala fedha.

### 1. Mapambo ya dhahabu na fedha.

Kitengo cha kwanza: Mapambo yaliyokusudiwa kwa lengo la kuhifadhiwa au kuwekwa kama akiba ya baadaye kunapotokea jambo, au imenunuliwa kwa nia ya kufanya biashara, basi zaka hapa ni lazima kutoa.

Kitengo cha pili: Mapambo yaliyokusudiwa kwa lengo la kutumiwa, basi uzuri zaidi ni kuitolea zaka ili kijiepusha na lawama, kwa hakika mwanamke mmoja alimjilia Mtume ﷺ pamoja na binti yake, na mkononi mwa binti yake kuna bangili mbili [ Imepokewa na Abu Daud.] nzito za dhahabu, (Mtume ﷺ) akamwambia: " Je watolea zaka hizi bangili) Akasema: Hapana. Akasema (Mtume ﷺ): (Je utafurahia Mwenyezi Mungu akuvalishe bangili kwa hizi bangili mbili za moto?) Akasema: Yule binti akazivua, akampatia Mtume ﷺ, kisha akasema: "Hizo ni za Mwenyezi Mungu na Mtume wake" [Imepokewa na Abu Daud.]

Na kuna wanavyuoni ambao hawawajibishi mapambo ya wanawake kutolewa zaka; kwasababu hayo mapambo sio mali inayotarajiwa kukua, lakini ni pambo la mtu binafsi yuwatumia na kunufaika nayo kama vile nguo na fanicha na vyombo, na ni katika mahitajio ya mwanamke na virembesho vyake, na asili ya mali ni kukua au kuweza kukuzwa ndio ilazimike kutolewa zaka.

Na ubora wa hali ni mtu kutoa zaka kwa mapambo yaliyokusudiwa kwa matumizi ambayo si kinyume na sheria na kwa lengo la kujirembesha; kwasababu kauli hii iko katika hali nzuri zaidi na kujiondoa kwa lawama; kwa kauli ya Mtume ﷺ: (Wachana na linalokutia shaka na ufanye lile lisilokutia shaka) [Imepokewa na Bukhari].



Mapambo ya dhahabu.



Mapambo ya fedha.

## 2. Mapambo Yasiyo kuwa ya Dhahabu wala Dedha.

Kama vile almasi, yakut, lulu, na mfano wa hizi, basi vitu hivi havitolewi zaka hata vikawa vingi kiasi gani, isipokuwa vikikusudiwa kwa lengo la biashara vitatolewa zaka vitakuwa vimeingia katika mali ya biashara.



Lulu


Yakut


Almasi

# Zaka ya Mali ya biashara

## Maana ya Mali ya biashara

### mali ya biashara

Kila kilichoandaliwa kwa lengo la kuuzwa na kununuliwa ili mtu apate faida.
Ziliitwa hivi, kwasababu hazidumu, bali hutokeza na kupotea, kwani mfanyi biashara huwa hataki hizi bidhaa ki-uhakika, bali anataka faida ya pesa.

Na bidhaa za biashara zimekusanya vitu vyote vya sampuli zote za mali ambayo sio pesa zinazotumika kununulia vitu, kama vile magari, nguo, vitambaa, vyuma, mbao, na vyenginevyo vilivyoandaliwa kwa biashara.



Vyuma



Gari



Mbao



Nguo

## Hukumu ya zaka ya Mali ya biashara.

Ni lazima; kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U: {Enyi mlioamini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyokutoleeni katika ardhi} (Al-Baqarah: 267).
Jumla ya wanavyuoni wametaja kwamba makusudio ya aya hii ni: Zaka ya mali ya biashara, na kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U: {Chukua kutoka kwa mali zao sadaka} (At-tawbah: 103) , na mali ya biashara ni katika mali zilizo dhahiri, basi Kwa ajili hii ikawajibika kutolewa zaka.

## Masharti ya kulazimika mtu kutoa zaka ya Mali ya biashara.

1. Kiwango chake kifikie nisabu, na nisabu inakadiriwa kwa kipimo cha dhahabu na fedha.
2. Ikamilishe mzunguko wa mwaka mzima.
3. Iwe imekusudiwa kwa lengo la biashara; na hii ni kwamba iwe imekusudiwa kama kuchuma; kwa kauli ya Mtume (saw): “Hakika ya matendo ni kwa niya ya mtu” [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Mtu atakapobadilisha niya yake kutoka kwa biashara na kutumia bidhaa hizo basi hukatika hisabu ya mzunguko (mwaka), na akirudia niya ya biashara ataanza tena upya kuhisabu mzunguko mpya, ila akiwa amekusudia kufanya udanganyifu kwa lengo la kuondosha jukumu la kutoa zaka, basi hapa mzunguko haukatiki.

- Mfano: mtu anunue ardhi mwezi wa mfungo nne kwa nia ya kufanya biashara kisha alipofika shabani akageuza nia na akakusudia kujenga nyumba ya kukaa, hapa mwaka utakatika, kisha mfungo mosi akamua kuifanyia biashara mwaka wake utahisabiwa mfungo mosi ila kama alifanya hivyo kwa njia ya hila na kukimbia asitoe zaka basi mwaka hautakatika.

## Jinsi ya kutoa zaka ya Mali ya biashara

Mali yanapo pitiwa na mwaka zinakaguliwa bidhaa alizouza na kupewa bei ile ambayo kwamba iko sasa sokoni, kisha inatolewa zaka ya hayo mali kwa kutolewa bidhaa zenyewe au kima chake kwa njia ya pesa, kulingana na mahitaji ya mafakiri.

## Vipi mfanyi biashara atafanya hisabu ya zaka ya mali ya biashara?

1. Atahisabu vitu vyote alivyonavyo katika bidhaa za biashara kwa kima cha wakati wa sasa.
2. Ataongeza pesa zote alizonazo, sawasawa iwe pesa zile alizitumia katika biashara ama hakuzitumia.
3. Aongeze vyote anavyodai watu katika madeni.
4. Aondowe chochote anachodaiwa.
5. Atoe Zaka kwa yatakayobakia (baada ya kufanya hivi vyote), nayo ni robi ushuri (2.5%)

Zaka inayowajibika kutolewa = (kima cha bidhaa za biashara + pesa + madeni anayodai watu – madeni anayodaiwa) x (kiwango cha kutolewa Zaka 2.5%).

- kuhisabu zaka za biashara hutizamwa mali ya zaka yaliko atazifafanua na azitie kima siku ile yakupasa zaka akijisaidia na orodha ya hisabu ya mali bila yakuzingatia faida au hasara katika hisabu ya faida na hasara
- Vitu viliyo tayarishwa kwa ajili ya kubebea mali kama mifuko au mikebe havitiwi kima pekeyake ikiwa havikununuliwa kwa ajili ya kuviuza pekeyake, ikiwa zitatumiwa kwa kuviuza kibiashara

basi vitatiwa kima vikiwa hupita kima cha mali yale. ikiwa havizidi kwa kima kama karatasi za kukunjia hivingii katika kutuwa kima.
- kutia kima huwa kwa Mfanya biashara yeyote awe ni wakuuza jumla au rejareja kwa thamani ambayo aweza kununuliya mwisho wa mwaka kima cha mabadaliko Nacho hutofautiana na bei ya kuuza na kima cha kuuza sokoni au cha tarehe au nukuu.
- bei zikitofautiana wakati wa kupasa zaka na wakati wakuzitoa inazingatiwa yatapewa siku ya kupasa ni sawa zizidi ama zipunguwe.
Na kuhusiana na suala la kutoa zaka kwa bidhaa zinazo safirishwa kabla ya kuzipokea, zaka za bidhaa hizi zitamuhusu yule anayezimiliki. Na umiliki wake unapatikana kwa kuzipokea bidhaa iliyonunuliwa kwa maelezo ya kuwa ipo njiani. Ikiwa imenunuliwa kwa mfano makabidhiano ya msingi yawe katika bandari (gati) la muuzaji. Umiliki halisi utapatikana kwa kupokea shehena hiyo. Na ikiwa imenunuliwa na makabidhiano ya msingi yawe katika bandari (gati) la mnunuzi basi umiliki wa mali hii unapatikana na kwa kitendo cha kufika tu shehena ya mali hiyo katika bandari (gati)..
- mali ya biashara yakiwa ni ya pesa mbali mbali, au ni dhahabu au fedha basi hutiwa kima kwa kujuwa kiwango kinacho pasa kutowa kwa sarafu ambayo aitumia mfanya biashara na hilo ni kwa bei ilioko siku ya kupasa zaka.
- na mizigo ya biashara ambayo mwenye kununua alitangulizia kuilipia lakini hajapokea ile mizigo basi zaka zake hazimpasi mwenye kununua bali humpasa mwenye kuuza.

## Zaka za malighafi yakutumika kwa sanaa na vyenye kusaidia

1. Ama malighafi ya kimsingi yaliyo tayarishwa kwa ajili ya sanaa kama chuma kwa ajili ya kutengeneza magari, na mafuta ya kutengeneza sabuni, inapasa kutolewa zaka kulingana na thamani

ambayo zilo nunuliwa mwisho wa mwaka, haya vilevile ni kwa wanyama na nafaka na mimea na kama hivyo.
2. Vitu vya kusaidia ambavyo haviingi kwenye orodha za kufanyia vitu vya sanaa kama vitu vya kuchomea havina zaka ni kama mali thabiti.
3. Zaka za bidhaa zisokuwa za sanaa na ambavyo havijesha kutengezwa:
4. Hutolewa Zaka zisizokuwa za sanaa
Na ambazo hazijesha kutengenezwa, zaka za mali ya biashara kulingana na thamani yake kwenye yalivo hivi sasa mwisho wa mwaka
- Kukusanyika sababu nyengine ya zaka pamoja na mali ya biashara
Yakikusanyika pamoja na mali ya biashara mali mengine yakutolewa zaka kama mali yamakulima hutolewa zaka za mali ya biashara

## Sampuli ya Mali Yasiyopaswa Zaka

- Mali yanayo toka baharini kama lulu, na marijani, na Samaki, ila yakiwa ni Mali ya kufanyia biashara hutolewa zaka za Mali ya Biashara.
- Mali yaliyo tayarishwa kuajirishwa kama majumba na magari hayana zaka, zaka zake ziko kwenye ijara lake likifikia kiwango cha zaka na kupitiwa na mwaka.
- Vyombo vya dharura zake kama gari na nyumba hayana zaka.

### Kumiliki Nisabu

Je inashurutishwa kumiliki nisabu katika kipindi chote cha mwaka, mwanzo wa mwaka hadi mwisho wa mwaka? Ama yatosha kukamilika kwa nisabu mwanzo wa mwaka na mwisho wake? Ama mazingatio ni kukamilika kwa nisabu mwisho wa mwaka?
Mazingatio ni kukamilika kwa nisabu mwanzo wa mwaka na mwisho wake; kwa ugumu wa kuweka vipimo vya kipindi chote

cha mwaka mzima, basi inazingatiwa mwanzo wa mwaka kwa kupatikana sababu ya kulazimika kutolewa kwa zaka, na mwisho wa mwaka kukamilika mzunguko wake, na wepesi kwa muislamu ni kujiwekea mda maalumu kama vile mwezi wa Ramadhani au mwezi wowote ule kuhisabu mali yake na kuitolea zaka.

Zaka ya Raslimali

Kinachotolewa zaka katika mali za biashara ni raslimali ambayo kwamba imekusudiwa kwa lengo la kununua na kuuza ili mtu apate faida, ama raslimali ambayo kwamba ni ya mali za kukaa hazizunguki katika biashara yaani si za kununuliwa ili ziuzwe, basi raslimali kama hii haihisabiwi wakati wa kuhisabu bidhaa za biashara wala haitolewi zaka, mfano wake ni kama makabati, na jokofu/firiji ambazo zinahifadhi bidhaa za kuuzwa, na magari yanayobeba bidhaa, na vyombo vya kubebea bidhaa, na mfano wake.

## Zaka za Hisa

### Maana ya Hisa

Hisa.

Sehemu anayolipwa mtu baada ya kupatikana faida katika sehemu zilizo sawa kutokana na raslimali ya mtu aliyotowa kwenye shirika la umoja wa kuchanga

Mfano wake: Shirika la umoja wakuchanga lina raslimali Dolari milioni tatu, iligawanywa raslimali yake wakati wa kufunguliwa kwake vigawanyo elfu kumi, kila kigawanyo Dolari (300), kigawanyo hichi ndio hisa, na mwenye hisa ni mshiriki katika shirika kwa kiwango cha alichonacho katika hisa.

### Hukumu ya kuzunguka kwa zaka ya Hisa.

Ni Mubah, Inaruhusiwa iwapo kazi ya shirika hilo si haramu, au haina mambo yaliyoingiliana na riba.

### Namna ya kutoa zaka za Hisa

Idara ya kampuni itabeba jukumu lakuwatolea zaka kwa niyaba yao ikiwa imeelezwa hilo kwenye mpango wake wa kimsingi, au awe ametegemezea hilo Yule mwenye hisa

- Idara ya kampuni ikibeba jukumu la kutoa zaka kongamano la fiqhi la umoja wa mua'tamr wa kislamu kwamba zaka zimefungamanishwa na kapuni kwa kuizingatia kuwa ni mtu wakimazangatiwa likichukuliwa kutoka kwenye kaida ya kuchanganya iliyoko kwenye sunna takatifu kuhusu zaka za wanayama, na wamezieneza baadhi ya wanavioni wa fiqihi kwa mali yote kwa kuwa huzingatiwa mali ya wote wenye kuchangia ni kama mali ya mtu mmoja na hufardhiwa zaka kwa mazingatiwa haya kuhusu kiwango na kiyasi cha zaka na mfano wa hayo
- Msimamo wa jumhuri ya wenye ilimu nikutoishika kaida ya kuchangaya katika zaka za makampuni bali huangaliwa fungu la kila mwenye kushiriki peke peke.
Na ni muhimu kutaja kwamba mkutano wapili la kongamano la kiutafiti wakiilimu umefuata maoni ya jamhuri kwenye kadhia haukushika kaida ya kuchangaya bali iliyatizama kila mali peke yake kwa hivyo ukapitisha yafuatato:
- Kwenye makampuni haya ambayo wanashiriki watu kadha hautizamwi mkusanyiko wa faida za kampuni bali huangaliwa kila yenye kumkhusu mwenye kushiriki pekeyake
- na niwajibu juu ya idara ya kampuni kuweka mbali hisa zisizopaswa na zaka kama hisa za waqfu ya mambo ya kheri, na hisa za makundi ya mambo ya kheri, na asili ya mali thabiti, ambavyo hayapaswi na zaka kama majengo, na maofisi na vyombo, na magari mahsusi na kampuni ikitowatolea zaka hapo itawalazimu wenye hisa kujitolea wenyewe kwa namna ifuatayo:
1. Hisa za makampuni za makulima hutolewa zaka zake kama zaka za nafaka na matunda.
2. Hisa za makampuni ya biashara hutolewa zaka zake, mali ya asili na faida zote, na hukisiwa hisa kwa kima cha sokoni wakati wakuwajibika zaka.
3. Hisa za makampuni ya sanaa hutolewa zaka zake faida safi wala sio vyombo vya kukodisha na majengo na mfano wake.
4. Akiuza mwenye hisa hisa zake wakati wa kupitiwa na mwaka yatakuswanya thamani ya mali yake, na atayatolea zaka, ama

mwenye kunuwa atatolea hisa alizo nunuwa kwa namna ilivo tangulia.

# Zaaka ya wanyama wa mifugo

## Maana ya wanyama wa mifugo

Wanyama wa Mifugo
Ngamia, Ng'ombe, Kondoo na Mbuzi.

## Hukumu ya Zaka ya Wanyama wa Mifugo

Ni lazima; kwa kauli ya Mtume (saw): (Hakuna mwenye ngamia, wala ng'ombe, wala kondoo na mbuzi, ambaye hatoi Zaka ya vitu hivi isipokuwa atakuja (mnyama huyu asiyetolewa Zaka) siku ya Kiama hali ya kuwa amenona sana, (Mnyama huyo) atampiga mtu wake kwa pembe zake, na atamkanyaga kwa kwato zake [ Kwato: sehemu ya chini katika mguu wa mnyama anyotumia kukanyagia na kutembelea.], kila anapoisha wa mwisho anarudi tena wa kwanza, mpaka watakapohukumiwa watu wote) [Imepokewa na Muslim].

## Masharti ya kuwajibika kwa mtu kutoa Zaka ya Wanyama wa Mifugo

1. Wanyama wawe wamekamilisha mwaka mzima wakiwa kwa mwenye kuwamiliki; kwa kauli ya Mtume(saw) : (Hakuna Zaka kwa mali yoyote mpaka ipitiwe na mzunguko mwaka) [Imepokewa na Ibn Maajah].
2. Awe ni mnyama wa kwenda malishoni; kwa kauli ya Mtume (saw): "Kwa kila ngamia wa kwenda malishoni, kwa kila ngamia arubaini (toa zaka) ibn labun mmoja" [Imepokewa na Nasaai.].

Na ngamia anayekwenda malishoni: Ni yule ambaye chakula chake ni mimea ya ardhini, na nyasi zilizoruhusiwa – Nazo ni zile zilizomea kwa kujaaliwa na Mwenyezi Mungu bila kupandwa na mtu; ama ikiwa chakula cha mnyama huyo ni kile ambacho mfugaji anakipanda mwenyewe, basi mnyama huyo haihisabiwi kuwa ni mnyama wa kwenda malishoni hivyo basi hatolewi Zaka mnyama huyo.

3. Awe ni mnyama aliyekusudiwa kufaidisha watu kwa Maziwa yake na kuongeza idadi kuzaa au kuzalisha, asiwe mwenye kubebeshwa Mizigo, na ngamia mwenye kubeba mizigo: Ni yule anayetumika kulima shamba au kunywesha Maji Ardhi au kubeba vyombo au kubeba mizigo mizito.Na ngamia mwenye kubeba mizigo hawajibiki kutolewa Zaka, kwasababu kwa hali hii anaingia katika mahitaji ya mtu ya ki-asili kama vile nguo. Ama akikusudiwa kwa lengo la kukodishwa basi Zaka yake itakuwa ni katika yale yanayopatikana kwenye malipo ya kukodishwa, pindi utakapokamilika mwaka.
4. Wawe wanyama wamefika nisabu ya kisheria ya zaka.

## Nisabu ya kisheria ya zaka ya Wanyama wa Mifugo

### Kwanza: Nisabu za ngamia na kiwango kinachowajibika mtu kutoa kwa kila Nisabu.

Kutoka kwa Anas Ibn Malik radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie, kwamba Abubakar Swidiq radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie

alimuandikia: (Hii ni faradhi ya Zaka ambayo kwamba ameifaradhisha Mtume (saw) na wakaitekeleza waislamu, na ambayo kwamba Mwenyezi Mungu amemuamrisha Mtume wake (saw), kwa kila ngamia ishirini na nne na chochote kilichoko chini ya hapo katika mbuzi. Katika kila ngamia watano (atoe Zaka) mbuzi mmoja. Na wakifika ngamia ishiri na tano hadi thelathini na tano atoe binti makhaadhw mmoja [ Binti makhaadhw: Ni ngamia wakike aliyekamilisha mwaka moja.] wa kike. Wakifika thelathini na sita hadi arubaini na tano atoe binti labun mmoja [ Binti labun: Ni ngamia wakike aliyekamilisha miaka miwili.] wa kike. Wakifika arubaini na sita hadi sitini atoe hiqqah mmoja [ Hiqqah: Ni ngamia wakike aliyekamilisha miaka mitatu.]. Wakifika ngamia sitini na moja hadi sabini na tano atoe jadh.a' mmoja [ Jadh-a': Ni (ngamia wakike) aliyekamilisha miaka mine.]. Na ambaye hana isipokuwa ngamia wanne basi hana Zaka ya kutoa isipokuwa mfugaji mwenyewe akitaka kutoa, na wanapofika ngamia watano atatoa mbuzi mmoja [ Wala hairuhusiwi katika kondoo au mbuzi anayetolewa isipokuwa kondoo aliyefikisha miezi sita, na mbuzi aliyefikisha mwaka mmoja..] " [ Imepokewa na Bukhari.].

## Nisabu na zaka ya Ngamia

| Idadi ya ngamia | kiwango kinachowajibika kutolewa Zaka |
|---|---|
| 5 : 9 | Mbuzi mmoja |
| 10 : 14 | Mbuzi wawili |
| 15 : 19 | Mbuzi watatu |
| 20 : 24 | Mbuzi wane |
| 25 - 35 | Binti makhaadhw (aliyefikisha mwaka) |
| 36 - 45 | Binti labun (ali efikisha miaka miwili) |
| 46 - 60 | Hiqqah (aliyefikisha miaka mitatu) |

| | |
|---|---|
| 61 - 75 | judh'a |
| 76 - 90 | Binti labun wawili |
| 91 - 120 | Hiqqah wawili |
| 120:.... | Nakwakila ngamia 40 Binti labuni<br>Na kwakila ngamia 50 Hiqqah |

## Pili: Nisabu za Ng'ombe na kiwango kinachowajibika kutoa kwa kila Nisabu.

Kutoka kwa Muadh Ibn Jabal radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie asema: (Mtume (saw) alinituma kwenda Yemen, akaniamrisha nichukue (yaani Zaka kutoka kwa watu wa Yemen) kwa kila ng'ombe thelathini tabia' mmoja [ Tabii' na Tabiia': Ni ng'ombe aliyekamilisha mwaka mmoja.], na kwa kila ng'ombe arubaini musinna mmoja) [ Musinna: Ni aliyekamilisha miaka miwili.]" [Imepokewa na Abu Daud.].

## Nisabu na zaka ya za Ng'ombe

| Idadi ya ng›ombe | Kiwango kinachowajibika kutolewa Zaka |
|---|---|
| 30 – 39 | Tabii' (ng'ombe aliyefikisha mwaka mmoja) |
| 40 – 59 | Musinnah (ng'ombe aliyefikisha miaka miwili) |
| 60 – 69 | Tabii' wawili |
| 70 – 79 | Tabii' mmoja na Musinnah mmoja |

## Tatu: Nisabu za Kondoo na Mbuzi, na kiwango kinachowajibika kutolewa Zaka kwa kila Nisabu.

Imepokewa kutoka kwa Anas radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie, kwenye Hadith iliyotangulia: (Na Zaka ya kondoo na mbuzi wanaokwenda malishoni ikiwa wamefikia arubaini hadi mia na ishirini ni mbuzi mmoja, wakizidi mia na ishirini hadi mia mbili watolewe mbuzi wawili, wakizidi mia mbili mpaka mia tatu watolewe mbuzi watatu, na wakizidi mia tatu basi kwa kila mia atoe mbuzi mmoja, na ikiwa mtu ana kondoo au mbuzi wanaokwenda malishoni lakini ni chini ya arubaini

basi mtu huyu hana Zaka yakutoa, isipokuwa mfugaji akipenda mwenyewe kutoa) [Imepokewa na Bukhari.].

### Nisabu na Zaka ya Kondoo na Mbuzi

| Idadi ya kondoo au mbuzi | Kiwango kinachowajibika kutolewa Zaka |
|---|---|
| 40 - 120 | Mbuzi mmoja |
| 121 - 200 | Mbuzi wawili |
| 201 - 300 | Mbuzi watatu (na kila wakizidi mia anazidi mbuzi mmoja) |

## Sifa ya Mali yanayo wajibika zaka

Wajibu katika kutoa zaka ni zitokamane na mali ya katikati siyo yale yaliyo bora mno wala yalio maovu, ni wajibu wa msimamizi wa zaka atunze miaka yenye kupasa kwa kuwa hazitoshelezi duni ya hizo, kwa sababu ni kuwadhuru mafukara, wala hatukiwi ya mali juu yake kwa sababu ni kuwadhulumu matajiri, na vile vile hachukui mgonjwa na mwenyeila na mkubwa mkongwe, kwa sababu hamnufaishi fukara, kwa upande mwingine hamchukuwi wakuliwa aliyenona aliye tayarishwa kuliwa, wala aliye mlezi mwenye mtoto wala mwenye mimba wala wenye kupendeza macho ambayo ni yale mali matukufu ambayo kuyachukuwa ni kumdhuru tajiri kwa kuwa mtume alisema (Tahadharini na mali yao matukufu) [Imepokewa na Bukhari]

## Kuhusu kuchanyisha wanyama

Nao ni sambuli mbili

### kuchanganya wanyama wenyewe

Nako nikuwa yale mali yameshirikiana, baina ya wawili katika kumiliki kwa kueneya kati mwao kiyasi chakuwa fungu la mmoja halijipambanui na la mwingine, na kuchangaya huku huwa kwa kurithi au kwa kununua

### Sampuli ya pili kuchanganyisha kwa sifa

Nako nikuwa fungu la kila mmoja nilenye kulibaini kwa kujulikana na hukusanywa pamoja kwa ujirani tu.

Nako kwa sampuli zake zote mbili huyafanya mali hayo kuwa kama mali ya namna moja, mkusanyiko wake ukifikia kiwango, Na awe washirika wa wiwli ni miongoni mwa wenye kupaswa kutoa zaka, ikiwa mmoja wao ni kafiri kutangamana hakusihi, wala hakuwi na athari, na hushirikiyana mali mawili kwenye kulala pamoja na kuishi na yashirikiyane kwenye kwenda malishoni wanakwenda pamoja na kurudi pamoja na kukamuliwa maziwa, na malisho na fahali wa kupiga awe ni mmoja, yakipatika masharti haya mali mawili huwa nikama mali ya namna moja, kwa neno lake Mtume (saw) (Havikusanywi vilio tafauti wala haviwekwi mbali vilo pamoja kwa kuogopa kutoa zaka na yenye kuwa yawashirika wawili wataregeleyana kati mwao kwa usawa) [Imepokewa na Ibnu Khuzeymah]

kuchanganyisha kuna athari kuhusu kupasa zaka nakuto pasa, na hilo la husiana na wanyama tu.

Na mfano wa kukusanya kati ya walio mbali mbali

Ni watu wa tatu kila moja amiliki wanyama 40 wote ni mia na ishirini lau tungemzingatia kila mmoja peke yake wangepasa kutoa mbuzi watatu, lakini tukiwakusanya mbuzi wote hapasi ila mbuzi moja, hapa huwa wamekusanaya walio mbalimbali ili wasipaswe na mbuzi wa tatu bali mbuzi moja.

Na mfano wakuweka mbalimbali yaliyo pamoja

Ni mtu akawa na mbuzi arubaini akija mwenye kukusanya zaka akawaweka mbali mbali ishirini ishrini, ili wasichukuliwe zaka kwa kutofikia kiwango

## Aina nyengine za zaka

## Zaka ya madeni

### Deni

Mali ambayo ni lazima kulipwa na mtu aliyechukua mkopo.

### Hukumu ya zaka ya madeni yanayowajibika kulipwa na mtoaji zaka.

Ikiwa mtu ana deni kiwango chake chafika nisabu au kiko chini ya nisabu basi deni hili halimuwajibishi mtu huyu kutoa zaka. Na ikiwa deni halipunguzi nisabu basi atatowa kutoka kwa mali yake kiwango cha deni hilo, na atowe zaka katika mali iliyobaki.

Mfano: Ikiwa mtu ana (Dolari 10000), na deni (anadaiwa) (Dolari 10000), basi haimlazimu kutoa zaka; kwasababu deni hilo limemaliza nisabu, na vile vile ikiwa deni ni (Dolari 9950), basi deni hili linapunguza nisabu hivyo basi hawajibiki kutoa zaka, ama ikiwa deni lake ni (Dolari 4000), basi atapunguza kutoka kwa mali yake kiwango cha deni hilo, na itabakia na (Dolari 6000) ambazo zinawajibika kutolewa zaka

Isipokua achukue mtu deni na asitumie kwa lengo la kibiashara, kama mtu anunue nyumba kwa njia ya kulipa kidogo kidogo (hire purchase)au atumie deni kwa kufanya miradi ambayo inaokadiriwa kwa mamilioni ya pesa, huenda akaamua mmoja wa wafanyi biashara kupanua biashara yake, na kunua kutoka kwa pesa hizo jambo la kuzalisha, je deni hilo lilo zalisha mali itaangusha zakaa?

Kusema hizo ni kupotea mali inaopaswa kutoa zakaa kwa mafukara, pia inamaana kua wafanyi biashara wa leo hawaruhusiwi kutoa zakaana limemelizika kungamao lilofanywa kuweit mwaka wa 1409 hijri sawa na 1989 Miladi kwa yanayofuata:



### Hukumu ya zaka ya madeni yanayostahiki mtoaji zaka kutoa.

1. Ikiwa kuna udhuru wa kutolipwa deni, kama vile kufilisika kwa anayedaiwa, au ni mkaidi katika kulipa, halazimiki hapa mwenye kudai kutoa zaka kila mwaka, isipokuwa atatoa zaka mwaka mmoja tu pale atakapolipwa.
2. Ikiwa hakuna udhuru wowote wa kulipwa deni, kama vile awe anayedaiwa si mzito wa kulipa, na ametia nia kulipa, basi hapa yamlazimu mtu kutolea deni hili zaka kila mwaka; kwasababu iko katika hukumu ya vitu alivyonavyo.

## Zaka ya shahada na stakbadhi za viashirio vya umiliki au kima cha pesa

### Shahada ya kiashirio cha umiliki au kima cha pesa.

Ni shahada au stakbadhi inayowalazimu watoaji shahada kumpatia aliyobeba shahada hio kiasi cha pesa zilizo tajwa wakati akistahiki kupewa, pamoja na kutoa faida ya masikizano iliyo sawa na kima cha kutajwa katika shahada hiyo.
Na hii ni riba iliyowazi kabisa na ni haramu; kwasababu deni hili limeambatanishwa na faida, basi hizi shahada kwa ujumla hazifai; kwa sababu ni deni pamoja na faida waziwazi, basi ni juu ya kila anayehusika na mambo haya kuomba toba kwa Mwenyezi Mungu U.

### Hukumu ya zaka ya shahada za viashirio vya umiliki au kima cha pesa, na kiwango cha kutolewa zaka.

Zaka ya shahada ya kiashirio cha umiliki au kima cha pesa inachukuwa hukumu ya zaka ya deni, basi inawajibika kutolewa zaka pale inapofikia nisabu yenyewe, au pale inapochanganywa na anavyomiliki mwenye mali katika pesa zake au bidhaa za biashara, na ikakamilisha mwaka mzima, basi itatolewa robo ushuri. Na ikiwa shahada hizo haziwezi kuvunjwa kubadilishwa pesa ila baada ya muda fulani, basi bado zaka yake ipo pale pale, lakini itatolewa zaka wakati wa kuvunjwa kubadilishwa pesa kwake kwa kila mwaka uliyopita.

## Zaka ya malipo ya ziada ya mwisho wa kazi na malipo ya ziada ya uzeeni na mishahara ya uzeeni

### Malipo ya ziada ya mwisho wa kazi

Ni kiwango cha pesa kinachokatwa kutoka kwa mfanya kazi, anastahiki mfanyakazi kutoka kwa muajiri wake mwisho wa kuacha kazi kwa mujibu wa kanuni na nidhamu, yanapotimia masharti yaliyowekwa kwa jambo hili.

### Malipo ya ziada ya uzeeni

Ni kiwango cha pesa kinachokatwa. Inatolewa na serikali au mashirika maalumu kupewa wafanyikazi au mfanyikazi anayehusika na kanuni za bima ya jamii, ikiwa mtu huyu hakukamilisha masharti yanayohitajika kwake ili kupata mishahara ya uzeeni.

### Mshahara wa uzeeni

Ni kiwango cha pesa anachostahiki kupewa mfanyikazi wa serikali au shirika maalumu kwa kila mwezi, baada ya kumaliza miaka yake ya huduma ya kazi kulingana na kanuni na nidhamu, ikiwa ametimiza masharti yanayohitajika.

### Hukumu yake.

Hamlazimu mfanyikazi kutoa zaka mda wake wote anaofanya kazi kwa ajili ya malipo haya ya mwisho, kwa kukosekana umiliki uliyokamilika ambao kwamba ndio sharti la mtu kuwajibika kutoa

zaka, kwa maana mfanyikazi huyu hawezi kutumia pesa hizo ndani ya kipindi chake cha kufanya kazi, wala hana haki yoyote ya umiliki wa pesa hizo katika kipindi chake cha kazi.
Pesa hizi inapopitishwa sheria ya kuhisabiwa na kupewa mfanyikazi zote kwa pamoja, au kupewa kwa kipindi cha mizunguko fulani (kama kila mwezi hivi) hapa itakuwa ni mwenye kumiliki mali hii kiukamilifu, na atatoa zaka kile atakachopata miongoni mwa hizo pesa (alizopata kwa mara moja) zaka ya mali yakufaidisha.

## Zaka za mali zinazo kodishwa

### Mali zinazi kodishwa

Kila kilicho andaliwa kwa ajili ya kukodishwa na sio andaliwa kwa ajili ya biashara katika vitu venyewe hasa, kama majengo na magari na viwanda vinavo zalisha
Wamekubaliana wanavyoni kwaba hakuna zaka ya vitu hiyo, na zakae zinatolewa zaka ya faida yake inayopatikana inajumushwa na nisabu na mwaka kwa kile anachomilili katika pesa na mali ya biashara na atatowa robo ya fungu lakumi 2.5% zaka yake ni kama zaka ya pesa

## Zaka ya mali ya bima inayotolewa na mfanyikazi.

### Mali ya bima

Pesa ambazo mfanyikazi anazitanguliza kwa mwenye kazi kwa mkataba (yaani mfanyikazi hachukuwi pesa hizi- zinakaa kwa mwenye kazi ili mfanyikazi apate huduma fulani pindi anapokumbwa na matatizo).
Haimlazimu mfanyikazi kuitolea zaka; kwasababu haimiliki mali hii, hivyo basi hajapata umiliki uliokamilika, ambao ni sharti ya mtu kuwajibika kutoa zaka.

## Zaka ya haki za Hisia

### Haki za Hisia

Ni utawala wa mtu juu ya kitu kisichonekana na kushikwa, sawa kiwe kitu kile ni matokeo ya juhudi yake ya kiakili, kama vile haki ya mwandishi katika vitabu vya mambo ya sanyansi na adabu, ama uvumbuzi wa kitu katika viwanda,. Ama matunda ya harakati za biashara alizofanya mwanabiashara ili kuwavutia wafanyikazi, kama katika jina la biashara na nembo za biashara.

### Hukumu ya Zaka ya haki za Hisia.

Haki za hisia zimekuwa katika ada ni zenye kima cha mali inayotambulika kisheria, basi inafaa kuitumia haki hii kulingana na mipaka ya kisheria, nacho ni kitu cha kuhifadhi hadhi ya mtu haifai kuiendea kinyume.

Wala haimlazimu mtu kutoa Zaka katika haki ya uandishi na uvumbuzi wa kitu, kwa kule kukosekana masharti ya mtu kuwajibika kutoa Zaka, lakini inapokuwa ni machumo ya pesa itabidi kwa anayepokea machumo haya kuchukua hukumu ya mali ya kufaidisha [ Qadhwaayaa fiqhiyatu muaa'swirah Dr: Swallaah Asswaawy; uk. 60 na za mbele yake.].

## Zaka ya malipo ya kibaruwa, mishahara, na faida ya kazi za mtu binafsi

### Malipo ya kibaruwa na mishahara

Kile anacholipwa mfanyikazi kulingana na kazi atakayofanya.

### Hukumu yake.

Mali haya hayana zaka wakati ya kuyakabidhi bali hukusanya na mali mengine ya mtu yanayo wajibika kutolewa zaka ikiwa yatafikia kiwango na kupitiwa na mwaka basi atayatolea zaka yote na mali ya faida katikati ya mwaka atayatolea zaka mwisho wa mwaka japokuwa mali yote hayatakuwa ya mepitiwa na mwaka madamu yale mali yake mingine ya mefikia kiwngo na kupitiwa na mwaka kwa jumla. Na kiwango cha kutolewa Zaka ni robo ushuri (2.5%).

## Zaka ya Mali Haramu

## Mali ya Haramu

Kila mali iliyokatazwa na sheria kuichuma, au kuitumia, sawa uharamu wake ni kule kupatikana madhara au uchafu kama maiti na tembo, ama uharamu wake.kwa sababu ya tumo lake ama kuchukuwa mali bila ya ruhusa ya mwenyewe, au kuchukuwa kwa njia isio kubalika kisheria hata kama ataridhika kama vile riba au hongo.

## Hukumu ya Zakka ya mali haramu

Mali iliyo haramu yenyewe- kama mali iliyochumwa kutokana na biashara ya tembo/pombe, na nguruwe – haifai kutolewa Zaka, na vile vile mali iliyo haramu kwa kusababishwa na jambo fulani lililotokea kinyume na sheria – kama mali ya kuibwa; kwasababu ya kukosekana umiliki wamali hayo, ambao ni sharti ya kuwajibika kutowa zaka.na endapo anapo imiliki mali hiyo mwenyewe itampasa kutoa zaka mwaka mmoja hata kama amepitiwa na miaka kwa rai iliochaguliwa

Na mwenye kumiliki mali ya haramu na asimregeshe mwenyewe na akatoa kiwango katika mali hiyo, dhambi itabaki vile vile na alilicho kitoa ni sheria amempasa kufanya hivyo, na haizingatiwi alichokitoa kua ni zaka, na dhima yake itabaki vile vile isipokua amregeshe mwenyewe, au atoe sadaka ikiwa ameshindwa kujua mwenyewe

## Maelekezo (Jinsi ya kutumia mali haramu)

a) Anayekusanya mali haramu kwa makosa aliyofanya kwenye njia ya kuichuma hafai kuimiliki mali hayo hata ikawa umepita mda mrefu kiasi gani, na inamlazimu kuirudisha kwa mwenyewe, au kwa aliorithi - ikiwa anamjua-, akishindwa kumjua inamlazimu aitumie mali hayo katika mambo ya kheri; ili amalize mali hayo, na akusudie kwamba anamtolea sadaka mwenye mali.

b) Anapolipwa mtu pesa kwa kufanya kazi iliyo haramu basi mwenye kulipwa anafaa kuitumia katika mambo ya kheri, wala asiirudishe kwa aliyempa; kwa vile kumrudishia itakuwa ni kusaidiana katika mambo maovu.

c) Hairudishwi mali haramu kwa mtu aliyechukua kwake ikiwa anajua kwamba anashughulika na mambo yaliyo kinyume na sheria ambayo yamesababisha uharamu wa mali yake, kama vile faida za riba; bali pia utazitumia katika njia za kheri.
d) Ikishindikana kuirudishwa mali haramu yenyewe, inamlazimu mtu huyu kurudisha mali mfano wake; au kima chake kwa mwenyewe ikiwa anamjuwa, ikiwa hamjuwi ataitumia hiyo iliyo mfano wa aliopata, au kima chake katika njia ya kheri, na aikusudie kwamba ni sadaka anamtolea mwenye mali
[ Qadhwaayaa fiqhiyatu muaa'swirah Dr: Swallaah Asswaawy; uk. 61 na za mbele yake.]
e) ikishindikana kuregesha mali ya haramu yenyewe itampasa kuregesha mfano wakeau thamani yake kwa mwenyewe akimjua, venginevvyo mfano wake au kima chake katika mambo ya kheri, na akusudie sadaka hio kwa mwenyewe

# Wanaostahiki kupewa Zaaka na kutowa Zaaka

## Wanaostahiki kupewa Zaka

Ni wale ambao kwamba wanastahiki kupewa Zaka, nao watu aina nane ambao kwamba Mwenyezi Mungu U Amewahisabu katika kauli yake: {Sadaka hupewa (watu hawa): - Mafakiri na Masikini na Wanaozitumikia na Wanaotiwa nguvu nyoyo zao (juu ya Uislamu) na katika kuwapa Uungwana watumwa na katika kuwasaidia wenye deni na katika (kutengeneza) mambo aliyoamrisha Mwenyezi Mungu na katika (kupewa)

Wasafiri (walioharibikiwa). Ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima} (At-Twba – 60).

### 1. Mafakiri

Mafakiri

Ni wingi wa fakiri, naye ni yule ambaye hawezi kujitosheleza mahitaji yake ya dharura na mahitaji ya aliyechini yake, katika chakula na kunywa na mavazi na makazi.

Na yuwapewa katika Zaka kitakachomtosha yeye na familia yake kipindi cha mwaka mzima.



### 2. Masikini

Masikini

Ni wingi wa masikini, naye ni yule ambaye kwamba anapata nusu ya mahitaji yake, au zaidi ya nusu, kama yule ambaye ana mia moja, na anahitaji mia mbili. Na anapewa mtu kama huyu kiasi kitakachomtosha sawa na mahitaji yake na familia yake kwa mda wa mwaka mzima kutoka katika Zaka.



### 3. Wanaotumikia Zaka

Wanaotumikia Zaka

Wale ambao kwamba wanakusanya Zaka kwa idhini ya viongozi, na wanachukua jukumu la kugawa Zaka hiyo kwa wanaostahiki kupewa.

Na watapewa katika mali ya zaka kiyasi ya ujira wao na kazi yao hata kama wako nauwezo, kwa sababu ameacha kazi yake kwa ajili ya kazi hii, isipokuwa kama walipwa na serekali basi hawatopewa zaka, na huhisabiwa ni wenye kukusanya zaka kila anae shughulika, anaye kusanya na anaye andika na anelinda na anaegawanya wote hawa wanasahiki kupewa zaka

Kupewa Zaka wanaoitumikia Zaka

Anapewa zaka mwenye kukusanya zaka na mwenye madeni hata kama ni matajiri, na mwenye uwezo wakufanya kazi ikiwa amejishughulisha nakutafuta ilimu ya kisheria na ikawa hana mali, kwa sababu kutafuta ilimu ni jihadi katika njia ya mwenyezi mungu, na vile vile mwenye kupigana jihadi na wanaotiwa nguvu nyoyo zao kwa ajili ya kusilimu.ama mwenye kukaa nakufanya ibada na akacha kufanya kazi hali yakuwa anaweza kufanya kazi huyu hatapewa zaka kwa sababu ibada faida yake ya mrudia yeye mwenyewe tafauti na mwenye kutafuta ilimu.{ Enyi mlio amini! Toeni katika vile vizuri mlivyo vichuma, na katika vile tulivyo kutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msinge vipokea ila ingekuwa mmefumba macho. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha na Msifiwa. Shet'ani anakutieni khofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu. Na Mwenyezi Mungu anakuahidini msamaha na fadhila zitokazo kwake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.} [Al-Baqara: 267-268]

### 4. Waliosilimu wanaotiwa nguvu nyoyo zao juu ya Uislamu.

wanaotiwa nguvu nyoyo zao juu ya Uislamu.

Viongozi wanaoheshimika katika jamii yao, kwa wanaotarajiwa kwamba kupewa kwao kunaweza kuwa sababu ya kusilimu, au kuzuia shari zao, au kutia nguvu imani zao, au kuwakinga waislamu dhidi ya maadui zao miongoni mwa maadui zao.

Na wanapewa Zaka kwa kiwango ambacho kitafikisha kwao kutiwa nguvu nyoyo zao.



## 5. Watumwa ili waachwe huru

### Watumwa ili wa achwe huru

Mtumwa, na Mukaatib: ni Yule Mtumwa alie andikiyana na bwanake amlipe pesa ili ajikomboe nafsi yake na utumwa, huyu atapewa zaka kulipia deni lake walilo andikiyana

Ili awe huru kila mmoja miongoni mwao kuweza kufanya harakati za kimaisha, na awe ni kiungo chenye manufaa kwa jamii, na atulizane vizuri katika kumuabudu Mwenyezi Mungu kiukamilifu, na hapa pia inaingia kuwakomboa mateka wa kivita waliotekwa nyara miongoni mwa waislamu.



## 6. Wenye kudaiwa madeni.

### Wenye kudaiwa madeni.

Wingi wa mwenye kudaiwa madeni, naye ni yule anayefaa kulipa deni.

Na wenye kudaiwa madeni wako sampuli mbili:

Ya kwanza: Ni yule mwenye deni linalomuhusu yeye mwenyewe, basi anapewa katika Zaka kitakacho kamilisha kulipwa kwa deni lake ikiwa ni fakiri.

Ya pili: Ni aliye na deni kwasababu ya kuleta suluhisho kati ya makundi mawili ya waislamu, basi anapewa katika Zaka kitakacho kamilisha deni hilo, hata kama ni tajiri.



## 7. Kwa njia ya Mwenyezi Mungu

### Kwa njia ya Mwenyezi Mungu

Wale wanaopigana jihadi kwa njia ya Mwenyezi Mungu.

Watu hawa hupewa kinachowatosha katika jihadi kwa njia ya Mwenyezi Mungu.

Na inaingia ndani yake mambo mengi katika mambo ya kulingania dini ambayo yanahisabiwa kuwa ni jihadi kwa njia ya Mwenyezi Mungu na wala hayakupata katika sadaka kitakachosimamia harakati zake.

## 8. Msafiri (Alioharibikiwa).

### Msafiri (Alioharibikiwa)

Msafiri ambaye kwamba amekatikiwa na safari yake wala hakubakia na chochote katika mali.

Anapewa katika Zaka kitakachomfikisha kwao, hata kama huko kwao ni tajiri.

Mambo yanayofaa kuzingatiwa

1. Zaka haitolewi kwa watu ambao hawako katika makundi haya yaliyotajwa, hata kama ni kwa lengo la kufanya wema na hisani, kama vile kujenga msikiti, na madrasa, na mahspitali/zahanati, na

mengineo katika mambo ya kheri na ambayo kwamba waweza kuyafanya katika sadaka.
2. Sio lazima kufanya uchambuzi wa kina kwa haya makundi manane yaliyotajwa wakati wa kutoa Zaka, bali yaruhusiwa kutoa kwa kundi lolote kati ya haya makundi manane.

## Wale ambao hawafai kupewa Zakah.

### 1. Matajiri, na watu wenye nguvu nauwezo wa kukidhi mahitaji yao.

Kwa kauli ya Mtume (saw): (Wala hakuna fungu la kupewa tajiri, wala mtu mwenye nguvu anayechuma) [Imepokewa na Abuu Daud.].

### 2. Walio asili yako baba na mama, na walio vizazi vyako mototo, na mke, ambao ni jukumu lako kuwalisha.

Haifai kumpa Zaka muislamu ambaye ni jukumu lako wewe kumlisha, kama vile baba, mama, babu, nyanya, watoto, na wajukuu; kwasababu kuwapa Zaka watu hawa kutawatosheleza wao kula kwao ambako ni jukumu lako juu yao, hivyo basi kuondosha jukumu la kuwalisha, na hatimaye yarudi kutoa faida ya Zaka kwako mwenyewe, kama kwamba umejipa Zaka mwenyewe.

### 3. Makafiri wasiotiwa nguvu

Haifai kuwapa Zaka makafiri ikiwa simakusudio kuwatia nguvu, katika uislamu kwa kauli ya Mtume (saw): (Huchukuliwa kutoka kwa matajiri wao, na kupewa mafakiri wao) [Imepokewa na Bukhari.].
Yaani: Matajiri wa kiislamu na mafakiri wao pasina kuwapa wasiokuwa wao, na kwasababu miongoni mwa makusudio ya Zaka ni kuwatosheleza mafakiri wa kiislamu, na kuzidisha mapenzi na udugu kati ya w jamii ya kiislamu, na hivi haifai kwa makafiri.
Kupewa Zaka wanaoitumikia Zaka

Anapewa zaka mwenye kukusanya zaka na mwenye madeni hata kama ni matajiri, na mwenye uwezo wakufanya kazi ikiwa amejishughulisha nakutafuta ilimu ya kisheri na ikawa hana mali, kwa sababu kutafuta ilimu ni jihadi katika njia ya mwenyezi mungu, na vile vile mwenye kupigana jihadi na wanaotiwa nguvu nyoyo zao kwa ajili ya kusilimu.ama mwenye kukaa nakufanya ibada na akacha kufanya kazi hali yakuwa anaweza kufanya kazi huyu hatapewa zaka kwa sababu ibada faida yake ya mrudia yeye mwenyewe tafauti na mwenye kutafuta ilimu.{ Enyi mlio amini! Toeni katika vile vizuri mlivyo vichuma, na katika vile tulivyo kutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msinge vipokea ila ingekuwa mmefumba macho. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha na Msifiwa. Shet'ani anakutieni khofu ya ufakiri na anakuamrisheni mambo machafu. Na Mwenyezi Mungu anakuahidini msamaha na fadhila zitokazo kwake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua.} [Al-Baqara: 267-268]

### 4. Aali zake Mtume (saw) (Aalu Nnabiy: jamaa za mtume ni baniy Haashim)

Haifai kuwapa Zaka Aali zake Mtume ﷺ kwasababu ya utukufu wao, kwa kauli ya Mtume (saw): (Hakika hii Zaka ni uchafu wa watu (unaosafishwa), kwa hivyo haifai kupewa Muhammad, wala Aali ya Muhammad) [Imepokewa na Muslim.].

### 5-Vijakazi vya Jamaa zake Mtume (saw)

Nao ni watumwa ambao kwamba wamewachwa huru na Jamaa zake Mtume (saw); kwa Hadit: (Hakika ya Zaka sio halali kwetu, na hakika watumwa wa watu ni miongoni mwao) [Imepokewa na Tirmidhi.].

Yaani: Hukumu ya watumwa hao ni kama hukumu ya wenye kuwamiliki, hivyo basi ni haramu kupewa Zaka watumwa wa Bani Hashim.- Vijakazi vya Aali zake Mtume (saw)

### 6. Mtumwa anayemilikiwa

Haifai kupewa mtumwa Zaka, kwasababu mali ya mtumwa ni katika milki ya bwana wake, hivyo basi akipewa Zaka itakwenda kwa bwana wake, na kwasababu jukumu na kulishwa kwake ni la bwana wake. Na imevuliwa kutoka hukumu hio Almukataba (mtumwa alioandikana mkataba na bwana wake), kwani wao hupewa Zaka kiwango kitakacholipa deni la mkataba wao, na mfanyikazi wa kukusanya Zaka – pia- akiwa ni mtumwa anayetumikia Zaka atapewa Zaka, kwasababu ni kama malipo, na mtumwa anafaa kuajiriwa kwa ruhusa ya bwana wake.

## Kutoa Zaka

### Wakati wake

Ni lazima kutowa zaka kwa haraka inapo fika wakati wakuwajibika kwake pamoja nauwezo wakufanya hivyo, na haifai kuicheleweshа kutoa iwajibikapo kutolewa ila kwa dharura, kama vile mali kuwa mbali na mji wake au mfano amefungwa na mfano wa hayo.

na dalili ya kuwajibika kuitoa kwa haraka ni kwa neno lake Mwenyezi Mungu {Na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake} [Al-an'aam 141]

Na kwa neno lake U { Na simamisheni Swala na toeni Zaka, na mti'iin Mtume ili mpate kurehemewa.} [Al-nnuur 56]

Na amri yatakikana kutekeleza kwa haraka bila ya kucheleweshа

### Hukumu ya kutoa zaka Mapema

Inafaa kutanguliza kutoa zaka kwa miaka miwili au chini ya hapo, ikiwa imefikia Nisabu yakutolewa zaka Wakati wakuitanguliza kwake.

### Sehemu ya kutoa Zaka

Ubora ni kuitoa zaka katika mji ambao ndipo mali yalipo, lakini inafaa kusafirisha zaka zake kupeleka mji wakaribu au wambali kwa haja, mfano ukawa mji wambali watu wake ni mafukara zaidi, au mtu awe ana jamaa zaka mafukara katika mji ule kama mafakiri wa mji wake, kwa sababu kuwapatia mafukara ambao ni

jamaa zake kuna maslahi, na kwake itakuwa ni sadaka na kuunga kizazi na kauli hii ya kufaa kusafirisha zaka ndio kauli sahihi kwa kuenea neno lake mwenyezi mungu {Wa kupewa sadaka ni mafakiri na masikini na wanao zitumikia, na wakutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye madeni, na katika njia ya Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua Mwenye hikima.} [Tawba 60] Yaani mafakiri na masikini wakila sehemu.

## Mali yanayofaa kutolewa zaka na yasiyofaa kutolewa

Mali yanayo tolewa zaka ni mali ya kati na kati sio mali ya hali ya juu wala mali mbaya, haimlazimu kumtoa mnyama aliemnono au mwenye mimba au dume katika wanyama, wala tende nzuri, isipokua akiridhia kwa jambo hilo na akaridhia nafsi yake.

Kama vilevile hafai kutoa kitu kibovu na kuacha kizuri, isipokua mali yake yote yawe ni mbaya, na wanyama wake wote wawe ni wagonjwa, hapo inafaa kutoa mmoja wao.

Amesema Mwenyezi Mungu { Enyi mlio amini! Toeni katika vile vizuri mlivyo vichuma, na katika vile tulivyo kutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msinge vipokea ila ingekuwa mmefumba macho. Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha na Msifiwa.} [ Al-Baqara: 267]

na katika hadhithi ( Hatolewi zaka mnayama mkongwe [ harim: mnyama aliomzee.]. wala tongo[ mwenye aibu: mwenye amabaye hakubaliwi katika mauzo.]. wala dume [ mbuzi dume ambae hajafikia umri wa kibeberu wala hana manufaa yoyote wala hana kizazi.]. ila anapotaka mwenye kutoa zaka) [Imepokewa na Bukhari.].

Na Amesema Mtume (saw) Kumwabia Muadh: (Tahadharini na mali yao matukufu) [Imepokewa na Bukhari.].

## Maelekezo

1. Inampasa kwa mwenye kutoa zaka kuwatafuta wanaostahiki kupewa zaka, wala asiwape wasio stahiki kwa neno lake mtume s.a.w (hapana bahati kwa tajiri wala mwenye nguvu za kutafuta) [Imepokewa na Abuu Daud.].

2. Na mwenye kutoa zaka afanye bidii kumtafuta anaestahiki kupewa zakaa na mwenye haja, na kila zinapozidi sifa nyengi kwa mtu kwa anaestahiki kupewa zakaa basi anastahiki zaidi kupewa zakaa kama kua ni fakiri katika jamii yako, au fakiri anaetafuta ilimu na mfano wa hao

Anaestahiki zaidi kupewa Zaka

Inaetaka kutoa zaka afanye bidii kutafuta anaestahiki kupewa zaka na anaekuwa na haja zaidi na kila alie kusanya sifa za kupewa zaka huyo ndie anaestahiki kupewa zaka. Kama jamaa alie fakiri, au mwanafunzi fakiri, na kadhalika.

## Mambo muhimu katika Zaka

### Kima cha kutolewa Zaka

Asili ya Zaka ni kutoa kitu asili (chakula) katika kilichowajibika kutolewa, lakini yaruhusiwa ikiwa kuna haja au maslahi yanayokubalika kutoa kima chake.

### Mahusiano ya Serekali na Zaka

Asili ya Zaka ya mali ni kazi ya mtawala, wala hawaachiwi wanaotoa Zaka na watu binafsi kujifanyia vipimo, basi utawala ukizembea katika jukumu hili itakuwa jukumu ni kwa mtu mwenyewe binafsi (kuangalia utekelezaji wake wa Zaka).

### Kuzalisha mali ya Zaka kwa maslahi ya wanaostahiki kupewa Zaka.

Yaruhusiwa kuzalisha mali ya Zaka kwa miradi yenye manufaa yanayorudi kwa wanaostahiki Zaka hiyo, ikiwa hakuna umuhimu wa haraka wa kutumia mali hayo unaopelekea matumizi ya mara moja.

## Je katika mali kuna haki isiyokuwa Zaka kwa mfano kama ushuru?

Zaka ni haki ya mzunguko iliokadiriwa katika mali, na ambayo ni lazima wa kutolewa ulazima wa asili ya mali kwa wanaoweza.
- Na katika mali kuna haki nyengine isiyokuwa Zaka, ambayo imejitenga kwa kuwa ni yenye kutokea ghafla, wala haikupimwa kwa kiwango maalumu, wala si yenye kudumu hali yake kama kudumu kwa Zaka, nayo haiwajibiki kwasababu ya mali, bali inawajibika kwasababu nyenginezo, na mali ni sharti ya kuwajibika kwake, na mfano wake ni kulisha wazazi wawili, na jamaa wa familia, na mke, na kuondosha madhara wakati wa matatizo, ikiwa haitoshi kufanya haya mali yalioko katika hazina ya serikali ya kislamu.

- Ushuru hautoshi hata kama itakuwa kiwango sawa na Zaka, kwa maana Zaka ni ibada miongoni mwa ibada, na ushuru ni jukumu la kikanuni, wala mojawapo haitoshelezi nyengine.

# Zaaka ya fitri

## Maana ya zaka za fitri

### Zaka ya fitri

Zaka aliyoifaradhisha Mtume (s.a.w)wakati wa kufungua katika kumalizika kwa mwezi wa Ramadhan.

Na imeitwa Zaka ya fitri kwasababu inawajibika pale mtu anapofungua kwa kumalizika mwezi wa Ramadhani.

## Hukumu ya Zaka ya Fitri

Zaka ya Fitri ni lazima kwa kila Muislamu anayemiliki siku ya Idi na usiku wake pishi ya chakula cha ziada ya chakula chake cha siku na cha familia yake (nayo ni karibia kilo mbili na nusu).
Na yamlazimu mwenye kutoa Zaka ajitole Zaka nafsi yake, na mke wake, na wale ambao ni jukumu lake kuwalisha, hata mtoto alioko kwenye tumbo la mamake. Na dalili ya kuwajibika kwake ni ilivyopokewa kutoka kwa Ibn Umar radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie asema: (Amefaradhisha Mtume (s.a.w) Zaka ya Fitri Pishi moja ya tende, au Pishi moja ya Shayir (aina ya nafaka) kwa mtumwa na muungwana, na mume na mke, na mdogo na mkubwa katika waislamu, na akaamrisha itolewe kabla ya watu hawajatoka kwenda kuswali (Idd) [Imepokewa na bukhari na muslim.].



Tende



Ngano

## Wakati wa kutolewa Zaka ya Fitri

Wakati bora wa kutoa zaka za fitri ni kutoa siku ya idd baada ya kutokeza kwa alfajiri na kabla ya swala ya Idd na yaruhusiwa

kutanguliza kuitoa kwa siku moja au siku mbili kabla siku ya Idd; kwa utkelazaji wa maswahaba. Wala haifai kuichelewesha hadi baada ya swala ya Idd; kwa Hadith ya Ibn Umar iliyotangulia: “Na akatuamrisha tuitoe kabla ya watu kutoka kuswali (Iddi)” Na katika Hadith ya Ibn Abbas t: “Atakayeitoa kabla ya swala basi ni Zaka inayokubaliwa, na atakayeitoa baada ya swala basi ni sadaka miongoni mwa sadaka” [Imepokelewa na abi daud.].

## Kiwango cha kutolewa Zaka ya Fitri

Pishi moja [ Pishi ni sawa na kilo mbili na gramu arubaini (2.040 grms).]. kwa kila mtu, na kiwe ni chakula cha binadamu (kula) kama mchele, na tende, na ngano, kwa Hadith ya Abu Saii’d Alkhudhry radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie asema: (Ilikuwa tunatoa katika wakati wa Mtume (s.a.w) siku ya Fitri pishi moja ya chakula”. Na akasema: “Na kilikuwa chakula chetu ni Shayir (aina ya nafaka), na zabibu, na aqitwu (Maziwa yaliyokaushwa) [ Aqtw: Maziwa yaliyokaushwa.]. na tende) [ Imepokewa na Bukhari]..

Na pishi ni sawa na 3.25kg kulingana na dhehebu la hanafia, ama jumhuri ya wanavyoni ni sawa na 2.040kg.

Na hukadiriwa vile vile kwa kujaza mkono mara nne kwa mwanamume wasitani




## Wanaostahiki kupewa Zaka ya Fitri.

Inatolewa Zaka ya Fitri kwa yale makundi manane ambayo kwamba yanapewa Zaka, kwa maana (Zaka ya Fitri) ipo ndani ya

kauli ya Mwenyezi Mungu: {Sadaka hupewa (watu hawa) – Mafakiri} (At-Tawbah: 60).

### Hekima ya kutoa Zaka ya Fitri.

1. Kumsafisha aliyefunga kutokana na mambo ya upuzi na uchafu, kama ilivyopokewa kutoka kwa Ibn Abbas asema:
(Amefaradhisha Mtume (s.a.w) Zaka ya Fitri kwa aliyefunga ili kumsafisha kutokana na upuzi na uchafu [ Arrafarh Uchafu: Maneno yanayosemwa ovyo.]., na ni chakula cha masikini) [Imepokewa na Abu Daud.].
Na hii ni kwamba aliyefunga mara nyingi haepukani na michezo, na maneno ya upuzi, na mambo yasiyo na faida katika maneno, basi ikawa hii Zaka inamsafisha aliyefunga kwa aliyoyafanya katika matamshi haya yaliyoharamishwa, au yaliyochukizwa kufanywa, ambayo kwamba yanapunguza thawabu za matendo, na kuharibu saumu.
2. Masikini na mafakiri kupata nafasi nzuri ya kimahitaji siku ya Idd ili kuepukana na kuomba ambako kuna udhalilifu na unyonge siku ya Idd, jambo hili (Zaka fitri) litawafanya wawe na furaha na bashasha, ili washirikiane na watu wengine katika kufurahia Idd.

# Sadaka ya kujitolea

### Maana ya sadaka ya kujitolea

Sadaka ya kujitolea
Ni kinachotolewa kwa lengo la kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu pasina kuwa ni lazima.

Na kwa maana hii inatolewa zawadi na mfano wake kuwa ni katika mambo yanayotolewa kwa lengo la kuzidisha mapenzi, hivyo basi vitu hivi haviingii katika vinavyoitwa sadaka maalumu zilizowekwa na hukumu za sheria.

## Hukumu ya sadaka ya kujitolea

Sadaka ya kujitolea ni yenye kupendekezwa kwa wakati wowote ule, na hasaa ikiwa ni wakati unaohitajia kitu, na imehimizwa katika Qur'an na sunnah ya Mtume ﷺ miongoni mwayo ni:

- Maneno ya Mwenyezi Mungu U: {Ni nani atakaye mkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema ili Mwenyezi Mungu Amzidishie mzidisho mwingi} (Al-Baqarah: 245).
- Kutoka kwa Abu Hureirah radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie asema: Amesema Mtume ﷺ: (Atakayetoa sadaka ya tende nzuri alizozichuma kwa kichumo kizuri cha halali – na Mwenyezi Mungu hakubali ila kizuri – hakika Mwenyezi Mungu anakubali sadaka hii kwa Mkono wa kulia, kisha anamkuzia mwenyewe, kama vile anavyokuza mmoja wenu ndama wa farasi wake – mpaka inakuwa mfano wa jabali) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
- Mtume ﷺ amemuhisabu mwenye kuficha sadaka anayotoa miongoni mwa watu saba watakao finikwa na kivuli cha Mwenyezi Mungu, siku ambayo hakuna kivuli isipokua kivuli Chake (Na mtu aliyetoa sadaka akaificha, hata mkono wake wa kushoto usijuwe kilichotolewa na mkono wa kulia) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
- Na kutoka kwa Ka'b Ibn u'jrah radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie kwamba Mtume ﷺ amesema: (Na sadaka zinafuta madhambi kama maji yanavyozima moto) [Imepokewa na Tirmidhi.].

## Adabu za sadaka za kujitolea

### 1. Adabu za lazima

1. Kufanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu U (Ikhlaas) – Anatoa Zaka kwa lengo la kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, sio kwamba aonekane au atajwe vizuri na watu.

2. Kujiepusha na kujisifu (kwamba ni mtoaji) na kuudhi watu (kwa kutoa kwake) kwa kauli ya Mwenyezi Mungu U: { Enyi mlioamini! Msiharibu sadaka zenu kwa masumbulizi na udhia} (Al-Baqarah: 264).

### 2. Adabu zinazopendekezwa.

1. Inapendekezwa kwa muislamu kutoa sadaka kwa wanaohitajia miongoni mwa jamaa zake ambao sio jukumu lake kuwalisha, kama vile ami zake, na wajomba zakle, na mke kumpa mumewe aliyefakiri, na wengineo, na hivi ni bora kuliko kuwapa sadaka watu wasiokuwa hawa, Anasema Mwenyezi Mungu (s.w): "Yatima aliye jamaa (na asiyekuwa jamaa)" (Al-Balad: 15).

Na katika Hadith: (Hakika ya sadaka kwa masikini ni sadaka, na kwa jamaa yako ni mambo mawili: sadaka na kuunganisha kizazi) [Imepokewa na Nasaai.].

2. Kuchagua katika mali yake mali iliyohalali, nzuri, yanayompendeza nafsiyake. Anasema Mwenyezi Mungu U: {Hamtoweza kuufikia wema (khasa) mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda} (Aali Imran: 92)

3. Kufanya siri katika kuitoa; kwa kuwa hivi ndio karibu zaidi na Ikhlas, na ni mbali sana na kuonesha watu na kutaka kusifiwa, na ni karibu zaidi katika kumkirimu fakiri, Anasema Mwenyezi Mungu U: {Mkizidhihirisha sadaka ni vizuri, na mkizificha mkawapa mafakiri kwa siri basi hivyo ni kheri } (Al-Baqarah: 271).

Na ikiwa katika kuitoa kwa kuonekana kuna maslahi, kama vile watu kuiga kutoa, na kuwatia moyo waliohudhuria, basi inapendekezwa kuitoa wazi, pamoja na kuchunga muislamu niya yake nakuilazimsha juu ya ikhlas

Kutoa sadaka anayoweza hata kama ni kidogo sana, amesema Mtume ﷺ: (Uogopeni moto japo kwa ubali wa tende) [Imepokewa na Bukhari.].

## Faida za sadaka za kujitolea

### Kwanza: Faida zinazorudi kwa mtu mwenyewe.

1. Kusafisha nafsi, Amesema Mwenyezi Mungu U: { Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na kuwatakasa kwa ajili ya hizo (sadaka zao) } (Tawba: 103).
2. Kumuiga Mtume ﷺ, kwani miongoni mwa tabia zake ni utoaji na ukarimu, na alikuwa akitoa sana kiasi cha kuwa haogopi ufukara, na akimwambia Bilal: (Toa ewe Bilal, wala usiogope kwa Mwenye Arshi (Allah SW)kupungukiwa ) [Imepokewa na Al-Bazzar.].
3. Mwenyezi Mungu atamlipa chochote alichokitoa, na atanyanyuliwa daraja mwenye kutoa, kwa kauli ya Mwenyezi Mungu kwa hili: { Na chochote mtakachotoa, basi Yeye Atakilipa, Naye ni M'bora wa wanaoruzuku} (Saba: 39).
4. Kusafishwa mali kutokana na upuzi wa biashara, kutoka kwa Qays Ibn Abu Gharaza radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie asema: Tulikuwa wakati wa Mtume ﷺ tukijiita madalali [ Samaasira: Madalali Wanakusudiwa wauzaji.]. Mtume ﷺ akatupitia pale tulipokuwa na akatupa jina lililokuwa bora kuliko hilo, akasema: (Enyi wafanyi biashara, hakika uuzaji unafwatiliwa na maneno machafu na viapo, basi changanyisheni [Fashuubuhu: Basi zichanganyeni: Kuamrisha kuchanganyika kwa maana wachanganye mambo yao na utoaji wa sadaka ili iwe kafara ya (kusafisha makosa) kwa Kapitikana baina yao mambo ya uongo na mengineo]. kwa kutoa sadaka) [Imepokewa na Abu Daud.].
5. Kupata malipo mengi, na kusemehewa madhambi kwa kauli yake Mtume ﷺ: "Atakayetoa sadaka ya tende nzuri

alizozichuma kwa kichumo kizuri cha halali – na Mwenyezi Mungu hakubali ila kizuri – hakika Mwenyezi Mungu anakubali sadaka hii kwa Mkono wa kulia, kisha anamkuzia mwenyewe, kama vile anavyokuza mmoja wenu ndama wa farasi wake – mpaka inakuwa mfano wa jabali) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

6. Kunufaika Muislamu na sadaka yake ya kuendelea kwa kupata thawabu baada ya kufa. Imepokewa na Abuhureirah radhi za Allah zimfikie kutoka kwa Mtume ﷺ alisema: ( Akifariki mwanaadamu matendo yake yote yanakatika isipokuwa mambo matatu: Sadaka ya kuendelea, au Ilimu yenye manufaa, au Mtoto mwema anaye muombea mzazi wake) [Imepokewa na Muslim.].

7. Kutoa sadaka inazidisha mali na kukuza, na kuonyesha kushukuru kwa mja juu yanema aliyo pewa na Mwenyezi Mungu U na mwenye kushukuru ameahadiwa kuzidishiwa Asema mwenyezi Mungu {Mkishukuru nitawazidishieni } [Ibrahim 07]

Pili: Faida inayorudi kwa jamii.

1. Sadaka inakamilisha ujumbe wa Zaka kwa jamii.

2. Kupatikana kule kutoshelezana na kusaidiana na kupata umakinifu na mapenzi katika jamii ya kiislamu.

# HIJJAH

makka na sehemu ya ibada ya hijja

## Tarehe ya Makka na hali ilivyokuwa na ilivyo sasa

### Makka

Ni jina linalotokana na neno (bakka) lugha ya Kisamia ambalo maana yake ni bonde

Neno la Makka pia limekuja kwa tamshi la Bakka katika neno la Mwenyezi Mungu : {Hakika nyumba ya kwanza iliyowekewa watu ni iliyo Bakka, hali ya kuwa ni yenye baraka na uongofu kwa viumbe wote} [3: 96].

Tarehe ya Makka inakwenda nyuma hadi karne ya kumi na tisa kabla ya kuzaliwa Mtume Issa u, katika kipindi cha bwana wetu Ibrahim na Ismail, amani ziwashukie, kwani walikuwa ni watu wa mwanzo wa kukaa hapo. Mwenyezi Mungu U Anasema, Akimtolea hikaya Ibrahim: {Mola wetu! Hakika mimi nimewakilisha watu wa nyumbani kwangu kwenye ardhi isiyokuwa na mazao, kwenye Nyumba yako tukufu, ewe Molawetu!, ili watekeleze Swala. Basi zifanye nyoyo za watu ziwaelekee wao kwa mapenzi na uwaruzuku matunda ili washukuru} [14: 37].

Na kwa fadhila ya dua ya bwana wetu Ibrahim u yalitembuka maji ya Zamzamu kutoka chini ya nyayo za Ismail u alipomalizikiwa na maji na chakula mama yake, Hajara. Na kutoka wakati huo, makabila yalikusudia kuja hapo kwenye maji, na mahali hapo pakaanza uhai.

Na makabila yakaendelea kuja hapo na kuzaana, mpaka utawala wa mahali hapo ukaja kwa Makureshi. Na Makureshi wakaendelea kutawala mpaka kudhihiri Nabii Mohammed(saw) ambaye alikuwa na athari kubwa zaidi katika kugeuza maisha ya Makka tukufu na ulimwenguni kote.

Nabii Mohammed (saw) alitumilizwa Makka, na Alkaba ikawa ni kibla cha Waislamu, na Makka ikawa ndio kituo cha ulinganizi wa Kiislamu, lakini watu wake walikuwa wakali zaidi katika kuwaepusha watu na Uislamu na kuwaadhibu waliosilimu, mpaka wakalazimika Waislamu kuhamia Madina iliyonawirishwa, na dola ya Kiislamu ikasimama huko. Kisha Mtume (saw) akarudi Makka kuikomboa, ikawa kuanzia wakati huo, ni mji mkubwa wa Kiislamu mpaka zama zetu hizi.

Na kwahakika mji wa Makka ulipata umuhimu mkubwa kutoka kwa makhalifa na viongozi wakiislamu. Na wakajitolea kujenga Makka na kuupanua mji, na wakafanya makka ni kituo cha kusambaza nuru ya Dina ya Kiisalamu katika ulimwengu wote

## Utukufu wa Makkah

### 1. Ni amani kwa anayeingia

Mwenyezi Mungu U Anasema: {Na Mwenye kuingia atakuwa kwenye amani} [3: 97], yaani Haramu ya Makka.

### 2. Haingi Dajjaal mji wa Makka, wala magonjwa hatari yenye kuambukiza na kuua.

Abu Huraira t amepokewa akisema kwamba Mtume (saw) alisema: (Madina na Makka imezungukwa na Malika, katika kila pembe [ Naqab: njia.] yake kuna Malaika. Haingiliwi na Dajjaal wala magonjwa hatari ya kuambukiza na kuua) [Imepokewa na Ahmad.].

### 3. Kuswali kwenye Msikiti wa Haram thawabu zake ni Swala elfu mia moja.

Jabir t alipokewa akisema kuwa Mtume (saw) alisema: (Swala moja ndani ya Msikiti wa Haramu ni bora kuliko Swala elfu mia moja katika misikiti mingine) [Imepokewa na Ibnu Maajah.].

### 4. Makka ni ardhi inayopendwa zaidi na Mwenyezi Mungu U

Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw): (Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Wewe ni ardhi ya Mwenyezi Mungu

njema zaidi, na ni ardhi ya Mwenyezi Mungu inayopendwa zaidi na Mwenyezi Mungu) [Imepokewa na Tirmidhi.].

## Hukumu zinazohusu Makka peke yake na eneo la Haram

### 1. Onyo kali kwa anayetia nia kufanya ovu huko Haram, awe amelifanya au hakulifanya

Mwenyezi Mungu U Amesema: {Na yoyote mwenye kutaka kupotoka na kuleta udhalimu huko, basi tutamuonjesha adhabu kali} [22: 25].

Imepokewa na Ibn Abbas t kuotoka kwa Mtume (saw) Akisema: (Watu wanaochukiwa sana na Mwenyezi Mungu ni watu watatu) na akataja miongoni mwao ni (Mwenye kupotoka -kupinga Sharia ya Mwenyezi Mungu- katika Haram) [Imepokewa na Bukhari.].



Makka

### 2. Uharamu wa kupigana na kumwaga damu humo

Amesema Mwenyezi Mungu (saw): {Na tulipoijaalia Nyumba ni mahali pa watu kukusanyika na mahali pa amani} [2: 125].

Mwenye kuingia Makka ataaminika humo, kwa neno la Mtume (saw): (Si halali kwa mmoja wenu kubeba silaha Makka) [Imepokewa na Muslim.].

Na amesema Mtume (saw): (Mwenyezi Mungu Ameiharamisha Makka na si watu walioiharamisha. Kwa hivyo, si halali kwa anayemuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho

kumwaga damu huko wala kukata mti) [Imepokewa na Bukhari.]



Kuuwa na kumwaga damu

### 3. Kuharamishwa kuingia makafiri na mushrikina haram ya Makka

Amesema Mwenyezi Mungu U: {Enyi mlioamini! Hakika washirikina ni najisi, basi wasikaribie Msikiti wa Haram (Makka) baada ya mwaka wao huu} [9: 28].

Na Mtume (saw) aliamrisha nayeye yuko Mina kutangazwe: (Asihiji mshirikina baada ya mwaka huu, na asitufu Al-Ka'ba mtu akiwa uchi) [Imepokewa na Bukhari.].

### 4. Uharamishaji wa kuwinda, kukata miti na kuokota kwenye Haram ila kwa mwenye kukijulisha

Ibnu ‹Abbas t alipokewa kutoka kwa Mtume (saw) akisema: (Mwenyezi Mungu Ameiharamisha Makka, si halali kwa yoyote kabla yangu wala kwa yoyote baada yangu. Mimi nilihalalishiwa kipindi kichache cha mchana. Mimea yake mibichi haikatwi, na pia miti yake haikatwi, na kiwindwa chake hakifukuzwi, na kilichopotea chake hakiokotwi isipokuwa kwa mwenye kukitangaza) [Imepokewa na Bukhari.].

## Sehemu za ibada ya hija

Sehemu za ibada ya hijja

Alama zake zilizo wazi zinazoipambanua ibada ya Hijja

### 1. Arafaat

Arafaat: ni wingi wa Arafah. Na imeitwa hivyo kwa kuwa Adam na Hawa walijuana hapo, au kwa kuwa watu hapo hukiri makosa yao.
Napo ni mojawapo ya alama iliyo nje ya mipaka ya Haram. Na iko upande wa Kusini Mashariki wa Msikiti wa Haram kwa umbali wa kilomita ishirini. Na jumla ya eneo lake ni kilomita 10, 4 mraba, n hapo mahujaji wanakusanyika siku ya tisa ya Mfungotatu.



Arafaat

## Msikiti wa Namirah

Namirah: ni jabali lilioko upande wa Magharibi wa Msikiti, na kwa sababu ya jabali hilo msikiti unaitwa msikiti wa Namirah.
Na Mtume (saw) alishuka hapo kwenye bonde la ‘Urana, akahutubu na akaswali, na ukajengwa msikiti pale alipohutubu na kuswali, katikati ya bonde la ‘Urana mwanzo wa ukhalifa wa Kiabasia. Na ulimalizika kupanuliwa na kuuamirisha katika kipindi cha ufalme wa Kisuudi, mpaka likafikia eneo lake zaidi ya mita 110 mraba. Na mahujaji wanakusanyika hapo terehe tisa ya Mfungotatu.



Masjid Namirah

## Msikiti wa Swakharaat

Nao uko Arafa, chini ya Jabali la Rehema upande wa kulia wa mwenye kulipanda. Na hapo pana mawe makubwa ambayo Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alisimama hapo jioni ya siku ya Arafa. Mahujaji wanakusanyika hapo siku ya tisa ya Mfungotatu..



Masjid Swakharaat

## Jabali la Rehema

Ni jabali dogo lenye jiwe kubwa, liko umbali wa kilo ishirini Mashariki ya Makka, na ardhi yake imelingana sawa pana. Na mzunguko wake ni kilomita 640 mraba. Mahujaji wanakusanyika hapo siku ya tisa ya Mfungotatu.



Jabalu-Rahma

## 2. Mina

Iliitwa Mina kwa sababu ya damu zinazomwagwa.
Nayo iko baina ya Makka na Muzdalifa kwa umbali wa kilomita saba, Mashariki ya Msikiti wa Haram. Mahujaji wanalala hapo masiku ya tarehe 11-12 ya Mfungotatu kwa anayefanya haraka, na

usiku wa 13 kwa anayejicheleweshа. Napo ni mahali pa ibada ya Hija palioko ndani ya mipaka ya Haram. Na hapo pana Msikiti wa Khiif, na jamaraat, sehemu ya kutupa vijiwe



Mina

## Jamaraat

Na viguzo vitatu vya ibada ya Hija hapo Mina ni: Kiguzo kidogo, cha katinakati na cha mwisho, nazo ni viguzo vya mawe vilivyo ndani ya mabirika matatu, vikiwa ni alama ya mahali alipodhihiri Shetani na bwana wetu Ibrahim akamrushia mawe. Na masafa baina ya kiguzo cha mwisho na cha kati ni kadiri ya mita 247, na baina ya cha katinakati na kidogo ni kadiri ya mita 200.




## Msikiti wa Khaif

Uko kwenye kilele cha jabali la Mina lilioko upande wa kusini, karibu ya Kiguzo kidogo.



Msikiti wa Khiif

### 3. Muzdalifa

Muzdalifa ni mahali baina ya Mina na Arafa. Hapo Mahujaji wanalala baada kusimama Arafa.

Na katikati ya Muzdalifa kuna al-Mash'ar al-Haraam, napo mahali panapopendekezwa Mahujaji wasimame hapo wamuombe Mola wao Aliyetukuka, wamtaje na wamshukuru. Na hapo ni malazi ya mahujaji wanapoteremka kutoka Arafa baada ya jua kuzama la tarehe 9 ya mfungotatu.



Muzdalifa

### 4.Msikiti wa Haraam

### Alkaba tukufu

Alkaba tukufu vile ilivyo ni kichemraba

### Hijri ya Ismail

Nayo ni sehemu ya upande wa kaskazini wa Alkaba ambao matumizi ya Makureshi yalishindwa kumaliza ujenzi walipotaka kuijenga Alkaba, wakaweka ukuta uliyozunguka upande mmoja ili kutanabahisha kuwa sehemu hiyo ni ya Alkaba. Na jina hili ni la kupewa na watu si la kisheria.

## Jiwe Leusi


Nalo liko kwenye nguzo ya upande wa kusini wa Alkaba tukufu, nalo linatoka Peponi. Na Jiwe Leusi limevunjikavunjika halikusalia isipokuwa vijiwe vinane vidogo sana kama mbae za tende.

## Nguzo ya upande wa Yaman

Nayo ni nguzo ya Alkaba iliyoko upande wa kusini Magharibi, na inaitwa Nguzo ya Yamani, kwa kuwa iko kwenye mkabala wa yamani. Na miongoni mwa mambo yanayohusika na nguzo ya yamani ni kuwa iko kwenye misingi ya mwanzo ya Alkaba iliyoinuliwa na Ibrahim na ismail, amani iwashukie.


## Multazam

Nayo ni sehemu iliyo baina ya Jiwe Leusi na mlango wa Alkaba. Na kadiri yake ni mita mbili. Napo ni mahali pa kuitikiwa dua. Imesuniwa kuomba dua hapo pamoja na kuambatisha mashavu, kifua, mikono na vitanga vya mikono.






Jiwe Leusi



Nguzo ya upande wa Yamani



Multazam

# Hukumu za Hija na Umra

## Hijja

### Maana ya Hijja

Hija kilugha

Kukusudia na kuelekea

Hijja kisheria

Ni kukusudia Makka katika kipindi maalumu ili kutekeleza ibada ya Hijja.

## Hukumu ya Hijja na fadhla zake

Hijja ni mojawapo ya nguzo za Kiislamu. Mwenyezi Mungu Alioyetukuka Ameilazimisha kwa waja wake. Anasema Mwenyezi Mungu U: {Ni haki ya Mwenyezi Mungu kwa watu waihiji Alkaba, kwa anayeweza kwenda huko. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi Hawahitajii walimwengu} [3: 67]

Na amesema Mtume (saw): (Uislamu umejengwa juu ya misingi mitano: Kukubali kuwa hapana mola isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake, kusimamisha Swala, kutoa Zaka, kuikusudia Alkaba kwa Hija na kufunga mwezi wa Ramadhani) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na amsema Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw): (Mwenye kuhiji asiseme maneno machafu [ Rafath: ni neno linalotumika kumaanisha maneno machafu.] na asitoke kwenye utiifu wa Mwenyezi Mungu [ Fusuuq: maasia.], atasamehewa dhambi zake zilizotangulia) [Imepokewa na Tirmidhi.].

Na Hijja ni lazima kwa umri mara moja.

## Masharti ya Hijja

### 1. Uislamu

Hijja haimlazimu kafiri, na akihiji haisihi hijja yake.

### 2. Kuwa na akili

Hija haimlazimu mwendawazimu, kwa neno lake (saw): (Watu watatu hawaandikiwi dhambi: aliyelala mpaka azunduke, mtoto mapaka abaleghe na mwendawazimu mpaka apate akili) [Imepokewa na Abu Daud.].

### 3. Kubaleghe

Hijja haimlazimu mtoto mdogo, na lau mtoto mdogo atahirimia hija basi hija yake itasihi. Lakini haimtoshelezi na Hijja ya Uislamu, na itahesabiwa ni Sunna. Hii ni kwa hadithi ya Ibnu ‹Abbas t kwamba mwanamke mmoja alimuinulia Mtume wa

Mwenyezi Mungu (saw) mtoto, na akasema: «Je, huyu ana Hija? Mtume akasema: (Ndio, nawe una thawabu) [Imepokewa na Muslim.].



Mtoto Mdogo anafaa kuhirimia Hijja

## 4. Uhuru

Hijja haimlazimu mtumwa, kwa kuwa Mtume (saw) amesema: (Mtumwa yoyote aliyehiji kisha akaachwa huru, basi itamlazimu Hija nyingine) [Imepokewa na Muslim.].

## 5. Uwezo

Nao ni kuwa na matumizi [ Zaad: Vitu anvyovihitajia kama chakula, kinywaji na mavazi.] na kipando [ Raahilah: Kipando anachokipanda kama gari au ndege au meli..], kwa neno lake Mwenyezi Mungu U: {Ni haki ya Mwenyezi Mungu juu ya watu waikusudie Alkaba kwa ibada ya Hija kwa anayeweza kwenda huko} [3: 97]

## 6. Kuweko na maharimu [ Mahram: ni yule ambaye ni haramu kwa mwanamke kuolewa naye kama baba, ndugu na mjomba.] ya Mwanamke

Kwa hadithi ya Ibnu ‹Abbas t kuwa alisema: Nilimsikia Mtume (saw) akisema: ( Hasafiri mwanamke isipokuwa pamoja na mtu maharimu yake).

Akainuka mtu mmoja akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mke wangu ametoka kwenda kuhiji, na mimi nimejisajili

katika vita kadha na kadha. Akasema Mtume (saw): (Toka uende kuhiji na mkeo) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

## Kuhijiwa (kuwakilisha mtu)

Asiyeweza kuhiji au kufanya Umra kwa uzee au maradhi yasiyotarajiwa kupoa, au kwa udhaifu katika mwili wake kwa namana ya kutoweza kupanda kipando, itamlazimu yeye amwakilishe mtu wa kumhijia au kumfanyia Umra, na hilo linamtosheleza yeye hata kama atapona baada ya kuwa ule mwakilishi wake ashahirimia kwa Hijja au Umrah. Fadhl bin ‘Abbas t Alipokewa akisema kwamba mwanamke wa ukoo wa Khath’am alisema: (Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Baba yangu ilimjia faradhi ya Hija akiwa mzee mkongwe hawezi kulingana juu ya mgongo wa ngamia. Mtume(saw) akasema “Mhijie”) [ Imepokewa na Tirmidhi.].



Mtu asiyeweza kuhiji

Imesharutishwa kwa mtu anayemwakilisha mwingine kumuhijia masharti mawili:

1. Masharti ya Hijja yaliyotangulia yawe yamepatikana kwake.
2. Awe yule aliyewakilishwa ameshajihijia nafsi yake. Mtu lau amhijia mwingine, na yeye bado hajajihijia nafsi yake, Hija yake ya kumhijia mwingine haisihi na itazingatiwa kuwa amejihijia mwenyewe Hija ya Uislamu. Na dalili yake ni hadithi iliyothubutu kutoka kwa Ibnu Abbas t kuwa Mtume (saw) alimsikia mtu akisema: (“Labeka kwa niaba ya Shubrumah”. Mtume akasema: “Ni nani Shubrumah?” Akasema: “Yeye ni jamaa yangu au ndugu yangu”. Akasema: “Je, umjihijia nafsi

yako?” Akasema “La, bado”. Akasema Mtume: “Jihijie nafsi yako kisha mhijie Shubrumah”) [Imepokewa na Abuu Daud].

## Umra

### Maana ya Umra

Umra kilugha

Ziara

Umra kisheria

Ni kuizuru Nyumba Takatifu (Alkaba) wakati wowote mtu anapotaka, kwa kutekeleza matendo ya ibada maalumu.

### Hukumu ya Umra na fadhla zake

Umra ni wajibu wa mara moja katika umri wa mtu kama vile hijja, kwa kauli yake Mtume (saw): (Uislamu ni ukubali kwamba hakuna mola isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na usimamishe Swala, na utoe Zaka, na uikusudie Alkaba kwa ibada ya Hija na ufanye Umra, na uoge kutokana na janaba, na ukamilishe udhu, na ufunge Ramadhani) [Imepokewa na Ibnu Khuzaimah. ]

Na amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw): (Umra mpaka Umra ni kafara ya dhambi baina yake, na Hija iliyokubaliwa haina malipo isipokuwa Pepo) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

# Nyakati (mawaaqiit)

## Maana ya miiqaat

### Nyakati kilugha

Kuweka mpaka baina ya vitu viwili.

### Nyakati kiistilahi ya sheria

Ni mipaka iliyowekwa na sharia kwa ajili ya ibada na yawakati na Namahali.

# Aina ya nyakati

## Kwanza: Nyakati za mahali

### Nyakati za mahali

Ni sehemu zilizowekwa na Sheria kuhirimia kutoka hapo
Haifai kwa anyetaka kuhiji au kufanya Umra azipite sehemu hizo isipokuwa awe amehirimia. Nazo ni sehemu tano [Al-Mawaaqiit wa Ab›aaduhaa. Sheikh Abdullah Al-Bassaam, Gazeti la Majma' al-Fiqh al- Islaami, Idadi: 3, Juzu: 3, ukurasa 1553]:

## 1. Dhul Hulaifah

Nayo ipo upande wa kusini wa mji wa Mtume wa Madina, na unaitwa «Abyaar ‹Ali». Iko mbali na Makka kwa masafa ya kilimita 420.
Nayo ni mahali pa kuhirimia watu wa Madina.



Dhul Hulaifah

## 2. Juhfah:

Nayo iko karibu ya mji wa Raabigh, na ina umbali wa kiasi cha kilomita 186 kutoka Makka.
Nayo ni mahali pa kuhirimia watu wa Shaam, Masri na nchi za upande wa maghribi



Juhfah

## 3. Yalamlam:

Nayo ni bonde kubwa kwenye njia ya watu wa Yaman kwenda Makka.
Kwasasa inaitwa: Assa›diyyah, na iko mbali na Makka kwa kiasi cha kilomita 120.
Nayo ni mahali pa kuhirimia watu wa Yaman.



Yalamlam

## 4. Qarnul Manaazil:

Na sasa inaitwa ( Assaylul Kabiir), na iko mbali na Makka kwa kiasi cha kilomita 75.
Nayo ni mahali pa kuhirimia watu wa Najd na Twaif. Na juu yake, kwenye njia ya Twaif upande wa Hadaa kuna mahali panapoitwa Waadii Muharram.
Na pote pawili ni sehemu ya kuhirimia watu wa Najd na wale wanaokuja kupitia njia ya Twaif.



Qarnul Manaazil

## 5. Dhaatu ‹Irq:

na sasa inaitwa ( Dhariibah au Khuraibaat).
Napo ni mahali upande wa Mashariki ya Makka. Umbali wake na Makka ni kiasi cha kilomita 100. Na kwa sasa hapo mahali pamehamwa.
Nayo ni mahali pa kuhirimia watu wa upande wa Mashariki (Iraki, Irani na nchi za nyuma yake. Na dalili ya yaliyopita ni ni riwaya iliyopokewa kutoka kwa Ibnu Abbas t kuwa alisema: (Mtume wa Mwenyezi Mungu(saw) aliwawekea watu wa Madina Dhulhulaifah iwe ni mahali pa wao kuhirimia, akawawekea watu wa Sham hapo Juhfa. Akawawekea watu wa Najd hapo Qarnulmanaazil, Akawawekea watu wa Yaman hapo Qarnulmanaazil na akasema: ”Sehemu hizo ni zao wao na wanaokuja hapo kati wa watu wa maeneo mengine wanaotaka kuhiji au kufanya Umra”) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
Ama Dhaatu ‘Irq haikutajwa kwenye hadithi iliyotangulia, na lililowekwa ni ‘Umar ibnu l- Khattaab [Imepokewa na Bukhari.].



Dhaatu ‹Irq



Maelezo

- Mwenye kuvuka sehemu hizi za mikati bila ya kuhirimia ni lazima kurudi na kuhirimia ikiwezakana, na isipoweza kufanya hivyo basi atawajibika kutoa fidiya, nao ni mbuzi atakae mchinja makka na agawanye nyama yake kwa masikini wa makka.
- Mwenye kupita sehemu za Mikaati kwa mtu asie kuwa ni wasehemu hiyo basi atahirimi hapo, lau mtu wakutoka najdi amekuja kwa njia ya watu wa madina atahirimia sehemu ya watu wa madina (Abyaar Ali)
- Mtu ikiwa nymba yake iko ndani ya sehemu ya kuhirimia kwa upande wa makka basi Mtu huyu atahirimia hija na umra sehemu alipo Mfano wa watu wa Jiddah na Bahra na Ashraa'i.
- Mwenye kuja kwa njia ya anga na bara, na bahari, huyu atahirimia akiwamkabala na sehemu ya Mikati iliyo karibu. Kwa kauli ya umar binl-khatwab (angaliyani mkabala wake kutoka kwenye njia yenu) [Imepokewa na Bukhari.]
- Mwenye kutia nia ya kuhiji kwa mtu wa makka au asie kuwa mtu wa makka huyu atahirimia makka, ama akitaka kufanya Umra atatoka kwenda tan'iim na Ji'iraan nazo ni sehemu ziko nje ya mipaka ya haram

## Pili: Nyakati za kuhirimia

Nyakati za kuhirimia

Zama za kuhiji na kufanya Umra

## A. Nyakati za Hijja

Ni miezi ya Hija nayo ni: Mfungomosi, Mfungopili na siku kumi za Mfungotatu.

### B. Nyakati za Umra

Ni mwaka mzima

# Kuhirimia

## Maana ya ihram

#### Kuhirimai kilugha

Ni kuzuia

#### Kuhirimia kisheria

Ni nia ya kuingia kwenye ibada ikifungamana na mojawapo ya matendo ya Hijja

Na haifungamani Iharamu ila kwa nia, Mtu hahisabiwi kuwa amehirimia kwa kule kuazimia kwenda hijja au Umra kwa sababu toka aliposafiri mji wake huwa ameazimia kuhiji au kufanya umra, na wala hawi ni mwenye kuhirimia kwa kuvaa ihram au kuleta talbiya bila kutia nia ya ibada ya hijja kwa neno lake Mtume (saw) (Hakika amali zote ni kwa nia na kila mtu hulipwa kama alivyo nuiya) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

## Mambo yanayo pendekezwa katika ihramu

### 1. Kuoga

Khaarijah bin Zaid bin Thaabit t alipokea kutoka kwa baba yake kwamba alimuona Mtume(saw) akivua nguo na kuoga kwa sababu ya kuhirimia Hija [Imepokewa na Tirmidhi.].



## 2. Kujisafisha

Nako ni kuondoa nywele za makapwa yake na kinena chake na kupunguza masharubu yake na kucha zake.







## 3. Kujitia manukato

Kwa hadithi iliyopokewa na Aishah t kwamba alisema: (Nilikuwa nikimtia manukato Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya ihramu yake anapohirimia) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
Wala hazitii manukato nguo zake, kwa kauli ya Mtume (saw): (Na msivae nguo yoyote iliyopakwa zafarani wala manukato ya wars [ Alwars: nimmea wa majano wenye harufu mzuri])
[ Imepokewa na Bukhari na Muslim.].



Manukato

4. Kuvua nguo za kushona [Makhiitw: Kila nguo iliyoshonwa kwa kipimo cha kiungo au juu ya mwili wote, mfano wa kanzu na suruali.] kabla ya kuhirimia [Ama baada ya kuhirimia, ni lazima kwake avue nguo za mzunguko, kwa kuwa hizo ni miongoni mwa vitu] na kuvaa shuka ya chini na ya juu zilizo nyeupe na viatu.

Kwa kauli yake Mtume (saw): (Na ahirimie mmoja wenu akiwa na shuka ya chini na ya juu na viatu. Akikosa viatu, avae khofu mbili, na azikate mpaka kwenye vifundo vya mguu)
[Imepokewa na Ahamad]

Ama mwanamke atavaa nguo anazo taka, wala hakuna nguo ya rangi maalumu, lakini ajiepushe na kufanana na Wanaume na nguo za mapambo, na wala havai nikabu na soksi za mikono [ Quffaaz: nguo inayovaliwa na mwanamke kufinika mkono] katika kuhirimia.ila akiwa kati ya wanaume ajnabi atateremsha nguo yake na kuufunika uso wake, kwa ilivyo thubutu kutoka kwa bibi Aisha t Amesema (Ulikuwa msafara unapo pita mpele yetu na sisi tukiwa na Mtume (saw) Kwenye ihraamu

wakiwa mkabala na sisi akitermsha mmoja wetu jilbabu yake akifunika uso wake wakitupita tukifunuwa) [Imepokewa na Abuu Daud.]



Viatu alie kwenye ihram



Niqabu kwa aliye kwenye ihram



Soksi za mikono kwa mwanamke aliye kwenye ihram



Kikoi na nguo ya juu kwa aliye kwenye ihram

# Mambo yaliyoharamishwa kwa ajili ya ihramu

## 1. Kufinika kichwa cha mwanamume kwa kitu chenye kuambatana nacho.

Kwa hadithi iliyopokewa na Ibnu Umar t kwamba mtu alisema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Huyu aliye kwenye ihramu atavaa nguo gani. Mtume wa Mwenyezi (saw) akasema: (Msivae kanzu wala vilemba wala suruali [ Nayo ni ile inayojulikana kama bantaal.] wala kanzu zilizoshikana na kofia [ Baraanis: kila nguo ambayo kofia yake imeshikana nayo.]) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na amesema(saw) kuhusu mtu aliyekufa na yeye yuko kwenye ihramu: (Msimfinike kichwa chake kwa kitambara [ Laa tukhammiruu ra'sahu: Msimweke mtandio kichwani mwake, nao ni wakufinikia kichwa.], kwani atafufuliwa Siku ya Kiyama akileta Labbaika..) [Imepokewa na Bukhari.].

Ama ikiwa hakikushikana na kichwa kama kutumia mwavuli uo hema au sakafu ya nyumaba au gari hakuna ubaya wowote



Kofia kwa aliye kwenye ihramu



Kilemba kwa aliye kwenye ihramu



Kuvaa suruali kwa aliye kwenye ihramu



Mwavuli kwa aliye kwenye ihramu

## 2. Kuvaa nguo ya kushonwa kwa mwanamume

Maana ya nguo ya kushonwa: ni iliyoshonwa kwa kadiri ya mwili au sehemu ya mwili, kama vile suruwali, kanzu, khofu (soksi nzito), soksi, soksi za mkononi na mfano wake, kwa hadithi iliyopokewa na Ibnu Umar iliyotangulia: (msivae kanzu, vilemba, suruali, Kanzu zilizoshikana na kofia wala khofo.) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Akitopata mwenye kutaka kuhirimia Hija isipokuwa kikoi, basi inafaa avae suruali mapaka atakapopopata kikoi [ Kama mtu aliyesahau mavazi ya kuhirimia kwenye sanduku la safari ndegeni au melini na asiwe na kikoi, basi inafaa avue nguo zake na ahirimie akiwa amevaa suruali na alitatie shati lake liwe ni kama kishali, mpaka atapofika kwenye bandari atatoa mavazi y ake ya kuhirimia na atayavaa na halazimiwi na kitu chochote.]. Na akitopata viatu, inafaa avae khofu, kwa kauli yake Mtume(saw): (Akitopata viatu na avae khofu mbili na azikate mpaka zifike kwenye vifundi vya miguu) [Imepokewa na Ibnu Khuzaimah.].



Khofu (soksi nzito) kwa aliye kwenye ihramu



Buti



Kuvaa nguo ya kushonwa kwa aliye kwenye uhramu

### 3. Kuua kiwindwa wa barani au kumwinda

Kwa neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Msiuwe viindwa na nyinyi mmehirimia Hija} [5: 95].

Yaani na nyinyi muko kwenye ihramu ya Hijja na 'Umra. Na neno lake Aliyetukuka: {Na mmeharamishiwa viindwa vya barani daima mnapokuwa katika hali ya ihramu} [5: 96].

Na maana ya kiwindwa cha barani ni kinachokuwa cha mwituni miongoni mwa wanyama na ndege.

Ama mnyama wa kufugwa si kiindwa. Hivyo basi inafaa kwa aliye kwenye ihramu kuchinja kuku, wanyamahoa (mbuzi, ngo'mbe, ngamia) na mfano wao. Ama kiindwa cha baharini kinafaa, kwa neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka : {Mmehalalishiwa kiindwa cha baharini na chakula chake} [5: 96].

Ama mnyama aliye haramu kuliwa kama nyoka na nge. inafaa inafaa kwa aliye kwenye ihramu kumuua mnyama yoyote anayemshambulia iwapo hakuna njia nyingine ya kujikinga naye isipokuwa hiyo.



Nyoka



Ngekitumbo



Kiindwa cha bahari ni halali kwa aliye kwenye ihramu




Yafaa kuchinja mnyamahoa



Kiindwa cha bara miongoni mwa ndege

## 4. Kunyoa nywele, kuzipunguza au kuzisumua

Kwa neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Na msinyoe vichwa vyenu mpaka wafike wanyama wa kuchinjwa kwa ibada ya Hija mahali pake} [2: 196].
Makatazo haya yanakusanya nywele za mwili wote kwa kukisia nywele za kichwa.



Kunyoa au kupunguza

## 5. Kukata kucha

Sawa ziwe ni kucha za miguu au mikono.



Kukata kucha za mikono



Kukata kucha za miguu

## 6. Kujipaka Manukato mwilini na nguoni

Imekatazwa kwa mwenye kuhirimia Hija kutia manukato mwilini mwake au kwenye nguo yake baada ya kuingia kwenye ihramu, au kuyanusa kwa kusudia, kwa hadithi iliyopokewa na Ibnu ‹Umar iliyotangulia ambayo ndani yake yamo maneno haya: (wala msivae nguo yoyote iliyotiwa zafarani au wars [ Wars: ni mmea rangi ya manjano wenye harufu nzuri hutumiwa kwa kupaka.] ) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.],
na kwa hadithi ya ule aliyekufa katika hali ya ihramu ambayo alisema (saw): (Na msimtie manukato [ Tuhannitwuuhu: tumieni hanuutw. Nayo ni mafuta mazuri yanayochanganywa kafani za maiti.] ) [Imepokewa na Bukhari.].



Kuzipaka Manukato nguo za kuhirimia



Kujipaka manukato mwilini

## 7. Kufunga ndoa

Kwa hadithi iliyopokewa na Uthmaan (R.A.) kwamba Mtume wa Mwewnyezi Mungu (saw) alisema: (Aliye kwenye ihramu haoi wala haolewi wala haposi) [Imepokewa na Muslim.].

## 8. Kuundama

Nako ni kujamii kwenye tupu ya mbele, kwa neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Yoyote anayeingia kwenye ibada ya Hija, basi asiuundame`} [2: 197].

Ibnu ‘Abbas t amesema: “Huko ni kujamii”. Nalo ni jambo kubwa zaidi lililoharamishwa kwa sababu ya ihramu.

### 9. Kustarehe kwenye sehemu isiyokuwa tupu

Kama vile kubusu na kushika, kwani hizo ni njia za kupelekea kuunadama kulikoharamishwa.

### Mambo yaliyoharamishwa kwa mwanamke aliye kwenye ihramu

Mwanamke ni kama mwanamume katika mambo yaliyoharamishwa kwa sababu ya ihramu, na anatafautiana namwanamume katika mambo yafuatayo:

1- yeye afaa kuvaa nguo ya mzunguko.

2- anafaa kufinika kichwa chake.

3- Haifai kujifinika uso [ Niqaab: ni kile ambacho mwanamke anajifinikia uso wake kwacho.] na kuvaa soksi za mikono [ Quffaaz: kinachovawa mkononi.] kwa kauli ya Mtume (saw): (Na asijifinike uso mwanamke aliye kwenye ihramu na asivae soksi za mikono) [Imepokewa na Bukhari.]

Na mwanamke ajifinike uso wake mbele ya wanaume wa nje bila kuvaa nikabu nako ni kuteremsha nguo kichwani mwake. Na inafaa kwake kuvaa dhahabu.

## Maelekezo

1. Swala inayoitwa Swala ya sunna ya kuhirimia haina asili katika Sheria, pia hakuna katika Sheria kujilazimisha na dua fulani katika kuhirimia.

2. Lau mtu asafiri kwa ndege na akakhofia asimakinike kuvaa nguo za ihramu anapofikia mahali pa Kuhirimia, basi atavaa nguo zake kutoka nyumbani au kwenye kiwanja cha ndege, na hatahesabiwa kuwa amehirimia mpaka atie nia ya ihramu kabla hajakaribia mahali pa kuhirimia.

3. Baadhi ya mahujaji wanaacha wazi mabega yao ua upande wa kulia wanapovaa nguo za ihramu, kunakoitwa idhtwibaa'. Hili si sahihi, kwani idhtwibaa' inafanywa wakati wa tawafu ya kufika Makka (quduum) peke yake. Ama tawafu nyinginezo atafinika mabega yake.



Kuliacha wazi bega la kulia katika kuvaa ihramu

## Naswaha kwa Mahujaji wote

Akiazimia muislamu kusafiri kwenda hija au umra ni lazima afuate muongozo yanayo fuata:
1. ausie jamaa zake na watu wake kumcha mwenyezi mungu, nako ni kutekeleza maamrisho yake na kujiepusha na makatazo yake.
2. aandike watu anowadai na wanao mdai na ashuhudishe juu ya hilo
3. afanye haraka kutubia twaba iliyo yakweli kutokamana na madhambi yote Amesema Mwenyezi Mungu {Enyi Mulio amini tubuni kwa Mwenyezi mungu Toba iliyo ya kweli } [ATtahriim: 8]
4. Ikiwa atakuwa na dhuluma za watu kutokana na nafsi au mali au hishima awaregeshee wenyewe au awaombe msamaha kabla ya hajasafiri, kama ilivyo sihi kutoka kwa Mtume (saw) (Yoyote atake kuwa na dhuluma ya ndugu yake kutokamana na mali au hishama amuombe msamaha hapa duniani kabla yakutofaa dinari na dirhamu: ikiwa atakuwa na amali njema yatachukuliwa apewe Yule alie mdhulumu, na ikiwa hana

mema yatachukuliwa maofu ya mwenzake abandikwe yeye) [Imepokewa na Bukhari.]

5. achague katika mali yake mali ya halali ya kuendea hijja au umra Amesema Mtume (saw) ( Hakika Mwenyezi mungu ni Mzuri hakubali ila kizuri) [Imepokewa na Muslim.]

6. Akusudie hijja yake au umra yake Radhi ya Mwenyezi Mungu U na Nyumba ya akhera na kujikurubisha kwake kwa linalo mridhisha Mwenyezi Mungu kutokamana na maneno na vitendo na atahadhari sana kukusudia hija yake mambo yakidunia kama kutaka kusifiwa na kujifakhiri kwa hilo.

7. Na yatakikana kwa mwenye kutaka kwenda hijja au umra kujifunza mambo muhimu yatakao kuifanya hija yake kuwa sahihi, kwa kuuliza asilo lijuwa na kuondosha mushkili, ili afanye ibada yake akiwa mjuzi, na jambo lakusikitisha ni kuwa baadhi ya watu wanaenda hija au umra bila ya kujifunza hukumu zake na kufanya mambo yenye kuharibu hija zao bila kujua.

## Miongoni mwa hukumu za ihramu

Aliye kwenye ihramu akisumukwa na nywele tatu anapopangusa kichwa katika kutawadha au kuoga, hilo halimdhuru. Pia lau baadhi ya nywele za masharubu au ndevu zilisumuka au ukucha wake ukakatika, hilo halitamdhuru, isipokuwa akizisumua kwa kusudi. Na mwanamke analingana na mwanamume katika hilo la kutodhurika na kusumukwa na nywele au kucha.

Inafaa kwa aliye kwenye ihramu kufunga uzi mguuni mwake akihitajia hilo au kukiwa na maslahi ya kufanya hivyo.

- Uwekaji masharti katika nia

Ambaye ni mgonjwa, au anaogopea kutokewa na jambo lenye kumzuia kukamilisha ibada yake ya Hijja, ni sunna kwake aweke sharti wakati wa kuhirimia na aseme: «Tunaitikia mwito wako wa Umra (au Hija) iwapo kutatokea kitu chochote chenye kunifunga mimi nisimalize ibada yangu, basi mahali pangu pa kutahalali ni pale uliponifunga».

Aishah t amepokewa akisema kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) aliingia kwa Dhuba›ah binti Zubair akamwambia: (Huenda ulitaka kuhiji) Aksema: “Najikuta naumwa [ Waj›ah: mgonjwa mwanamke.]”. Akamwambia: (Hiji na ujiwekee sharti na useme ‘ Ewe Mola! Mahali pangu pa kujifungua na ihramu ni pale uliponifunga) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Akisema hivyo, kisha akapatikana na jambo la kumzuia, basi itafaa atahalali (ajifungue na ihramu) bila kulazimiwa na kitu.

# Nusuk na Talbiya

## Ibada ya Hijja (nusuk)

### Maana ya Ibada ya Hija (nusuk)

#### Nusuk Kilugha

Ibada

#### Nusuk kisheria

Ni maneno yanayosemwa na vitendo vinavofanywa na Mwenye kuhiji au kufanya Umra.

### Nia ya ibada ya Hijja (nusuk)

Anapomaliza kuoga na kujinadhifisha yule anayetaka kuhirimia, akavaa nguo za ihramu, na mwanamume akatoa nguo za mzunguko, atanuilia kuingia kwenye ibada ya Hijja au Umra.

Na inapendekezwa aitamke aina ya ibada anayoikusudia. Aseme akikusudia Umra kisha kujistarehesha mpaka Hijja:

«LABBAYKA ALLAHUMMA UMRATAN MUTAMATIAN ILAA-L HAJJI Nakuitikia, ewe Mola, kwa kufanya Umra hali ya kujipumzisha nayo mpaka nifanye ibada ya Hijja» au aseme: LABBAYKA ALLAHUMMA UMRATAN «Nakuitikia kwa kufanya Umra» kisha wakati wa Hijja aseme: LABBAYKA ALLAHUMMA HAJJA «Nakuitikia kwa kuhiji». Na mwenye kuzishikanisha pamoja Hijja na Umra»Nakuitikia kwa Hijja na Umra».

Kwa hadithi ya Anas t kuwa alisema: (Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akisema: "Nakuitikia Kwa kuhiji na kufanya Umra") [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na asipotamka chochote nia ya moyoni inamtosheleza.

## Aina za ibada ya Hija

### 1. Tamattu›:

Nayo ni ahirimie Umra katika miezi ya Hijja mpaka amalize na ajitoe kwenye ihramu yake, kisha katika mwaka huohuo ahirimie Hija.

Na mwenye kufanya tamattu' anapo fika makka atafanya amali ya Umra nayo: Nikutufu, na kufanya sai kati ya Swafaa na marwa, na kunyoa au kupunguza, kisha atajitoa kwenye ihramu yake na avae nguo zake, ikifika tarehe nane mwezi wa mfungotatu, atahirimia hija kisha atafanya amali za hijja na atawajibika kuchinja kwa kupumzika kwake

### 2. Qiraan:

Nayo ni ahirimie Hijja na Umra kwa pamoja., au ahirimie Umra kisha anuilie kufanya hija kabla ya kuanza kufanya tawafu, na mwenye kufanya Qiraan atabaki kwenye ihramu yake mpaka amalize kufanya hija, na atalazimika kuchinja kwa kule kuhirimia pamoja kwa amali ya hija na umra.

### 3. Ifraad:

Nayo ahirimie Hijja peke yake.na mwenye kufanya ifraadi atabaki na ihramu zake mpaka amalize kuhuji na hatolazimika kuchinja.

Na nusuk bora katika hizo tatu ni tamattu kwa sababu Mtume (saw) Aliwaamrisha maswahaba zake wafanye tamattu [ Kwa hadithi iliyopokewa na ‹Aisha t iliyoko kwenye Sahihi ya Muslim.] Kisha ni Qiraan kisha ni Ifraad

## Tafauti kati ya aina tatu za ibada ya Hijja

| | Kujitoa | Qiraan | Ifraad |
|---|---|---|---|
| Wasifu | Umra kisha Hijja | Umra na hijja | Hijja pekeyake |
| Ihramu | Anahirimia mara mbili, ya kwanza kwa ajili ya ‘Umra kisha atahalalika baada ya hapo, kisha anahirimia kwa ajili ya Hijja | Atahirim hijja na umra kwa pamoja | Atahirimia hija mara moja pekeyake |
| Talbiya | Katika kuhirimia mwanzo anasema: “Nimekuitikia ewe Mola wangu ‘Umra” anapohirimia kwa ajili ya Hijja anasema: “Nimekuitikia ewe Mola wangu Hijja” au anasema: “Nimekuitikia ewe Mola wangu ‘Umra na nitapumzika kwayo hadi Hijja” | Atasema wakati wa kuhirimia (Naitikikia umra na hijja) | Atasema wakati wa kuhirimia (Naitikia hijja) |
| Kichinjo | Inapasa kuchinja | Inawajibika kuchinja | Hawajibiki kuchinja |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kutufu | Kuna twawafu mbili, ya kwanza kwa ajili ya 'Umra na ya pili kwa ajili ya Hijja | Inalazimu twawafu moja nayo ni twawafu ya hajji | Inalazimu twawafu moja nayo ni twawafu ya hajji |
| Sai' | Kuna sai' mbili, ya kwanza kwa ajili ya 'umra na ya pili kwa ajili ya Hijja | Ina sai moja peke nayo ni sai ya hijja | Ina sai moja peke nayo ni sai ya hijja |

## Kuleta Talbiya (Labeka)

### Maana ya kuleta Talbiya

Kuleta Labeka

Ni Kusema Mwenye kuhirimia: LABBAYKA ALLAHUMMA LABBAYKA, LABBAYKA LAA SHARIKA LAKA LABBAYKA, INNAL-HAMDA, WANNI'MATA LAKA WALMULKA, LAA SHARIIKA LAKA (Nimekuitika ewe Mola nimekuitika! Nimekuitika Huna mshirika Nimekuitika! Sifa njema zote na neema ni zako. Huna mshirika)

Kwa Hadithi iliyopokewa na Ibnu Umar t kwamba Uletaji Labeka wa Mtume wa Menyezi Mungu(saw) ulikuwa hivyo [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na maana ya "Labbaika Allahumma Labbaika" ni "tumekuitikia baada ya kukuitikia".

Uletaji Labeka umekusanya kumsifu Mwenyezi Mungu na kumshukuru, kutii amri Yake, kudhihirisha kumpwekesha Yeye na kujiepusha na ushirikina.

### Hukumu ya uletaji Talbiya (Labeka)

Uletaji Labeka ni sunna.

Mwanamume atainua sauti yake kwa hiyo Labeka na mwanamke ataifanya chini sauti yake, kwa kuchelea fitina

### Wakati wa uletaji Talbiya na sehemu zake

Mwenye kuhirimia ataanza kuleta Labeka kwa wingi akiwa njiani baada ya kuhirimia.
Na inatiliwa mkazo katika mahali pengi miongoni mwako ni: Akipanda sehemu zilizoinuka juu, au akateremka kwenye bonde, au akaswali Swala ya faradhi, au ukaingia usiku au mchana.
Na ataikata kuleta Labeka akiwa kwenye ibada ya Umra anapoiona Alkaba na akalipa mkono Jiwe Leusi. Na akiwa katika ibada ya Hija ataikata Labeka akianza kukirushia vijiwe kiguzo cha mwisho siku ya Idd.

# Namna ya kuhiji na kufanya Umra

## Namna ya kuhiji

Mwenye kuenda hija, ima huwa ametia nia ya kufanya (Tamattu' ) Kufanya umra kisha kupumzika mpaka wakati wa haji au ametia nia ya ( Qiraan ) nayo nikutia nia ya umra na hija pamoja, na ima awe ametia nia ya(Ifraad) hija pekeyake mwenye kutia nia yatamatt' huwa ametoka kwenye amali ya hija na akatoka kwenye ihram, ama mwenye kufanya qiraan na ifraad watabaki kwenye ihram zao, na shughuli za Hijja zinaanza terehe nane Mfungotatu. Mpaka siku ya kumi na tatu, Na maelezo yake ni kama yafuatayo kwa masiku:

### Siku ya nane ya Mfungotatu (siku ya Tarwiyah)

1. Siku ya nane ni sunna kwa mja kuhirimia hijja kabla ya adhuhuri atahirimia pale alipo, ataoga, atajitia manukato, na atavaa nguo za ihramu na atasema: LABBAYKA ALLAHUMMA

LABBAYKA, LABBAYKA LAA SHARIKA LAKA LABBAYKA, INNAL-HAMDA, WANNI'MATA LAKA WALMULKA, LAA SHARIIKA LAKA (Nimekuitikia, ewe Mola, kwa Hija! Nimekuitika ewe Mola nimekuitika! usiokuwa na mshirika nimekuitika! Sifa njema zote na neema ni zako, na ufalme, Usiokuwa na mshirika) [Imepokewa na Bukhari.].

2. Ataelekea Mina, ataswali huko Adhuhuri, Alasiri, na Magharibi, Isha na Alfajiri ya siku ifuatayo. Ataswali kila Swala kwa katika wakati wake. Atazipunguza Swala za rakaa nne-nne azifanye mbilimbili. Na atasalia hapo Mina mpaka kutokea jua la siku ya tisa.



kuoga



kuhirimia



Mina



Kujipaka manukato

## Siku ya tisa ya Mfungotatu (siku ya Arafa)

1. Jua linapo chomoza siku hii ya tisa mahujaji wataelekea Arafa na huku wakileta talbiya (labbayka allamuhmma labbayka), na ni Sunna kukaa (Namirah) mpaka jua lipinduke na kuingia wakati wa Adhuhuri, na wakati unapo ingia ni sunna kwa kiongozi wa kiislamu au naibu wake awahutubie mahujaji hutuba yenye kunasibiana na hali yao, awakumbushe kumpwekesha mwenyezi mungu na awafunze hukumu za hijja na mambo muhimu kuhusu dini yao.

2. Kisha atawaswalisha adhuhuri na alasiri kwa kuzikusanya, kutanguliza na kuzipunguza, na huruhusiwa mahujaji kwa siku hii aelekee kibla, na azidishe kumuomba mungu na ajitahidi sana katika kuomba, na adhihirishe unyonge wake na udhaifu wake na kumuhitajia kwake mwnezi mungu U na akariri maombi

Amesema Mtume (saw) (Dua bora ni dua ya siku ya Arafa, na maneno bora niyale niliyo yasema mimi na manabii kabla yangu hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki ila

Mwenyezi mungu pekeyake hana mshirika ufalme ni wake, na kusifiwa ni kwake yeye, na yeye ni muweza wakila kitu)
[Imepokewa na Tirmidhi]
na afanye pupa kuomba dua zilizopokelewa kwa Mtume (saw) na ajiepushe na dua ya kujikalifisha, na asome Qur'ani kadiri anavo weza, na akithirishe kumswalia Mtume (saw).

3. Kisha wataondoka mahujaji kutoka arafa wakielekeya Muzdalifa baada jua kuzama na haifai kuondoka kabla ya kuzama kwa jua, na akiondoka kabla kuzama kwa jua itamlazimu arudi hata kama ni usiku na asiporudi itamlazimu yeye damu kuchinja nayo ni kuchinja mbuzi au fungu la saba la ngamia ama fungu lasaba la ngombe



Muzdalifa



Namirah



Arafa

Maelekezo

1. Inahisabika kuwa mtu amesimama arafa kwa kuweko mwenye kuhiji uwanja wa arafa siku ya tisa, sawa akiwa amesimama ama amekaa ama amelala ama amepanda, na silazima kuwa amesimama.

2. Kusimama arafa ni nguzo miongoni mwa nguzo za hijja na haisihi hija ya mtu ikiwa hakusimama Arafa, na mwenye kukosa kusiamam arafa huwa ameikosa hija kwa neno lake Mtume (saw) (Hija ni Arafa) [Imepokewa na Ahmad]

3. Unaanza wakati wa kisimamo cha Arafa kuanzia kutoka kwa alfajiri siku ya tisa mpaka alfajiri ya siku ya kumi, mwenye kusiama Arafa katika wakati huu japo kidogo hali yakuwa ni mtu afaaye kusimama hija yake itasihi, na mwenye kukosa kusimama wakati huu hija yake haikusihi Amepokea Ibnu Abbas kutoka kwa Mtume (saw) Amesema (Mwenye kuipata arafa kabla ya Alfajiri basi ameipata hija) [Amesahihsha Al'albaniy katika swahihil-jaami' No(5995)]

4. Arafa yote ni uwanja wa kisimamo, na Mtume (saw) alisimama kwenye jabali karibu na swakharaat hali yakueleka kibla na wala hakupanda juu ya jabali Amesema (Nimesimama hapa na Arafa yote ni sehemu ya kisimamo) [Imepokewa na Muslim], ikiwa ataweza kusimama alipo simama Mtume ni uzuri na asipo weza atasimama sehemu yoyote, wala haifai kusimama kwenye jangwa wala kupanda jabali,

5. Ni juu ya mwenye kuenda hijja akumbuke kuwa siku ya arafa ni siku kubwa na ina fadhla kubwa, na mwenyezi mungu anawakirimu waja wake, na ajifakhiri mbele ya malaika wake, na nisiku ambao watu huacha huru na moto.Amesema Mtume (saw) ( Hakuna siku ambao Mwenyezi Mungu huacha waja wake huru na moto kuliko siku ya Arafa, na siku hiyo Mwenyezi Mungu anakurubia kisha anajifakhirisha na waja wake, na anasema: wataka nini wajawangu?) [Imepokewa na Muslim], yatakikana kwa hajji kufaidika na masaa ya siku hii tukufu, na kujadidisha Tawba na kujihisabu nafsi yake wala asipoteze wakati wake kwa kuzunguka ovyo na kuzungumza upuzi na kufanya mijadala.

## Usiku wa wa siku yakumi kuondoka kuelekea Muzdalifa na kulala hapo

1. Mahujaji wataondoka kutoka Arafa kuelekea muzdalifa baada ya jua kutwa, na nisunna kwa mahujaji kuondoka kwa utulivu na upole bila ya kuwaudhi watu, na aondoke hali ya kuleta talbiya na kumtaja mwenyezi mungu U.
2. Atakapofika muzdalifa atanza na swala ataswali Maghrib na ishaa kwa kuzikusanya na kupunguza swala ya isha, kabla kuteremsha mizigo na vitu vyake.
3. Nilazima kulala Muzdalifa usiku wake na ataswali alfajiri mapema, na haifai kuondoka muzdalifa kabla ya alfajiri ila kwa wenye udhuru, kama watu madhaifu katika wanawake, na watoto na kwa wale wanaofuatana nawao, ambao wanawatumikia wao yafaa kuodoka nawao mwisho wa usiku mwezi unapo zama.
4. Anapo maliza kuswali alfajiri inapendekezwa kwa mahujaji aende kwenye Mash’aril haram, na aeleke kibla na azidishe dhikri na dua hali yakuwa ameinuwa mikono yake na ataendelea kufanya hivyo mpaka kupambazuke sana, na sehemu yoyote atakapo simama muzdalifa yafaa, kwa neno lake Mtume
(saw) (Nimesimama hapa na jam’u yote ni mahali

pakisimamo) [Imepokewa na Muslim] na makusuduio ya Jam’u ni Muzdalifa.

5. Anapoondoka haaji kutoka muzdalifa inapendekezwa aokote vijiwe saba pekeyake kwa ajili yakutupa kwenye jamaraat, ama masiku yalio baki ataokota vijiwe mina au sehemu yoyote atakapo okota yafaa

## Siku ya kumi ya Mfungotatu (Siku ya Idd)

1. Ataswali Alfajiri, kisha atajishughulisha na kumtaja Mwenyezi Mungu na kuomba dua mpaka kabla ya jua kuchomoza kwa muda mchache.

2. Ataondoka kutoka Muzdalifa kuelekea Mina kabla ya jua kuchomoza.na atazidisha njiani kuleta talbiya na afikapo wango wa muhassira atafanya haraka, nao ni wangwa kabla ya mina baina yake na Muzdalifa

3. Afikapo Mina ataenda kwenye Kiguzo cha mwisho upande wa mina, na cha kwanza kutoka upande wa makka atakapo fika hapo ataacha kuleta talbiya (labayka) na akirushie vijiwe saba kwa mfululizo, kimoja baada ya kingine, akipiga takbiri katika kila kijiwe anachokirusha. Na unaanza wakati unaopendekezwa kurusha vijiwe kuanzia wakati wa alfajiri ya siku ya iddi, na ikiwa atarusha kabla ya alfajiri mwisho wa usiku itasihi na itamtosheleza, na unaendelea wakati wa kutupa mpaka alfajiri siku ya kumi na moja

Maelekezo

- Muislamu ajiepushe na kuwaudhi ndugu zake Mahujaji wakati wa kutupa vijiwe jamaraat, nawakati wakufanya ibada nyinginezo za hija.
- Ahakikishe kuwa kijiwa kimeingie kwenye ndani ya birika, baadhi ya watu wanakosea wakidhani kuwa unapo rusha kijiwe ni kulenga kiguzo na kijiwe kisingie kwenye birika, na baadhi hutupa kijiwa akiwa mbali na birika na kijiwe kisingie kwenye birika basi mwenye kutupa namna hiyo huwa hakutekeleza wajibu wa kutupa.

- Na ni juu ya muislamu asivuke mipaka katika kurusha vijiwe asitupe jiwe kubwa au kurusha viatu, sunna ni kijiwe kiwe kikubwa kidogo kuliko dengu kwa Hadithi ya Jaabir bin Abdillah t Nakasema (Nimemuona Mtume (saw) Akilitupia jamara kwa kijiwe kidogo mfano wa koko ya tende) [ Imepokewa na Muslim. Na vjiwe vyakutupa ni vidogo atavishika kwa vidole viwili na kutupa].

- Na akitupa vijiwe vyote kwa mara moja hahisabiwi ila kijiwe kimoja, na lau ataviweka kwenye kitu avirushe vyote kwa pamoja haitasihi bali ni lazima kupatikane kurusha.

4. Atanyoa kichwa chake chote au atapunguza, na kunyoa ni bora, na Mwanamke atapunguza nywele zake kadri ya ncha za kidole,

5. Atateremka Makka atufu twaafu ya Ifaadhah, nayo ni twawafu ya Hija, na katika twawafu hii hakuna kufanya Raml kutembea haraka wala kufunguwa bega na baada ya kutufu ataswali rakaa mbili, na ubora katika twawafu hii avue nguo za ihraam na avae nguo zake zakawaida na ajipake manukato kwa kauli ya bibi Aisha t Nilikuwa nikimpa Mtume (saw) manukato kwa ajili ya kuhirimia kwake wakati wakuhirimia na wakati wakujitoa kwenye ihrama kabla ya kufanya twawafu. [Imepokewa na Bukhari na Muslim. ]

6. unaanza wakati wakufanya twawafu baada ya alfajiri ya siku iddi, na itamtosheleza kabla ya Alfajiri mwisho wa usiku aliyeondoka Muzdalifa mapema kwa sababu ya udhuru kama watu wazima, na yafaa kuchelewesha kufanya twawafu siku ya iddi lakini si bora kufanya hivyo.

7. Na baada ya kufanya Twawafu ya Ifaadhwa, atafanya sai kwa Mutamatti' ama alie tia nia ya Qiraan na Ifraad kama walifanya sai katika twawafu ya Quduum hawatafanya sa'i baada ya twawafu ya ifaadhwa, na haji akimaliza kufanya twawafu ya ifaadha na akafanya sa'i kwa atakae kuwa na sai huwa ashakamilisha matendo ya siku ya Idd, na itamlazimu arudi mina akalale usiku wa kumi namoja




Kutupa vijiwe kwenye jamarul-Akaba.




kuchinja Mnyama wa tunu





Kunyoa na Kupunguza




Kufanaya Twawafu




Kufanya sai baina ya swafaa na marwa




Kulala Mina

## Mpangilio wa Matendo katika Siku ya Iddi

Sunna katika mipangilio ya siku ya idd ni kama inavo fuata: Kutupa vijiwe, kisha kuchinja, kisha kunyoa au kupunguza, kisha kufanya Twawafu, kisha kufanya sai kwa mwenye sai, na lau atatanguliza moja katika mambo haya juu ya jengine yafaa na hakuna ubaya wowote, kwa sababu mtume (saw) Aliruhusu hilo, lau mtu atanyoa kwanza kisha akatupa mawe itasihi, na lau atachinja kwanza kisha akafanya Twawafu kisha akatupa vijiwe ni sawa, kwa sababu hakulizwa mtume kwa mwenye kutanguliza jambo na kuakhirisha jengine ila akisema (Fanya na hakuna ubaya) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.]

Kuhalalishiwa Mara ya Kwanza na Kuhalalishiwa Mara ya Pili:-

- Kuhalalishiwa ya kwanza: Ni kuhalalishiwa yote yale yalokuwa ni haramu kufanya kwa mwenye kuwa katika ihram isipokuwa kufanya tendo la ndoa au kufunga ndoa itakuwa si halali kwake kufanya hivyo, na inapatikana mtu kuhalalishiwa kwa kufanya mawili katika yanao fuata: kutupa vijiwe kwenye jamaraat,

kunyoa au kupunguza, kufanya Twawafu pamoja nakufanya sai kwa atake kuwa na sai

- Kuhalalishiwa mara ya pili: ni kuhalalishiwa kufanya yote yale yaliokuwa ameharamishiwa kufanya alipokuwa kwenye ihram, na hupatikana uhalali wapili kwa kufanya yale yalio tangulia yote pamoja.

- Kuchinja haina mafungamano na kuhalalishiwa, lau atachelewesha kuchinja mpaka siku ya pili siku ya kumi na moja, na akafanya yale mengine siku ya idd atakuwa amehalalishwa.

## Masiku ya Tashriiq

Ni siku tatu, siku ya kumi na moja na siku ya kumi nambili na siku ya kumi na tatu katika Mwezi wa Mfungotatu zimeitwa kwa jina hilo kwa sababu nyama za Udh'hiya zikikatwakatwa na kuanikwa juani ili zikauke na Mtume Alisema kuhusu masiku haya (Jueni ya kuwa masiku haya ni masiku ya kula nakunywa na kumtaja Mwenyezi Mungu) [Imepokewa na Abuu Daud]

## Siku ya Kumi na Moja na Usiku wake

Nilazima kwa mahujaji kulala mina usiku wa siku ya kumi namoja na siku yakumi na moja baada ya kupinduka juwa wataenda kutupa vijiwe katika jamarati zote kwa kila jamara atatupa vijiwe saba

- Namna ya kutupa Vijiwe

Atanza kwenye Jamarati ya Kwanza: atavirushia vijiwe saba kwa kufuatana, na atapiga takbiri (Allahu Akbar) kwa kila kijiwe, na nilazima ahakikishe kuwa kijiwe kimeingia kwenye lile birika, kisha atasongea mbele kidogo asimame amuombe Mwenyezi Mungu hali ya kuinuwa mikono yake juu.

-Kisha atarusha kwenye jamara ya katikati atatupa vijiwe saba kama alivyo fanaya kwenye jamara ya kwanza kisha atasimama amuombe Mwenyezi Mungu hali yakuinuwa mikono yake.

-kisha atarusha kwanye jamara ya mwisho atatupa vijiwe saba wala hataomba dua



Kiguzo kidogo



Kiguzo cha Mwisho



Kiguzo cha katinakati

## Siku ya Kumi na mbili na Usiku wake

Nilazima kualala minaa usiku wa siku ya kumi na mbili, na mchana wake jua litakapo pinduka atatupa vijiwe kwenye jamarati zote kama alivyo fanya siku ya kumi na moja.

Ikiwa atataka kufanya haraka kuondoka siku hii, basi akisha maliza kutupa ataondoka mina kabla ya kutwa jua, ikiwa jua litazama nayeye yuko minaa basi itamlazimu kulala mina na kulazimaka kutupa vijiwe siku ya kumi na tatu, nao nikuzidisha kheri kama alivyo sema Mwenyezi Mungu U {Na mtajeni

Mwenyezi Mungu katika zile siku zinazo hisabiwa.Lakini mwenye kufanya haraka katika siku mbili (akaregea) si dhambi juu yake na mwenye kukawia pia si dhambi juu yake, kwa mwenye kumcha mungu} [Al-Baqara: 203]

Na makusudio kwa mwenye kufanya haraka siku mbili katika masiku ya tashriiq ni siku ya kumi na moja na siku ya kumi na mbili na mwenye kuchelewa na akatimiza siku ya kumi natatu.

## Siku ya kumi na tatu na usiku wake

Na baada ya kupinduka jua siku ya kumi na tatu atatupa vijiwe kwenye jamarati zote kwa namna alivyo fanya katiku siku mbili zilizo pita, na unamalizika wakati wa kutupa baada ya kutwa jua siku hii

## Kuchelewesha Kurusha

Lau mwenye kufanya hijja ataakhirisha kutupa vijiwe mpaka siku ya pili yake yafaa kwa sababu masiku ya tashriiq yote ni masiku ya kutupa.

## Namna yakutupa kwa alie akhirisha kutupa

Ni aanze kutupa siku ya kwanza katika jamrati zote, kisha arudi atupe tena akianza jamaraat ya kwanza mpaka amalize zote, na harushi isipokuwa baada ya kupinduka jua

## Twawafu ya kuaga

Anae fanya haji akitaka kutoka makka atafanya twawaafu ya kuaga, nayo ni wajibu miongoni mwa wajibu za hija, na hafanyi sai na hupomoka twawafu ya kuaga kwa mwanamke menye hedhi na nifasi

## Kuichelewasha Twawafu ya Ifaadha mpaka kwenye Twawafu ya Kuaga

Lau mwenye kufanya hija ataichelewesha Twawafu ya Ifaadha mpaka kwenye Twawafu ya kuaga yafaa kufanya hivyo lakini si bora kufanya hivyo, na itamtosheleza twawafu ya ifaadha kwa sharti atie nia ya ifaadha itamtosheleza na twawafu ya kuaga hata kama atafanya sai baada yake.

## Namna ya Kufanya Umrah

1. Atakayefanya Umra afikapo mahali pa kuhirimia, ataoga, atajitia manukato, atavaa mavazi ya kuhirimia na atanuilia Umra hali ya kusema: (Tunakuitikia kwa ibada ya Umra).



Kuoga



Manukato



Mavazi ya ihramu

2. Katike kuleta Labeka, Sheria imeweka aseme: (Tumekuitikia, ewe Mola, tumekuitikia! Huna mshirika tumekuitikia! Sifa njema na neema ni zako na ufalme! Huna mshirika!) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].

Na ataendelea kuleta Labeka mpaka aione Alkaba na alisalimie Jiwe Leusi.

3. Atakwenda aingie Msikiti wa Haram, aanze kwa mguu wake wa kulia na aombe dua ya kuingia msikitini.

4. Anaikata Labeka na aanze kutufu Alkaba, kuanzia kwenye Jiwe Leusi, alishike na alibusu ikiwezekana- ikiwa haikuwezekana ataliashiria kwa mkono wake na atasema: (Kwa jina la Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mkuu. Ewe Mola! Ninatufu Kwa kukuamini Wewe na kukiamini Kitabu Chako, na kwa kutekeleza ahadi Yako na kwa kufuata mwendo wa Nabii Wako Muhammad ﷺ).

5. Atafanya twawafu mara saba huku Alkaba ikiwa upande wake wa kushoto, akianzia kwenye Jiwe Leusi na kumalizia hapo.

6. Imesunniwa kwa mwanamume atembee kwa haraka katika mizunguko mitatu ya mwanzo.na afunguwe bega lake la mkono wa kulia

Masharti ya kutufu

Inashurutiswa kwa mwenye kufanya Twawafu: kutia nia na kujitoharisha na kusitiri tupu, na azunguke mara saba, na aanze kwenye jiwe leusi, na aijaliye Alkaba upande wake wa kushoto na afuatanishe bena ya mzunguko ila inapo kimiwa swala au ikiswaliwa janaza ataswali kisha ataendelea pale alipokoma kwenye twawafu yake, na aizunguke alkaba yote lau ataingia kwenye hijri haitosihi twawafu yake kwa sababu hijri ni katika Alkaba.

7. Ataomba atakalo katika kutufu. Na akikaribia Nguzo ya Upande wa Yamani aishike kwa mkono na apige takbiri. Akitoweza atoiashiria na hatopiga takbiri. Na akiwa baina ya Nguzo ya Upande wa Yamani na Jiwe Leusi aseme: (Mola wetu! Tupe jema la ulimwenguni na jema la Akhera na utuepushe na adhabu ya Moto) [Imepokewa na Abuu Daud]

8. Baada ya kutufu Alkaaba ataswali rakaa mbili nyuma ya Makaam Ibrahim - ikiwezekana kama haikuwezekana ataswali sehemu yoyote msikitini

Maelekezo

1. Ni juu ya muislamu kutoingia kwenye zahma pamoja na wenye kutufu ili asijitie kwenye tabu yeye na kuwatia wenzake, katika kutaka kulisalimia jiwe jeusi ama kulibusu, na vilevile hata fanya raml kufanya haraka katika kuzunguka alkaba ikiwa atawaudhi wenye kufanya twafu.
2. ataomba kwenye twawafu kwa atakavo weza, na twawafu haina dua maluum isipokuwa yale yalio tanguliya, na lau atasoma qur'ani katika twawafu yake hakuna ubaya wowote kufanya hivyo.
3. kufanya idhtibaa (kufungua bega) ni sunna katika Twawafu ya umra au twawafu ya quduum katika mizungu yote.
4. Na mwanamke ajiepushe kudhihirisha mapambo katika twawafu yake na kujipaka manukato, na kuinuwa sauti katika kuleta dhikri na dua
9. Atatoka kuelekea Jabali la Swafaa, akilikaribia atasoma neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Hakika Swafaa na Marwah ni miongoni mwa sehemu za ibada ya Hija, basi anayehiji au kufanya Umra, si makosa kwake kusai baina hayo mawili. Na mwenye kujitolea kufanya mambo ya kheri, Mwenyezi Mungu ni Mwenye kushukuru, ni Mwingi wa ujuzi} [2: 158].
10. Atapanda juu ya Swafaa na ataelekea Kibla, atainua mikono yake na atamtukuza Mwenyezi Mungu na kumsifu na atasema: (Hapana mola anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Peke Yake, Asiye na mshirika. Ni Wake Yeye ufalme na ni Zake Yeye sifa njema. Na Yeye kwa kila kitu ni Muweza Tunarudi makwetu, tunatubia kwa Mola wetu, tunamuabudu, tunamsujudia na tunamsifu. Mwenyezi Mungu Ametimiza ahadi Yake, Amemnusuru mja Wake na Ameyashinda mapote Peke Yake) [Imepokewa na Bukhari.]
Kisha ataomba baada ya hapo, kisha airudie hiyo dhikiri mara ya pili, kisha aombe, kisha airudie dhikiri mara ya tatu.
11. Atashuka Swafaa akielekea Marwah, aharakishe mwendo wake anapokuwa baina ya alama mbili za rangi ya kijani [ Nazo ni

alama mbili za mahali alipopakimbia Bibi Hajra kwa kusai baina ya Swafaa baina na Marwah], apande Marwah na atafanya namna hiyo akiwa Swafaa.

12. Atasai baina ya Swafaa na Marwah mara saba.

13. Baada ya kusai, mwanamume atapunguza nywele zake za kichwa kwa namna ya kuonekana wazi kuwa zimepunguzwa. Na mwanamke atapunguza kwenye pambizo zote za nywele za kichwa chake kadiri ya ncha ya kidole.

Na lililo bora kwa mwanamume ni kunyoa, kwa hadithi iliyothibiti kutoka kwa Abu Huraira t kwamba alisema kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) Alisema: (Ewe Mola! Warehemu walionyoa. Wakasema: " na waliopunguza pia?" Akasema: "Ewe Mola! Warehemu walionyoa." Wakasema: "Na waliopunguza pia?" Akalikariri hilo mara tatu, kisha akasema "na waliopunguza pia") [Imepokewa na Bukhari.].

14. Atajitoa kwenye ihramu yake.

Na kwa hivyo atakuwa amemaliza Umra yake.



Kufanya sai kati ya Swafaa na Marwa

# Nguzo, Wajibu na Sunna za Hija

## Nguzo za Hijja

1. Kuhirimia:
kwa neno la Mtume (saw): ( Hakika matendo mema yategemea nia, na hakika kila mtu atapata lile alilonuilia) [Imepokewa na Bukhari.].
2. Kusai baina ya Swafaa na Marwah:
kwa neno lake (saw): (Saini, kwani Mwenyezi Mungu Amewafaradhia kusai) [Imepokewa na Ahmad.].
3. Kusimama Arafa:
kwa kauli ya Mtume (saw): (Hija ni Arafa) [Imepokewa na Tirmidhi.].
4. Twawafu ya Ifaadhah:
kwa neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Na ili waitufu Nyumba ya Zamani} [22: 29].
- Tanabahisho
Mwenye kuacha nguzo moja miongoni mwa nguzo za Hijja, ikiwa ni kuhirimia basi ibada yake haikubaliki kwa sababu hakutia nia na ibada haikubaliki bila ya nia na ikwa ni nguzo nyingine ya Hijja haitatimia mpaka ailete.

## Wajibu za Hijja

1. Kuhirimia kwenye sehemu zilizowekwa kuhirimia:
kwa neno lake (saw) baada ya kuzitaja sehemu za kuhirimia: (Hizo ni za watu wa sehemu hizo na wale wanaokuja hapo kati ya watu wa sehemu nyingine miongoni mwa wale wanataka kuhiji au kufanya Umra) [Imepokewa na Bukhari].
2. Kusimama Arafa mpaka jua kuzama kwa aliyesimama mchana:
Kwa kuwa Nabii (saw) alisimama mpaka jua likazama.
3. Kulala hapo Muzdalifa:

kwa sababu Mtume (saw) alilala hapo na akasema: (Umma wangu wachukue ibada yao ya Hija kutoka kwangu, kwani mimi sijui pengine huenda nisikutane nao baada ya mwaka wangu huu) [Imepokewa na Ibnu Maja.].

Na kwamba yeye (saw) aliwaruhusu Waislamu madhaifu baada ya nusu ya usiku. Hilo linaonyesha kwamba kulala hapo Muzdalifa ni lazima. Na Mwenyezi Mungu Ameamrisha atajwe katika Mash'ar al-Haraam.

4. Kulala Mina masiku ya siku za tashriiq:

kwa ilivyothubutu kwamba Nabii (saw) aliwaruhusu wachungaji kulala kando ya Mina [Imepokewa na Abu Ya›laa katika Musnad yake.].

Hii inaonyesha kwamba asili ni kuwa kulala Mina ni wajibu.

5. Kuvirushia viguzo vijiwe,

kwa kauli Yake Aliyetukuka: {Na mtajeni Mwenyezi Mungu katika siku zinazohesabika} [2: 203].

Na siku zinazohesabika: ni siku za ashriiq.

Na kurusha vijiwe ni miongoni mwa kumtaja Mwenyezi Mungu, kwa neno la Mtume (saw): (Hakika kutufu Alkaba, kusai baina ya Swafaa na Marwah na kuvirushia viguzo vijiwe ni miongoni mwa kusimamisha utajo wa Mwenyezi Mungu) [Imepokewa na Abu Daud.].

6. Kunyoa au kupunguza,

kwa neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Mtaingia- mtaingia Msikiti wa Haram mkiwa kwenye amani, Mwenyezi Mungu Atakapo, hali ya kunyoa vichwa vyenu na kupunguza} [48: 27].

7. Kutufu twawafu ya kuaga:

kwa haditi iliyothubutu kutoka kwa Ibnu 'Abbas t kuwa alisema: (Wameamrishwa watu kuwe kule kutufu twawafu ya kuaga iwe shughuli yao ya mwisho kwenye Alkaba, isipokuwa mwenye hedhi alirahisishiwa) [Imepokewa na Muslim].

## Sunna za Hijja

Lisilokuwa nguzo na wajibu ni Sunna, kama inavyofuata:
1. Kuoga wakati wa kuhirimia.
2. Kuhirimia kwa kikoi cheupe na shuka ya juu nyeupe.
3. Kuleta Labeka kwa sauti ya juu.
4. Kutufu twawafu ya kufika Makka kwa anayechanganya Hija na Umra na anayehiji peke yake.
5. Kwenda haraka katika mizunguko mitatu ya mwanzo twawafu ya kufika Makka (kwa ibada ya Hija) au Umra. Ramal ni kutembea kwa haraka.
6. Kufanya idhtibaa' katika twawafu ya kufika Makka (kwa mwenye kuhiji) au Umra, nako ni kuiweka shuka yake ya juu chini ya kapwa la mkono wa kulia.
7. Kulala Mina usiku wa Arafa.
8. Kulibusu Jiwe Leusi.
9. Kukusanya swala ya Maghrib na isha katika Muzdalifa kwa kuchelewesh
10. Kusimama Muzdalifa kwenye mash'aril haraam kuanzia Alfajiri mpa karibu na kuchomoza jua akiweza kufanaya hivyo, asipo weza sehemu yoyote ya Muzdalifa ni sehemu yakisimamo.

### Sunna za Hijja

Mwenye kuiacha sunna moja miongoni mwa sunna za Hija, halazimiwi na kitu chochote, na Hija yake ni sahihi.

### Wajibu wa Hajji

Mwenye kuacha wajibu itamlazimu kuchinja mnyama ili kuunga upungufu huu.

# Nguzo, Wajibu na Sunna za Umra

# Nguzo za Umra

## 1. Kuhirimia:

kwa kauli ya Mtume (saw): (Hakika matendo yanazingatiwa kwa nia, na hakika ni kwamba kila mtu atapata lile alilonuiilia) [Imepokewa na Bukhari.].

## 2. Kusai baina ya Swafaa na Marwah:

kwa kauli ya Mtume (saw): (Fanyeni Sai, kwa kuwa Mwenyezi Mungu Amewafaradhia kusai) [Imepokewa na Ahmad.].

## 3. Alkaaba:

kwa neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {na waitufu Nyumba ya Zamani} [22: 29]



Kuhirimia





## Wajibu za Umra

1. Kuhirimia kutoka kwenye mahali palipowekewa kuhirimia,
kwa neno lake mtume (saw) baada ya kutaja sehemu za kuhirimia: (Sehemu hizo zimewekewa watu wa hapo na wasiokuwa watu wa hapo kati ya wale wanaofika hapo miongoni mwa wanaotaka kuhiji au kufanya Umra) [Imepokewa na Bukhari.].

2. Kunyoa au kupunguza,
kwa neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Mtaingia-mtaingia Msikiti wa Haram mkiwa katika amani apendapo Mwenyezi Mungu, hali ya ya kunyoa vichwa vyenu na kupunguza} [48: 27].



Kuhirimia



Kunyoa na Kupunguza

## Sunna za Umra

Sizokuwa nguzo na wajibu ni sunna.
- Matanabahisho
1. Mwenye kuacha nguzo moja miongoni mwa nguzo za Umra, ibada yake ya Umra haitatimia mpaka ailete.
2. Mweye kuacha tendo moja la wajibu miongoni mwa wajibu za Umra, itamlazimu achinje mnyama (mbuzi au kondoo, au fungu moja kati ya mafungo saba ya ngombe au ngamia.
3. Mwenye kuacha sunna ya umra haimlazimu chochote, na umra yake ni sahihi.

# Fidiya na hady

# Kwanza: Fidia

## Maana ya fidiya

### Fidia

Ni kitu kinachomlazimu mwnye kuhiji au mwenye kufanya Umra kwa sababu ya kuacha tendo la wajibu au kufanya tendo lililokatazwa

## Kwanza: Fidia ya kuacha tendo la wajibu

Mwenye kuacha wajibu miongoni mwa wajibu za Hija au Umra, kama aliyeacha kulala Muzdalifa au kunyoa au nyinginezo, itamlazimu fidia, nayo ni kuchinja mnyama.

Na mnyama anayekusudiwa ni fungu moja kati ya mafungu saba ya ngamia au ng›ombe au ni mbuzi aliyemaliza mwaka mmoja au kondoo aliyepita miezi sita. Atachinja katika Haramu ya Makka na nyama yake atagawia mafukara wa Makka.

Akikosa mnyama wa kuchinja, atafunga siku kumi: siku tatu akiwa Hija ikiwezekana, na siku saba arudipo kwa watu wake. Mwenyezi Mungu U Anasema: {Asiyepata (cha kuchinja) atafunga siku tatu huko Hija na siku saba mtakaporudi. Hizo siku kumi kamili. Hukumu hiyo ni kwa yule watu wake si wakazi wa eneo la Msikiti wa Haram. Na mcheni Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kutesa} [2: 196].

## Pili: Fidia ya kufanya tendo lililokatazwa

### 1. Fidia ya kuvaa nguo ya mzunguko, kufinika kichwa, kujitia manukato, kunyoa nywele na kukata kucha.

Mwenye kufanya mojawapo ya matendo haya atachaguzwa baina ya mambo matatu:

a. Kufunga siku tatu.

b. Kuwalisha masikini sita, kila masikini nusu ya pishi ya chakula kama mchele na mfano wake.

c. Kuchinja mbuzi.

Dalili ni neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Na msinyoe vichwa vyenu mpaka wanyama waliotunukiwa kwa ibada ya Hija wafike mahali pa kuchinjwa. Basi mtu atakayekuwa mgonjwa, au ana vitu vya kumkera kichwani mwake, atatoa fidia ya kufunga, kutoa sadaka au kuchinja} [2: 196].


Na neno la Mtume (saw) kumwambia Ka'b bin 'Ujrah t na yeye yuko kwenye ihramu: (Je, hao niwadudu wa kichwani mwako?). Akasema: "Ndio". Mtume (saw) akamwambia: (Nyoa kichwa chako kisha uchinje mbuzi ikiwa ni ibada au funga siku tatu au lisha masikini sita pishi tatu za tende).

Mwenye kufanya katazo miongoni mwa makatazo matano yaliyotajwa kwa kukusudia, au akahitaji kulifanya na akalifanya, kama ilivyotokea kwa Ka'b t, basi atatoa fidia ya kero.

Na mwenye kufanya lolote miongoni mwa haya yaliyokatazwa kwa kusahau, basi hana makosa



Kunyoa nywele



Kukata kucha



Kujipaka manukato



Kuvaa nguo ya kushonwa



Kufunika kichwa kwa kitu cha kushika

## 2. Fidia ya kustarehe sehemu isiyokuwa tupu ya mbele na kuundama katika Hija baada ya tahaluli ya kwanza (kujitoa ka kwanza kwenye vikwazo vya kuhirimi)

Hii fidia yake ni kama ile ya kero iliyotangulia

## 3. Fidia ya mtu kuundama akiwa Hija kabla ya tahaluli ya kwanza.

Nayo ni kuchinja ngamia [ Ngamia]. Akikosa atafunga siku tatu katika Hija na siku saba anaporudi kwa watu wake, na hija yake

itakuwa imeharibika, na itamlazimu aikamilishe na ailipe mwaka unaokuja.

### 4. Fidia ya mtu kuundama katika Umra

Nayo ni mbuzi au kondoo, na Umra yake itakuwa imeharibika. Na itamlazimu ailipe.

### 5. Fidia ya kuua kiwindwa:

Kikiwa kiwindwa kina mfano, Aliyewinda atachaguzwa baina ya kutoa mfano, au kukitia kima (thamani) na kununua kwa kima hicho chakula na kukigawanya kwa mifuto (vibaba): kila masikini mifuto miwili [Almuddani: Nusu ya pishi nikipimo 1020 grm], au afunge kwa kila mifuto miwili siku moja.

Makusudio ya kiwindwa ni kile chenye mfano. Yaani: kuna mnyama mwenye kufanana nacho kiasi fulani, na sio kufanana kikamilifu, kwani kufanana namna hiyo haimkiniki.

Mfano wa hilo: Lau mtu aliwinda mbuni, basi itampasa achinje ngamia mmoja, sababu mbuni anafanana na ngamia, au amtie thamani ngamia na anunue kwa thamani yake chakula kama vile mchele au mahindi, na amlishe kila masikini mifuto miwili ya hiko chakula, au afunge kwa kila mifuto miwili siku moja. Na lau aliwinda pundamilia, basi itamlazimu ng'ombe na namna hiyo.

Na iwapo kiwindwa hakina mfano miongoni mwa wanyama hoa, kama vile nzige na kisigi (ndege mdogo), basi atapewa hiari baina ya kununua chakula kwa thamani ya kile kiwindwa na kuwalisha masikini au afunge kwa kila mifuto miwili siku moja. Na wenye kukitia thamani ni watu wawili waadilifu.

Haifai kufungisha ndoa kwa mwenye kuhiji na mwenye kufanya umra wala hana fidiya mwenye kufanya hivyo



Mbuzi au kondoo



Ngamia

## Pili: Wanyama wanaotunukiwa

### Maana ya mnyama wa tunu

Wanyama wanaotunukiwa

Ni wanyama hoa wanaotunukiwa sehemu takatifu kwa kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, au ilio wajibishwa kwa sababu ya Tamattu'au Qiraan au kufungizika

### Aina ya wanyama wanaotunukiwa

### 1. Tunuku ya Tamattu› na Qiraan

Anayechanganya Hija na Umra kwa njia ya Tamattu› au Qiraan itamlazimu achinje mnyama wa tunuku: naye ni mbuzi au fungu moja la mafungu saba ya ngamia au ng›ombe. Akikosa mnyama atafunga siku kumi: siku tatu ziwe katika Hija na siku saba ziwe baada ya mwenye kuhiji kurudi kwa watu wake. Hili humlazimu Yule ambaye si mkazi wa Makka, iwapo ni miongoni mwa wakazi wa Makka, hatalazimika kuchinja mnyama wa kutunuku wala kufunga, kwa neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Mwenye

kujistarehesha kwa Umra mpaka Hija, basi itamlazimu achinje mnyama wa kutunuku aliye sahali kwake, na asipopata atafunga siku tatu katika Hija na saba mtakaporudi. Hizo ni kumi kamili. Hukumu hiyo inamhusu yule ambaye watu wake wa nyumbani si wakazi wa maeneo ya Msikiti wa Haram} [2: 196].

## 2. Mnyama wa kutunuku wa kujiotolea

Naye ni mnyama ambaye mwenye kuhiji tu au anayefanya Umra ya kujitolea anamtunuku, au yule ambaye mwenye kufanya Hija ya Qiraan au ya Tamattu› anamtunuku ikiwa ni zaidi ya wajibu, au ni mnyama ambye hutunukiwa Makka na mtu ambaye hako kwenye ihramu kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Mnyama anayetunukiwa kwa kujitolea na yule wa Hija ya Tamattu' au Qiraan, inafaa kwa yule anayemtoa kula kitu katika nyama yake, bali ni sunna kufanya hivyo. Hii ni kuambatana na kitendo cha Mtume (saw) kwa kuwa (Aliamrisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw)katika kila mnyama aliyemtoa kuchinjwa, apatiwe sehemu [Imepokewa na Bukhari.]. Basi ikapikwa na akanywa supu yake) [Imepokewa na Tirmidhi].

## 3.Kuchinja mnyama wa kutunuku kwa kuzuiliwa kuhiji

Ihswaar: Ni kuzuiliwa kutimiza Hija au Umra au yote mawili. Mwenye kuhirimia Hija au Umra, akazuiliwa na adui kuifikia Alkaba, au akatukiwa na jambo likamfanya asiweze kufika kwenye Alkaba, basi atachinja mnyama mahali alipo, kisha atajitoa kwenye vikwazo vya ihramu, kwa neno la Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Basi mkizuilika kuendelea na ibada ya Hija au Umra, chinjeni kilichokuwa sahali} [2: 196].

Na wanyama wa kuchinjwa kwa sababu ya kuzuilika ni mbuzi/kondoo au fungu moja kati ya mafungu saba ya ngamia au ng'ombe.

## Mahali pa kuchinja mnyama wa kutunuku

Tunuku ya Hija ya Tamatta' au Qiraan au ya kujitolea, huchinjwa ndani ya mipaka ya Haram na hugawiwa masikini wake. Iwapo atachinja nje ya mipaka ya Haram haitomtosheleza.
Na mnyama wa tunuku kwa sababu ya kuzuiliwa atamchinja mahali alipozuilika.

### Wakati wa kuchinja mnyama wa kutunuku

1. Tunuku ya Hijja ya Tamattu', Qiraan na ya kujitolea
Wakati wake unaanza baada ya Swala ya Idd ya siku ya Idd ya kuchinja mpaka jua la siku ya mwisho ya siku za Tashriiq kuzama, nayo ni siku ya 13.
2. Tunuku ya kuzuilika
Wakati wake ni pale kizuizi kinapotokea

Miongoni mwa hukumu za Hadyi (Kuchinja mnyma)

Inafaa kwa mwenye kuhiji kumuwakilisha mtu wa kumchinjia ikiwa Hijja yake ni ya Qiraan au Tamattu› na akiwa aliyewakilishwa ni mwaminifu. Na lililo bora ni kuwa mwenye kuhiji afanye mwenyewe kwa kuwa Mtume( SAW) ndivyo alivyofanya.
Fidia haitoshelezi iwe ni badala ya kudhahi, kwa kuwa fidia ni ya kuchanganya Hija na Umra, ama kudhahi ni sunna ya anayehiji na asiyehiji.

# Mnyama wa kudhahi (kuchinja siku ya Idd)

## Maana ya mnyama wa Udh'hiya

Mnyama wa kudhahi
Ni yule anayechinjwa miongoni mwa wanyama howa siku za idd ya kuchinja kwa kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka.

## Hukumu ya kudhahi

Ni sunna iliyotiliwa mkazo, kwa neno lake Mwenyezi Mungu Aliyetukuka: {Basi mswalie Mola wako na uchinje} [108: 20]. Na kwa hadithi ya Anas t kwamba Nabii (saw) alidhahi (alichinja) kondoo wawili wazuri [ Amlah: Mnyama mwenye weupe na weusi, na weupe ukawa ni mwingi zaidi.] wenye pembe [ Aqran: mwenye pembe.]. Aliwachinja kwa mkono wake. Akapiga bismillahi na akaleta takbiri na akaweka guu lake juu mbavu zao [Swifaahuhumaa: ni wingi wa swafhah nao ni upande wa shingo.]) [ Imepokewa na Tirmidhi].

## Wakati wa kuchinja mnyama wa Udh’hiya

Wakati wa kuchinja unaanza baada ya Swala ya Idd ya kuchinga mpaka jua la siku ya mwisho wa siku za tashriiq kuzama (Siku ya kumi na moja, kumi nambili na kumi na tatu za mwezi wa Mfungotatu).

## Mnyama wa Udh’hiya anayetosheleza

1. Mbuzi au kondoo mmoja anamtosheleza mtu mmoja. Na anaweza kumshirikisha anayemtaka katika thawabu, kwa kuwa Mtume alipotaka kuchinja mnyama wake wa kudhahi alisema: (Bismillahi. Ewe Mola mtakabalie Muhammad na jamaa za Muhammad na umma wa Muhammad) [Imepokewa na Bukhari na Muslim.].
2. Ngamia mmoja na ng’ombe mmoja wanawatosheleza watu saba. Basi yafaa kwa watu saba kushirikiana katika ngamia au ng’ombe, kwa kauli ya Jabir: (Akatuamrisha Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ tushirikiane katika ngamia na

ng’ombe, kila watu saba miongoni mwetu kwa ngamia mmoja [Badanah: ni ngamia, awe ni mwanamke au mwanamke.] ) [Imepokewa na Muslim.].

## Miaka ya mnyama inayotosheleza kwa Udh’hiya

Jadha› wa kondoo: Naye ni mwenye miezi sita.
Thanii wa mbuzi: ni mwenye mwaka mmoja.
Thanii wa ng’ombe: ni mwenye miaka miwili.
Thanii wa ngamia: ni mwenye miaka mitano.

## Mnyama bora wa Udh’hiya

Mnyama bora ni ngamia ikiwa atatolewa mzima kwa sababu thamani yake iko juu na nimanufaa kwa mafakiri kisha ni Ngo;mbe ikiwa atatolewa mzima kisha Mbuzi, kisha fungu la saba la Ngamia kisha fungu la saba la Ngo’mbe


## Aibu za mnyama wa Udh’hiya

### 1. Aibu zinazozuia kutosheleza [ Inazuilia kutosheleza: Haisihi kumchinja kama mnyama wa kudhahi.]

‹Awraa’: Ni mnyama mwenye ila machoni mwake, na anaingia ndani ya huyo mnyama kipofu.
‹Arjaa›: Ni mnyama asiyeweza kutembea.
‹Ajfaa’: Ni mnyama aliyekonda asiye na mafuta.
mgonjwa ambaye ugonjwa wake uko wazi:
Dalili ya hayo ni Hadithi iliyopokewa na Baraa› bin ‹Aazib t kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ﷺ alisema: (Haifai kudhahi kwa mnyama mwenye jicho moja ambaye kasoro katika jicho lake iko wazi, na mnyama kiguru ambaye kiguru chake kiko wazi, na mngonjwa ambaye ugonjwa wake uko wazi, na aliyekonda asiye na mafuta [ Laa tanqii: hana duhu (mafuta).] ) [Imepokewa na Muslim.].
Na zinakutanishwa na hizi, aibu ambazo hufanana na hizi au ni mbaya zaidi kuliko hizi.



Aliyekonda



Kipofu wa jicho moja



Kiguru

## 2. Aibu zisizozuia kutosheleza kudhahi

AL-Batraa›: Asiye na mkia.

AL-Jammaa›: asiye na pembe kimaumbile.

AL-Khaswiyy: Kondoo ailiyekatwa konde zake za dhakari.

Alie na mpasuko kwenye sikio lake au tundu, au pembe yake imevunjika.

Haya yaliyotajwa kuhusu kinachotosheleza katika kudhahi ndiyo hayo hayo kuhusu tunuku na fidia.



Aliyevunjika pembe



Asiye na pembe



Asiekuwa na mkia

## Kugawanya nyama ya Udh’hiya

Imeruhusiwa na sharia kwa mwenye kudhahi ale theluthi ya nyama yake, na akiitoa sadaka yote inafaa, na akila nyingi ya ile nyama pia inafaa.

Faida

Mwenye kutaka kudhahi, haifai akate nywele zake na kucha zake na kitu chochote mwilini mwake ungiapo mwezi wa Mfungotatu mapaka achinje. Hii ni kwa hadithi iliyopokewa na Ummu Salama

t kwamba Mtume (saw) alisema: (Siku kumi zinapoingia na akataka mmoja wenu kudhahi, basi asiondowe chochote katika nywele zake na mwili wake) [Imepokewa na Muslim.]. Ama wale ambao wanafanyiwa tendo la kudhahi, kama mke na watoto, si haramu kwao kuondoa nywele au uchafu wa mwilini kama kucha.

# Kuzuru Madina: fadhila zake na utukufu wake

## Majina ya mji wa Mtume wa Madina

### 1. Madina:

Amesema Mwenyezi Mungu Aliyetukuka {Wanasema: lau tutarudi Madina watawatoa walio watukufu zaidi wale walio wanyonge zaidi} [63: 8].

### 2. Twaba:

Amepokewa Jabir bin Samurah t akisema: « Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: (Hakika Mwenyezi Mungu Aliyetukuka Ameipa Madina jina la Twaba) [Imepokewa na Muslim.].

### 3. Twayiba:

Amepokewa Zaid bin Tahabit t akisema kumpokea Mtume: (Hiyo ni Twayiba, inaondoa dhambi kama ambapo moto unaondoa uchafu wa fedha) [Imepokewaq na Bukhari na Muslim.].

## Fadhila za Madina ya Mtume

1. Sa›d bin Abii Waqqaasw t amepokewa akisema kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: (Madina ni bora kwao lau walikuwa wanajua. Haiachi mtu yoyote kwa kutoipenda isipokuwa Mwenyezi Mungu humweka mtu bora kuliko yeye awe ni badala yake. Na yoyote atakayevumilia shida zake [ La'waa': Shida na dhiki za maisha.] na usumbufu wake, nitakuwa ni muombezi wake au shahidi wake Siku ya Kiyama) [Imepokewa na Muslim.].

2. Abu Huraira t amepokewa akisema kwamba Mtume amesema: (Nimeamrishwa kwenye kitongoji [ Nimeamrishwa kwa kitongoji: nimeamrishwa nigurie hapo, niteremkie hapo na niishi hapo.] kinachokula vitongoji [ Kinachokula vitongoji: watu wake wata washinda watu wa miji mingine na kitakuwa ni kituo cha majeshi ya Kiislamu.], wanakiita Yathrib [ Wanakiita Yathrib: Watu wake walikiita Yathrib wakati wa jahilia, na sasa kinafaa kiitwe Madina.], nayo ni Madina, inawaondoa watu [ Kinawaondoa watu: Kinawatoa wabaya miongoni mwao.], kama vile kiriba [ Kiriba: ni kile kinachovuviwa na mfuzi wa chuma ndani ya moto.] kinvyoondoa uchafu wa chuma [ Uchafu wa chuma: uchafu wake na takataka zake.]) [Imepokewa na Bukhaeri na Muslim.].

## Miongoni mwa mambo yanayo husu Mji wa Madina

1. Ni mji mtakatifu wa amani kuanzia eneo la ‘Ayr mpaka Thaur. nayo ni majabali mawili. miti yake haikatwi na wanyama wake hawawindwi.

Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: (Madina ni takatifu, kuanzia ‘Ayr mpaka Thaur. Basi yoyote mwenye kuzusha uzushi humo au akampa himaya mzushi, itamshukia yeye

laana ya Mwenyezi Mungu, Malaika na watu wote) [Imepokewa na Bukhaeri na Muslim.].

Na Mtume Aliujalia mji wa Madina kuwa ni haram kama alivyo ujalia nabii Ibrahim Mji wa Makka, Amepokea Abdullah bin Zeyd kutoka kwa Mtume (Hakika ibrahim u Alijalia Makka kuwa ni haram na akauwombea, na mimi nimeujalia mji wa madina kuwa ni haram kama alivyo ufanya Ibrahim Makka, na nimeombea katika mudi wake na pishi yake Mfano alivyo ombea nabii Ibrahim mji wa Makka) [Imepokewa na Bukhaeri.]

Tafauti ilioko baina haramu ya Makka na haramu ya Madini, nikuwa haram ya Makka imekuja nasi na kwa ijmai ya wanavyooni ama haram ya madina kuna khilafu baina ya wanachuoni lakini kauli sahahi ni kuwa ni haram



Jabali la Thaur



Jabali la ‹Ayr


2. Kuswali humo thawabu zake zinaongezwa mara nyingi zaidi

Amesema Mtume : (Swala moja kwenye msikiti wangu huu ni bora kuliko Swala elfu moja kwenye msikiti mwingine

usiokuwa huo, isipokuwa Msikiti wa Haram) [Imepokewa na Bukhaeri.].

3. Ndani yake kuna bustani miongonimwa mabustani ya Pepo, na imesunniwa kuswali hapo:

Abu Huraira t alimpokea Nabii  akisema: (Baina ya nyumba yangu na mimbari yangu ni bustani miongoni mwa mabustani ya Peponi, na mimbari yangu iko juu ya Birika (hawdh) yangu) [Imepokewa na Bukhaeri na Muslim.].



Raudha tukufu

4. Masiih Dajali atakaekuja zama za mwisho hataingia humo, na janga la maradhi mabaya ya kuenea na kuua: [ Twaa›uun: maradhi mabaya.]

Anas bin Malik amepokewa akisema kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: (Dajali atakuja Madina awakute Malaika wanaulinda. Basi ugonjwa hatari wa kuambukiuza hautaingia humo wala Dajali hataingia, Mwenyezi Mungu Akitaka) [Imepokewa na Tirmidhi.].

5. Mtume  aliuombea mji wa Madina baraka:

Anas t alisema kwamba Nabii  alisema: (Ewe Mola! Ijaalie Madina baraka mara mbili zaidi ya ulivyoijaalia Makka) [Imepokewa na Bukhaeri na Muslim.].

6. kuwinda Makka mtu hupata madhambi na atalipa na kuwinda Madina mtu hupata madhambi lakini halazimiki na kitu chochote na madhambi ya kuwinda makka ni makubwa zaidi kuliko kuwinda Madina [Tazama Almumti' juzuu ya 7-ukurasa 257]

## Hukumu ya kuzuru Msikiti wa Mtume ﷺ

Kuuzuru Msikiti wa Mtume  si miongoni mwa masharti ya Hija wala nguzo zake wala wajibu zake. Hilo ni sunna, na inafaa ifanywe wakati wowote.
Na ni wajibu liwe lengo la ziara ni kuswali kwenye huo Msikiti na sio kaburi. Abu Huraira t amepokewa akisema kumpokea Mtume kuwa alisema: (Hakufungwi safari isipokuwa kwenda kwenye misikiti mitatu: Msikiti wa Haram, Msikiti wa Mtume ﷺ na Msikiti wa Aqswa) [Imepokewa na Muslim.].
Amesema Shekhe wa Uislamu Ibnu Taimiyya: “Iwapo lengo lake la safari ni kuzuru kaburi ya Mtume  na sio kuswali kwenye Msikiti wake…. Basi msimamo wa maimamu na wengi wa wanavyuoni ni kuwa hili halikuwekwa na Sheria wala halikuamrishwa…Na hadithi kuhusu kuzuru kaburi ya Mtume zote ni dhaifu kwa itifaki ya wajuzi wa Hadithi, bali ni hadithi zilizobuniwa. Hakuna yoyote miongoni mwa wakusanyaji wa vitabu vya sunna za Mtume  aliyepokea hadithi hizo, na hakuna yoyote aliyesimamisha hoja kutegemea hadithi yoyote katika hizo” [Majmuu’ al- Fataawaa, juzu. ii, uk. 26].

## Hukumu za ziara na adabu zake

1. Mwenye kuzuru afikapo msikitini ni sunna kwake atangulize mguu wake wa kulia na aseme: (Ewe Mola! Nifungulie milango ya rehema zako) [Imepokewa na Muslim.].
2. Ataswali rakaa mbili za kuuamkia msikiti, na ikiwa ataziswali kwenye sehemu ya Raudha (Bustani ya Pepo) basi ni bora zaidi.
3. Ni sunna kuizuru kaburi ya Mtume  na marafiki zake wawili: Abu Bakr kisha ‘Umar.
4. Ni sunna kwa mwenye kuuzuru Msikiti wa Mtume  aswali Swala Tano ndani ya Msikiti wa Mtume, na amtaje Mwenyezi Mungu na kumuomba kwa wingi na kuswali sunna ya ziada hasa-hasa kwenye sehemu ya Raudha tukufu.
5. Ni sunna azuru msikiti wa Baqii’ kwa ajili ya kuswali humo, ingawa kuuzuru siku ya Jumamosi ni bora zaidi, kwa hadithi

iliyopokewa na Ibnu ‘Umar t kuwa alisema: (Alikuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu  akienda kwenye msikiti wa Qubaa’ akiwa anapanda na akiwa anatembea, na akiswali hapo rakaa mbili). Na katika tamshi lingine: (Alikuwa akiujia msikiti wa Qubaa, yaani: siku ya Jumamosi) [Imepokewa na Muslim.].
6. Ni sunna kuzuru makaburi ya Baqii’ [ Baqii’: ni mahali ambapo Mswahaba wengi walizikwa hapo.], makaburi ya mashahidi na kaburi ya Hamza, kwa kuwa Nabii  alikuwa akiwazuru na kuwaombea na kusema: (Amani iwashukie nyinyi watu wa nyumba za Waumini na Waislamu. Na sisi, Mwenyezi Mungu Akitaka, ni wenye kukutana na nyinyi. Tunajiombea Mwenyezi Mungu uzima na tunawaombea na nyinyi) [Imepokewa na Muslim.].

## Makosa na matanabahisho katika kuzuru

1- Kusafiri na kujisumbua kwa safari kwa lengo la kuzuru kaburi na sehemu za turathi zilizoko Madina. Lililowekwa na Sheria ni kufunga safari kuuzuru Msikiti wa Mtume , na ziyara ya kaburi yake inaingia ndani.
2- Kuelekea upande wa kaburi Wakati wa kuomba dua
3- Kumuomba Mtume  na kutaka haja kwake, badala ya Mwenyezi Mungu Aliyeshinda na Aliyetukuka, ni miongoni mwa ushirikina mkubwa kabisa.
4- Kujipukusa na kuta za Chumba alichozikwa Mtume ndani yake kwa lengo la kupata baraka ni miongoni mwa mambo ya uzushi yaliyoharamishwa na ni miongoni mwa njia zinazopelekea kwenye ushirikina.
5- Kuinua sauti kwenye kaburi ya Mtume  na kisimamo kirefu, na kukariri salamu kwa mbali kila anapoingia na kuweka mkono wa kulia juu ya wa kushoto juu ya kifua wakati wa kutowa salamu kama vile anavyo fanya akiwa kwenye Swala.